*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

## Kikao cha Thelathini na Sita – Tarehe 25 Mei, 2021

*(Bunge Lilianza saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae. Tunaendelea Wabunge na mkutano wetu wa tatu, leo ni Kikao cha Thelathini na Sita. Katibu

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Randama ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Fungu Na. 48 na Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Fungu Na. 3 kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali tunaendelea na utaratibu wetu kama ule wa jana, nashukuru sana majibu mengi ya Serikali leo yanajaribu kujielekeza vizuri na utaratibu ni uleule kwamba mara nyingi muuliza swali anapata jibu kabla ya swali lake halijaulizwa yeye mwenyewe, nadhani utaratibu huo unaendelea.

Kwa kuwa unapata jibu kabla swali halijajibiwa hapa maana yake unakuwa umeshasoma, kwa hiyo kama una nyongeza basi inapaswa kuwa nyongeza kweli sio tena unauliza lilelile ambalo na jibu umeshapata na limeshasomwa ndani ya Bunge. Tunaanza na Ofisi ya Mheshimiwa Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, swali la Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mzava, Mbunge wa Viti Maalum, uliza swali lako Mzava.

Na. 294

### Fedha za Ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Msalala

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itazirejesha fedha za ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Msalala zilizorudishwa na mfumo baada ya mwaka wa fedha 2019/2020 kuisha?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ilipatiwa shilingi milioni 500

kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri. Hadi Juni 30 mwaka 2020, Halmashauri hiyo ilikuwa imetumia shilingi milioni 22.4 pekee na hivyo shilingi milioni 477.59 zilirejeshwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti Namba 11 ya Mwaka 2015 na Kanuni zake za mwaka 2015. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya Msalala shilingi bilioni 1 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Msalala kwa awamu hadi ujenzi wa hospitali hiyo utakapokamilika.

**SPIKA:** Safi kabisa, Mheshimiwa Dkt. Mnzava swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa ajili ya majibu ya Naibu Waziri. Maswali mawili ya nyongeza; nini *commitment* ya Serikali kuhusu tabia ya kuzichelewesha fedha na baada ya muda mfupi kuzirejesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili...

**SPIKA:** Rudia la kwanza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Nini *commitment* ya Serikali kuzichelewesha fedha kuzipeleka Halmashauri na baada ya muda mfupi kuzirejesha?

**SPIKA:** Swali lako halisomeki, la pili na la mwisho.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Je, halmashauri itakuwa...

**SPIKA:** Aah! Umechelewesha unarejeshaje tena ulichokichelewesha.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** mfumo unazichukua zile fedha...

**SPIKA:** Naam.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Kwamba inachelewesha kutuma fedha mpaka mwezi wa tano au wa nne lakini baada ya muda mfupi tu mfumo unazirejesha kwenda Hazina kabla zile fedha hazijatumika.

Nini *commitment* ya Serikali... *(Makofi)*

**SPIKA:** Rudia mara ya mwisho

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Swali la mwisho je Halmashauri...

**SPIKA:** Hilohilo hujaeleweka

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Sijaeleweka, nasema hivi...

**SPIKA:** Unajua anatoka Shinyanga ni Msukuma huyu sasa inakuwa tabu kidogo.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Nini *commitment* ya Serikali kuhusu suala la kuchelewesha fedha kuzituma katika halmashauri husika na baada ya muda mfupi kuzirejesha kupitia huo mfumo?

**SPIKA:** Yaani anachosema hela inacheleweshwa kupelekwa kwenye halmashauri hadi kwenye mwezi wa nne / tano si bajeti inaisha mwezi wa sita halafu wakishazituma kwenye halmashauri mwezi ule wa nne/tano baada ya wiki mbili/tatu wanazichukua tena fedha zilezile ndicho anachojaribu kukieleza. *(Makofi)*

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa *elaboration*.

**SPIKA:** La mwisho.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, la mwisho; je, halmashauri itakuwa inatenda kosa ikizikatalia zile fedha zisirejeshwe kwenye mfumo?

**SPIKA:** Haya, majibu ya maswali hayo tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 inaeleza vizuri utaratibu wa fedha zinazopelekwa kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zimepangiwa majukumu mahususi lakini hazitatumika mpaka tarehe 30 Juni ya mwaka husika wa fedha.

Utaratibu uliolekezwa na sheria ni kwamba Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wakishaona fedha zimeingia kwa kuchelewa na kwa mazingira halisi hawawezi kuzitekelezea majukumu yake *by* tarehe 30 Juni ya mwaka husika wanatakiwa kuandika barua kwa Katibu Mkuu Hazina kupitia Katibu Mkuu TAMISEMI kuomba maombi maalum na kutoa sababu za msingi kwamba fedha zile hazitaweza kutumika kwa tarehe husika na hivyo wapewe kibali maalum cha kutumia fedha zile ndani ya robo ya kwanza ya mwaka wa fedha unaofuata kwa maana ya Julai, Agosti na Septemba ya mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Spika, changamoto iliyopo, Wakurugenzi wengi wamekuwa hawaitekelezi ipasavyo sheria hiyo na nichukue nafasi hii kutoa wito na maelekezo kwa Wakurugenzi wa halmashauri kwanza kuhakikisha wanaongeza kasi ya utekelezaji wa miradi mara wanapopokea fedha lakini pili kutekeleza sheria hiyo kwa kuomba kibali maalum cha matumizi ya fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, pili; mifumo ambayo kimsingi inatumika katika kupeleka hizi fedha na kutumia katika mazingira hayo zina changamoto zake lakini Serikali inaendelea kuboresha kuhakikisha karibu na mwisho wa mwaka mifumo hii inafanya kazi na kuwezesha miradi ya maendeleo kutekelezwa.

**SPIKA:** Hili tuendelee tu lakini Serikali inabidi mliangalie. Mwezi huu wa tano unapeleka bilioni moja kwa ajili ya kujenga shule ya sekondari unajua kuna mambo ya *procurement* na mambo yake yalivyo halafu unataka wewe hazina Mkurugenzi wa Ngara akuandikie wewe hazina kukwambia kwamba aah siwezi kuzitumia, yaani wewe huoni unapeleka hela mwezi wa tano ukijua tarehe 15 mwezi wa sita unazichukua tena hela zilezile, sio sawa. Yeye mwenyewe anapaswaa kujua kwamba zile hela nilizozipeleka ni za miradi sina haja kwa sababu ni za miradi. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mwantumu Mzamiri Zodo mliangalie hilo ndani ya Serikali la kuchukua hela sio sawa kwa wananchi; umeshapeleka hela acha zifanye kazi. Mheshimiwa Mwantumu Zodo kwa niaba yake ndiyo Mheshimiwa nimekuona.

Na. 295

**Upungufu wa Walimu Nchini**

**MHE. CECIL D. MWAMBE K.n.y. MHE. MWANTUM M. ZODO** aliuliza:-

Kada ya Elimu inakadiriwa kuwa na upungufu wa walimu takribani 60,000.

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka kukabiliana na changamoto hiyo?

**SPIKA:** Majibu hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA - (MHE. DAVID E. SILINDE):** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantum Mzamili Zodo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Serikali ni kuendelea kuajiri na kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa walimu waliokoma utumishi wao kwa sababu mbalimbali kama vile kufariki, kustaafu na walioachishwa kazi kwa mashauri mbalimbali ya kinidhamu. Aidha, Mwezi Mei 2021 Ofisi ya Rais-TAMISEMI imetangaza ajira 6,949 za walimu wa shule za msingi na sekondari ili kukabiliana na changamoto ya uhaba wa walimu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuajiri walimu wa shule za msingi na sekondari nchini kadri ya upatikanaji wa fedha.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Serikali haioni umuhimu sasa wa kupeleka majina ya waajiriwa moja kwa moja kwa Wakurugenzi ili Wakurugenzi wawapangie vituo vya kufanya kazi badala ya kupangwa moja kwa moja kutoka TAMISEMI?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Wakurugenzi ndio wanaofahamu idadi ya upungufu wa walimu, ukiangalia Jimbo la Ndanda Wilaya ya Masasi kwa mfano, sasa je, Serikali haioni haja ya kuwapa nafasi Wakurugenzi kupendekeza nafasi za ajira kutokana na watu wanaostaafu au kufariki kwenye maeneo yao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, aHsante sana, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa tumekuwa na taratibu tofauti hususani kwa walimu ambao wamekuwa wakiajiriwa kuwapeleka katika maeneo yao husika na moja utaratibu ni kwamba sisi tumekuwa tukiwatuma katika halmashauri husika katika vituo ambavyo wao wenyewe

wamekuwa wakiomba. Kwa hiyo, wao wanaoomba zile ajira huwa wanaainisha maeneo gani wanataka kwenda kufanyia kazi na sisi tumekuwa tukitekeleza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili kuwapa mamlaka Wakurugenzi ni taratibu za kiutumishi na Serikali inafanya kazi baada ya kupata kibali kutoka Ofisi ya Rais (Utumishi) ambao wanatuletea namna, vigezo na sababu mbalimbali za mtu kuajiriwa. Kwa hiyo, kama kuna mapendekezo hayo ya kutaka kubadilisha ni Bunge lako Tukufu ndio lenye mamlaka hiyo, ahsante sana.

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Mbunge wa Longido uliza swali lako.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna uhaba mkubwa wa walimu nchini na Serikali imekuwa inawaajiri kwa awamu kidogo kidogo na bado pengo ni kubwa, imebidi shule nyingi zitumie walimu wa kujitolea na ajira zinapotangazwa unakuta mwalimu aliyejitolea amepangiwa kwenda shule mbali na ile aliyojitolea.

Je, Serikali haioni sasa ni muhimu wale walimu wote waliojitolea na walimu wale wakuu wamewapendekeza kwamba ikitokea ajira waajiriwe palepale walipojitolea?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kiruswa, Mbunge wa Longido kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli tungetamani walimu wote ambao wanajitolea katika maeneo yao husika wapangiwe maeneo hayo lakini bahati mbaya inatokana na ule uhaba ambao unatokana. Kwa mfano kama sasa hivi tuliomba taarifa za walimu wote wanaojitolea mashuleni tukaletewa nafasi walimu wanaojitolea 70,000 na nafasi ambazo

zimetangazwa na Serikali ni 6,000 kwa hiyo nafikiri unaweza kuona ni changamoto kiasi gani tunapitia katika kukabiliana na janga hili.

Mheshimiwa Spika, Serikali bado ina nia njema kuhakikisha kwamba itaendelea kuajiri walimu kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha na bajeti ambayo tutakuwa tunajipangia na kila mwaka tutakuwa tunaendelea kufanya hivyo walau kuhakikisha kwamba tuna *accommodate* hili ambalo Mheshimiwa Mbunge amelieleza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Ummy Mwalimu majibu ya nyongeza.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Kiruswa kwa swali lake la nyongeza kwa nini tusiajiri walimu ambao wanajitolea. Ni kweli kigezo kikubwa ambacho tutakitumia katika kuangalia wenye vigezo ni wale ambao wanajitolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kukiri sasa hivi yapo malalamiko hata hao wanaojitolea kuna wengine wameleta barua za *fake* za kusema kwamba wanajitolea wakati hawajitolei. Kwa hiyo, jana tumepokea pia maelekezo yako suala hili ni tete, nafasi ni 6,949 mpaka juzi walioomba wameshafika 89,958. Kwa hiyo, suala hili naomba utuamini Serikali tutatenda haki; hata hao wanaojitolea tutawachambua kama ni kweli wanajitolea.

Mheshimiwa Spika, pia kuna walimu wamemaliza 2012, 2013, 2014, 2015 hawajaajiriwa kwa hiyo upo pia mtazamo ndani ya Wizara labda tuangalie hawa ambao wamemaliza siku nyingi wanajitolea na hawajapata ajira kwa sababu muda wao wa kuajiriwa pia unapungua kwa sababu lazima waajiriwe kabla ya miaka 45. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana uiamini Serikali suala hili ni tete, walioomba wenye vigezo ni wengi, nafasi ni

chache lakini tutatenda haki kama ulivyoelekeza bila kubagua dini, kabila, jinsia wala upendeleo wa nafasi yoyote. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida nilikuona.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, pamoja na jitihada ambazo Serikali inafanya juu ya kuajiri walimu lakini kuna changamoto kubwa kwenye maeneo ya vijijini kukosa walimu wa kike.

Ningependa kujua mkakati wa ziada wa Serikali inafikiri nini juu kuondoa hizo changamoto ambazo watoto wa kike wanakutana nazo shuleni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni swali zuri na mimi kama mama tunahitaji pia kuwa na walimu wanawake katika shule zetu za msingi na sekondari ni moja ya kigezo tutaki-*take into consideration* katika kutoa ajira mpya lakini pia kufanya *reallocation* ya walimu katika shule zetu za msingi na sekondari hususani za vijijini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, walimu sina takwimu lakini ninavyohisi walimu wanawake kwa wanaume, walimu wanawake ni asilimia 80 walimu wanaume ni asilimia 20. Mijini huko unaweza kukuta shule ina walimu 60, wanaume 2, 58 wanawake. Kwa hiyo, mkizidi sana kuongeza upande huo! Tunaendelea na Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) swali la Mheshimiwa Maida Hammad Abbdalah... nyie wanaume mnakaakaa hapa mtaisha ninyi. Mheshimiwa Maida. *(Kicheko)*

Na. 296

**Utekelezaji wa *TASAF* III Awamu ya Kwanza**

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH** aliuliza:-

Vipo baadhi ya Vijiji vilivyoorodheshwa kwa ajili ya kufikiwa na miradi ya *TASAF III* Awamu ya Kwanza upande wa Zanzibar lakini bado havijafikiwa na mradi unaelekea mwisho:-

Je, Serikali inasemaje juu ya maeneo ambayo hayajafikiwa na Mradi?

**SPIKA:** Ahsante sana, majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Ndejembi, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) naomba kujibu swali la Mhe. Maida Hammad Abdalla Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *TASAF* haujafika mwisho na *TASAF* itafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba kaya zinazotambuliwa na kuandikishwa kwenye mpango ni zile kaya maskini sana.

Mheshimiwa Spika, kipindi cha pili cha utekelezaji wa Mradi wa *TASAF* kimeanza baada ya uzinduzi uliofanyika tarehe 17 Februari, 2020. Zoezi la utambuzi na uandikishaji wa kaya za walengwa katika Vijiji/Mitaa/Shehia 5,590 ambazo hazikufikiwa na mpango wakati wa kipindi cha kwanza kimeanza tarehe 19 Aprili mpaka tarehe 6 Mei, 2021 kwa mzunguko wa kwanza.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Zanzibar jumla ya Shehia 304 tayari zinanufaika na mpango wa *TASAF.* Hata hivyo, jumla ya Shehia 157 ambazo hazikuwa kwenye mpango zimeshaandikishwa na ifikapo mwezi Julai, 2021 Shehia hizo zitaanza kunufaika na Mpango wa *TASAF.*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwasisitiza viongozi katika Vijiji/Mitaa na Shehia zote kutoruhusu vitendo vya upendeleo na kuingiza kaya ambazo hazina vigezo kwenye Mpango. Maeneo ambayo yatabainika kuwa na kaya zisizo na vigezo, viongozi watachukuliwa hatua za kinidhamu kwani watakuwa wamehusika kufanya udanganyifu na kuingiza wasiohusika kwenye Mpango. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Muuliza swali Mheshimiwa Maida, swali la nyongeza.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa utekelezaji wa *TASAF III*, Awamu ya Kwanza wapo wafaidika 1,000 na zaidi wanaotoka katika Shehia 78 za Pemba ambao walikuwa katika utaratibu wa malipo na majina yao yaliachwa. Je, Serikali inasema nini kuhusu kulipwa fedha zao wafaidika hawa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa wananchi hawa maskini waliingia katika mikopo mbalimbali kwa kutegemea kwamba fedha wanazoendelea kuzipata zinawasaidia katika kujikimu kimaisha. Je, Serikali inaweza kututhibitishia kwamba ni bajeti ipi itawalipa fedha hizi kwa sababu mradi wa *TASAF III,* Awamu ya Kwanza umeisha?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maida, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka jana mwezi Juni ulifanyika uhakiki wa kaya zote ambazo zinapokea fedha za *TASAF*.

Kaya zile ambazo hazikutokea kwenye uhakiki ziliondolewa kwenye mpango mpaka pale watakapokuja tena kuhakikiwa ili malipo yao yaweze kuendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa kesi hii ya Pemba kwenye Shehia 78 kuna walengwa 1,200 ambao hawakujitokeza kwa ajili ya kufanyiwa uhakiki na malipo yao yalisitishwa. Hata hivyo, ilipofika uhakiki wa awamu ya pili uliofanyika mwezi Desemba, 2020 walengwa 300 walijitokeza na walengwa 900 bado hawajajitokeza kufanyiwa uhakiki.

Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pale tu walengwa hawa watakapojitokeza kufanyiwa uhakiki basi malipo yao yatarejeshwa na wataendelea kupokea fedha hizi za *TASAF*.

Mheshimiwa Spika, swali lake la nyongeza la pili ameuliza ni nini Serikali inafanya, kama nilivyojibu kwenye swali lake la nyongeza la kwanza ni pale tu hawa 900 watajitokeza kufanywa uhakiki basi malipo yao yatarejeshwa na wataendelea kuwepo kwenye mpango.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na swali linalofuata, nadhani Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge wa Kilolo.

Na. 297

**Ujenzi wa Makao Makuu ya Polisi ya Wilaya ya Kilolo**

**MHE. LAZARO J. NYAMOGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Makao Makuu ya Polisi ya Wilaya ya Kilolo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lazaro Justin Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua hitaji la ofisi ya Makao Makuu ya Polisi Wilaya ya Kilolo na eneo linalohitajika kujengwa ofisi limeshapatikana na ni eneo la Luganga na lina ukubwa wa hekari 16. Zoezi la kufanya tathmini ili kulipa fidia wananchi limeshafanyika tangu mwezi Julai 2020 kupitia wataalam toka Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo na kupata makadirio ya shilingi 110,092,554.00 zinazohitajika kulipa fidia wananchi hao.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi inatafuta fedha kwa ajili ya kulipa fidia wananchi na mara baada ya kuwalipa wananchi fidia kwa mujibu wa sheria na taratibu ujenzi utaanza mara moja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Kilolo.

**MHE. LAZARO J. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Serikali inatarajia kupata fedha hizo lini ili wale wananchi waweze kulipwa fidia badala ya kuendelea kusubiri kwa muda mrefu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kutokana na umbali uliopo kati ya Makao Makuu ya Wilaya na Kituo cha Polisi ambacho kinatumika kama Makao Makuu ya Polisi, Serikali ina mpango gani wa kuongeza fedha za *OC* ili ofisi ile ya Polisi ya Wilaya iweze kujiendesha bila karaha wala kuombaomba fedha kwa wadau wengine?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ameuliza, je, lini Serikali italipa fidia? Nataka nimjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inao mpango na italipa fidia wananchi hao kwa ajili ya eneo hilo kwa sababu inatambua umuhimu wa uwepo wa Kituo hicho cha Polisi ili wananchi waweze kupata huduma hizo. Kubwa zaidi tayari tumeshatoa maelekezo na wameshafanya tathmini wataalam kutoka Halmshauri ya Wilaya ya Kilolo inayohitajika kwa ajili ya fidia hiyo na tayari tumeshaelekeza pa kwenda kupata fedha hizo kwa ajili ya kulipa fidia wananchi hao. Kwa hiyo, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea kufanya juhudi kuona namna bora ya kuwalipa fidia wananchi hao. Kubwa Mheshimiwa Mbunge aendelee kuzungumza na wananchi wake ili waendelee kuwa na subra jambo hilo limo mbioni kushughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili anauliza kama Serikali ipo tayari kuongeza *OC*. Niseme tu kwamba Serikali ipo tayari kuongeza *OC* lakini ni pale ambapo tutakuwa na fedha ya kutosha kufanya hivyo. Kwa hiyo, kwa sasa waendelee kuwa na subra hivyo hivyo tubananebanane lakini tunao mpango huo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo upo mbadala ambao tumeshauchukua, kwanza tumeongeza operesheni ama doria za mara kwa mara katika maeneo ambayo wananchi wako mbali na vituo vya polisi ili waweze kupata hizo huduma za ulinzi. Vilevile tunaendelea kusisitiza ulinzi shirikishi ambapo inasaidia huduma za ulinzi kufika mpaka maeneo ya vijijini kwenye kata. Lengo na madhumuni ni wananchi waendelee kupata huduma za ulinzi na waishi kwa amani.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nyamoga kusema ukweli swali lako la msingi halijajibiwa, Waziri hapa amepiga Kiswahili tu na ulitakiwa umwambie hivyo kwamba swali lako halijajibiwa. Mheshimiwa Naibu Waziri hamjajibu swali maana umeulizwa ni lini yaani Serikali iko mbioni, sasa mbioni siyo jibu. *(Makofi)*

Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mbunge wa Mtambwe.

Na. 298

**Mabadiliko ya Sheria ya Mikopo ya Elimu ya Juu**

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali italeta Bungeni Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Mkopo wa Elimu ya Juu ili kuwapunguzia mzigo mkubwa wa malipo wanufaika wa mkopo huo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Omari Kipanga, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mbunge Mtambwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikifanya mapitio katika tozo na makato yanayohusu mikopo ya elimu ya juu ili kuwapunguzia mzigo wa tozo na makato wanufaika wa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuanzia tarehe 01 Julai, 2021 Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, itafuta Tozo ya Asilimia Sita (6%) ya kulinda thamani ya fedha inayotozwa kwa wanufaika wa mikopo hiyo. Vilevile, Bodi ya Mikopo itatekeleza maelekezo yangu ya kuondoa tozo ya asilimia kumi (10%) ya wanufaika wanaochelewa kurejesha mkopo baada ya muda wa miezi 24 kupita baada ya kuhitimu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kupunguzwa kwa mzigo wa makato na tozo, nitoe wito kwa wanufaika wote wa mikopo ya elimu ya juu ambao hawajajitokeza, kuanza kurejesha mikopo hiyo ili fedha hizo ziwasomeshe Watanzania wengine wahitaji.

**SPIKA:** Ahsante sana. Muuliza swali Mheshimiwa Khalifa.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuondoa tozo ile lakini pia mpango ambao Wizara ya Elimu inaupanga kuondoa tozo ya asilimia 10 kwa wanufaika baada ya grace *period*. Hata hivyo nina maswali mawili madogo ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa Serikali inakata asilimia 15 ya *gross salary* ya mnufaika baada ya kuajiriwa, je, haioni asilimia 15 ni kubwa haiwezi kuipunguza mpaka kufikia angalau *single digit*; asilimia 5, 6 mpaka 9? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwa kuwa mfuko huu unanufaisha wale *degree holders* haioni sasa wakati umefika kushuka chini katika vyuo vya kati kama vile *VETA, FDCs* na kadhalika?

**SPIKA:** Ahsante sana umeeleweka. Majibu ya maswali hayo, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Omari Juma Kipanga, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba sasa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Khalifa, Mbunge wa Mtambwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli wanufaika hawa huwa wanakatwa asilimia 15 kutoka kwenye mshahara wao ghafi kwa ajili ya kurejesha mikopo hii. Lengo la kukata asilimia 15

ni ili kuweza kurejesha fedha zile kwa haraka na kwa muda mfupi. Hata hivyo, tupokee mapendekezo ya Mheshimiwa Mbunge ya kuangalia namna gani tunaweza kupunguza eneo hilo. Kwa vile tarehe 4 na 5 ya mwezi huu tuliwasilisha bajeti yetu hapa na miongoni mwa mijadala iliyotokea ni kuhusiana na hii Bodi ya Mikopo na kwa vile tutakuwa na mjadala mpana wa kitaifa, nimuahidi Mheshimiwa Mbunge tunakwenda kulijadili na hili tuweze kuangalia namna gani tunaweza tukalizingatia.

Mheshimiwa Spika, swali la pili anauliza mikopo hii imewalenga sana wale wanaochukua elimu ya juu kwa maana ya *degree,* ni namna gani tunaweza tukafikia zile kada za vyuo vya kati. Kwa vile tutakuwa na mjadala mpana wa kitaifa juu ya mwelekeo ya elimu katika Taifa letu basi na hili nalo tutakwenda kulijadili kwa kina na ninyi Waheshimiwa Wabunge mtakuwa ni sehemu ya mjadala huo, tunaamini tutapata mawazo endelevu kuona ni namna gani tunaweza nalo hili tukaliingiza kwenye mpango.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunafurahi kusikia habari ya mjadala mpana wa kitaifa lakini bado suala la Wabunge watahusikaje katika mjadala huu mpana wa kitaifa hamjaliweka vizuri likaeleweka, ni namna gani Wabunge watashiriki katika huo mjadala mpana wa kitaifa kuhusu masuala ya elimu.

Tunaendelea na bado tuko Wizara hiyohiyo ya Elimu, Sayansi na Teknolojia sasa ni swali litakaloulizwa na Mheshimiwa Stella Ikupa Alex.

Na. 299

**Malipo ya Elimu ya Juu kwa Watu Wenye Ulemavu**

**MHE. STELLA I. ALEX** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa Mikopo ya Elimu ya Juu kwa Watu wenye Ulemavu kama ruzuku badala ya mikopo kama ilivyo sasa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo kuhusu walemavu kupatiwa mikopo kwa ruzuku, Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mikopo inayotolewa na Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu inaongozwa na Sheria ya Bodi ya Mikopo (SURA 178) ambayo inabainisha kuwa fedha na mikopo hiyo ni kwa ajili ya wanafunzi wahitaji (*needy*) wenye sifa za kujiunga na taasisi za elimu ya juu (*eligible*). Lengo la matakwa haya ya kisheria ni kuwawezesha wanafunzi wote wahitaji, wenye ulemavu na wasio na ulemavu, wanaotoka kwenye familia zenye uwezo mdogo wa kiuchumi kufikia ndoto zao za kupata elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, sheria pia inaipa Bodi mamlaka ya kuweka vigezo vya ziada ambapo katika mwaka wa masomo 2020/2021, Mwongozo wa Utoaji Mikopo ulitoa kipaumbele kwa makundi maalum wakiwemo wenye ulemavu au waombaji mkopo wenye wazazi wenye ulemavu. Kwa kutumia kigezo hiki, katika mwaka wa masomo 2020/2021, jumla ya wanafunzi 92 wenye ulemavu au wazazi wenye ulemavu walipangiwa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 350.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kutoa ruzuku badala ya mikopo, Serikali italifanyia kazi kwa kuzingatia dhana nzima ya utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wenye uhitaji na kuwa na mfuko endelevu wa mikopo ya elimu ya juu nchini.

**SPIKA:** Ahsante sana, tunapoelekea mpunguze majibu yawe mafupi Zaidi. Mheshimiwa Stella Ikupa, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuweka ulemavu kama kigezo kimojawapo cha upatikanaji wa mikopo kama ambavyo Bunge la Kumi na Moja liliweza kushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali hili si mara yangu ya kwanza naliuliza ndani ya Bunge hili, lakini pia mara kadhaa nilipopata kuchangia niliweza kuchangia na jibu limekuwa ni hili. Kama ambavyo jibu limesema kwamba Serikali italifanyia kazi, ni lini Serikali itaanza kulifanyia kazi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo kwa kifupi sana, ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SANYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ikupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishajibu katika majibu yangu ya swali la msingi kwamba Serikali inaendelea kulifanyia kazi suala hili. Kama nilivyokwishaeleza hapa punde kwamba katika mjadala wetu wa bajeti tulisema kwamba tunakwenda kuwa na mjadala mpana kuhusiana na elimu yetu nchini kwa maana kwamba tunaenda kuangalia Sera yetu ya Elimu ya mwaka 2014, lakini tunaenda kuangalia Sheria yetu ya Elimu ya mwaka 1978. Hili nalo kwenye mjadala huo litakwenda kujadiliwa kwa kina na kuona ni namna gani tunaweza kuyafikia makundi haya badala ya kuwapa mikopo tukatoa ruzuku. Nadhani kabisa katika mjadala huo tunaweza tukayaingiza.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Lembulis Saputi.

Na. 300

## Fidia kwa Wananchi wa Vijiji vya Lengijape, Ilkurot na Olkejulenderit – Arumeru

**MHE. NOAH L.S. MOLLEL aliuliza:-**

Je, ni lini Serikali itawalipa fidia ya kupisha njia kubwa ya umeme wananchi wa Vijiji vya Lengijape, Ilkurot na Olkejulenderit katika Jimbo la Arumeru Magharibi?

**SPIKA:** Mheshimiwa kwa nini wewe huitwi Ole Saputi? *(Kicheko)*

Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mollel, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la Umeme *TANESCO* inaendelea kukamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 400 kutoka Singida hadi Namanga. Lengo kuu la mradi huu ni kuimarisha upatikanaji wa umeme katika Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TANESCO* imeshalipa fidia kwa wananchi wote jumla ya shilingi bilioni 52.67 zikiwa ni fidia kwa wananchi 4,526 katika mikoa yote mitatu iliyoguswa na mradi huu wakiwemo wananchi wa Vijiji vya Lengijape, Ilkurot na Olkejulenderit katika Jimbo la Arumeru Magharibi. Aidha, Serikali kupitia *TANESCO* imeshalipa fidia kwa taasisi zilizopo katika vijiji vyote vya Wilaya za Singida Vijijini, Hanang, Babati na Longido.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya ulipaji wa fidia shilingi bilioni 314.675 kwa maeneo ya taasisi na vijiji 38 katika

Wilaya za Monduli, Arumeru na Manispaa ya Sindida yanaendelea na maeneo ya vijiji na taasisi hizo yatalipwa fidia kupitia Wakurugenzi wa Halmashauri husika ifikapo mwezi Juni, 2021.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saputi.

**MHE. NOAH L.S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, kwanza jina langu naitwa Noah Lemburis Sabutu Mollel.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza kabisa, namshukuru Naibu Waziri kwa kurekebisha kwamba siyo milioni 314 badala yake ni bilioni 314 ndiyo inayodaiwa na Halmashauri *Arusha DC.*

**SPIKA:** Amerekebisha wapi.

**MHE. NOAH L.S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, kwenye majibu ya maswali hayo iliandikwa milioni 314 badala ya bilioni 314.

**SPIKA:** Sasa wewe ndiyo unatutaarifu hilo Mheshimiwa, siyo walitakiwa waseme wao kama hivyo ndivyo? Endelea na swali lako lakini.

**MHE. NOAH L.S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali yangu mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa suala hili la ulipaji wa fidia ya umeme lilikuwa liende sambamba na usambazaji wa umeme kwenye Jimbo la Arumeru Magharibi na vijiji vyake hasa ukizingatia kwamba mkandarasi amechimba mashimo ameacha, ameweka nguzo ameacha ajaweka waya, ni lini sasa Serikali itamaliza tatizo hilo?

**SPIKA:** Tatizo gani?

**MHE. NOAH L.S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, la kutokuwepo kwa umeme kwenye jimbo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa sasa hali ni tete kwenye jimbo kuhusu masuala hayo mawili ya fidia na usambazaji wa umeme, Naibu Waziri yupo tayari tuweze kuongozana naye kwenda kuokoa jahazi ambapo hali ni tete kwenye jimbo?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muwe mnajitahidi kusoma majibu ya maswali haya ili mpate ile picha kwa sababu kumbukumbu hizi zinakaa miaka mingi sana na ndizo kumbukumbu ambazo wananchi hata baadaye wanachukua kuangalia miaka hiyo kulikuwa na nini kinaendelea na Serikali ilisema nini kuhusu tatizo fulani. Serikali inapojibu kitu katika nchi; inaweza ikajibu kwenye mkutano wa hadhara na sehemu nyingine lakini inapojibu Bungeni inapaswa kujibu jibu ambalo ndiyo lenyewe. Ndiyo maana nataka kusisitiza kuhusu umakini wa kujibu Bungeni kwa sababu jibu la Bungeni ndiyo lenyewe. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Wizara ya Nishati unakuja Mheshimwa Naibu mjitahidi kujibu maswali. Kwa nini nasema hivyo? Mmetuambia Serikali kupitia *TANESCO* imeshalipa fidia kwa wananchi wote jumla ya shilingi bilioni 52 zikiwa ni fidia ya wananchi 4,500 katika mikoa yote mitatu. Wakati huo mmeshalipa yote bado anasema kwamba hakuna chochote sasa pale inakuwa tabu. Mheshimiwa Naibu Waziri naona amesimama Waziri mwenyewe, karibu.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye swali la msingi naomba niliweke vizuri hoja ya Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine ambao wanapitiwa na mradi wa *kilovolt* 400 wa kwenda Namanga. Ni kweli Serikali imetoa shilingi bilioni 52.67 katika maeneo yote ambako laini inapita. Lakini kila eneo ilipewa fidia yake kulingana na idadi ya watu waliofanyiwa tathmini kwa hiyo pesa hiyo inagawanywa katika maeneo yote ambako *line* imepita.

Mheshimiwa Spika, juzi nilikuwa Arusha na kati ya changamoto ambazo nilikutana nazo ni pamoja na hii,

akiwepo na Mheshimiwa wa Longido, nilitoa maelekezo ya jumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wananchi ambao hawajalipwa fidia kwa sasa ambao pesa zao zimeshapelekwa tayari kwa Wakurugenzi wao walipwe fidia hizo mara moja toka juzi. Ni kweli zinaweza zikawa zinatofautiana kiwango kwa kiwango kila wilaya lakini ya jumla ya fedha zake ni hizi. Lakini majibu ya jumla nishatoa juzi, kwa Mheshimiwa Mbunge wa Longido na wananchi walilidhika na Wakurugenzi walikubali na Wakuu wa Wilaya kuanza kulipa fidia hizo mara moja kutoka juzi ndani ya siku 10.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili kuhusiana na maeneo ambayo amezungumza ambayo ajapelekewa umeme nimetoa maelekezo na wakandarasi wote wako *site* na leo tunakutana nao, maeneo yote ambayo awajapatiwa umeme wakandarasi wameanza kazi toka Mwezi Machi na katika wilaya za Arusha wameanza wiki iliyopita na watapelekewa umeme ndani ya miezi 18 kutoka mwezi Machi hadi mwezi Mei. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri hayo ndiyo yangekuwa majibu tusinge kuwa na swali lolote kutokea mwanzo tusingekuwa na shida hiyo ahsante sana tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano Teknolojia na Habari, Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil Mbunge wa Koani.

Na. 301

**Shirika la Posta Kurejesha Faida kwa Jamii – Kwahani**

**MHE. YAHYA ABDULWAKIL AHMED** aliuliza: -

Je, Shirika la Posta Zanzibar halioni umuhimu wa kuchimba kisima katika Jimbo la Kwahani katika Kitongoji kilichopo karibu na Ofisi hiyo ili kukuza ujirani mwema?

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdul Wakil ili swali naliruhusu leo lakini siku zijazo maswali kama haya nitayafuta tunapaswa

tuulize maswali ambayo ni moja kwa moja yanakwenda kwa Waziri katika mambo ambayo yako katika *portfolio* yake. Waziri huyu unamuuliza ni wa posta anayejibu swali hili lakini unamuuliza Habari ya kisima cha maji sasa posta kazi yao kuchimba visima vya maji ndio hii nasema kuhusu maswali lazima twenda na utaratibu, Mheshimiwa waziri majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Abdul Wakil Ahmed Mbunge wa Kwohani kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Shirika la Posta Tanzania ni taasisi ya Kimuungano ambapo kwa upande wa Zanzibar ina jumla ya Ofisi tisa, kati ya Ofisi hizo, Unguja kuna Ofisi tano ambazo zipo Kijangwani, Shangani, Mahonda, Jambiani na Makunduchi; na Pemba kuna Ofisi nne zilizopo Chakechake, Wete, Mkoani na Kengeja.

Mheshimiwa Spika, Shirika limekuwa na utaratibu kila mwaka wa kutekeleza shughuli mbalimbali za kijamii kwa kuzingatia mtiririko wa fedha na bajeti ya mwaka husika. Kwa kipindi cha miaka mitatu yaani 2018 hadi 2020 Shirika katika kuchangia huduma za kijamii kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar – SMZ imefanya yafuatayo: -

(i) Mwaka 2018, Shirika lilitoa vifaa mbalimbali katika Kituo cha wazee cha Amani ili kusaidia matunzo ya wazee katika kituo hicho.

(ii) Mwaka 2019, Shirika lilitoa vifaa mbalimbali katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ili kusaidia akinamama wanaojifungua.

(iii) Mwaka 2020, Shirika lilitoa msaada wa vifaa mbalimbali kwa ajili ya kusaidia wazee wanaotunzwa katika kituo cha kulelea Wazee cha Welezo kilichopo Unguja.

Mheshimiwa Spika, Shirika linaendelea na utaratibu wake wa huduma kwa jamii kulingana na bajeti. Shirika litaangalia uwezekano wa kuchangia uchimbaji wa kisima katika kitongoji kilichopo karibu na ofisi katika kuendeleza ujirani mwema kadri ya upatikanaji wa fedha utakavyoruhusu, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Abdul Wakil ndio maana wamekujibu hivyo kwamba shirika litaangalia uwezekano kwa sababu sio jukumu lao la kimsingi. Kwa hiyo, tunaendelea na swali linalofuata la Mheshimiwa Katani Ahmad Katani Mbunge wa Tandahimba.

Na. 302

**Tatizo la Mawasiliano Kata za Litehu, Ngoja na Mkwiti – Tandahimba**

**MHE. KATANI A. KATANI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itapeleka Mawasiliano ya Simu yenye usikivu katika Kata ya Litehu, Ngunja na Mkwiti Wilayani Tandahimba?

**SPIKA:** Majibu ya swali la hili Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari naomba kujibu swali la Mheshimiwa Katani Ahmed Katani Mbunge wa Tandahimba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote unatekeleza miradi saba katika kata sita za Jimbo la Tandahimba kupitia Mradi wa Awamu ya nne na tano . Miradi hiyo inatekelezwa katika Kata za Chaume, Mdimba Mnyoma, Mkoreha katika Kijiji cha Chikongo, Ngunja. Kuna miradi miwili mmoja uko Kijiji cha

Ngunja na mwingine Namindondi Juu, lakini katika Kata ya Mihambwe, na Namikupa utekelezaji wa mradi uliopo katika hizo Kata unaendelea.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na jitihada hizo za Serikali, bado kuna maeneo mengi ya Jimbo la Tandahimba ambayo yana changamoto za mawasiliano. Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano imevifanyia tathmini vijiji vya Kata za Litehu, Ngunja na Mkwiti katika Jimbo hilo.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba zinaingizwa katikazabuni ya mradi wa mipakani na kanda maalumu ya Kanda Maaalum awamu ya sita yaani *Border and Special Zone Phase* six Mradi huu unatarajiwa kutangazwa kabla ya kuisha kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Katani.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nataka sasa kujua.

Je, ni mchakato gani unapitia mpaka minara hii kuwa imekamilika kwenye maeneo yetu kwa sababu inachukuwa muda mrefu sana?

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili Kata ya Michenjele ambayo iko mpakani na Msumbiji nako kuna tatizo kubwa la usikivu wa mawasiliano ya simu hakuna hata mnara wa aina moja ambao unapatikana kule Michenjele

Je ni lini Serikali itapeleka huduma hii kwenye maeneo yale ya mpakani?

**SPIKA:** Rudia swali lako la kwanza

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, la nyongeza.

**SPIKA:** La kwanza hujaeleweka ulikuwa unauliza nini?

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, la nyongeza. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Umeuliza maswali mawili; la kwanza hujaeleweka ulikuwa unataka ujibiwe nini hasa, Serikali ikujibu nini?

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza nimeuliza ni utaratibu gani unatumika mpaka mnara ule uwe unakamilika kwenye maeneo yale ya vijijini kwa sababu kuna maeneo kunakuwa na changamoto wakati wa uwekaji wa minara na kunakuwa na shida hizo.

**SPIKA:** Waheshimiwa utaratibu gani unatumika mpaka mnara ukamilike kweli! Jibu swali la pili Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Katani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kata ya Michenjele ipo katika vijiji ambavyo vimeshafanyiwa tathmini kwa ajili ya Awamu ya Sita ya mipakani na *border and special zone.* Lakini kata hizi ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja kwa mfano Kata ya Mihambwe tayari kuna mtoa huduma wa *airtel* ambao anaendelea na utekelezaji wa ujenzi wa minara.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Kata ya Mdimba kama ambavyo nilijibu katika swali langu la msingi kuna mtoa huduma tayari ambaye ni *tigo* ambaye anaendelea na utekelezaji lakini pia kina Kata ya Chaume ambapo tayari kuna mtoa huduma ambaye anaendelea na ujenzi wa mnara katika maeneo hayo. Ahsante.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Joseph George Kakunda Mbunge wa Sikonge uliza swali lako.N

Na. 304

## Kumaliza Tatizo la Ujenzi Holela Mijini

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kusamehe kodi za miaka ya nyuma Taasisi za Dini zilizokuwa zikiendeshwa kwa utaratibu usiolenga kupata faida na kuziwekea utaratibu Taasisi hizo kuanza kulipa tangu walipojulishwa kutakiwa kulipa kodi?

**SPIKA:** Swali hili majibu yake Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula kuhusu tatizo sugu la ujenzi holela mijini.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Wa Ardhi, Nyumba Na Maendeleo ya Makazi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti na kukabiliana na ujenzi holela mijini wizara imeandaa *program* ya utambuzi upangaji na umilikishaji wa ardhi yote katika kipindi cha miaka kumi, aidha katika bajeti ijayo wizara kwa kushirikiana na mamlaka za upapangaji imetenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mkakati ya utambuzi na upangaji upimaji na umilikishwaji wa ardhi nchini.

Mheshimiwa Spika, rai yangu kwa mamlaka zote 184 za upangaji kuendelea kutenga bajeti ya kutosha ili kuongeza kasi ya upangaji upimaji na umilikishaji wa ardhi ili kuwa na maeneo mengi yaliyopimwa ili kukabiliana na tatizo sugu la ujenzi holela. Ubunifu wa mbinu mpya ya upimaji ambayo ni shirikishi inayotumia teknolojia rahisi ya simu janja imeongeza kasi na usahihi wa kuimarisha majira nukta kwa kutumia *GPS* yaani *Global Position System*.

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2023 maeneo yote yaliyoendelezwa bila kufuata taratibu za ujenzi mjini yawe yametambuliwa na kurasimishwa ambako program ya urasilimishaji ya miaka kumi yani 2013 mpaka 2023 itakuwa imefikia ukomo.

Mheshimiwa Spika, nizitake mamlaka zote za upangaji waongeze kasi ya utambuzi wa maeneo ambayo hayajaendelezwa kwa ajili ya kuyapanga na kuyapima na hivyo ujenzi holela mjini kukoma.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizi ofisi ya Rais-TAMISEMI pia inatekeleza *program* ya uboreshaji mfumo wa udhibiti wa ujenzi holela mijini *Development Control strategic Program* kwa kushirikiana na benki ya dunia. *Program* hii itawezesha mamlaka zote kuanzia ngazi ya mtaa kusimamia kudhibiti uendelezaji holela na kutoa taarifa za uendelezaji unaokiuka taratibu za ujenzi mijini ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda uliza swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwanza naipongeza Serikali kwa majibu hayo na hasahasa kupima viwanja 56,792 katika kipindi kidogo cha miezi tisa, lakini Sikonge pale Mjini niao wananchi 2000 kwenye maeneo ya Ukanga wana viwanja 1400 na Majengo viwanja 6000 jumla viwanja 2000 kwa muda mrefu sana zaidi ya miaka 10 wanaomba hati hawajapatiwa.

Mheshimiwa Spika, sasa je, swali langu la kwanza wizara inawasaidieje wananchi wa Sikonge waweze kupata hati zao kwa haraka?

Mheshimiwa Spika, la pili je, Serikali haioni kwamba sasa hivi hapa nchini kuna uchumi mgumu kiasi ambacho wananchi wanapata shida kupata laki 150 kwenye miji ya vijiji kama Sikonge kupima kiwanja kimoja je, Serikali haioni kwamba hasa kuna wakati umefika wa kuwapa ruzuku...

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** ili waweze kupata hati zao za ardhi

**SPIKA**: Majibu ya maswali hayo mawili Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Mabula tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kakunda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza anataka kujua tu kwamba ni lini utoaji hati utafanyika katika maeneo hayo. Tayari tulishafungua ofisi za mikoa na katika kasi ya utoaji hati sasa hivi inakwenda kwa kasi kubwa naomba nimuhakikishie tu kwamba ofisi yetu ya Tabora Mjini itakwenda kukamilisha hiyo na kwa kupitia majibu ninayotoa sasa basi wafike katika hayo maeneo mawili ndani ya Sikonge yenye viwanja 2000 ambao nasema kwamba hawajapewa hati mpaka leo, iwapo watakuwa wamekamilisha taratibu zote za umilikishaji.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili anazungumzia suala la ruzuku kwamba 150,000 katika suala zima la upimaji ni gharama kubwa. Naomba niseme tu kwamba gharama hii si kubwa kama tunavyofikiri lakini pia inategemea na eneo husika maana kuna maeneo mengine mpaka sasa wanalipa 60,000 wanalipa 90,000. Wakiwa watoaji ni wachache unakuta kwamba ile gharama hata ya yule anayeenda kupima inakuwa kidogo ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuwa na watu wengi kwa wakati mmoja wanayohitaji gharama zile zinashuka kwa hiyo gharama zinashuka kutegemeana na *volume* ya kazi ambayo mpimaji anakwenda kufanya pale. Niwaombe wananchi kwamba suala la urasimishaji linakwenda kuisha 2023 kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwa sababu ilikuwa programu ya miaka kumi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, waongeze kasi sasa hivi ili kazi ile iishe halafu tuendelee na upimaji wa kawaida

ambao hautakuwa na zoezi la urasilimishaji ambao majengo yale yamekaa kiholela na upimaji wake unakuwa kidogo ni mgumu ahsante.

**SPIKA:** Nilikuoona Mheshimiwa Halima Mdee uliza swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika nashukuru, changamoto ambayo inakumba Sikonge ya ujenzi holela inakumba pia jiji la Dar es Salaam sasa tofauti na Sikonge Dar es Salaam tayari tuna *Dar es Salaam City Master Plan* ya 2012 mpaka 2032 ambayo tumeshaipitisha katika ngazi zote inasubiri tu utekelezaji. S nataka waziri uniambaie ni lini Serikali itaanza kutekeleza mkakati wa *Dar es Salaam City Master Plan* ili mji wetu upangike vizuri na uonekane na changamoto zote za mji kutokupangwa?

**SPIKA:** Jibu la swali hili Mheshimiwa Naibu Waziri Ardhi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Halima Mdee Mbunge wa viti maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Dar es salaam tayari inayo *master plan* na ilishapitia katika nganzi zote lakini changamoto iliyopo pale katika utekelezaji wake bado katika halmashauri zinazohusika katika kufanya kazi ile kwa sababu ule utekelezaji unakwenda awamu kwa awamu kutegemeana na utaratibu wa mpangilio wa majenzi waliyoyaweka.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa sasa utekelezaji unaoendelea hawaruhusu pia hata katika ujenzi unaoendelea kuweza kujenga nyumba pengine katika maeneo ambayo *master plan* inazungumzia habari ya kwamba pana magorofa kadhaa, ukiomba kujenga nyumba ya kawaida unazuiliwa. Kama ni eneo la viwanda ukiomba kujenga nyumba ya kawaida unazuiliwa. Kwa hiyo,

utekelezaji umeanza japokuwa *space* yake ni ndogo kutegemea jinsi mtu mji wenyewe wa Dar es Salaam ulivyokuwa umejengeka katika taratibu ambazo siki mipango miji katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lazima twende nao taratibu namna ya kuweza *adapt* kile ambacho tayari kimepangwa na wenye halmashauri zao ili kuweza kuhakikisha ile *master plan* inatekelezwa. Kwa hiyo, sisi kama wizara tutaendelea kushirikiana na TAMISEMI ili kuweza kuona ni jinsi gani ile *master plan* inatekelezwa bila kuleta athari kwa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma nilikuona ulisimama.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika,nakushuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza, Halmashauri ya Geita Vijijini yenye makao makuu yake Nzela tumepima viwanja vikakamilika mwezi wa 12 mwaka jana na mwezi wa kwanza tulileta barua ya maombi kwa ajili ya kupitisha ile kamati ya ugawaji wa viwanja toka mwezi wa kwanza mpaka leo hatujawahi kupata majibu kutoka Ofisi ya Katibu Mkuu ambaye ndio mwenye idhini ya kuidhinisha hiyo kamati.

Je nini kauli ya Serikali kuhusiana na barua hiyo ya kuidhinisha hiyo kamati ilituendelee kuuza viwanja ambavyo viko tayari?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo sijui kama atakuwa nayo lakini ngoja ajitahidi Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nilichukuwe swali la Mheshimiwa Musukuma kama alivyosema kama kweli wameshaleta ofisini nikitoka hapa mchana nakwenda kuangalia kama yapo na tuweze kujua kwa nini mpaka leo haijaidhinishwa. Kwa sababu taratibu tunasema kamati zile zikishaletwa kazi ya waziri ni kuweza kuridhia ili zikaanze kufanya kazi. Sasa haiwezekana iwe imekuja kwa muda wote

huo halafu majibu hajapa naomba nilichukuwe ili mchana niweze kuangalia nitampa majibu yake.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Musukuma kama barua itakuwa barua haijafika waambie tu wakutumie na halafu na wewe unampa waziri wakati wowote ule. Swali la mwisho kwa siku ya leo Mheshimiwa Dkt. Charles Steven Kimei Mbunge wa Vunjo.

Na. 304

**Kuzisamehe Kodi za Miaka ya Nyuma Taasisi za Dini**

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI** aliuliza: -

Je, Serikali haioni umuhimu wa kusamehe kodi za miaka ya nyuma taasisi za dini 7 zilizokuwa zikiendeshwa kwa utaratibu usiolenga kupata faida na kuziwekea utaratibu taasisi hizo kuanza kulipa tangu walipojulishwa kutakiwa kulipa kodi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, tafadhali.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria za kodi, taasisi za dini ambazo zinajiendesha kutokana na sadaka kutoka kwa waumini wao ama misaada inayotolewa na taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi, hazikatwi na hazitakiwi kulipa kodi ya mapato, isipokuwa taasisi zenye sifa kama hizo husajiliwa na kupewa Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi *(TIN)* kwa madhumuni ya kuziwezesha kushughulikia masuala mbalimbali yanayohusu Mamlaka ya Mapato kama vile kuwasilisha kodi zinazokatwa kutoka kwa watumishi wa taasisi hizo na usajili wa mali mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, aidha, taasisi za dini zinazofanya shughuli za kiuchumi kwa lengo la kujipatia faida kutokana na shughuli hizo zinatakiwa kusajiliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kama wafanyabiashara wengine na kulipa kodi ya mapato kulingana na faida inayopatikana.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikipokea maombi ya kusamehe kodi za miaka ya nyuma kutoka taasisi mbalimbali ikiwa ni pamoja na taasisi za dini. Serikali inaendelea kutathmini maombi hayo ili kuona hatua zinazoweza kuchukuliwa bila kuathiri matakwa ya sheria zilizopo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei, nimekuona umesimama.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri na nampongeza Waziri kwa kutoa majibu haya ambayo yanatoa faraja sana kwa hawa wanaoendesha shughuli hizo. Hata hivyo, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, je, Serikali itakuwa tayari kurejesha kodi iliyokusanywa kutoka kwenye taasisi hizo kwa shinikizo na hatimaye kuzidhoofisha sana?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Serikali iko tayari kuchukua hatua za kinidhamu kwa hawa maafisa wa *TRA* wanaokiuka sheria? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, tafadhali.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, Serikali ina utaratibu wa kurejesha fedha ambazo zilichukuliwa na kwa mujibu wa sheria zinatakiwa kurejeshwa kwa utaratibu ulio wa kawaida wa kufanya *refund* na *refunds* hizo huwa zinafanyika kwa mujibu wa sheria. Kwa maeneo ambako

kuna makosa ya ukiukwaji wa kisheria, taratibu za kisheria huwa zinafuatwa na hatua stahiki za kinidhamu kuchukuliwa kwa wale wanaokiuka sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama kuna maeneo ambako maafisa wetu wamekiuka sheria, taratibu za kisheria zitafuatwa na hatua za kisheria kuweza kuchukuliwa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa, mtaona muda wetu wa saa moja umeisha na *almost* tuko palepale, hii inatusaidia kwenda vizuri ili wachangiaji wapate nafasi ya kuchangia kama kawaida.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha, haukuwa umefika wakati tunaanza kipindi cha maswali, kulikuwa na swali la kwanza la Mheshimiwa Mnzava kuhusu Hazina kuchukua fedha za maendeleo zilizopelekwa kwenye halmashauri mbalimbali akitolea mfano Hospitali ya Msalala.

Sasa hili tulilizungumzia na tunaendelea kulikumbushia kama Wabunge, kwamba utaratibu huu siyo mzuri kwa sababu wanaoathirika ni wananchi; wananchi wamepelekewa hela za hospitali halafu tarehe 15 au tarehe fulani Juni zinachukuliwa tena, sasa ile hospitali itajengwaje? Haiwezekani!

Mwaka huu bajeti ni tarehe 10 Juni, leo tarehe 25, mtakapozichukua kabla ya tarehe 10 Juni, maana yake hata siku kumi zijazo ni nyingi lakini unazichukua kwa ajili gani? Kwa nini unazichukua wakati ni hela za mradi? Anayeathirika ni mwananchi, sijui Mkurugenzi hakuandika barua, sijui nani hakufanya nini. Kwa nini taratibu za kiutawala ziwaathiri wananchi? Haina sababu. *(Makofi)*

Pia kuna ile huwa wanasema halmashauri haitapewa fedha za miradi kwa sababu imepata sijui hati chafu au yenye mashaka, utaratibu ule vilevile siyo mzuri. Hatutazami anayeathirika ni nani, inakuwa kama wale watendaji wanakomoana wao kwa wao wakati anayeathirika ni mwananchi. *(Makofi)*

Kwa mfano mwaka huu kuna hati zenye mashaka kwa halmashauri zote za Mkoa wa Dodoma ukiacha Jiji; zote za Singida ukiacha nadhani Manispaa; zote za Tabora ukiacha Manispaa. Kwa hiyo, sisi tusipate fedha za maendeleo eti kwa sababu Mhasibu sijui hakuonesha vocha, sijui hakufanyaje. *(Makofi)*

Masharti ya namna hii ni vizuri Serikali ikayaangalia. Kama kuna utendaji mbovu ndani ya watendaji wachukue hatua zinazotakiwa lakini wananchi wasinyimwe fedha za maendeleo kwa sababu za kimfumo na kiutaratibu. *(Makofi)*

Wakati mwingine hawa wanaliopata hati yenye mashaka wanapofika *PAC* au *LAAC* unawakuta wako *clean,* wako safi tu, hoja zao zote zimekuwa *checked out* lakini kule alishahukumiwa kwamba alipata hati yenye mashaka na hawapati fedha za maendeleo. Kwa hiyo, tunashauri hilo nalo Serikali ilitazame.

Wizara ya Fedha waangalie kwamba haya ni masuala ya maendeleo ya wananchi. Siyo tu chukua, leta, tena wanazichukua kwenye mfumo yaani hakuna mwenye taarifa, mnashtukia tu sifuri kwenye akaunti. Kwa hiyo, hili mliangalie sana, litatugombanisha na Wabunge wetu na wananchi wetu.

Upande wa matangazo wageni walioko Jukwaa la Spika, ninao wageni wanne kutoka Kongwa; Ndugu Irene Kimwenye; karibu sana Irene. Amefuatana na Neema Fungo, Zamoyoni Mololo na Omary Hans; karibuni sana. Hawa ni vijana ambao wanajishughulisha na masuala ya maendeleo kule Kongwa, wako *based* zaidi Kibaigwa lakini ni mfano wa kuigwa, *story* yake nitawapa siku nyingine, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 26 wa Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, Waziri wa Kilimo, ambao ni marafiki zake na wafanyabiashara 22 kutoka Rombo, Mkoa wa Kilimanjaro, wakiongozwa na Evod Shayo. Wale wa Rombo; karibuni sana ndugu zetu kutoka Rombo. Mbunge

wenu, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, yupo, anafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Kulikuwa na hoja miaka ya nyuma kwamba Rombo wanaume wote walikuwa wameishia kilabuni kunywa gongo, sasa sijui wamesharudi nyumbani au bado wako huko. Basi mtatupelekea salamu huko Rombo, karibuni sana ndugu zangu, karibuni Bungeni. Ilikuwa ni hoja nzito sana wakati fulani, akina mama walitaka kuandamana. *(Kicheko/Makofi))*

Pia wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Profesa Mkenda ambao ni wadau wa kilimo, Ndugu Edith Lazaro na Ndugu Fortunata Chuwa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine wawili wa Mheshimiwa Profesa Mkenda ambao ni Mtendaji Mkuu wa *ESRF* na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya *PASS Trust,* Dkt. Tausi Mbaga na Mtendaji Mkuu wa *PASS Trust,* Ndugu Anna Shanaringingwa. Karibuni sana, wako pale kwenye *Gallery* ya Spika, karibuni sana, tunajua *PASS* mnafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Wageni 33 wa Mheshimiwa Hussein Bashe, Naibu Waziri wa Kilimo ambao ni Wenyeviti 10 wa Halmashauri za Wilaya Mkoani Tabora wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Uyui, Mheshimiwa Said Ntahondi. Karibuni sana Wenyeviti wa Halmashauri. Mmesikia tunavyotetea hela zenu zisipokwe. Karibuni sana Wanyamwezi ninyi. *(Makofi)*

Wako Wajumbe 14 wa Baraza Kuu la Umoja wa Vijana CCM Taifa wakiongozwa na Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana Mkoa wa Dodoma, Ndugu Billy Chidabwa. Karibuni sana vijana. Vijana ndiyo jeshi lenyewe hilo; karibuni sana vijana. *(Makofi)*

Wageni wengine tisa wa Mheshimiwa Bashe ambao ni wafanyabiashara wa Klabu ya Samunge wanaongozwa na Ndugu Wakili Mambo. Samunge ni maarufu kwa kikombe cha babu sasa sijui na ninyi mnatoka kulekule Loliondo au? Karibuni sana ndugu zangu wa Samunge. Mbunge wa

Ngorongoro lazima ajue Samunge ni maarufu kuliko Wasso ambako ni Makao Makuu ya Wilaya. Kijiji ni maarufu kuliko makao makuu ya Wilaya. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Antipas Mgungusi ambao ni viongozi na jamaa kutoka Malinyi Mkoani Morogoro, wakiongozwa na Ndugu Moses Chogo. Wale wa Malinyi karibuni sana, tunatumaini mmetuletea mpunga. *(Makofi)*

Wageni 13 wa Mheshimiwa Ezra Chiwelesa ambao ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi na jamaa kutoka Malinyi, Mkoani Morogoro wakiongozwa na Ndugu Japhet Masumbuko. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni tisa wa Mheshimiwa Noah Lemburis ambao ni Madiwani kutoka Jimboni Arumeru Magharibi Mkoani Arusha, wakiongozwa na Diwani wa Arusha Mjini, Mheshimiwa Ezra Kornelio. Karibuni sana wale wa kutoka Arumeru Magharibi, karibuni Bungeni. Ni jambo jema mnapotutembelea Bungeni na hasa Waheshimiwa Madiwani. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Michael Kembaki ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)* kutoka Jimboni kwake Tarime Mjini, Mkoa wa Mara, wakiongozwa na Ndugu Monica Dungu. Karibuni sana, natumaini hamjaja na mapanga. Mbunge wenu, Mheshimiwa Kembaki yuko hapa anapiga kazi vizuri kabisa. *(Makofi/Kicheko)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa George Mwenisongole ambao ni wafanyabiashara wa nguo za kiume (suti), kutoka Jijini Dodoma, Ndugu Levina Mwakang'ata na Ndugu Neema Massawe. Wapo kule, mnawaona akina dada hawa? Hebu wapigieni makofi jamani. *(Makofi)*

Makofi haya siyo kwa sababu hizo mnazofikiria, makofi haya ni kwa sababu hawa ni wafanyabiashara wa suti za kiume. Kwa hiyo, wanajitahidi sana. *(Makofi)*

Wageni 30 wa Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Janejelly Ntate, Mheshimiwa Freddy Mwakibete na Mheshimiwa Irene Ndyamkama ambao ni watumishi wa Mungu kutoka Mbeya na Dodoma, wakiongozwa na Mchungaji Elikana Gonda. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wako wageni wa Mheshimiwa Oliver Semuguruka ambao ni marafiki zake kutoka Mkoani Shinyanga, Ndugu Martha Njashi, Ndugu Mary Magessa na Ndugu Rachel Edward. Karibuni sana. Siku hizi hata Wasukuma wanapendeza pia, kweli nchi imeendelea hii. *(Makofi/ Kicheko)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambao ni viongozi wa *Ruaha Sports Academy* ya Mjini Iringa ambao ni Ndugu Paul Ngalawa na Ndugu Lameck Mnyalape. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni wageni 61 ambao ni walimu na wanafunzi kutoka Shule ya Feza ya Jijini Dodoma ambao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyoendeshwa wakiongozwa na Ndugu Maulid Omary. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hawa ni Feza ya hapahapa Dodoma, maana watu mmezoea Feza za Dar es Salaam. Kwa hiyo, hapa Dodoma Feza ipo ya wasichana na wavulana. Tutumie fursa na *facility* hiyo kwa ajili ya elimu ya watoto wetu. Karibuni sana watoto wetu, tunawapenda sana, mnaweza mkakaa. Ila nauli ya kwenda Feza inabidi ujipange kidogo, siyo kama nauli ya kwenda Kongwa, hapana. *(Kicheko/Makofi)*

Tunao wageni wawili kutoka Jijini Arusha ambao wamekuja kujifunza masuala ya Bunge ni Ndugu Zakaria Masawe na Ndugu Rosemary Zakaria. Ahsante, wale pale. *(Makofi)*

Wageni wanne kutoka Jijini Dar es Salaam ambao ni madaktari bingwa wakiongozwa na Daktari Bingwa wa Mifupa na Magonjwa ya Ajali, Dkt. Kennedy Nchimbi. Madaktari hawa wamekuja kujifunza namna Bunge linavyofanya kazi. Ahsanteni sana madaktari, karibuni sana. *(Makofi)*

Tulikuwa tumesitisha matangazo ya ibada, kwamba Waheshimiwa Wabunge muwe mnaelezana wenyewe kupitia mitandao yenu, lakini leo kuna ibada maalum kwa hiyo hii inabidi niitangaze. Mheshimiwa Anna Lupembe, Mwenyekiti wa *Chapel* ya Bunge, anawataarifu wale wageni mliopo na Wabunge ambao mnasali kule kwamba leo kutakuwa na ibada, lakini mhubiri wa leo ni maalum kabisa. Mhubiri wa leo ni Mtumishi wa Mungu, Mheshimiwa Livingstone Lusinde, yeye ndiye atakayehubiri katika ibada ya leo. Niwahakikishie wale msiofahamu kwamba Mheshimiwa Lusinde ni mhubiri, anamzidi Mheshimiwa Askofu Gwajima *by far. (Makofi/Kicheko)*

Katika utumishi wake kabla hajawa Mbunge aliwahi kuwa Katibu Msaidizi wa Chama cha Mapinduzi Wilayani Kongwa, alikaa kule kama miaka mitatu. Siku ambayo Lusinde alikuwa anakwenda kuhubiri kanisani palikuwa hakuna nafasi ya kiti ambayo iko wazi. Ni kweli, sitanii, ni mhubiri mzuri sana pamoja na machachari yake yote aliyonayo. Kwa hiyo, mfike huko muweze kuona neno la Mungu, leo hayuko anafanya maandalizi. *(Kicheko)*

Basi baada ya hayo, nadhani tuendelee sasa, Katibu.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba kupata mwongozo wako kwenye swali namba 294 ambalo wakati wa majibu, hayakutoa mwafaka

mzuri pamoja na kwamba umejaribu kuliona kwa kuwa na wewe ni Mbunge na sisi ni Wabunge tunaotoka vijijini. Nilikuwa natoa mfano kwenye Jimbo la Geita Vijijini ambalo tulileteWa pesa ya kujenga hospitali ya wilaya mwaka 2019, lakini kutokana na umbali na mazingira yenyewe ya ujenzi zikafumaniwa mule shilingi milioni 298, mpaka leo hazijarudi, tumefuatilia, imeshindikana.

Mheshimiwa Spika, lakini mwaka huu pia tumepata pesa ya kujenga makao makuu ya halmashauri, shilingi bilioni moja, ambayo kwa mujibu wa taratibu zenyewe za TAMISEMI tunatakiwa tuajiri taasisi za Serikali, SUMA-JKT. Taratibu zimekamilika mwezi Februari na kwa upande wetu sisi kama Geita upatikanaji tu wa *material* kama kokoto lazima yatoke Mwanza na *term* hii inaonekana bado tunakwenda kukamatiwa pesa nyingine na hatuna ujanja jinsi ya kuzitumia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo mazuri uliyoyatoa, labda ungewapa *timeframe* kwamba wakakae waliangalie suala hili na lini Serikali ilete majibu ili watendaji wetu kule halmashauri waweze kufanya kazi kwa ufanisi kwa sababu wana presha, tunaweza kuharibu baadhi ya kazi kwa sababu ya kuogopa kukamatiwa pesa.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako.

**SPIKA:** Tulishalitolea maelekezo Mheshimiwa Musukuma, haina haja tena ya kupandanisha maelekezo. Hoja yetu ni hiyohiyo, angesimama kila Mbunge hapa aeleze kwake matatizo yako hivyohivyo, kwamba Serikali bahati nzuri kwa kweli tunaipongeza sana inapeleka fedha kwenye maeneo yetu, kabisa. Kama kuna wakati ambapo Serikali imekuwa ikipeleka fedha, ninyi fuatilieni mtaona jinsi ambavyo fedha zinakwenda vizuri na kwa wakati; hilo tunawapongeza. *(Makofi)*

Tatizo letu inapofika mahali pa kuzichukua tena fedha zile za maendeleo, mradi unaendelea halafu zinaondoka. Nafikiri tumeshalieleza kwamba wenzetu wa Wizara ya Fedha walitazame jambo hili, si jambo zuri hata kidogo. *(Makofi)*

Hii habari ya sijui aandike barua au asiandike, hiyo sisi haituhusu, hiyo wafanye wao ndani. Hata kama kuna umuhimu wa kuandika barua lakini zisirudishwe kwa sababu hiyo. Kama wanavyosema, hospitali ilikuwa ijengwe mpaka leo ni gofu wakati hela zilienda mwaka ule, halafu zikanyang'anywa zikarudi. *(Makofi)*

Inawezekana hata Mkurugenzi mwenyewe aliandika hiyo barua kwa sababu tu ya ukiritimba wa Serikalini humu masijala, wapi ikawa hivi ikawa vile, bado si sababu ya kuchukua zile fedha na kuzirudisha wakati ni maendeleo ya wananchi. Nakushukuru sana kwa hilo.

Katibu, tuendelee.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Mjadiliano yanaendelea, yaani wachangiaji ni wengi sijui tufanyeje ili wote hawa waweze kuchangia. Tuchangie kwa dakika tano ngapi?

**WABUNGE FULANI:** Tano.

**SPIKA:** Nashauri tujaribu dakika sita kwa kila mmoja. Jitahidi tu uende moja kwa moja kwa sababu kwa kweli nina orodha ndefu sana ya wachangiaji.

Tuanze na Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru sana kwa hotuba nzuri iliyosheheni mikakati mizuri ya kuboresha na kuinua sekta ya kilimo. Naamini wakipata fedha hizi ambazo zinaombwa basi wataweza kutubadilishia sura ya kilimo na pengine tutaona tija ikiongezeka kwa kasi katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa mtizamo wa kinadharia kwamba, duniani kote tija kwenye kilimo inaongezwa kwenye nchi zote tija inaongezeka kuliko idadi ya watu, watu wanaongezeka kwa asilimia mbili au chini ya asilimia mbili wakati tija kwenye kilimo, kwenye mataifa takribani yote inaongezeka kwa asilimia siyo chini ya saba.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naamini kwamba kutokana na hilo ni kwamba tunachangamoto kubwa ya kuhakikisha kwamba bei za wakulima zitapanda, haziwezi kupanda ikiwa kwamba *supply* inaongezeka kuliko *demand.* Na pili hili linajitokeza hapa kwetu pia kwamba mwaka ambapo tumepata neema ya mvua zao likawa kubwa, mahindi walikuwa wanasema bei za mahindi zinashuka kwa zaidi ya nusu inashuka *by more than fifty percent* na nyingine hata *thirty percent* ya mwaka ule ambapo kumekuwa na changamoto za uzalishaji inashuka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, na kwamba mkulima anajaribu sana anatumia gharama nyingi lakini inapokuja kuuza kwa sababu ni *cobweb theory* iko hapo inaitwa *cobweb theory* inakuwa kama mkulima hawezi kuwa tajiri. Kwa hiyo, njia pekee ya kuweza kuwa wakulima wenye kupata utajiri ni lazima tujitofautishe na wengine duniani tujue kwamba ni zao lipi ambalo likizalishwa lina soko. Kwa mfano, tukiweza kuwahamasisha watu kutumia *organic crops* tukaweza kuotesha bila kutumia nanii sana unakuta kwamba bahati nzuri ndiyo unapata bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, unatofautisha zao lako na la wengine duniani iwe Kahawa iwe chochote kile lakini *organic* ndiyo kinatafutwa, lakini pia kuna mazao kama maparachichi/*avocado* hizi ambazo pia na zenyewe zinaweza kupata *demand* kubwa ni vitu vya kuhamasisha

tusing'ang'anie vilevile vya zamani, tusing'ang'anie tu mahindi tung'ang'anie vitu ambavyo tunaweza tukauza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashangaa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri hajazungumzia masuala mazima ya *horticulture*, mboga mboga, matunda na vituo kama hivyo ambayo kweli unaweza ukaotesha mara tatu, mara nne hasa ukiwa na umwagiliaji ukaotesha *throughout the year* na ukawa tajiri. Lakini nataka kusema kwamba hilo ni jambo ambalo lazima walivalie njuga kwa sababu linahitaji mkakati ambao ni endelevu ili tuweze kulitekeleza hili.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine watu wameonyesha changamoto sana kwenye ushirika lakini nataka niseme kwamba, nadharia ya ushirika inabakia palepale ni nadharia nzuri hatuwezi kuwasaidia wakulima bila kuwa na ushirika. Tatizo la ushirika ni nini? utawala bora na hiyo lazima sheria hii ya ushirika ibadilishwe ili kuwe na udhibiti zaidi kwa wale wanaochaguliwa kuongoza taasisi hizi, waweze kutoa mrejesho kwa kuwa na *financial statements* zinazotoka na zinaenda kwa wanachama wake na wanazijadili na wale viongozi wanaoshindwa wanatolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafikiri hilo ni jambo la msingi na matatizo yote bila Serikali kujikita na Mrajisi ile Ofisi ya Mrajisi kuwa na uwezo hatutaweza kuleta nidhamu kwenye ushirika na kila wakati tutasema kwamba ushirika ni wezi na nini lakini wataendelea kuiba kama hawana udhibiti wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna *issue* ya skimu za umwagiliaji, kule kwetu kuna skimu ya Kahe hasa ile ya Mawala kule kunachangamoto sana na naomba kwamba kusema kweli tumeorodheshewa nyingi kwenye kwenye kiambatisho tuliyopewa na Mheshimiwa Waziri, lakini naamini kwamba kuna ambazo ni kubwa na zinahitaji marekebisho makubwa haraka sana na hasa hii ya kwetu za Kahe kule ndiyo

tunazalisha, Kilimanjaro hatuna Mpunga isipokuwa sehemu hizi za Kahe.

Mheshimiwa Spika, naomba pia tuangalie mambo mengine kwa mfano kuwezesha wakulima kupitia *constituency* au *ward mechanization centers* tusiseme kwamba tunawasaidia wakulima kwa kuwapa mmoja mmoja lazima tuwe na *center* moja ambayo itachukua na vifaa vile mtu anaweza akakodisha kwa bei nafuu au akakodishiwa bila kuchajiwa mpaka akaja akakatwa wakati anapouza mazao yake.

Mheshimiwa Spika, lakini ni vigumu mkulima kununua trekta na mwisho waziri amezungumzia hili la kuongeza mitaji kwa wakulima. Lakini nafikiri badala ya kuwapa fedha tuwape *lease arrangement* ambapo yaani wanapewa mashine halafu wanalipa polepole wanapoendelea kuuza vifaa vyao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kufirikia hilo la kwamba *financing* ni kitu cha msingi na naona amesema anaunda kamati ambayo itamsaidia kufirikia zaidi namna gani wakulima wapate mikopo ya riba nafuu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mwenyekiti wa Kamati Dkt. Christine Ishengoma tuanzishie mjadala wa leo.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kunipatia nafasi na nianze kwa kuunga mkono hoja na pili naunga yote yaliyoongelewa kwenye taarifa ya kamati.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kuwa ili tufanikiwe katika kilimo chetu kwa kuzalisha kwa tija lazima tuangalie kweli masoko kwa sababu tukiangalia masoko mambo yote yatajituma na wakulima watajituma wenyewe

kwa wenyewe. Kwa mfano, tukiangalia kuna kitengo cha masoko katika wizara, nilikuwa nakuomba kuwa Mheshimiwa Waziri akiangalie hicho kitengo cha masoko kifanye kazi kisikae tu kitafute masoko kusudi wakulima waweze kupata masoko ya mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kuna mazao ya miwa, Mheshimiwa Waziri alitembelea viwanda vyote vya miwa anajua matatizo yote ya viwanda vya miwa, anajua matatizo yote ya skimu zote za miwa, nilikuwa nashauri kuwa Mheshimiwa Waziri tulikuwa wote kwenye baadhi ya viwanda naomba kuwa matatizo yote yaweze kutatulika. Leo asubuhi nimeongea na wakulima wa miwa Kilombero, Iyovu bado matatizo yapo palepale, kwa upande wa masoko naamini kuwa wale wakulima miwa matatizo yote yakitatuliwa wakulima wa miwa hawatakuwa na tatizo la masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na hapa Tanzania tutaweza kuzalisha sukari ya kutosha kuweza kuwa hatutakuwa na *deficit* yoyote kwenye sukari. Kwa mfano kule Iyovu wanatupa miwa ambayo haiwezi kuzalisha kwa sababu kiwanda ni kidogo, lakini kulikuwa na tatizo la kupanua kiwanda, hilo tatizo likiisha wataweza kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tatizo wanachoma miwa ya wakulima na hiyo miwa hainunuliwi inakaa tu, ukienda Dakawa kiwanda bado hakijaisha, ukienda kule Mtibwa bado wanamatatizo yao kwa hiyo matatizo yakiisha hiyo ni mfano mmoja wa masoko. Kwa mfano kama masoko yapo chukulia kuwa uzalishaji wa wakuku wa singida unaona kuwa wanauzwa tu kwa sababu masoko yapo ili masoko yaendane pamoja na miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikisema miundombinu naelezea barabara za mashambani, nikisema miundombinu naelezea viwanja vya ndege, kwa mfano wakulima wa parachichi, wakulima wa mazao ya bustani najua Mheshimiwa Jacqueline yupo pale wakati mwingine wanapata matatizo kwa sababu ya usafirishaji kwenda nje lakini soko lipo. Kwa

hiyo Mheshimiwa Waziri tuangalie mazao ya bustani kwa sababu yanazalisha kwa mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naongea haraka haraka nakwenda kwenye pembejeo, najua wewe ulisemea pembejeo hasa kwenye mbegu, mbegu za alizeti kama kamati pamoja na wizara tuliwaambia kuwa lazima tusimamie uzalishaji wa mbegu za alizeti na kweli tutasimamia kusudi hizo mbegu za alizeti ziweze kuzalishwa kwa wingi na hasa kilimo cha umwagiliaji kama mlivyoona kuwa hela nyingi zitakwenda kwenye kilimo cha mbegu na hasa kwenye umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia upande wa mbolea pamoja na viwatilifu lazima na vyenyewe viangaliwe kusudi tuzalishe kweli kilimo chenye tija lazima tuangalie masoko, tuangalie pembejeo pamoja na kilimo cha umwagiliaji. Ukiangalia sasa hivi tuna tatizo la mvua kama hatutajikita kwenye kilimo cha umwagiliaji tutakaa tunasema tunalima, lakini tunalima vitu vyetu vinakauka. Uvunaji pamoja na mabwawa pamoja na skimu zetu lazima zitengenezwe tuweze kupata kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni tafiti, tafiti hapa nasema tafiti wa udongo lazima udogo ufanyiwe utafiti huwezi kuweka mbolea tu kama utafiti kwenye udogo haujafika ili tuzalishe vizuri lazima tutoe hela za tafiti, lazima tufanye tafiti kwenye sehemu mbalimbali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, Mwisho Afisa Ugani pamoja na bajeti lazima itolewe na mfumo wa ushirika lazima uangaliwe. Ahsante nakushuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana mwenyekiti. Mheshimiwa Edward Olelekaita Mbunge wa Kiteto atafuatiwa na Cecil Mwambe.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi na kwanza kabisa nimpongeze *professor* Waziri wa Kilimo, Naibu Waziri na timu yake na nawapongeza sana kwa sababu kwenye hotuba hii walau Kiteto imetajwa mara mbili tu, ukurasa wa 30 na ukurasa wa 127, lakini nawapongeza tena zaidi kwa sababu walau ninyi mmefuatilia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, na tunaka kila wizara tufuatilie Ilani hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukisoma Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ukurasa wa 42 tulijiwekea malengo ya kutengeneza tani laki 710 za alizeti, lakini kwenye hotuba hii nyinyi mmeweka tani milioni moja *excellent* tunataka tuwe na mwelekeo huu wa Ilani yetu. Lakini vilevile ukurasa wa 42 tulisema tutajenga maghala 14 kwenye mikoa hii ipo hapa *excellent. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tumesema kwenye ukurasa wa 43 tutawapatia vijana 400 kutoka mikoa tisa vifaa ipo kwenye hotuba yenu hapa safi sana. Lakini sasa nataka muongeze hivi vijana 400 mikoa tisa, kila mkoa tunataka mgawanye mlete *mathematics* ni vijana 44, na mkifika kwenye mikoa ile tunataka mtuambie mkoa ina wilaya ngapi na vijana wangapi watoke humo mimi nimeshapiga mahesabu nisipopata vijana sita kutoka Kiteto, Manyara mtakuja kutueleza mmefuata nini sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la umwagiliaji Kiteto ambayo nilikwisha kusema ni *bread basket,* kilimo cha mvua ni asilimia 99.9 kati ya hekta 1385 ambazo tumetenga kwa ajili ya umwagiliaji ni 0.00 *percent* ndio inatumika haiwezekani. Ni lazima tuwe wakweli kabisa tunaposema kilimo, kilimo inachangia pato la Taifa asilimia 29, 28 au 26 *data* zenu zote zinasema hivyo na inawaajiri watanzania asilimia 65 halafu tunapokuja kwenye bajeti tunawatengea bilioni 300, haifiki hata bilioni 300 *honestly* watafanya nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Maputo *declaration* na Malaba *declaration* inasema nchi zime-*commit* kuongeza asilimia 10 kwenye *agriculture,* hii haifiki hata *percent* moja, hata hii

*program* tunayosema tunafuatilia hii *program* ya kuendeleza kilimo ya pili ili-*commit* bilioni 13 kwa ajili ya kilimo *we are not even one percent* kwa hiyo, lazima tuwe *serious* tunapozungumzia *agriculture*. Imeajiriwa watanzania 65 pato la Taifa kubwa namna hiyo halafu tunawekeza sijui kwenye masekta gani huko tuwe *serious* kwa kweli tunapozungumzia *agriculture. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na Ilani yetu imesema vilevile Chama Cha Mapinduzi tunataka kutoa wakulima kwenye jembe la mkono na kwenda kwenye matrekta, yamekuja matrekta hapa ya Urususi hapa wakulima wangu Kiteto wamechukua karibu matrekta 100, halafu mnawapeleka kwa Wizara ya Viwanda *is a confusion* yanatakiwa matrekta haya yawepo kwenye Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kwa sababu nyinyi mpo karibu na wakulima hawa halafu mnawaambia kwamba yale matrekta yale yalikuwa ya bei nafuu ni uongo mtupu, trekta bilioni 45, trekta milioni 55, sasa kuna unafuu gani hapo halafu mabovu kwanza, hebu tuwapatie wakulima matrekta haya wapate kuzalisha. Namshukuru sana waziri kwenye hotuba yako umewashukuru wakulima kwa sababu ni kweli, kilimo nchi hii ingekuwa wakulima wale hawalimi wala tusingekuwa na chakula. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Edward.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika baada ya hayo nashukuru naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Edward tunatamani tungeendelea kukusikiliza unavyochambua, lakini muda haupo upande wetu Mheshimiwa Olelekaita hata mimi nilikopa Urususi inanipasua kichwa, Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa ...

**SPIKA:** Atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia, maalum kabisa ninataka niongee na Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake hasa zaidi waweze kutusaidia sisi wakulima na kipekee kabisa niongee kuhusu wakulima wa korosho.

Mheshimiwa Spika, ukifika Mtwara maeneo yote ambayo utapita wananchi wa kule wanalima korosho, lakini kwa bahati mbaya kabisa ukilinganisha maisha yao halisi na sifa tunazopeana hapa ndani Bungeni kwamba wananchi wa Mtwara na Lindi pengine wa kusini kwa ujumla ni wakulima wa korosho wanaongeza pato kwenye mapato ya nchi yetu hawafanani kabisa na hicho tunachokisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanaonufaika ni wasimamizi au wa Ushirika au wasimamizi wa Bodi ya Korosho au Wasimamizi wa Vyama Vikuu vya wanaosimamia manunuzi, lakini wakulima kama wakulima hawanufaiki. Mheshimiwa Waziri nilimpa taarifa na nilipeleka mchango wangu pia kwenye maandishi na Mheshimiwa Naibu Waziri pia kwamba kuna ubadhirifu mkubwa sana umefanyika ndani ya Bodi ya Korosho, Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Korosho ndiyo maana Wabunge wote hapa wanaotokea maeneo hayo wamelalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba ukafanye ukaguzi pale ndani kuna pesa zaidi ya shilingi bilioni 1.5 zimetumika nje ya utaratibu kabisa na tunamwambia hapa Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anamaliza na ku-*windup* hapa atueleze hatua anazochukua dhidi ya Mkurugenzi huyu kwa haraka kwa sababu vinginevyo sisi tunakwenda nyumbani kufanya mikutano na wananchi wetu na tutakwenda kuwaeleza kwamba Waziri anamlinda na kumtetea Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho kwa sababu labda ana maslahi binafsi na yeye, lakini sisi hatusaidii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtu mwingine ni Meneja wa Chama Kikuu cha Msingi cha Mtwara ambaye ni Meneja wa

*MAMKU* Mheshimiwa Naibu Waziri anamfahamu naye ni mmoja wa watu wanaonufaika sana na zao la korosho bila kuwa na shamba hata nusu eka nyumbani kwake na wenyewe tunaomba kabisa na siku ya uchaguzi mkuu pale wakulima walimkataa, wakataka kabisa na kuandamana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri mwenyewe alihusika kupiga simu akawaambia jambo hili tutahakikisha tunapata suluhisho siku chache zijazo, sasa hivi mwezi mzima umepita hakuna hatua yoyote aliyochukua Mheshimiwa Bashe na yeye tunamuomba kama ana maslahi binafsi na huyu ndugu basi amuondoe Mtwara ampeleke kwao Tabora akasaidie kwenye mazao mengine kwenye Korosho hawezi kufanya kazi. *(Makofl)*

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ni suala la, masuala ya stakabadhi ghalani, Mheshimiwa Mulugo hapa jana aliongea kwa uchungu mkubwa kabisa suala la stakabadhi ghalani akiomba Serikali iondoe mfumo huu. Mheshimiwa Bashe hapa alikuja akaongea mwenyewe ndani ya Bunge hili labda kama alikuwa ameamua kufanya utani na sisi Wabunge kwamba mazao ya maeneo ya Dodoma, Songwe, Katavi wasitumie huu mfumo kwa sababu hawajiandaa kutumia huu mfumo.

Mheshimiwa Spika, lakini sisi kwetu kwenye zao la Korosho mfumo wa stakabadhi ghalani ni sehemu ya ukombozi na uhai, tunachotaka sisi kikubwa mfumo huu uboreshwe na siyo kuondoa kwa sababu umekuwa ukiwasaidia wakulima. Lakini pia, urasimishwe ukipata stakabadhi yako ya ghalani kabla hujalipwa kwenye ghala lako uweze kutumia stakabadhi kwenda nayo hata hospitali na hospitali zikutambue kwa sababu tuna hospitali za Serikali uweze kupata matibabu tuachane na hivyo vitu vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba yako pia uliyotuwasilishia hapa umeongea kuhusu skimu, lakini mimi naweza kukwambia umeleta utani mkubwa kwenye masuala ya skimu umeitaja skimu ya Ndemba halafu inaonyesha

kwamba ina eka moja na hii ni skimu ya Serikali, umeitaja skimu ya Maparagwe yenye eka 450, lakini Kijiji chenyewe cha Maparagwe hakifikii hata eka 30. Mheshimiwa umetaja hapa skimu ya Liputu yenye eka 10 hizi ni skimu za Serikali, umetaja Skimu ya Chingurunguru eka tano ni uongo kwa sababu Chingurunguru hata shida ya maji ya kunywa kule ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waambie watalaam waende hatuna hata maji ya kunywa tuanze sasa kutoa maji mengine ya kumwagilia hicho kitu hakuna. Umetaja skimu ya Ndanda yenye eka 350 eka zinazotumiwa pale hazizidi eka thelathini na wananchi wamekuwa na migogoro kila siku tunataka sasa tujue Serikali kama ilipeleka hapa pesa zimetumika namna gani kwa ajili ya watu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala hapa pia ambalo pia umelitaja na waheshiwa Wabunge wote wamelichangia kuhusiana na suala la pembejeo ambazo zinakwenda kugawiwa sasa na mfumo wa Serikali.

Waheshimiwa Wabunge wameshauri kwamba Serikali itafute pesa na ione namna sasa ya kulipa pembejeo hizi badala yakwenda tena kuwakata wakulima ambao wamekuwa wanakatwa kila wakati na sheria haiwezi kurudi nyuma.

Mheshimiwa Spika, kama mnataka kuanzisha huu utaratibu zile pesa ambazo zilikatwa shilingi bilioni 210 kabla sheria haijabadilishwa ziko wapi? Zilitumika kufanya jambo gani? Kwa nini hizi zisitumike wakati huu na sisi Serikali kuturudishia ili tuendelee kwenda mbele na tuweze kuongeza mavuno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine hapa ni suala la *TARI.* Wananchi wanakatwa shilingi 25 kwa ajili ya Mfuko wa *CBT* lakini wananchi pia wanakatwa shilingi 25 kwa ajili ya kupeleka kwenye vyuo vya utafiti. Tunataka Serikali itueleze shilingi ngapi mpaka sasa zimepelekwa kwenye utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii, nasubiri majibu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Cecil Mwambe. Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya atafuatiwa na Mheshimiwa Getere, halafu tutakwenda kwa wachache.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini naomba nimshukuru Waziri, Profesa Mkenda pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Bashe na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, nina hoja mbili kubwa, hoja ya kwanza ni kuhusu Mfuko wa Umwagiliaji na hoja ya pili ni kuhusu kilimo cha korosho Manyoni. Kwanza, niishukuru sana Serikali tulianzisha Tume ya Umwagiliaji, kuna Kanuni za Umwagiliaji za 2015, lakini kuna Sheria ya Umwagiliaji na vilevile kuna Mwongozo wa Tozo na Ada za Umwagiliaji, hii ni hatua kubwa sana kwenye sekta ya umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini niseme kwamba hatuwezi kuendeleza kilimo cha Tanzania iwapo Profesa hutaweka mkazo na uwekezaji kwenye umwagiliaji. Hiyo itabaki kuwa ndoto, naomba tuige nchi za wenzetu *Egypt*, Somalia, Sudan na nchi zingine ambazo zimeendelea.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni nini? Katika Jimbo langu la Manyoni Mashariki nina skimu zaidi ya 8, nina skimu za Udimaa, Ngait, Mawen, Chikuyu, Saranda, Msemembo, Kintinku na Mtiwe. Hata hivyo, nikipitia bajeti hii, sijaona sehemu ambako Profesa unaenda kuwekeza kuhakikisha kwamba ule uharibifu ambao ulisababishwa na mvua kubwa tunaenda kuwakomboa wakulima.

Mheshimiwa Spika, nina masikitiko makubwa kwa sababu kama hatutawekeza kwenye umwagiliaji...

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya sekunde moja tu, Waheshimiwa Wabunge sasa tumpe nafasi Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mbunge yeyote asiende pale ili apate kusikiliza

masuala ya kilimo kwa sababu ni muhimu sana. Anayemhitaji Waziri Mkuu tuna ofisi hapa *Administration* kuanzia saa 7.00 mchana mpaka saa 11.00 jioni mnaweza mkaenda kumuona. Sasa hivi muacheni ili asikilize hoja za Waheshimiwa Wabunge kuhusu matatizo halisi ya wananchi maana yeye ndiye Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Mheshimiwa Dkt. Chaya, endelea. *(Makofi)*

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni nini? Mwaka jana katika hizi skimu nyingi za umwagiliaji ambazo ziko katika Jimbo la Manyoni Mashariki zilipata adha kubwa sana ya mvua. Niliwasiliana sana na wenzetu wa Tume ya Umwagiliaji nawashukuru, waliahidi kuja kuturekebishia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfuko wa Umwagiliaji, nina hoja kadhaa ambazo napenda kulishauri Bunge. Kwanza huu mfuko ambao tumeuanzisha na umeanza kufanya kazi mwaka jana unategemea ada na tozo za wanachama. Sasa tunategemea huu mfuko uje ujenge skimu kubwa hapa Tanzania lakini unategemea skimu ambazo hazijaendelezwa. Profesa naomba uliangalie hili, tunahitaji kwanza kuwekeza kwenye skimu hizi, kuzirekebisha ili huo mfuko wako utune. Bila kuwekeza kwenye hizi skimu Profesa hizi skimu zitabakia kuwa ndoto na mfuko utabakia kuwa ndoto na umwagiliaji Tanzania utabakia kuwa ndoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine hivi vyama vya wamwagiliaji vimeanzishwa lakini havijapewa mafunzo na utendaji wake wa kazi upo chini sana. Napenda kujua Profesa umejipangaje kwenye bajeti yako kuhakikisha kwamba, kwa mfano kwenye zile skimu zangu 8, umeweka bajeti ya kuja kuviwezesha vile vyama vya umwagiliaji, uwape mafunzo, wajue jinsi ya kusimamia mifuko hiyo, jinsi ya kuchanga na hata jinsi ya kuchukua hizo tozo na kurudisha kwenye mfuko wa Serikali. Kwa hiyo, naona hii ni hoja ya muhimu na ningemshauri Waziri aweze kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la kilimo cha korosho. Mimi naishukuru sana Serikali tumeanzisha kilimo cha

korosho na baadhi ya Wabunge wetu humu wengi mna mashamba ya korosho kule Manyoni. Tunatumia *block farming system* ambapo wakulima wengi wameungana na nimshukuru sana Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni kuhakikisha kwamba kilimo cha korosho kinaenda kuwa na tija.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tumeanza uvunaji wa awamu ya kwanza wa korosho kule Manyoni. Hoja yangu hapa, nitatamani kusikia kutoka kwa Profesa kwenye bajeti hii, amejipangaje sasa kuhakikisha kwamba Manyoni kilimo cha korosho kinakuwa chenye tija? Je, mnawasaidia vipi watu wa Manyoni kwa kuja na mfumo rafiki sasa kwenye masuala ya masoko, maghala na kuwa na mfumo rafiki kuhakikisha kwamba wale wakulima wawe sasa na matumaini ya zao la korosho?

Mheshimiwa Spika, kuna sintofahamu kubwa sana kuhusu suala la korosho. Nimesikia ndugu zangu wa Mtwara na Lindi wakilalamika, hatutaki hayo makosa yatokee Manyoni na ningetamani kuona sasa Waziri anakuja kwenye bajeti yake na bajeti ambayo Manyoni itakuwa ni sehemu ya kipaumbele kwenye suala la korosho na hasa kipindi hiki ambapo tumeshaanza kuvuna ili wananchi na wakulima wetu wapate matumaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la miundombinu. Tutatamani kuona Waziri unakuja na bajeti ambayo kwa Manyoni ambapo Bodi ya Korosho inafanya kazi ni jinsi gani mnaenda kuwasaidia...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Chaya, dakika tano ni ndogo.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunawapongeza sana Manyoni, Waheshimiwa Wabunge ambao hamjawahi kutembelea Manyoni na kuona kilimo cha korosho ni *just two hours* kutoka hapa, siku za *weekends* ni vizuri *mkaji-arrange* mkaenda mkaona. Hii korosho wanayozungumza watu wa Kusini hamna kitu Manyoni kuna korosho, kina Katani hawa wanapiga kelele tu. *(Makofi/Kicheko)*

*Actually,* nawashauri Wabunge wa Kusini ambao hamjatembelea Manyoni *seriously* ni vizuri mkatembelea, mkaona kwa sababu hizo ndiyo zinaitwa *emerging markets* zinazokuja. Ninyi mikorosho yenu ni mizee na iliyochakaa, sasa mkaangalie mikorosho mipya na ya kisasa na kilimo ambacho ni kizuri sana. *(Makofi)*

Pia unaweza pia ukawekeza, ndio maana siku moja tukasema Mheshimiwa Waziri Mkuu yule Mkurugenzi wa Manyoni ikiwezekana abakibaki kidogo, kwa kweli ni katika Wakurugenzi ambao wamefanya kazi nzuri sana. Hata kama anaondolewa basi anatakiwa apatikane mwingine ambaye ana-*inclination* ya mambo ya kilimo haya kuliko akienda mtu mwingine. *(Makofi/Kicheko)*

Tunakushukuru Mheshimiwa Dkt. Chaya, Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara ya Kilimo. Nikupongeze wewe mwenyewe kwa jinsi unavyoendesha Bunge hili toka mimi nimeingia humu hii *term* ya pili, unaendesha Bunge vizuri sana mimi kwa kweli naku-*mind* yaani unafanya kazi vizuri sana. Kuna hospitali inajengwa kule kwangu Unyali ambako ulikuwa unaishi inaitwa Ndugai, ikikamilika nadhani tutakupeleka ufungue sasa hapo ndiyo utaona maisha yanaendaje huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niishukuru Wizara ya Kilimo viongozi wake wako vizuri sana, Waziri, Naibu Waziri, viongozi wote wako vizuri, kinachozungumzwa hapa ni matatizo ya kilimo ya muda mrefu. Wabunge wakiwa wakali hapa Mheshimiwa

Profesa Mkenda na Mheshimiwa Bashe msiseme wanawasema nyie, tunazungumza matukio ya kilimo toka uhuru yanaendaje, tatizo letu liko hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, naomba unipe nafasi kidogo niseme jambo moja. Kwa nini tusiunde kamati hata kama ni ya watu watano *professional* ambao watakuwa wanaangalia hizi Wizara? Waangalie katika bajeti hii 2020/2021 tumesema nini, bajeti ya 2022/2023 waje watuambie hapa tulichokisema wakati uliopita ili watakapokuwa wanazungumza kwenye bajeti mpya tuwe tunaona wametenda nini na wamepatia wapi? Haiwezekani kuzungumza habari ya kilimo cha pamba, korosho, alizeti miaka nenda rudi hakuna kinachotatuliwa. Lazima tujifunze jambo moja tujue ni wapi tumekamilisha jambo limeenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana ulikuwa unasema mambo ya tija, tunapozungumzia tija ni jambo kubwa sana. Tija ya mazao yote kwa mfano tija ya pamba, wenzetu wa Misri, Sudan, India heka moja ya pamba wanazalisha kilo 1,000 mpaka 1,200, Tanzania heka moja ni kilo 250 mpaka 300. Sasa fikiria tija ilivyo, ukizalisha 300 kwa heka moja ukauza kwa Sh.2,000/= ni Sh.600,000/=, ukizalisha 1,000 kwa heka moja ukiuza Sh.1,000/= ni Sh.1,000,000. Kwa hiyo, suala la tija hapa ni muhimu sana katika uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, sasa watu watuambie jamani mliyozungumza msimu uliopita sasa tumetekeleza. Kwa mfano Jimbo langu la Bunda, Tarafa ya Chamriho ndiyo wazalishaji wakubwa wa pamba Mkoa wa Mara, waje waseme pamba tumefikia kiwango hiki lakini sasa hivi kazi ni ile ile. Ukizungumza pamba, alizeti na ufuta tija hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbaya zaidi sasa mkulima anaanza kutayarisha shamba mwenyewe, kulima na kupanda mwenyewe, anatafuta mbegu mwenyewe, analinda usiku wanyama wa pori wakali mwenyewe, ikifika kwenye kuuza Serikali imefika, akitaka kuuza kila mahali

anazuiliwa, mambo ya ajabu haya duniani hapa. Kwa hiyo, nafikiri sasa ifike muda tumsaidie mkulima kwenye kuzalisha apate tija kubwa na sisi twende kuingia.

Mheshimiwa Spika, zao la pamba lilivyo kwa mikoa yote inayouza pamba, mkulima analima na kupanda mwenyewe, akienda kuuza anaenda kwenye ghala anakopwa. Siku ya kwanza anapeleka pamba *AMCOS* amekopwa, *AMCOS* wanachukua pamba wanapeleka kiwandani wamekopwa, kiwanda kinachukua fedha kinapeleka benki mkulima hajapata fedha, ni shida. Watafiti watuambie kwa nini mkulima wa pamba akipeleka pamba ghalani asipewe pesa pale pale, kuna hoja gani? Pamba ya mtu inakopwa kwa sababu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa huwa najiuliza maswali ya kiakili tu, hivi pamba imeenda ghalani, *AMCOS* haina hela, amekopa mkulima, hivi ghala likiungua analipa nani? Pamba imechukuliwa kwenye gari inapelekwa kiwandani sio ya kiwanda ni ya *AMCOS* hivi gari ikiungua atalipa nani? Kwa nini kama watu wana fedha wasiende kununua pamba kwenye maghala ili wakulima wapate fedha zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *AMCOS* hawana hela, hivi kuna haja gani ya kuwa na *AMCOS?* Kama kweli Serikali inataka *AMCOS* iwepo, iwape fedha kama ilivyokuwa zamani, Ushirika zamani walikuwa wanapewa fedha wanaenda kununua pamba. Sasa tuna *AMCOS* haina fedha, ni mawakala tu, wanasubiri mkulima alete pamba waanze kumdhulumu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, kilo moja mara 100, 200 …

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja lakini ndugu zangu rekebisheni yale mambo tunayozungumza humu ndani. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaenda upande wa pili, Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Mtinga Isack.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie kwenye bajeti ya Wizara ya Kilimo. Kabla sijachangia naomba ni-*declare interest* mimi ni muumini wa matokeo, yaani mimi ni mtu ambaye naamini kwamba maneno matupu yanachosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miaka na miaka tangu wazee wetu wako shuleni na pengine wengine wazee wetu baadhi walikuwa hawajazaliwa mpaka leo bado tunazungumza kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa. Nafikiri kauli hii ndio inayosababisha kutufikisha hapa leo. Unaweza kuvunja uti wa mgongo ukaendelea kuishi ila ukikosa *oxygen* utakufa.

Mheshimiwa Spika, nafikiri ipo haja ya kubadilisha kauli ya kilimo kwamba ni uti wa mgongo wa Taifa na tutafute kauli nyingine pengine inayofanana na kwamba kilimo ni *oxygen* ya uchumi wa Taifa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa mmesikiliza hoja yake, hoja kubwa kweli hii. *(Kicheko)*

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kilimo kimesemwa ni uti wa mgongo wa Taifa, ndiyo maana bajeti ya Wizara ya Kilimo tangu mwaka 2016 mpaka 2021 imetekelezwa chini ya asilimia 50. Ukitafuta *average* ya utekelezaji wa bajeti mwaka ambao ilitekelezwa kwa kiwango kikubwa ni asilimia 42 mwaka 2018/2019, *the rest* ukitafuta *average* ni asilimia 19 tu. Kwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo unaweza kuvunja uti wa mgongo ukaendelea kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa ndio maana sasa hivi ukienda Nane Nane Dodoma unakuta kuna pilikapilika za maandalizi ya Nane Nane, kikishafika kilele cha Nane Nane watu wanafunga biashara zao unakuta mapori. Hii ni kwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa, vijana wetu ambao wako Chuo Kikuu cha Kilimo (*SUA),* wanakaa miaka yote darasani wanakwenda *field* miezi saba tu, kujifunza kuotesha mbegu, kuweka mbolea na kuotesha kila kitu mpaka mwisho kwenda kwenye masoko. Kwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo Tanzania tuna eneo linalofaa kwa kilimo hekta milioni 44, lakini hekta milioni 29.4 zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji lakini mpaka sasa tumetumia hekta 561,383. *Target* ya Serikali ni kutumia hekta 1,200,000 ifikapo 2025 kwa sababu kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa, kwa hiyo unaweza kuvunja uti wa mgongo na ukaendelea kuishi.

Mheshimiwa Spika, kilimo chetu kina changamoto kubwa sana bado Tanzania tunalima kama Adamu na Hawa walivyolima Eden. Tunategemea mvua na kudra za Mwenyezi Mungu, katikati ya mabadiliko makubwa ya sayansi na teknolojia, katikati ya mabadiliko makubwa ya tabia nchi bado tunazungumza *agriculture* wakati dunia inazungumza *agritecture*. Dunia inakwenda kwa mabadiliko makubwa ya sayansi na teknolojia, kwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa, tunaendelea kuvunja uti wa mgongo tukitegemea tutafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya uchache wa muda niende kwenye kutoa ushauri tufanye nini. Jambo la kwanza, nashauri kilimo kisizungumzwe kama sekta ya maendeleo wala kisizungumzwe kama mfumo wa maisha *life style* kizungumzwe kama *big money-making business.* Kilimo kwa ujumla duniani ni dhahabu ya kijani, tuzungumze kama *money-making business* siyo desturi kwamba ni jambo la kimaendeleo, ndiyo maana tunafanya haya tunayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, michango ya Waheshimiwa Wabunge inaonesha namna gani tunakwama sehemu. Hatuwezi kutatua tatizo hili kwa kuweka *solution* za pamoja ni lazima tuwe na *solution* za muda mfupi na za muda mrefu. Jambo la kwanza na la msingi, tuna watu ambao wako kwenye *finger tips* zetu, Maafisa Ugani, ni watu wako Waziri, nashauri tu-*militarize* sekta ya kilimo, tuibadilishe sekta ya kilimo iwe *agricultural machinery*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukisoma bajeti ya mwaka jana ya Mheshimiwa Japhet Hasunga wakati yuko Waziri, vitu vilivyobadilika ni kipaumbele kilichokuwa cha tatu kinakuwa cha pili kilichokuwa cha nne kinakuwa cha sita. Mimi ni muumini wa mabadiliko, mimi ni muumini wa matokeo, tunataka matokeo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Bahati mbaya dakika tano ndio hizo. Ningekuwa na dakika za ziada ningekuongezea Mwalimu Nusrat Hanje, tunakushukuru sana kwa mchango wako. Inaonekana vijana wanakuja juu wanachangia vizuri halafu wako watu wanasema eti nimfukuze Mbunge kama huyo. *(Makofi/Kicheko)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Francis Isack Mtinga.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ambayo inabeba asilimia 70 ya uajiri wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Wilaya yangu ya Mkalama ina wakulima wa vitunguuu takribani 250, wanaolima karibia tani kuanzia 24,000 mpaka 94,000. Wakulima hawa wanalima kwa kilimo cha mvua na sio umwagiliaji, hivyo, inapofika wakati wa mavuno vitunguu vinajaa sokoni kwa wakati mmoja na hii inapelekea sasa wanunuzi kuamua wanunue kwa bei gani. Kwa hiyo, unakuta katika kipindi cha mwaka mmoja mkulima mwingine anauza gunia Sh.250,000/= mwingine anauza

Sh.20,000/= kutokana na kwamba vitunguu vimejaa sokoni. Pia hali hii inasababisha wale wanunuzi kuamua kipimo cha kununua, mwingine anajaza gunia anaweka na kilemba juu kwa sababu vitunguu vimejaa sokoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iwaangalie wakulima hawa wa vitunguu kwa kujenga maghala ya kutunzia vitunguu katika Kata yangu ya Mwangeza inayolima vitunguu. Hii itasaidia ili vitunguu vinapovunwa kwa wakati mmoja viwekwe kwenye maghala na viuzwe kwa utaratibu na siyo mtu auze vitunguu shilingi 20,000 kwa sababu vitunguu ni *perishable,* vinaoza haraka na mkulima anakuwa hana ujanja anapangiwa bei anayotaka mnunuzi.

Kwa hivyo, naomba Wizara ikajenge maghala na maghala ya vitunguu yanatakiwa yajengwe kitaalamu kwa sababu vitunguu ni *perishable* sio sawa na mahindi, ipeleke nguvu pale nguvu pale ijenge maghala ili kuwalinda wakulima hawa wa Mwangeza na Mkalama ambao wanalima kwa nguvu zao. Ndiyo maana *tannage* imeshuka kutoka 94,000 mpaka 24,000 kwa sababu hawana uhakika na soko limekuwa kama kamari, mnunuzi ndiye anaamua anunue kitunguu kwa bei gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara katika hotuba yao hawajaongelea kabisa kwa undani suala la kilimo cha mbogamboga na matunda. Katika kata yangu mojawapo ya Gumanga kuna kiwanda kimejengwa cha kusindika mazao ya mbogamboga kwa kutumia wananchi na shirika lisilo la Kiserikali la *Helvetas,* kiwanda hiki kimegharimu karibu milioni 106 hakifanyi kazi kwa sababu malighafi haipo.

Mheshimiwa Spika, niombe Wizara iwaangalie wakulima wa nyanya wa Gumanga kwa kuwawezesha kwa mbegu bora, visima vya umwagiliaji na utaalam ili kiwanda hiki kiweze kufanya kazi na kitasaidia hata mikoa ya jirani wanaolima mboga mboga na soko litapatikana hili ambalo tunahangaika kuimba sasa hivi kwa sababu kiwanda kimekaa tu hakina kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikuombe rafiki yangu Bashe pamoja na Waziri, nenda pale Gumanga ukaangalie kiwanda hiki tuwawezeshe wakulima hawa waweze ku-*supply material* ya nyanya ya kutosha katika kiwanda ambacho wamekijenga wao kwa nguvu zao pamoja na shirika lisilo la Kiserikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile niende kwenye suala la alizeti. Wote tunafahamu shida ya mafuta tuliyonayo na zao la alizeti katika hotuba ya Rais iliyopita lilitajwa kama zao la mkakati. Lakini katika hotuba sijaona huo mkakati jinsi ambavyo umeongelewa vya kutosha. Leo hii wakulima wa Mkalama analima hekari moja anapata gunia tatu. Anaona haina tija kulima kwa sababu tatizo kubwa ni mbegu, mbegu ambayo inaonekana kidogo inafanya vizuri, mbegu ya *hysan* inatoka nje. Kilo mbili ni 70,000, mkulima hawezi kununua mbegu hii.

Mheshimiwa Spika, niiombe Wizara, wakati mnafanya utaratibu wa kutafuta mbegu na utafiti, basi angalau mbegu hii iangizwe kwa *bulk* na ikibidi iondolewe kodi ili wananchi waendelee kutumia mbegu hii *hysun* ili kuweza kupata kipato lakini vile vile kuondoa tatizo kubwa la mafuta katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nikuombe sana Mheshimiwa waziri na Naibu Waziri mliangalie sual ahili la hii mbegu ya Hysan. Hakika mkiitupia jicho itashuka bei na itatupunguzia suala zima la tatizo la mafuta. Wakati huo huo, mkifanya utaratibu wa kutosha wa kutafuta mbegu ya kisasa ya utafiti itakayofanyika katika nchi yetu ili zao hili la alizeti liendelee kuwa zao kongwe na zao ambalo litatuondolea shida ya mafuta katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Singida, alizetu watu wameshaanza kuacha kulima. Mtu angaalia anapata gunia tatu, bora alime karanga apate gunia 12 au bora alime mahindi apate angalau gunia 10 kuliko analima alizeti anapoteza muda anapata gunia tatu. Tatizo ni mbegu na mbolea na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri jambo hili la alizeti hamjaonesha mkakati mnaotaka kuufanya katika kulinyanyua. Hamjaliongelea vizuri katika hotuba yenu nimepitia vya kutosha, hebu mlitazame ili tuweze kuondoa tatizo la mafuta katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa leo niliona niseme hayo. Nashukuru sana kwa nafasi hii. Naunga mkono hoja, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Francis Isack Mtanga kutoka Mkalama. Mheshimiwa Anthony Mavunde, atafuatiwa na Mheshimiwa John Marko Sallu.

**MHE. ANTHONY P. MAVUNDE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Ili kukiboresha kilimo cha zao la zabibu hapa Dodoma ni lazima Wizara sasa iweke nguvu kwenye kituo cha utafiti cha *TARI* Makutupora ili kuboresha huduma za ugani na kuwafanya wakulima waweze kuzalisha kwa tija.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kwa Dodoma wakulima wetu wanatumia gharama kubwa kulima kwenye shamba la hekari moja lakini wanachokipata ni tofauti na gharama waliyoitumia na hivyo kusababisha gharama kuwa kubwa sana. Ekari moja ya mkulima aliyelima vizuri zabibu Dodoma inaweza ikmapa mpaka tani tatu. Huyu ndiye aliyelima vizuri. Lakini ukienda Afrika Kusini, *Western Cape* mkulima anapata tani 12 kwa ekari moja.

Mheshimiwa Spika, niiombe Wizara, pamoja na kwamba tuna kituo pale cha Makutupora, tunaomba mafunzo yaendelee na ikiwezekana maafisa ugani hawa muwapeleke wakajifunze Afrika ya Kusini. Mheshimiwa Waziri, wasindikaji wa zabibu wa Dodoma walikuwa wako tayari kuwalipia maafisa ugani kwenda Afrika Kusini kujifunza. Itakuwa ni jambo la ajabu sana kama *private sector* wenyewe wakiwalipia maafisa ugani wa Serikali na Serikali ipo. Mheshimiwa waziri, nikuombe waende wakajifunze Afrika

ya Kusini ili tuongeze tija ya mkulima wa zabibu wa hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na hii ndiyo inasababisha *St. Anna* ya Afrika Kusini inauzwa shilingi 8,000 hapa Dodoma na Dompo ya Dodoma inauzwa shilingi 12,000 kwa sababu ya gharama za uzalishaji ni kubwa sana niiombe Serikali katika eneo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Hivi sasa Rwanda wame-*take advantage,* hivi sasa wanawakaribisha Wajerumani, muda sio mrefu wataanza kuwa wazalishaji wa *bulk wine* wakubwa hapa *East and Central Africa.* Wanyarwanda walikuwa wanakuja Mpunguzi, Mvumi na Chamwino kununua zabibu sasa hivi hawaji. Wameanza kulima wenyewe. Wakenya walikuwa wanakuja, sasa hivi hawaji, wanalima *Mount* Meru kule.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa Afrika, ukiondoa Afrika Kusini nchi nyingine hapa ya Kiafrika kama sisi kwetu hapa ni Tanzania peke yake ndiyo tunazalisha *wine* kwa kiwango kikubwa sana. Afrika ya Kusini wanazalisha tani lita bilioni 1 za *wine* kwa maana. Dodoma kwa maana ya Tanzania hatujawahi kuzidi lita milioni 15. Kuna kazi ya kufanywa hapa na niombe Serikali itusaidie katika hili. Wawapeleke wataalam wakajifunze, vinginevyo zabibu yetu itaendelea kulala na itaoza mashambani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo nataka nilichangie; Ilani yetu ya Uchaguzi inasema kuhusu ajira na naona ajira nyingi zinatengenezwa kwenye Sekta ya Kilimo. Nimesoma jarida *the global employment trend,* inasema sekta mbili zitachangia sana kwenye kutatua changamoto ya ukosefu wa waajira hasa kwa vijana, viwanda na kilimo. Hapa kuna mpango mkakati wa Wizara wa kuwahusisha vijana kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, iko fursa kubwa sana ambayo hatuitumii vizuri. Katika viwanda vya usindikaji wa matunda hivi sasa, hasa kutumia Mzee Bakhresa kwa viwanda vyake.

Wana mahitaji ya tani za matunda 120,000 za maembe kusindika lakini *capacity* iliyoko hivi sasa ni takriban tani 25,000 kwa hiyo iliyobaki yote wana-*import pulp* kutoka nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Bashe unafahamu mzee Bakhresa alikuwa tayari kuisaidia Serikali kwenye kuandaa mashamba na kuweka miundombinu ya umwagiliaji ili vijana wengi zaidi wapewe mashamba ya kutosha tuanze kuuza matunda hayo kwenye viwanda vya Bakhresa na Sayona ambapo mahitaji yao ni tani 120,000 lakini hivi sasa wanapata tani 25,000 tu. Serikali ione jitihada sasa, ione ulazima wa kutayarisha mashamba makubwa soko la uhakika lipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye ukwaju Bakhresa anahitaji tani 15,000 za ukwaju kwa mwaka. Sisi tuna uwezo wa tani 4,000, anaingiza *pulp* kutoka nje ya nchi. Hili ni eneo ambalo pia tunaweza tukalifanyia kazi vizuri. Mananasi yetu, mengi yaliyoko hayafai kutengeneza juisi na mananasi pekee ambayo yanafaa kwa Afrika ni *MD2* ambayo yaliingizwa miaka 42 iliyopita nchini Ghana kutokea Costa Rica ambayo ndiyo hata akina Bakhresa na Sayona wanayahitaji. Sasa tuna vijana hapa ambao wengi wangeweza kufanya kazi ya kilimo. Serikali, nawaomba kazi yenu nendeni mkatayarishe mashamba ya kutosha, wekeni miundombinu, soko lipo. Tukifanya hivyo tutakuwa tumewasaidia vijana wa Tanzania. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ANTHONY P. MAVUNDE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Anthony Mavunde. Nimeshakutaja Mheshimiwa John Marko Sallu na utafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji.

**MHE. JOHN M. SALLU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami nichangie kwenye Wizara hii ya Kilimo. Kwanza niwape hongera sana Waziri, Naibu Waziri, Makatibu

na watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya kusukuma gurudumu letu la kilimo. Nikija upande wa mbegu, mbegu ni kitu muhimu sana katika kilimo, kwa bahati nzuri uzalishaji wa mbegu wa ndani sasa unaanza kupanda kulinganisha na miaka ya nyuma ambako zaidi ya asilimia 70 ya mbegu ilikuwa inaagizwa kutoka nje, hapo niwape hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri ameainisha kwamba ataipa nguvu kubwa *ASA* ili iweze kuzalisha mbegu kwa wingi. Lakini hapo hapo naishauri Serikali isiwasahau wazalishaji binafsi kwa kuwawekea mazingira rafiki ili waweze kuzalisha kwa wingi kwani mpaka sasa hivi wazalishaji binafsi wanazalisha asilimia 90 ya mbegu. Kwa hiyo, hatutakiwi tuwaache nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watafiti wetu wa mbegu wanafanya juhudi kubwa kutengeneza mbegu zenye tija lakini mara nyingi zinaishia kwenye makabati, hazipati kutangazwa vya kutosha ili wananchi wakazifahamu. Ushauri wangu hapa, turudishe lile zoezi la kugawa mbegu kwa ruzuku. Wananchi wakipewa mbegu kwa ruzuku wakulima wadogo wadogo wataanza kutambua zile mbegu mpya zilizokuja na hivyo ikifikia kununua watakuwa wanazitafuta kwa majina zile mbegu mpya watalaam wetu walizozitengeneza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukija kwa upande wa umwagiliaji. Sisi wa Handeni vijijini tuna mto mkubwa unapita pale mto wa Pangani ambao haukauki mwaka mzima. Tuna mabonde mazuri ya umwagiliaji ambayo nilikuwa naomba Serikali iyatolee macho. Bonde la Masatu lililoko Kata ya Segera na Bonde la Jambe lililoko Kwamgwe. Kwa kutumia umwagiliaji, tunaweza kutengeneza mazao ya mbogamboga ambayo yanaweza kusaidia sana kiuchumi pamoja na ku-*export* nje ya nchi tukapata hela za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile kwenye mazao ya matunda, kwenye matunda, sisi wa Handeni Vijijini tunazalisha sana matunda ya maembe pamoja na michungwa. Lakini

kwa bahati mbaya tumevamiwa sana na wadudu waharibifu wa matunda hayo. Nzi weupe, kwa hiyo, naomba Wizara itoe macho itusaidie janga hili ambalo linadhuru sana machungwa na miembe iliyoko kwenye kata takriban 10. Nikizitaja kata ambazo zimeathirika sana ni Kata ya Kwedizinga, Segera, Mgambo, Kabuku, Kabukundani na Kwamgwe. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali itoe macho ili iweze kutusaidia janga hili la wadudu waharibifu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa muda niliopata. Naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge wa Handeni Vijijini Mheshimiwa John Marko Sallu. Nilikutaja Mheshimiwa Ashatu Kijaji na utafuatiwa na Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe.

**MHE. DKT. ASHATU K. KIJAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii muhimu kwa maendeleo ya watu wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa pongezi kwa Mheshimiwa Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan kwa mwongozo wake sahihi alioutoa na hasa kusababisha mfumo wa stakabadhi ghalani kusitishwa kwenye Mkoa wa Dodoma mwaka huu, 2021. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni uongozi makini na sina wasiwasi na uongozi wa Profesa Mkenda, nimefanya naye kazi ni kiongozi makini, nina uhakika atatuvusha Watanzania. Lakini pia Mheshimiwa Naibu Waziri, kaka yangu Bashe nikupongeze sana tumeanza mbali tangu tukiwa wanafunzi. Nafahamu uwezo wako, simama kwenye haki na Mwenyezi Mungu atakusimamia utatenda vyema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimepongeza kwa kufutwa kwa stakabadhi ghalani au kusitishwa kwa mwaka huu 2021. Lakini Wanakondoa wamenituma niulize kwa Serikali, je ni mwaka huu tu 2021? Au mfumo huu kwa mikoa ambayo hatuna

mfumo ambao ni *strong* wa ushirika, hauruhusiwi tena kufanya kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimetumwa kuuliza suala hili kwa sababu mwaka jana Mkoa wa Dodoma na hasa Kondoa tulipita kwenye mazingira magumu sana. Nilimsikiliza vizuri Mheshimiwa Mbunge wa Songwe jana Mheshimiwa Mulugo akiongea mpaka kufikia kutishiwa kwa ajili ya kutetea wananchi wake. Mheshimiwa Mulugo, mwenzako Kondoa mwaka jana ilikuwa ni zaidi ya kuuwawa, sasa sijui zaidi ya kuuwawa ni nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni hatari mno, unaposimama na wananchi unawaeleza mfumo wa stakabadhi ghalani ni nini? Mfumo wa stakabadhi ghalani hauji kwenye masoko peke yake. Tunapoongelea kwenye masoko hapa tunaukuta mfumo wa stakabadhi ghalani na *TMX,* hapa ni *climax.* Lazima uwe umeshaanza kufanya kazi kuanzia kwenye uandaaji wa mashamba ya wananchi. Wananchi wanaandaje mashamba? Wanapataje mbegu bora na sahihi? Wananchi hao wanatunzaje mazao yao? Wananchi hawa, je wana vyama vya msingi kwenye maeneo yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe unatoka Dodma, nimekusikia jana umesema na wewe unashukuru mwaka huu kusitishwa lakini wananchi wetu wameumia. Wapo wananchi wameamua kuacha kulima zao la ufuta kwa sababu ya mfumo huu wa stakabadhi ghalani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Waziri, Profesa Mkenda kaka yangu nikuombe sana hebu angalia huo mfumo. Kwanini wananchi wanaupigia kelele? Yaani Serikali inasema unamsaidia mwananchi halafu mwananchi anapiga kelele? Hapa mbona ni vitu viwili ambavyo havieleweki. Unakuja kufuta mfumo wa stakabadhi ghalani tayari wakulima wameacha kulima ufuta, umetusaidia kweli? Hebu tunaomba tuanzie mwanzo tusimame imara tuone ni jambo gani tunatakiwa kufanya. Kwanini mfumo wa stakabadhi ghalani?

Mheshimiwa Spika, walikuja pamoja, stakabadhi ghalani pamoja na *TMX,* na kwa hili naomba niishauri Serikali yangu tukufu. Soko lile la bidhaa *TMX* wamewekeza kiwango kikubwa kwenye miudnombinu ya TEKBOHAMA. Mifumo ile iliyowekezwa tusi-*-justify* kwa kuumiza wananchi wanyonge, hapana. Kwa hiyo, jambo la msingi kwenye mfumo ule wa *TMX* soko la bidhaa kwanza Serikali iangalie pale ambapo ipo Wizara ya Fedha ni sehemu sahihi ya kuweka soko la bidhaa? Soko la bidhaa linatafuta masoko. Masoko yanatafutwa na Wizara ya Viwanda na Biashara, inakuwaje *TMX* ina-*hang* kwenye Wizara ya Fedha. Inakuja inajiunganisha na Wizara ya Kilimo hapa katikati kuna kitu kinakosekana. Kwa hiyo, tusiende kuwaumiza wananchi wetu kwa sababu ya vitu ambavyo hatujavifanyia kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nim-*quote* Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika. Alisema maneno yafuatayo; *the future millionaires and billionaires of Afrika will come initially from agriculture.* Kilimo…

**SPIKA:** Ahsante sana. Dakika tano ni chache.

**MHE. DKT. ASHATU K. KIJAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja na naomba stakabadhi ghalani kwa Dodoma tuondoleeni, ni usumbufu mkubwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Dkt. Ashatu Kijaji. Mwaka jana Mheshimiwa Dkt. Ashatu kidogo awekwe ndani kwa sababu ya mfumo wa stakabadhi ghalani japo alikuwa Naibu Waziri. Ilikuwa shughuli kubwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

Nilikutaja Mheshimiwa Mpembenwe, halafu baada ya Mpembenwe, atafuata Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia katika Wizara hii ambayo ni muhimu sana. Kwanza kabisa nichukue nafasi

hii kuipongeza Wizara ya Kilimo kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wameendelea kuifanya kwa muda mrefu tangu nchi hii ipate uhuru.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika maeneo makubwa mawili. Eneo la kwanza litakuwa ni eneo A, hili litakuwa linahusu Mkoa wa Pwani na eneo la pili tutakuwa tunazungumzia suala zima la Kitaifa na imani yangu ni kwamba dakika tano zitatosha sana.

Mheshimiwa Spika, nina masikitiko makubwa sana katika bajeti ambayo imetoka kuzungumzwa katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri kwamba bajeti hii haikuugusa Mkoa wa Pwani kama vile ipasavyo. Ni masikitiko yangu makubwa sana kuona kwamba pale Pwani katika Wilaya ya Rufiji watu wa Kibiti sisi ni wahusika, watu wa Mkuranga ni wahusika. Kuna mradi mzuri sana pale katika Bwawa la Mwalimu Nyerere lakini bajeti/hotuba hii haikuzungumza chochote kuhusiana na suala zima la kilimo cha umwagiliaji sijui, sisi watu wa Kibiti, Pwani, Rufiji tumekosa nini kwa Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kama hivyo haitoshi masikitiko yangu mengine makubwa ni kwamba watu wa Pwani hasa watu wa Kibiti, Rufiji, Mkuranga, Kisarawe, Bagamoyo, Mafia sisi ndiyo wakulima kule wa zao la korosho wakizingatia kwamba pale Kibiti ndiyo barabara yao. Tunazalisha korosho kwa wingi sana. Tuna shida sana sisi pale Pwani kuhusiana na ubora wa korosho zetu na suala hili tumekuwa tukilijadili mara kwa mara. Waheshimiwa Wabunge tukiwa tunakutana na Mheshimiwa Ulega, Mheshimiwa Mchengerwa pamoja na Mheshimiwa Jaffo tulikuwa tunakaa tunajadili suala hili, jinsi gani tutakavyoweza kusaidia sasa Serikali ili iweze kutusaidia. Zao hili la korosho liwe na ubora wa kutosha kwa sababu kila mwaka zao hili pale Pwani bei yake iko chini zaidi.

Mheshimiwa Spika, g*rade A,* inayokuwa inauzwa kule kwa watoto wetu Kusini, pale Pwani inauzwa mpaka shilingi 400, hiki kitu hakieleweki. Nasikitika sana Profesa katika hotuba yako hujaeleza mkakati gani mlionao ili kuweza kutusaidia

sisi watu wa Pwani, ili ubora wa korosho zetu uwe mzuri na vilevile tuweze kupata bei ile ambayo inastahiki kama vile watoto wetu wa Kusini na watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo nataka nichangie ni la kitaifa zaidi. Hotuba hii haijajibu maswali ya msingi ya mkulima; leo mkulima anahitaji soko na *sustainability* ya *price.* Mheshimiwa Waziri amekuja hapa hakutuambia mikakati gani Wizara au Serikali inayo katika kuhakikisha kwamba wakulima wa korosho, ufuta, pamba na wakulima wa mazao mengine na kwa ndugu zangu hapa Wagogo, wana mkakati gani kuhakikisha tunapata soko. Tulikuwa tunategemea Serikali mnavyokuja hapa na hii bajeti, mnakuja kusema mipango kwamba tuna mpango moja, mbili, tatu wa kuweza kupata masoko. Mkulima huyu anakwenda kulima soko hamna mnategemea kitu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili la kusikitisha ambalo hili ni majonzi makubwa vilevile, Serikali haijaja na mpango wa kuweza kutuambia ni jinsi gani sasa wanaanza kufikiria jinsi ya ku-*control price* ya mazao haya. Wakulima wanapata shida kubwa sana, wanalima na kuuza katika mazingira magumu sana na wanavyouza vilevile *price* inayopatikana siyo ya kufurahisha, lakini malipo yenyewe vilevile hayapatikani kwa wakati. Tulikuwa tunategemea Serikijali ikija hapa mnakuja na mpango wa kutuambia kwamba katika bajeti hii mmejipanga kuweza kuona *price* inakwenda juu na vilevile wakulima wanakwenda kulipwa kwa wakati, lakini hilo halikuweza kuzungumzwa katika hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine cha kusikitisha zaidi hotuba hii haijagusa hata kidogo suala zima la matatizo ya ushirika. Sisi tulikuwa tunategemea kwamba Waziri akiwa anakuja hapa anakuja kutueleza kwamba jamani ushirika kule tunajua kuna matatizo kwa hiyo sisi kama Serikali tumejipanga sasa kwenda kufanya 1, 2, 3 ili kumkomboa mkulima huyu.

Mheshimiwa Spika, nataka nikwambie sisi katika Mkoa wa Pwani tuna kitu kinaitwa *CORECU,* ni shida. Tulikuwa

tumekaa Wabunge sisi tukajadili, Mheshimiwa Ulega akiwepo, Mheshimiwa Mchengerwa na Wabunge wengine ambao tuko katika Mkoa wa Pwani, tumekwenda mpaka tukafikia hatua kwamba tumebadilisha uongozi katika *CORECU* ili kuweza kuona jinsi gani tunakwenda kumsaidia mkulima. Cha kusikitisha zaidi Serikali hamjaja na mpango halisia wa kutuambia ni jinsi gani mnakwenda kutatua kero ya mkulima wa pamba, kahawa, korosho, ufuta, katika suala zima la ushirika. Wabunge wengi wamesimama wamezungumza suala hili.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine kubwa zaidi la kusikitisha, Serikali hamjaweza kutuambia mnafanyaje kuhusiana na ile *interference* katika suala zima la *agriculture. Interference* ina shida, mturuhusu sisi tulime.

Mheshimiwa Spika, *without prejudice* na kwa heshima na taadhima ya hali ya juu, sisi wakulima hatutegemei leo eti uende ukampe kishkwambi hicho Afisa Ugani aende kule chini Mchukwi, Ruaruke, Kipugila, Mkuranga kumsimamia mkulima, hiki kitu kinatoka wapi? Tuna *data base* ambayo tumeshaiandaa sisi kama Serikali, hakuna. Leo Mheshimiwa Waziri nikikuuliza kwamba tuna wakulima wangapi Tanzania *you haven't got a clue.*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mpembenwe dakika zako zimekwisha, lakini kwa dakika moja tu kabla hujakaa chini ulianza kwa kuwalaumu kidogo kwamba hawakuwa na mpango wowote kuhusu umwagiliaji kuhusiana na Bwawa la Mwalimu Nyerere, sikukuelewa hapo unataka kusema nini?

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mradi ule wa Bwawa la Mwalimu Nyerere unakwenda sambamba na mradi mzima wa umwagiliaji. Sisi watu wa Kibiti, Rufiji, Mkuranga, kuna ardhi nzuri kule tunategemea masuala ya *hot culture* yaweze ku-*take place.* Serikali hawajaja na mpango wa kueleza kwamba Bwawa

hili la Mwalimu Nyerere mbali ya kwamba linakwenda kutoa umeme lakini vilevile linakwenda kuwasaidia wananchi kule katika zile ekari 150,000 kuweza kuwa na kilimo cha umwagiliaji. Hii ilikuwa ni *concern* yangu kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, labda watajibu wenyewe. Ndiyo maana nilikuuliza kwa sababu bwawa lile *entirely* lote liko ndani ya *National Park.* Sasa *National Park* huwezi kuweka kilimo cha umwagiliaji wala chochote kingine. Kwa hiyo, ku-*link* moja kwa moja inataka kidogo, labda kama ni fedha zinazotoka huko baadhi yake zitengwe zikaboreshe kilimo *downstream* lakini kwenye umwagiliaji na bwawa lile ni vitu viwili ni tofauti kabisa.

Tunaendelea na Mheshimiwa Anatropia Theonest.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami nichangie katika Wizara hii nyeti ambayo inawagusa Watanzania wengi. Niseme natokea kwenye maeneo ambayo pia ni wakulima, Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Spika, wakati wengine wakiongelea miradi ya umwagiliaji, Kyerwa, Karagwe na majimbo mengine ya Mkoa wa Kagera hatuongelei miradi ya umwagiliaji. Wakati wengine wanalia na mbolea sisi hatuongelei mbolea, Mungu ametupa rasilimali, mvua ya kutosha, ardhi yenye rutuba na kila kitu, lakini tuna changamoto za kutosha.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kagera tunazalisha kahawa lakini badala ya kahawa kuwa faida imekuwa ni karaha. Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja Kyerwa wakati fulani, nadhani moja ya kati ya kitu alichowaambia wananchi wale akasema sasa kahawa imekuwa ni ngumu kuuza kwa sababu ya janga la *Corona,* lakini wale wakulima ambao wanategemea kahawa *per se* haujaweza kuwapatia masoko, unategemea nini kitatokea? Kwa hiyo, nieleze sisi Mkoa wa Kagera tuna changamoto ya masoko ya kahawa.

Mheshimiwa Spika, nimepitia takwimu, ukiangalia uuzaji au uzalishaji wa kahawa Afrika ya kwanza inakuwa Ethiopia, ya pili ni Uganda, lakini ukiangalia ukubwa wa nchi ya Uganda ukakalinganisha na Kagera au na Tanzania, Uganda ni sawa na Kagera tu, lakini kahawa inazalishwa maeneo mengi Tanzania, Uganda wanatuzidi nini? Ukweli ni kwamba Uganda wanaweza kupata kahawa kutoka Tanzania. Jibu liko *very simple* kwa sababu wanaweza ku-*offer price* nzuri. Jana Mheshimiwa Mama Rwamlaza ameeleza hapa na mimi nikaangalia *price* ya kahawa za maganda bado sisi tuko chini.

Mheshimiwa Spika, pia ukirudi kwenye *ranking* za nani anazalisha kahawa bora, baada ya Ethiopia Tanzania inakuwa ya pili. Kwenye kuzalisha kahawa kwa wingi Afrika tunajikuta tuko kama wa sita, *which means* sisi bado tuna-*advantage* ya kuzalisha kahawa bora na ku-*penetrate* kwenye soko lakini hatufanyi vizuri.

Mheshimiwa Spika, nini imekuwa changamoto yetu ya msingi? Changamoto ya msingi ni vyama vya ushirika na nimeongea hapa mara nyingi kwamba mfumo tulionao wa vyama vya ushirika haufanyi vizuri, ukweli tuuseme. Hatuwezi kuendelea kung'ang'ania mfumo eti kwa sababu Ilani ya Chama chenu imeongelea ushirika, haiwezekani!

Mheshimiwa Spika, lakini nimepitia kidogo *record* hapa, nilikuwa napitia *audited record* za vyama vya ushirika hapa ambayo mmeweka kwenye ripoti yenu. Wanasema kati ya vyama 6,021 vilivyopata hati yenye kuridhisha ni 289, hii ya mwisho anasema hati chafu ni vyama vya ushirika 1,670. Kwa hiyo, sasa na hao watu mnaowang'ang'ania hawawezi hata kuandaa *records* na ukweli ndio uko hivyo, wanakusanya, hawawezi kulipa kwa sababu hawana fedha, *it is obvious* wanategemea fedha kutoka benki za biashara, kutoka kwenye Benki ya Kilimo lakini inakuja kwa muda gani? Hawa wakulima wanataka fedha waandae mashamba na waweze kupeleka watoto shule. Imekuwa ni changamoto, mnapata kigugumizi gani kuruhusu mfumo huria ukafanya kazi, ndicho kinachofanyika Uganda. Nimeenda Uganda kwa

nauli yangu kwa ajili ya kwenda kuona wao wanafanyaje kuhusiana na zao hili la kahawa kwa sababu Kagera na Uganda ni *almost the same,* maisha na mazingira ni yaleyale, sisi tumekosea wapi?

Mheshimiwa Spika, mimi niwashauri naomba muache mfumo huria u-*take place* na badala yake mu-*intervene* kwenye haya makosa madogomadogo na yapo. Mheshimiwa Waziri umekuwa unaongelea butura, ni kweli butura ipo na inaumiza watu, lakini bado Serikali ina uwezo wa kusimamia na kuzuia hicho kitu kinachoendelea, lakini butura ina tofauti gani na biashara ya benki? Watu wanavyoenda kukopa benki si wanakopa kwa riba? Hata butura watu wanakopa kwa riba, cha msingi ni lazima muone mnaweza ku-*regulate* vipi ili wakulima wasiumie, hicho ndicho naweza kushauri. Mjue kwamba mnavyozidi kuwabana wakulima mnatengeneza maisha yao yawe magumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hoja yangu ya pili kwa sababu ya muda niongelee masoko ya kibiashara yale mliyoyajenga Murongo na Nkwenda na maeneo mengine ambayo katika swali la jana nilieleza yamesimama tangu mwaka 2013. Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kyerwa aliwahi kuuliza swali kuhusu umaliziaji wa haya masoko aliambiwa kwamba zimetengwa shilingi bilioni 1.9 kwa ajili ya kumalizia yale masoko. Swali lilelile akauliza Mheshimiwa Mama Rwamlaza, akaambiwa zimetengwa shilingi *2.5 billion.*

Mheshimiwa Spika, nikauliza swali lilelile kwenye Bunge lililopita nikajibiwa uwongo huohuo, nimerudisha hilo swali jana, majibu ninayopewa kwamba, wametenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya kwenda sasa kufanya *feasibility study* kuona yameishia wapi, waanzie wapi kuyajenga, *it is not fair* Mheshimiwa Waziri. Yale masoko mkiyajenga pale Murongo kwetu ni biashara. Kila kitu kinatoka Uganda upande wa pili kuja Tanzania, wanachokichukua Tanzania ni yale majani tu ya migomba kwa ajili ya kupika sijui wanafanyia na kitu gani kingine. Hii unaiona haiko sahihi. Bado tuna fursa za kufanya biashara, nimewaambia Mikoa ya Kagera hatuhitaji mbolea

au *irrigation,* tunachokitaka ni *intervention* ya soko basi, mengine tutafanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Anatropia Theonest. Sasa ni wakati wa Mbunge wa Jimbo, Mheshimiwa Innocent Bilakwate. *(Makofi)*

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa afya na nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara imeleta bajeti ambayo ina mambo mengi mazuri, lakini mimi niseme kama hatuna soko la uhakika, tunapoteza muda na hapa tunafanya ngonjera tu. Huu umekuwa ni wimbo wa kila siku na wewe Spika ni shahidi tumekuwa tukiambiwa tunaleta mbolea, mbegu bora, miche, lakini soko la haya mazao liko wapi? Kwa hiyo, hii ni changamoto kubwa na Wizara lazima ijipange kuhakikisha tunapata masoko. Mkulima amekuwa analima kilimo cha kubahatisha tu, anasema mwaka huu nimelima, lakini sina uhakika wapi nitauza mazao yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni muumini wa ushirika na hii iko kwenye ilani ya Chama cha Mapinduzi, lakini niseme kama ushirika hawatakuja na mbinu ambayo itaweza kumnufaisha mkulima, mimi sitaiunga mkono. Tunataka ushirika ambapo mkulima anapopeleka mazao yake aweze kupata pesa yake. Tunataka ushirika ambapo mkulima aweze kutatuliwa matatizo yake sio mkulima anaenda kukopwa. Kwa hiyo, lazima Wizara muwe wabunifu, ukitaka kuleta jambo jema na zuri, lazima uweke vitu ambavyo vitawavutia wale unaowaletea.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ni kipindi cha msimu wa kahawa. Asubuhi nimepiga simu kuuliza bei ya Uganda kahawa ni shilingi ngapi? Kahawa Uganda sasa hivi ni shilingi 3,500 ya Uganda ambayo kwa kwetu ni shilingi 2,300, lakini kwetu kahawa hiyohiyo ya arabika wanakwambia ni shilingi

1,500. Ukija kwenye kahawa ya robusta ambayo Uganda ni shilingi 2,500 kwetu ukipiga hesabu hela ya Tanzania ni shilingi 1,500 kwetu ni shilingi 1,100.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho mimi ninakishangaa huyu mkulima wakati anaanza kulima, anaanza kuandaa hii kahawa Serikali huioni popote, lakini kipindi cha msimu unapoanza utashangaa askari wanapelekwa mpakani. Sasa ninataka nikuulize Mheshimiwa Waziri, wewe unasema Uganda hawana bei nzuri, askari wale mnapeleka wa nini mpakani kahawa isiende Uganda? Wewe unasema majirani zetu hawana bei nzuri, sawa ninakubaliana na wewe; kwa nini msimu unapofika ndio mnapeleka maaskari, maana yake kule kuna bei nzuri ndio maana mkulima anakimbilia kule. Kipindi cha msimu kikifika ni kama vita, hili jambo halikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe sana haya mambo ya kuanza kukamata wananchi wanapoanza kuvuna kahawa, ooh, kahawa sijui haijaiva, sisi kule kwetu mtu ana mashamba zaidi ya matatu, analima kwenye kata hii na kwenye kata nyingine, sasa wakikuta unahamisha kahawa yako kuitoa kwenye kata nyingine ambako una shamba unaipeleka kuianika kwako wanasema kahawa unaipeleka Uganda, hili jambo halikubaliki. Kwa hiyo, niombe sana Serikali ijipange kuleta bei nzuri ya kahawa. Tuwe na masoko ya uhakika vinginevyo tunapoteza muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kiwanda cha *TANICA,* hiki kiwanda kiboresheni. Mtakapoboresha hiki kiwanda nina uhakika kitaweza kuongeza bei ya kahawa. Kiwanda kinaendelea kubaki vilevile, lakini ninyi kazi yenu ni kutegeshea msimu umefika mnatafuta pesa yenu ya Serikali, hili jambo sio sawa. Kwa hiyo, niombe sana Serikali iboreshe kwanda cha *TANICA* ili hiki kiwanda kiweze kuongeza bei nzuri kwa mkulima, vinginevyo niombe sana Serikali kama hamjajipanga waacheni wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi kitu ambacho siungi mkono ni suala la butura. Hilo mnapambana nalo kwa nguvu zote

kwa sababu linamnyonya mkulima, lakini wapeni uhuru wananchi kuuza kahawa wanavyotaka...

**TAARIFA**

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa, Mheshimiwa.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nalazimika kumpa Taarifa mzungumzaji, mtumishi wa bwana, butura inaingia kwa sababu ya ku-*fail* kwa mfumo wa ushirika. Butura kwa kwetu ni *continuous cash flow,* mkulima anahitaji *continuous cash flow,* anahitaji chenji. Kwa hiyo, akikosa chenji atachukua alichonacho kusudi apate pesa ya kutimiza majukumu yake, anaweza kuuza hata kitanda. Sasa yeye hauzi kitanda anauza kahawa aliyonayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali ilete *cash flow,* ilete *chenji,* Wahaya walikuwa wanaita *nyantakorakorwa*, *BCU* ilikuwa ina kitu kinaitwa chenji, *nyantakorakorwa* ndio iliondoa butura. Bila *nyantakorakorwa* butura itaendelea kuwepo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Taarifa hiyo inayohusu *nyantakorakorwa*? *(Kicheko)*

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, mimi ninachosema napokea hii Taarifa, lakini naishauri Serikali lazima ije na mpango wa kumsaidia huyu mkulima kabla hajauza kahawa yake aweze kupata pesa ya kumsaidia kuendeleza zao hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo mimi nasita kusema naunga mkono hoja kwa sababu bado wakulima wangu wanateseka. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Innocent Bilakwate. Kwa kweli, kuna siku inabidi tuje tuweke hoja hapa ya kujadili

kangomba, butura na nyingine zinazofanana ili tuweze kuishauri Serikali kuhusu mwelekeo wa mambo haya. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Jackson Kiswaga ndiye unayefuata. Baada ya Mheshimiwa Kiswaga atafuata Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu. Mwaka 2012 nilipata nafasi ya kuhudhuria mkutano ulioandaliwa na *USAID* pamoja na *SAGCOT* pale Ubalozi wa Marekani, wakati huo mimi nilikuwa msimamizi wa Idara ya Ukuzaji Biashara M-Pesa na nilikuwa nimekwenda pale kwa sababu ya kutaka kusaidia sekta ya kilimo ili kuona namna gani kwa kutumia mtandao tunaweza tukawasaidia kutoa taarifa mbalimbali zinazohusiana na kilimo, upatikanaji wa ardhi na pembejeo na vitu vingine kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, katika kikao kile alikuja Mkuu wa *USAID* duniani wa 16 kwa wakati huo, alikuwa anaitwa Rajiv Shah. Katika mazungumzo yake nilimsikia akisema: *"I am not convinced with a progress of SAGCOT and I therefore consider to withdraw."* Akiwa anamaanisha kwamba hakuridhishwa na hatua ambayo *SAGCOT* walikuwa wameifikia wakati ule na naamini alisema *statement* hiyo pengine wao walikuwa ni wafadhili wa huo mradi.

Mheshimiwa Spika, Nini ambacho hakuridhishwa nacho? *SAGCOT* ilitakiwa iandae ardhi kubwa kwa ajili ya uwekezaji, lakini mpaka wakati ule *SAGCOT* ilikuwa haijafanya hivyo na wawekezaji wa Marekani inaonekana walikuwa wanataka ardhi kubwa. Unajua mwekezaji wa Marekani anaweza akawekeza Mkoa wote wa Dodoma sasa *SAGCOT* ilikuwa haijafanikiwa kufanya hivyo kwa hiyo, inaonekana *USAID* walisema wanataka kujiondoa.

Mheshimiwa Spika, sasa ushauri wangu ni nini katika chombo hiki? Hiki chombo ni muhimu na kiliundwa katika Awamu ya Nne ya Serikali yetu na nia yake ilikuwa ni kutaka

kusaidia kilimo kiweze kukua, kutafuta masoko na ardhi ya uwekezaji. Sasa nataka niiombe Serikali katika chombo hiki ione uwezekano wa kukifanya chombo hiki kifanye kazi. Kama kwenye umeme kuna Mfuko wa *REA,* kwenye maji tumeweka *RUWASA,* lakini pia kwenye barabara tumeweka *TARURA* na kwenye kilimo tuitumie hii *SAGCOT* ili iweze kuwasaidia wakulima kutafuta masoko lakini kuleta wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa maendeleo tumesema hivi, kwamba tunataka tuandae mazingira wezeshi lakini pia tutafute ajira kwa ajili ya vijana pamoja na masoko, ukileta wawekezaji wakubwa huitaji kuisumbua Serikali kutafuta masoko kwa mfano ukienda pale Rungwe nilishakutana na mkulima mmoja anaitwa Robert Kruga yeye alitoka Zimbabwe analima pale anasoko lake yeye mwenyewe kwa wiki nafikiri anatakiwa kupeleka makontena 50 Ulaya ya Parachichi. Kwa hiyo, ametengeneza wakulima wengine wengi *out growers* hatuhitaji Serikali maana kule jamaa tayari ana soko.

Mheshimiwa Spika, ukienda Iringa pale ipo Asasi yeye anafuga na anatengeneza hizo *yogurt* lakini sasa hivi anapata lita 40,000 kwa siku na yeye anataka lita 100,000 kwa hiyo ametengeneza wafugaji wengi ili wamsaidie kupata maziwa na bado hayatoshelezi. Kwa hiyo, maana yake hii *SAGCOT* kama tunaiwezesha ikapata fedha lakini zamani nimeangalia hapa hii *SAGCOT* imekuwa ina *guarantee* ya Serikali ukiipa *guarantee* hii *SAGCOT* unaiwezesha iende ikatafute wafadhili yenyewe ili ikipata wafadhili wawekeze kwenye kilimo na hawa *SAGCOT* wakipata fedha hii *SAGCOT catalyst fund* itaweza kwenda kuwakopesha wakulima, itaenda kutoa elimu na kuweza kuwatafutia masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utakuta kwamba hatuna haja sasa ya kuona kwamba hawa wakulima wanahangaika na soko au wahangaike kwenye mabenki kupata zile riba kubwa na za muda mfupi *SAGCOT* inaweza kuamua kwamba iweze kutoa riba za muda mrefu na kuwasaidia wananchi. Lakini pia ukitengeneza viwanda vidogo vidogo kwenye kilimo soko litakuwepo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe mfuko huu wa *SAGCOT* uwezeshwe na Serikali na mpango wake wa kwanza ulikuwa kwamba huu mfuko ushughulikie sekta zote Mifugo pamoja na Kilimo, na kwa mpango huo nilikuwa ninashauri ikiwezekana huu mfuko usikae kwenye Kilimo ukae kwa Waziri Mkuu ili aweze kuuratibu kwa sababu sasa ushughulikie sekta zote na uweze kwenda nchi nzima usiende Nyanda za Juu Kusini peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na mengi naona muda wangu hautoshi ni hilo tu moja linatosha kuchangia kwa leo pengine mengine nitaandika ili Serikali iweze kuangalia nini cha kufanya, naunga mkono hoja ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jackson Kiswaga. Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka atafuatiwa na Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nichangie katika Wizara hii nyeti ya Kilimo. Labda niombe tu kusema kwamba nilisikia vizuri au nilijisikia vizuri nilivyoona Waziri akisema kwamba hiki kilimo ambacho kinaendeshwa na asilimia 65 ya Watanzania hakina tija. Kwa mantiki hiyo nika-*expect* kwamba atakuja na mpango mkakati wa kwamba tuwe na *commercial farming* ya *big farmers* ambao wataweza ku-*supplement* kulima kilimo hiki cha wenzetu hao wadogo.

Mheshimiwa Spika, mwisho nikajiuliza kwamba kwakweli sijaweza kuona kama tunasheria ya kulinda ardhi ya kilimo najua tunasheria ya kulinda mazao kahawa, tumbaku lakini sijui kama tuna sheria ambayo inalinda ardhi ya kilimo. Kwanini ninasema hivyo unakuta mara nyingi kumekuwa na hii migogoro ya kuingiliana Wafugaji na Wakulima moja, lakini la pili Serikali ikitaka kujenga mahali inakwenda kufukuza wakulima wanasema tunataka nafasi hii tugeuze tuwe tunajenga aidha Ofisi za Serikali au tujenge shule kiasi kwamba mkulima anajiona kama mtumwa katika nchi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe umeji-*establish* kwa miaka mingi ile sehemu umeitafuta ukajua kuna maji pake lakini sasa inakuja Serikali inasema itaku-*compensate* hakuna kukaa ku-n*egotiate* hakuna kuna kwamba unanihamisha unanipeleka wapi? Haiwatafutii hata mahali pa kusema ndio wana *settle* kwa ajili ya kujenga nyumba zao na kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matokeo yake mashamba ambayo mkulima ameyaboresha kwa muda mrefu anapewa fedha kidogo anaambiwa nenda utatafute sehemu nyingine, swali ni kwamba kule anakoenda kutafuta ana uhakika gani baada ya miaka mitano hatahamishwa tena kwa hiyo, nilikuwa ninaomba nipate hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini lingine sisi najua Tanzania hatuna uzoefu wa kulima kilimo cha umwagiliaji *in such commercially* sasa ninajiuliza hivi kwanini hatuendi kujifunza kwa wenzetu Kenya, kwanini hatuendi kujifunza kwa wenzetu *South Africa!* Kwamba ardhi lazima utenge ardhi kubwa kuonesha kwamba hizi hekta labda 100,000 au hekta 200,000 tuna-*specialize* kwenye mazao *say* Alizeti. *With that* tunakuwa *forward* na *backward linkages* ambapo utaweza kuweka miundombinu inayotakiwa, miundombinu ya umwagiliaji, miundombinu ya umeme na barabara hapo hapo unaweka kiwanda kitakacho-*process* tuna vijana wetu wanamaliza *SUA* tuna vijana wetu wanamaliza vyuo vingi hivi vya Kilimo, hawana ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini *suppose* Serikali ingekuwa imetenga haya maeneo makubwa na hati zipo wakatengeneza *infrastructure* wakawasaidia hawa vijana wakawapa mikopo ya kama miaka mitano bila kurudisha ili waweze ku-*produce* hiyo si inge-*create* ajira ambayo ingehakikisha vijana wetu wanashiriki katika uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, najua kwamba kuna-*documents in come across* imeandikwa na Mmarekani mmoja wanasema '*American needs to keep Africa impoverished* ili nchi za Marekani, Ulaya, Asia waendelee ku-*survivor. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sasa hivi kilimo chetu kinategemea fedha za umwagiliaji kutoka kwa *donners* na hivi fedha kwa *90 percent* hizi fedha haziji *intime.*

Mheshimiwa Spika, maana yake zitukwamishe ili tushindwe tuendelee kuwa *impoverished* kwa hiyo, ningeomba kwamba kama Serikali ipo *serious* itenge fedha za umwagiliaji nakumbuka mwaka 2019 kulinunuliwa mitambo ya kuchimba mabwawa Mheshimiwa Bashe labda anaweza kukumbuka lakini sijui kama ile mitambo mpaka leo imetumika na kama imetumika imetumika wapi? Kwa hiyo, ina maana nchi yetu tunaweza kuweka mikakati mizuri lakini utekelezaji ukawa mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia nchi zetu za Kiafrika, Afrika nzima ni kubwa inafikia ukubwa ukiunganisha Marekani, China pamoja na Europe lakini leo tunakwenda China kuomba misaada kwa nini, lazima tujiulize kwamba mipango yetu tunayoipanga siyo mizuri na kama Kilimo ndio tunategemea kitutoe basi lazima kipate *priority* na kiwe *well planned* ili tujue kwamba kweli tunaweza kutoka katika umaskini huu. Kwa hiyo, ninachoona ni kwamba Wizara zetu hazina mawasiliano. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti wa PCE ahsante sana. Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray atafuatiwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi uliyonipatia niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Kilimo kuwasemea waajiri wangu hususan wakulima na wananchi wetu wa Mkoa wa Manyara na pia nichukua nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa kazi kubwa inayofanya kupigania hii Wizara ya Kilimo, nimpongeze sana Waziri na Naibu Waziri wake kwa kazi kubwa waliyoifanya na kusaidia hasa Mkoa wetu wa Manyara kipindi ambacho tulikuwa tumepata janga la kuvamiwa na nzige kwa kweli

walifanya kazi kubwa sana hawakulala walihakikisha wamelitatua jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba Wizara hii ya Kilimo inatakiwa sasa iweke jitihada za pekee kuhakikisha kilimo kinamkomboa mwananchi ambaye anayejishughulisha na kilimo. Mkoa wetu wa Manyara ni Mkoa uliobarikiwa sana ni Mkoa ambao una ardhi nzuri sana lakini ni Mkoa ambao unajishughulisha na kilimo cha mazao ya aina yote yanayolimwa Tanzania hii.

Mheshimiwa Spika, lakini kulingana na changamoto inayoikumba hii sekta ya Kilimo wananchi wetu wengi wamekata tamaa na hasa kazi hii ya Kilimo, ikiwepo baadhi ya mazao sasa hivi katika Mkoa wetu watu wengi wameacha kushughulika nayo kwa maana ya kwamba wanakosa vitendea kazi wanakosa pembejeo ikiwepo mbegu na mbolea. Mbegu na mbolea katika Mkoa wetu wa Manyara vinachelewa sana kufika kwa muda muafaka wa wakulima.

Mheshimiwa Spika, hii imesababisha wananchi wetu wameacha sasa hivi kujishughulisha na Kilimo cha Ngano, wameacha kujishughulisha na Kilimo cha Pareto wamekatishwa tamaa kabisa na kujishughulisha hata na kilimo cha vitunguu saumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata mbolea zinapofika au mbegu zinapofika katika maeneo yetu upatikanaji wake ni mgumu lakini pia gharama ni kubwa ukilinganisha na hali halisi ya wakulima wetu. Sasa hivi ukiangalia wananchi wetu wanaojishughulisha hata na Kilimo cha ngano wanaojishughulisha na Kilimo cha Pareto Kilimo cha vitunguu saumu wale wachache waliobaki wanalima kilimo ambacho hakiendani hasa na hali halisi au kilimo kinachowaletea tija wananchi hawa wameendelea kutumia mbegu ambayo haistahili kabisa mwisho wa siku wanafanya kazi kubwa na matokeo ni madogo mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi hawa wanalima wanatumia nguvu kubwa sana wanatumia gharama kubwa

sana lakini hawanufaiki na Kilimo hicho. Niende sambamba katika kuelezea katika suala zima la masoko tunasema jembe halimtupi mkulima kiukweli sasa hivi kilimo kimekuwa ni kilio kikubwa sana kwa wananchi wetu, wananchi wetu wanatumia gharama kubwa sana katika kulima lakini wanapofika katika suala la masoko kiukweli mazao yao yananunuliwa kwa gharama ndogo mno kitu ambacho kinawakatisha tamaa kuendelea kufanya kazi ya kilimo lakini pia kuendelea kumdidimiza na kumgandamiza huyu mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna watu wanaitwa madalali hawa watu wanafika kwenye maeneo yetu kule mashambani wananunua mazao yakiwa mashambani, mkulima kwa sababu hana uhakika wa masoko anaamua kuuza kwa gharama ndogo sana na wanaofaidika ni wale madalali ambao wakishafanikiwa kununua kutoka kwa mkulima wanaenda kuuza kwa gharama kubwa kwa hiyo faida kubwa inakwenda kule kwa madalali. Sasa ni muda muafaka Wizara hii kuwahakikishia wakulima masoko yenye uhakika ili kama kweli tuna nia ya dhati kabisa kumkomboa mkulima, tuna nia ya dhati kabisa kufanya wananchi wetu na Watanzania na vijana wetu wafurahie kilimo ni kuwapatia soko la uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni namna gani sasa Wizara imejipanga kuangalia masoko ya uhakika ukizingatia kwamba katika ndani ya Afrika tuna masoko mengi ukiangalia kama nchi ya Congo, Zimbabwe.

Je, Wizara imejiandaaje sasa kutafuta masoko nje ili wananchi wetu wanapofika ule muda wakishavuna mazao yao waweze kupata soko la uhakika na kuuza mazao yao ili waweze kupata faida. Sambamba na hilo imeongelewa sana kuhusu kuamini kwamba tukitegemea mvua katika kilimo imekuwa sio njia sahihi na yenye uhakika kwanini sasa Wizara isione tuwekeze nguvu kubwa katika kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Regina.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi uliyonipa.

**SPIKA:** Ahasante muda haupo upande wetu. Mheshimiwa...

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Spika, naunga Mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jinamtemi.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata nafasi kuzungumza lakini afya yangu sio nzuri nitazungumza kwa shida, Jimbo langu la Same Mashariki asilimia 99 mfano, wote ni wakulima kwa hiyo wao bajeti yote wanasikiliza Wizara ya Kilimo. Ninamshukuru Mheshimiwa Waziri ninamshukuru Naibu Waziri wote ni wachapakazi ninafahamu, lakini ninaomba niwaambie tatizo langu kubwa, Jimbo la Same Mashariki lina tarafa tatu na katika tarafa tatu tarafa mbili zinalima tangawizi tarafa moja inalima mpunga.

Mheshimiwa Spika, wamelima haya mazao kwa muda mrefu na hayo mazao ndio yanayowafanya nao waishi. Tatizo ambalo liko Same Mashariki ni kwamba kuna tatizo kubwa la miundombinu ya kilimo, miundombinu ya kilimo imekuwa imechakaa sana nikisema hivyo nina maana hawa wanaolima mpunga wanategemea *scheme* ya kulimia ule mpunga *scheme* ile imechoka na niseme kweli hili jambo ya *scheme* yangu ya Kata ya Ndungu nimeliungumza sana na Naibu Waziri na Naibu Waziri nakiri kwamba umeanza kulifanyia kazi nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, lakini tarafa mbili Tarafa ya Gonja na Tarafa ya Mambavuna wananchi wangu wanalima sana tangawizi, na ninaomba niseme kweli katika Tanzania nzima Jimbo la Same Mashariki ndilo Jimbo pekee ambalo wananchi wanalima tangaziwi mno, sasa Mheshimiwa Waziri Jimbo ambalo wananchi ndio asilimia kubwa wanalima tangawizi na wanajitahidi sana. Ninaomba tukimaliza bajeti,

ili Bunge la Bajeti Waziri twende wote tukaone hao wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, alikuja Rais Kikwete kwenye Kata ya Miamba ambayo Mheshimiwa Mbuge wa Peramiho umekuja juzi alikuja Rais Kikwete mwaka 2014 nikasimama jukwaani nikamlalamikia kwamba Mheshimiwa Rais wananchi hawa wanalima tangawizi vizuri wanashirikiana na Mbunge na tumejengwa na kiwanda cha Tangawizi, miundombinu imekufa nikiri na nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Kikwete alitoa shilingi milioni 800 akanipa kusaidia ile miundombinu ya kilimo cha tangawizi hiyo ilikuwa ni Awamu ya Nne, Awamu ya Tano, sikuwa Mbunge kwa hiyo sijui nina uhakika aliyekuwa Mbunge hakuzitafuta fedha kwa hiyo wananchi hawakupata zile fedha, sasa hii ni Awamu ya Sita… *(Makofi)*

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka.

**TAARIFA**

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, msemaji anaposema sikutatufa fedha wakati alikuwa anasema kiwanda kinafanya kazi ningetafuta fedha ya nini lakini ajue kwamba *PSSSF* walileta mashine mpya, kiwanda kilichokuwepo kilikuwa ni bomu.

**SPIKA:** Unapokea taarifa hiyo Mheshimiwa Anne Kilango.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, sipokei huyu mama amechanganyikiwa ninaongelea Kilimo, naongea kilimo cha tangawizi siongei kiwanda amechanganyikiwa naendelea Mheshimiwa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ninachoomba sasa ninakwenda kwenye kazi sizungumzi mambo hayo nakwenda kwenye kazi.

Ninaiomba Serikali ya Awamu ya Sita, Serikali ya Awamu ya Nne iliona tatizo la miundombinu Rais akanipa shilingi milioni 800 na aliponipa alisema Mheshimiwa Anne Kilango jitahidi sana kila awamu ikupe fedha za miundombinu Awamu ya Tano sikuwepo Serikali haikutoa. Awamu ya Sita sasa ninaomba kwa unyenyekevu mkubwa Mheshimiwa Waziri tukimaliza Bunge hili ninafunga mizigo yangu ninakuja kukuchukua kwako, twende ukaona hayo matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matatizo ya wananchi wangu ni matatizo yangu mimi, wao wamenituma nije niwasemee mimi sikuja hapa kucheza niwasemee wananchi wangu na leo nimekuambia tangu jana ninaumwa lakini nimekuja ili niwasemehe wananchi wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakuomba Mheshimiwa Waziri Tarafa ya Bonja na Tarafa ya Mambavunda twende mimi na wewe ,tarafa ya Ndungu nitakwenda na Naibu Waziri naomba niseme ninaunga mkono hoja kwa sababu ninajua Mheshimiwa Waziri tutakwenda ninaunga mkono hoja tena sina mahali ninapoleta vuruga na wewe ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mheshimiwa Yustina, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwantumu Mzamili Zodo.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kunikumbuka na kunipa nafasi ya kuchangia sekta hii nyeti ya kilimo, ungetoa nafasi kwa kila Mbunge hapa angekuwa na jambo la kusema kuhusu sekta hii nyeti sana inayogusa maisha ya Watanzania na ni kwa sababu aidha kila mmoja hapa alikuwa na kura yake moja ya mkulima au mfugaji, na huenda karibu Wabunge wengi hapa ni wakulima.

Mheshimiwa Spika, sekta hii ya Kilimo inagusa maisha ya Watanzania wengi kwa asilimia zaidi ya 60 tukiongelea asilimia 65 hii ni kwa sababu ya wastani wa vijijini na miljini.

Mheshimiwa Spika, lakini ukienda kwenye Majimbo ya vijijini huko asilimia zaidi ya 90 ni wakulima lakini ndio sekta iliyokumbwa na changamoto nyingi tu ukiangalia katika hatua zote za mnyororo wa thamani katika sekta hii ya kilimo kwanza uzalishaji una changamoto nyingi kwasababu kuna uzalishaji mdogo kwa hekari, ukisogea kwenye usindikaji kuna changamoto ukienda kwenye masoko kuna changamoto kibao.

Mheshimiwa Spika, hatujaweza kuwekeza vya kutosha katika sekta ya kilimo ili kumtoa mkulima huyu katika hatua aliyonayo kumsogeza katika mapinduzi na kumtoa katika umaskini kwa sababu changamoto hizi zote zina dawa. Tunaongelea habari ya mbegu lakini kuna dawa, inatakiwa tutoe fedha katika mafiga matatu ya kuweza kutuletea mbegu bora wakiwepo *TOSCI, TARI* na *ASA* ili wakulima hawa wapate mbegu bora wanazozihitaji.

Mheshimiwa Spika, watu wanaongelea kuhusu habari ya alizeti, mbegu zinazotolewa na ASA ya *record* huwezi kufananisha na mbegu ya *hybrid* ambayo inauzwa bei ya juu takriban Sh.35,000 kwa kilo kwa sababu mbegu zinazotakiwa na wakulima ni mbegu bora na chotara. Ni kwa nini sasa tusitatue changamoto hii ya kutokuwa na mbegu bora wakati tuna fursa nyingi na za kutosha?

Mheshimiwa Spika, katika uzalishaji mdogo mimi naenda kugusa zao la ngano. Tabia ya ulaji ya Watanzania sasa imebadilika na kwamba ngano ni kati ya mazao muhimu ya chakula. Ngano sasa ni zao namba nne ikifuatiwa na mahindi, mihogo na mchele. Ukitaka kuhakikisha kwamba ngano utaona Tanzania sasa *bakeries* nyingi zimefunguliwa kila mtaa na ukienda kwenye vioski vya vijijini wanauza mikate na maandazi.

Mheshimiwa Spika, lakini inasikitisha sana kwamba Watanzania ngano tunayokula siyo ya kwetu, tunaingiza ngano kwa dola nyingi za Marekani. Sisi tunatafuta *foreign currency* kwa ajili ya kununua vitu vingine lakini kumbe

tunaagiza chakula. Hii haikubaliki kabisa. Watanzania kwenye miaka ya 70 hadi 80 *we were good producer of wheat*...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Longido unakata katikati ya mwongeaji na Spika, endelea Mheshimiwa.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunilinda. Naendelea kuelezea masikitiko yangu kwamba kwa kweli si sahihi na haikubaliki kwa Watanzania kuingiza ngano kwa fedha za kigeni kwa sababu tulikuwa na mashamba makubwa....

**TAARIFA**

**SPIKA:** Taarifa, nimekuona Mheshimiwa Asia.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, napenda tu kumpa taarifa mchangia hoja kwamba hata Wilaya ya Hanang ambapo ndiyo sehemu kubwa ya kilimo hiki cha ngano tunaiomba Wizara ije kuona kwa sababu mashamba mengine yamepewa wawekezaji lakini wawekezaji wale wanalima kiwango kidogo sana na eneo kubwa linabaki kuwa pori.

Mheshimiwa Spika, hata Serikali yenyewe ina eneo la ekari 12,000 ambapo halmashauri imechukua eneo dogo kwa ajili ya kukodisha wananchi lakini eneo lingine Serikali imeliacha limekuwa pori. Sasa tuombe kwa sababu Serikali ilishaamua kukikuza kilimo hiki cha ngano na kukifanya kuwa cha biashara basi waje wawekeze kweli kweli kuanzia kwenye mashamba ya wawekezaji lakini hata kwenye mashamba yenyewe ya Serikali. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Taarifa hiyo Mheshimiwa Yustina unaipokea?

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana mdogo wangu Asia, naipokea taarifa yake kwa mikono miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna historia kwa mfano kama alivyotoa mfano mdogo wangu Hanang tukishirikiana na Canada miaka hiyo yale mashamba yote sasa hivi yamegawanywa kwa wafugaji, wakulima wadogo wadogo na *private sector* wame-*fragment* mashamba yale makubwa katika vipisi vidogo vidogo hatuwezi tena kulima ngano. Kilimo cha ngano ni lazima kifanyike katika mashamba makubwa kwa sababu kilimo hiki ni *mechanical agriculture* kwa sababu ngano utapanda kwa *planter,* utapalilia kwa mashine na utakuja kuvuna kwa *combine harvester,* hatuwezi kuachia wakulima wadogo wadogo. Mashamba ya *NAFCO* yale wamechukua wawekezaji, yamekuwa *privatized* katika sekta binafsi na hatukuwapa *incentive* kwa sababu ngano ilikosa bei. Naishauri Wizara ije na mpango kwamba sasa hatutaendelea kulishwa ngano na nchi za nje na kwamba tutaokoa hela hizo za kigeni zinazoenda kununua ngano na kwamba mpaka miaka mitatu kuanzia leo tutakuwa tumejitosheleza kwa soko la ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mwingine unaenda kwenye upotevu wa mazao baada ya mavuno. Ni kweli kabisa tumeacha wakulima hawa wakihangaika. Nashukuru Wizara na naipongeza kwamba imekuja na teknolojia ya kutumia vifungashio ambavyo haviingizi hewa *(hermetic)*. Kuna *serial* za chuma, *plastics* lakini na mifuko hii ya *PICS*. Hii ni namna pekee ambayo wakulima hata sisi walaji wa chakula tutakuwa salama.

Mheshimiwa Spika, baada ya wakulima hawa kutumia viatilifu vingi vya unga mara nyingi wanakuta mahindi yao yamepekechwa na kwa ajili hiyo wanachanganya madawa mengi kina *Actel*, Duduba, unawakuta mahindi yako mazima sokoni kumbe tunaenda kula sumu. Kwa ajili hiyo hii mifuko ya *PICS* na vifungashio vingine ambavyo sasa vinauzwa ghali, *serial* ya chuma ya kuweka magunia matano inaenda mpaka laki na kitu, mifuko hii inauzwa Sh.5000, tunaomba sasa Serikali ifanye namna yoyote ya kuweza ku-*subsidies* ili angalau mifuko hii basi wakulima wapate kwa Sh.2,500 hadi Sh.3,000 waachane na kutumia viatilifu hivi ambavyo vina kemikali nyingi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Yustina Rahhi. Mheshimwa Mwantumu Mzamili Zodo atafuatiwa na Mheshimiwa Seif Hamis Gulamali.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia kwenye Wizara hii nyeti ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, wakati wa bajeti ya Wizara ya Elimu nilitoa mchango kuhusu ajira. Serikali yetu imekuwa na changamoto kubwa ya ajira hata Waziri wa TAMISEMI asubuhi alilithibitisha hilo. Kati ya nafasi za walimu 6,000 zilizotangazwa mpaka sasa watu 89,000 wameomba ajira hizo, kwa hiyo, tunaweza tukapata picha hapo.

Mheshimiwa Spika, mbadala wa hilo ambalo litaenda kutatua changamoto hiyo ya ajira kwa vijana wetu na Watanzania ni kupitia sekta hii ya kilimo. Hata hivyo, mkazo kwenye sekta hii ya kilimo ni mdogo mno na Watanzania wengi tunalima bila tija, tija yetu ni ndogo sana kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri tu, mimi natokea Mkoa wa Tanga, miaka miwili, mitatu iliyopita tulihamasishwa sana kulima mihogo na wewe mwenyewe nafikiri utakuwa ni shahidi, tukaambiwa kuna Wachina wanakuja kununua mihogo lakini watajenga viwanda vikubwa. Niko na jirani yangu hapa Mzee Mwijage nafikiri alikuwepo wakati huo Mzee wa Viwanda na yeye atakuwa ni shahidi na watu walihamasika sana walikwenda kuchukua mikopo mikubwa sana kwenye mabenki. Ilikuwa ukifika pale kwa Msisi Wilayani Handeni, kuna mashamba ambayo labda uzunguke kwa

bodaboda au upande juu ya mlima ndiyo hilo shamba lote unaweza kuliona.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwantumu, Kanuni zetu zinaruhusu kumuuliza Mbunge swali. Kwa hiyo, unaweza kumuuliza Mheshimiwa Mwijage vile viwanda ulivyoahidi viko wapi na mimi kwa kweli nitatoa nafasi ajibu. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nitafanya hivyo .

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa Mwantumu.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Spika, nachotaka kusema baada ya yale maagizo na sisi viongozi kuhamasisha wananchi hakuna kiwanda hata kimoja kimejengwa na hata wanunuzi wenyewe hawapo. Watu wale wamechukua mikopo mikubwa mabenki na mpaka sasa hivi watu wengine wana presha. Kwa hiyo, niiombe Wizara tuwe tuna taarifa za kutosha, tukisema tunapeleka viwanda na kuhamasisha wananchi kweli viwanda vije.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo sasa hivi tumeibua tena zao lingine la kimkakati, zao la mkonge kwa Mkoa wa Tanga. Namshukuru sana Waziri Mkuu ameshakuja karibu mara tatu na ukisoma mikakati ya Serikali wana mikakati mizuri sana. Kuna Bodi ya Mkonge pale na nafikiri Mkurugenzi wa Bodi ya Mkonge toka jana yuko hapa, anafanya kazi nzuri sana. Waziri Mkuu aliagiza wakati wa ziara yake kwanza yale mashamba matano yagawanywe na wale watu wa Bodi ya Mkonge waanze kugawanya yale mashamba kwa wale wananchi ambao wanaishi kwenye maeneo yale na baadaye ndiyo wajaribu kuangalia watu wengine. Kweli Bodi ya Mkonge inafanya hivyo wameanza kugawa kwa shamba lile la Hale, Mwelia, Magoma, Mgombezi na mashamba mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sasa watendaji wetu wa Serikali, huku juu mipango ni mizuri sana lakini sisi tuko kule chini tuna *deal* sana na watu wa kule chini wa ngazi za

mashina, matawi, huku chini hakuna taarifa kabisa yaani ukiacha wale wananchi wanaoishi kuzunguka mashamba yale ya mikonge, wale ambao hawaishi kwenye yale mashamba ya mikonge hawana taarifa kabisa. Wanakwambia tunasikia mkonge unalipa, tunasikia sasa hivi mkonge hekta moja ni shilingi 3,600,000, kwa hiyo na wao wenyewe wanasikia. Wakati hapo kuna Afisa Kilimo Mkoa ameajiriwa, kuna Afisa Kilimo Wilaya yuko pale kaajiriwa na anafanya kazi, kuna Maafisa Ugani japokuwa ni wachache lakini wapo, huyu Mkurugenzi peke yake wa Bodi ya Mkonge kama hatasaidiwa na hawa watendaji wengine wa Serikali hataweza kufanya kazi hiyo mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sasa Wizara iwaelekeze watendaji wao kushuka chini kwenye mikutano ya vijiji, mikutano ya kata na hata kwenye mikutano ya Majimbo; Wabunge wanajitahidi sana mara nyingi kuzungumzia suala hili, lakini watendaji wale wa Serikali hawazunguki kutoa hamasa. Wala huwezi ukajua kama kuna Afisa Ugani pale kwenye ngazi ya kata na hata ukimuuliza mwananchi hamjui kabisa. Wale watu wapo tu hawatoi elimu, kilimo kinaporomoka lakini wameajiriwa wanalipwa mishahara. Kwa hiyo, niiombe Wizara isimamie watu wake ili kuleta tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapo hapo kwenye kilimo niipongeze Wizara ya Kilimo nimeona kilimo kinaendelea kukua. Kwa mfano, mwaka 2019 kimekuwa kwa 4.4% na 2021 ukuaji wa kilimo ni 4.9%. Pia kwenye ajira kinaendelea kutoa ajira kutoka kwenye 58.1% mwaka 2019 mpaka 65%.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja lakini naomba Wizara sasa ihakikishe inafanya kazi kweli kweli kuleta tija kwani kwenye kilimo tija bado ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwantumu Mzamili Zodo kwa hoja zako. Ungemtolea hoja hapo Mheshimiwa Mwijage ningemsimamisha lakini sasa hukutoa. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Seif Hamis Gulamali atafuatia Mheshimiwa Josephat Kandege.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye hii Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, nianze na dodoso tulilopewa. Kila Mbunge amepewa dodoso hapa la kujaza skimu za umwagiliaji kwenye eneo lake, hekari lakini mwisho wa siku hili dodoso tunalipeleka wapi maana bajeti imeshapita. Kama ni skimu za umwagiliaji wanazo humo ndani, hii tunapewa kwa faida gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, skimu ambazo ninazo, ninazo Skimu za Utuja, Simbo, Nyandekwa, Ndembezi, Mwashiku, Choma na Buhekela zote Wizara wanazo. Leo wananiambia niandike zingine nazitolea wapi? Hata hizo walizonazo hawajatupa hela hata shilingi moja; siyo ya kutengeneza, kuboresha wala kujenga, hata bwawa hakuna. Dodoso hili ni kwa ajili ya mwaka ujao? Dodoso hili tulipaswa tupewe mwezi wa tatu, mwezi wa nne...

**TAARIFA**

**SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na mchangiaji anayeendelea kuzungumza Mbunge wa Manonga, Mheshimiwa Seif Gulamali kwamba huo ni ushahidi wa namna ambavyo kilimo chetu kinachezewa. Huwezi kuleta dodoso katikati ya bajeti unategemea watu watoe *input* uende ukafanye kazi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Unapokea taarifa hiyo Mheshimiwa Seif?

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, ni sahihi kabisa. Mimi nilitarajia humu tungeambiwa sehemu fulani angalia tunarekebisha labda tumekosea kwenye bajeti hebu hakikisha, hamna kuhakikisha, hili nilitakiwa nipewe mwezi wa tatu nijaze ili wakathibitishe. Sasa leo hakuna fedha na hapa kwenye bajeti hii sijaona ujenzi wa skimu yoyote na mimi nina mabonde makubwa na tunalima mpunga kwa wingi. Hapa sikubaliani na dodoso hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine, ninayo mawili tu, nina kiwanda kile kinachotengeneza mbolea cha Minjingu. Mheshimiwa Waziri Mkuu tumemuona akienda Minjingu akituambia tutumie mbolea ya Minjingu. Waziri aliyepita na wa sasa hivi Minjingu lakini mbolea zinaagizwa nje ya nchi. Sasa tunaboreshaje viwanda vyetu vya ndani wakati nyie mnaagiza mbolea nje ya nchi? Hapa hatuelewani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Minjingu mbolea yao wananunua Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Malawi sisi Tanzania tunafanya tafiti ya mbolea miaka mitano sasa. Tuna upungufu wa mbolea mahitaji tani laki tano Minjingu wanazalisha labda tani laki moja Wizara mmeshindwa kuchukua Minjingu tani zote laki moja halafu tani zingine laki nne mkawaambia wakaagiza nje ya nchi, mnaagiza zote nje ya nchi tani laki tano? Hapo hatuwezi kuelewana. Kama tunahitaji kulinda viwanda vya ndani, mnasema wenyewe watu wawekeze viwanda vya ndani anawekezaje wakati soko hana, soko lake nje ya nchi, haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri akija ku-*wind up* hapa atuambie ni jinsi gani watalinda viwanda vya ndani kwa maana ya wote wanaozalisha lakini pia ....

**T A A R I F A**

**SPIKA:** Mwenye taarifa endelea nimekuruhusu.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, naomba kumuuliza mchangiaji kwamba ile mbolea ya Minjingu ikiwekwa katika ardhi ya Tanzania itageuka kuwa sumu? Ahsante. *(Kicheko)*

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo naipokea kwamba tunataka mbolea ile itumike hapa ndani, haiwezekani nchi nyingine watumie sisi kwetu tunaendelea kufanya tafiti. Hivi tukichukua hii Minjingu ...

**T A A R I F A**

**SPIKA:** Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Soko kubwa la Minjingu liko kwenye nchi zinazotuzunguka kama Kenya, Burundi na Uganda. Nampa tu taarifa kwamba baada ya kuona mbolea ya Minjingu inafanya vizuri sana kule Burundi kwa wale wateja aliokuwa anawapelekea, sasa ameamua kuja kuwekeza hapa Dodoma ili aendelee kuiua vizuri hii Minjingu, ni vizuri Waziri ajipange kwa majibu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa Seif

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, taarifa naipokea. tunazungumza hivi kwa kulinda viwanda vyetu vya ndani, tunalindaje viwanda wakati hatulindi viwanda vinavyozalisha mbolea ambayo tunaweza tukatumia sisi wenyewe? Niwaombe Wizara wakati wanakuja kujibu watuhakikishie soko la viwanda vya mbolea vilivyoko ndani halafu inapopungua ile *gap* ndiyo vitolewe vibali vya kununua nje ya Tanzania siyo unatoa vibali kwa ajili ya kununua mbolea yote nje ya nchi halafu iliyopo hapa ndani iende wapi?

Mheshimiwa Spika, kiti chako pia kitoe mwongozo kwenye suala hili kwani hatuwezi kwenda kwa stahili hii *otherwise* viwanda vingi vitakufa kwa utaratibu huu. Kama Kiwanda cha Minjingu kinaweza kutendewa hivi, je, viwanda

vingapi vinaweza vikafanyiwa hivi? Kwa hiyo, tuombe kama kuna Wizara nyingine tofauti na Wizara hii inafanya utaratibu kama huu wa Wizara ya Kilimo tuuangalie tubadilishe. Ni lazima tulinde viwanda vyetu vya ndani.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali. Mheshimiwa Josephat Kandege atafuatiwa na Dkt. Thea Medard Ntara.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili na mimi niwe miongoni mwa Waheshimiwa Wabunge waliochangia katika bajeti ya Wizara hii ambayo ni Wizara muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri. Baada ya kumaliza kuwapongeza niendelee kuwapa pole, nawapa pole kwa sababu gani? Kilimo ni suala la kuwekeza kwa maana ya bajeti uone kwamba inaongezeka kwenda kwenye kilimo lakini kwa takwimu nilizonazo kwa mwaka 2018/2019, 0.5% ya bajeti ndiyo ilienda kwenye kilimo; mwaka 2019/2020 asilimia 0.63 pekee ndiyo ilienda kwenye kilimo; mwaka 2020/2021 ni asilimia 0.58 ya bajeti ndiyo ilienda kwenye kilimo na mwaka huu wa 2021/2022 ni asilimia 0.8 chini ya asilimia moja ndiyo inaenda kwenye kilimo. Tafsiri yake ni nini? Kama zaidi ya 65% ya Watanzania na 70% wakiwepo wanawake wanajishughulisha na shughuli za kilimo, lakini katika kutenga bajeti unaweka asilimia 0.8 tafsiri yake ni kwamba *we are not serious*. Kama tunataka kufanya *transformation* kuhakikisha kwamba Watanzania walio wengi wanaondoka katika lindi la umaskini ni kuweka fedha za kutosha kwenye sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu umefanya utaratibu mzuri naomba Waheshimiwa Wabunge katika hili tusimame pamoja. Kama tunataka yafanyike mapinduzi ya uhakika ni kuhakikisha kwamba Wizara ya Kilimo inaenda kuongezewa

bajeti. Na katika utaratibu ambao umeuweka kwa makusudi hizi Wizara zingine pamoja na kwamba bajeti zao zimepita, tuungane Waheshimiwa Wabunge kuhakikisha kwamba Wizara ya Kilimo inaenda kuongezewa pesa ili tuweze kufanya mapinduzi na kuwasaidia Watanzania. Kwa hiyo, haijalishi bajeti ipi imepita kwa sababu bajeti ya mwisho ni bajeti kuu na sisi kama Wabunge tuna uwezo kabisa wa kuhakikisha Wizara hii inaongezewa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo linazidi kushangaza na kusikitisha, sisi Mkoa wa Rukwa ni miongoni mwa mikao mitano ambayo ni *big five* katika uzalishaji lakini kichekesho chake kinakujaje, katika ambao wapo miongoni mwa *big five,* ndiyo mkoa ambao unaongoza katika lindi la umaskini. Tafsiri yake ni kwamba hiki ambacho mwananchi anazalisha kinakosa thamani, unazalisha mahindi lakini kama huwezi kuyauza maana yake huna uwezo wa kwenda ku-*transact* na kuweza kupata fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali kwa ujumla wake katika hali hii ambayo wananchi wapo kwenye lindi la umaskini na huku wamezalisha wanatizama hicho ambacho umetoa jasho na damu yao hakina thamani, Serikali ije na majibu. Wanaenda kuchukua hatua gani ya makusudi kuhakikisha kwamba wananchi hawa ambao wanafanyakazi kwa bidii lakini wanaendelea kuwa maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimuombe Mheshimiwa Waziri na timu yake, tumelima mahindi miaka nenda rudi lakini tunazidi kuwa maskini. Naomba Serikali itujie na mazao mbadala, sasa hivi Serikali tulipata kota kwa ajili ya kupeleka *soya beans* China lakini niambieni wapi soya inapatikana na sisi kwa Mkoa wa Rukwa ardhi hiyo inafaa kabisa kwa kilimo hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ni vizuri Waziri ukatujia na majibu, unaenda kusaidiaje ili tuachane na habari ya kilimo cha mahindi ambacho kinatupa umaskini twende kwenye mazao ya soya, tukalime ngano ili na sisi tuondoke katika

kundi la maskini na hiyo itakuwa imetusaidia. Vinginevyo tutakuwa tunalima, tunafanya kazi lakini tija haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miaka ya nyuma kidogo nchi ya Zambia ilikuwa kila mwaka wanategemea tulishe sisi Watanzania tuwalishe Wazambia lakini leo imebadilika *yield per acre* Wazambia kwa mahindi wanazalisha gunia 35, sisi Watanzania gunia 8 au 10, hatuwezi kufika. Pamoja na kuzalisha hizo 8 na 10 hata soko mwananchi hana la uhakika. Kama tunakubaliana sisi sote kwamba zaidi ya asilimia 65 au 70 wakiwemo wanawake lazima Wizara hii kwanza tuhakikishe kwamba bajeti inaongezeka ambayo ita-*reflect* uhalisia. Hii bajeti ambayo inakuwa chini ya asilimia moja hakika tutakuwa hatuwezi kufanya *transformation* ambayo inatakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa sababu naamini Wizara watakuja na majawabu ya uhakika badala ya majibu, naomba niunge mkono hoja, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Josephat Kandege, sasa hivi wabunge mmezidi kuwa mahiri katika kutumia dakika tano, mnazitumia vizuri sana hongereni sana. Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara atafuatiwa na Mheshimiwa Godwin Kunambi.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, niungane na wenzangu wasemaji waliopita kama Mheshimiwa Mpina aliongea jana na Mheshimiwa Aida na huyu wa leo kwamba inabidi bajeti ya kilimo iongezeke na tufuate kabisa ile *Maputo Declaration* ambayo ilizitaka nchi za Afrika zitumie angalau asilimia 10 ielekezwe kwenye kilimo. Sasa ikielekezwa huko kwenye kilimo fungu hili likiongezeka Wizara itaweza kukuza kilimo lakini pia itaweza kupata mbegu bora kupitia *seed science and research.* Bila hivyo tutaendelea kununua mbegu nje, kulima karanga Dodoma halafu mnasema hazioti; hili tatizo ni kwamba fedha Wizara ya Kilimo hazitoshi.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha atafute fedha ndiyo kazi yake, atafute fedha na zikipatikana ndiyo tunaweza kufanya vitu katika hii Wizara ya Kilimo. Haya mambo ya kuchukua mbegu kutoka nje au kutegemea nje maana yake ni kweli hatuna wanasayansi. Kuna Profesa anaitwa Susanne Nchimbi alitengeneza mbegu nzuri sana za maharage pale *SIA* na zikasambaa Tanzania. Kwa nini tusitumie hao wanasayansi wetu ili tupate mbegu ambazo hazitaleta utata zinavyooteshwa sehemu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia ni wakati sasa wa ku-*intensify*, kukuza na kupanua kitu kinachoitwa *commercial farming;* tusipokuwa na *commercial farming* hatuwezi kufanya biashara za kilimo. Tukifanya *commercial farming* ina maana kwamba hata hawa vijana wetu tutafanikisha hata hicho tunachosema *irrigation schemes* lakini kutegemea hizi mvua za misimu bado hatutaweza kuwa ni nchi inayoweza kuzalisha kwa ajili ya kuuza. Tukifanya *commercial farming* ina maana tutakuwa na mazao bora lakini pia tutaweza kutoa mafunzo *(practical skills)* kwa wanafunzi wetu wanaotoka katika vyuo vya kilimo lakini pia wanaotoka katika vyuo vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii tunasema hakuna ajira lakini hao Watoto wakiweza kwenda kujifunza kwenye hizo *commercial farms* itatusaidia hata wao kutengeneza vikundi na Serikali ndiyo hapo itapeleka fedha kwa hivi vikundi. Tunaweza kuwa na hivi vikundi kwenye mikao yote 26; wengine wakawa na kikundi wanalima karanga, wengine maparachichi Njombe, kikundi kingine cha hawa vijana ambao ni wasomi watapewa mikopo waweze kulima mahindi Ruvuma na wengine michikichi huko sijui Kigoma. Kwa hiyo, tukifanya hivyo tunaweza tukaendelea, watafute fedha.

Mheshimiwa Spika, kama *World Bank* inaweza/ imejipanga kufanya *investment* kwenye nchi za Afrika, dola bilioni 150 na Tanzania kwanini tukose hizo fedha. Waziri wa Fedha akatafute fedha, *IFAD* wanatoa mikopo tena ya bei

nafuu, wakatafute fedha ili iongezwe kwenye Wizara ya Kilimo. Tukiendelea hiki kilimo cha kijungujiko hatufiki. Sasa hivi inatakiwa tuwe na mashamba makubwa ndiyo tutaweza kuwapa hao vijana mikopo waweze kufanya ukulima wa kisasa na wenye tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kusema nawashukuru Wizara wameleta wanunuzi wa zao la soya huko Ruvuma lakini Ruvuma wanalima ufuta pia na mikoa mingine. Watafute na wanunuzi sio wanunuzi hawa wa kusema ulete sijui stakabadhi ghalani, tunataka mtu akipeleka zao anapata pesa yake palepale, wakulima ndiyo wanapenda hivyo. Lakini haya mambo ya kusema unaleta zao kama yalivyokuwa kule mambo ya tumbaku ndiyo yanaleta shida, upigaji unakuwepo mwingi sana hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa kule Tabora najua shida ya *AMCOS,* mtu akitoka kule ameiba hela ya wakulima anatoka pale ana pesa nyingi halafu anaingia mara Diwani, mara Mbunge. Walikuwa wanawaibia wakulima fedha siwasemi hawa wakina Mheshimiwa Gulamali lakini ndiyo kilichokuwa kinatokea kule Tabora. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Unga hoja.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ashante sana Dkt. Thea, kumbe Wanyamwezi ndiyo ujanja wao ulikuwa huo, ahsante sana. *(Kicheko)*

Alikuwa anachangia Mheshimiwa Kandege kwamba kule Zambia wanapata mazao mengi kwa hekari nadhani ni kwa sababu ya *commercial farming* kwa sababu Wazambia wamekuwa wakulima wazuri tangu lini.

Kwa hiyo, unachokisema ni hichohicho tunakushukuru. Mheshimiwa Kunambi na utafuatiwa na Mheshimiwa Kenneth Nollo.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa fursa hii muhimu, nianze kwa kuipongeza Wizara.

Mheshimiwa Spika, wakati umenitaja nichangie nilikuwa naangalia viongozi wakuu wa hii Wizara. Nimetazama Waziri naona ni Profesa...

**SPIKA:** Waheshimiwa naomba tusikilizane.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** nimetazama pia nafahamu kaka yangu Bashe yeye ana Masters lakini namuona pia Katibu Mkuu yeye naye bila shaka ana *Masters* lakini pia kuna Prof. Siza.

Mheshimiwa Spika, *normally people they do not care about how much you know until you know about how much you care*. Naomba nirudie *normally people they do not care about how much you know until you know about how much you care. Telling people, you are a professor/Ph.D holder/ Masters' holder is nonsense if you don't deliver services to the society*. Kuwaeleza watu kwamba mimi ni profesa, daktari, nina *masters* kama hutoi huduma kwa jamii ni kazi bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, changamoto sio weledi, sina mashaka na weledi wa viongozi wa wizara hii ni mahiri kabisa kwa maana ya *knowledge.* Changamoto kubwa niliwahi kusema hapa na hii ni kwa Watanzania tulio wengi ni mambo matatu; la kwanza ni mtazamo *(mindset),* la pili ni *commitment* na ya tatu ni uzalendo basi, sio fedha. Tunazungumza *financing,* kwenye kilimo hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme neno moja, nchi za Ulaya karne ya 16 zilianza mapinduzi ya kilimo *(agrarian revolution)* ndiyo wakaenda kwenye viwanda, walivyotoka kwenye mapinduzi ya kilimo wakaenda kwenye mapinduzi ya viwanda karne ya 18. Na walifanikiwa tu baada ku-*engage private sector,* kazi ya Serikali tusi-*engage* pia na kwenye masuala... kazi moja tu nishauri Wizara tuandae

mashamba mazuri yaliyopimwa vizuri, tutafute *private sector* tuwaambie tunawakabidhi haya; ukienda Zambia wanafanya hivyo na nchi zote zilizofanikiwa kwenye kilimo wanafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, leo hii hata tukisema hapa bajeti ya Wizara ya Kilimo iongezwe kutoka asilimia 0.8 hiyo fedha unatoa wapi, haipo; turuhusu sekta binafsi. Kazi ya Wizara iwe ni namna ya usimamizi...

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Pokea taarifa Mheshimiwa Godwin

**T A A R I F A**

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwanza anachochangia ni sahihi sana na kimsingi sio kwamba tutafute *private investors* kwenye ishu ya kilimo, wapo vijana ambao wanafanya vizuri ambao hata Wizara ni mashahidi na watu wa *SUA* ni mashahidi. Vijana kama Malembo Farm ambao wanafanya *consultation*, RAYMAK wapo Miyuji tu hapa Dodoma ambapo pia Wabunge wanaweza kwenda pale kuona RAYMAK yupo pale anafanya *agribusiness*. Kwa hiyo, wapo vijana ambao wameshajitolea kufanya hiki na wanafanya mpaka *greenhouse*, wanafanya vitu vikubwa sana. Kwa hiyo, tunaweza tukaanza na hao kuwapa hata ruzuku waendelee kufanya shughuli zao, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Unaipokea hiyo taarifa Mheshimiwa.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, nadhani anaendelea kuniunga mkono.

Mheshimiwa Spika, niendelee kusema tu kwamba lakini pia *financing agriculture,* tutafute benki ambazo zisikae Dar es Salaam, Dodoma wala zisikae mijini ziende kwenye maeneo ya kilimo. Yaani mkulima anaweza kukopa benki iwe kwenye Kata yake. Leo hii ukimwambia mkulima kuna

benki zinazo-*finance* kilimo hawajui, hawajui kabisa. Kwa hiyo, twende kwenye private sector kama nilivyosema awali tutenge maeneo maalu, lile shamba lipimwe liwe na hati mkulima anaweza kukopesheka. Kwa hiyo, Wizara hizi zishirikiane; Wizara ya Kilimo, Wizara ya Ardhi na Wizara ya Viwanda wafanye kazi kama timu moja. Naamini tunakwenda kufanya mapinduzi makubwa ya kilimo ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nijikite kwenye eneo hili la zao la mpunga; tumekuwa tukizungumzia mahindi. Duniani kote chakula kinacholiwa na watu walio wengi ni mchele kwa maana ya mpunga, sio mahindi, mahindi wakati mwingine Marekani wanakula Wanyama lakini mpunga/mchele wanakula wanadamu duniani kote, ukienda Japan wapi. Sasa zao la mpunga leo hii ukiuliza soko la mpunga na hii niiseme nisije nikasahau wakati Mheshimiwa Waziri unakwenda kuhitimisha bajeti yako nisaidie umejipangaje hasa kwenye soko la zao la mpunga. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jimbo langu nalima zao la mpunga kwa maana ya Mkoa wa Morogoro ukiondoa wenzetu wa Mbarali na Kyela, Jimbo la Mlimba tunashika nafasi ya tatu kwa kilimo cha zao la mpunga lakini wananchi wangu mpaka leo. Mwenyewe nimefungia gunia 70 ndani sina mteja. Sasa na mimi mkulima pia, nataka ni-*declare interest* hapa. Kwa hiyo, nimefunga mpunga wangu upo ndani sina mteja wa kuuza, Mbunge sina je wananchi wangu ikoje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, itoshe kusema tusijikite kwenye mahindi ambayo wakati mwingine yana *alternative*, mpunga hauna *alternative*. Kwa hiyo, tutafute masoko kwenye zao, hata maghala huwezi kuona ghala la mpunga; lipo ghala la zao la mpunga, hamna hata maghala tu. Kwa hiyo, zao hili ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, nirudi tu moja kwa moja nijikite kwa wananchi wangu wa Jimbo la Mlimba ambao wamenituma nifanye kazi hii. Pale Kata ya Mngeka kuna shamba la Serikali la hekta 5,000. Shamba hili hekta 3,000 tayari zina

miundombinu ya umwagiliaji lakini huu ni mwaka wa nne shamba lile Serikali imelitelekeza; leo tunasema *irrigation scheme* iko pale hatuitumii.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Wizara ya Fedha imeanza kuchukua hatua, kulikuwa kuna deni la NMB kuna mwekezaji uchwara alienda pale sijui akafanya nini akaondoka akaacha deni kama bilioni 10, jana Mheshimiwa Waziri wa Fedha amenipa matumaini amesema sasa wamechukua jitihada wanakwenda kulipa lile deni lakini changamoto hizi hekta 5,000 zinakwenda kufanya nini.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mlimba miaka ya 1985 wakati Hayati Baba wa Taifa amepata msaada wa nchi ya Korea ili nchi yetu ijikimu katika chakula, alipata msaada huo Wakorea wakaja wakajenga mitambo kila kitu hadi umeme tunafua pale wenyewe *megawatt* karibu 350 tunatoa pale ile mitambo iko pale kama *park elephant*.

Mheshimiwa Spika, sasa nikanasema namshukuru Waziri wa Fedha, akishalipa hilo deni la *NMB*, hizo bilioni 10 msimu ujao kama Serikali haijatuletea mwekezaji pale nitawaambia wananchi wangu tukalime, hatuwezi tukaacha maeneo yanakaa tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitachukua hatua tu, nitaenda kuhamasisha wananchi wa Mlimba, tukalime hizo hekta 5,000 nadhani tutasimamiwa na Halmashauri yetu ya Mlimba.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kumpa taarifa mzungumzaji, niko Kamati ya Nishati na Madini sijawahi kusikia kama Mlimba tuna megawatt 350, kilowatt au megawatt ili kumbukumbu zikae sawa.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, sipokei taarifa kwa sababu haihusiani na hoja ninayojenga hapa, naomba niendelee.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema nini? Nazungumzia suala la zima la namna gani tunaweza kufanya kilimo chetu kiwe na tija, kwa mfano, tunaeleza kwa Habari ya asilimia 65 ya wakulima, na kule ukienda kijijini wako wazee tu sisi vijana wote tuko mijini kwanini kilimo hakituvutii kwa sababu Serikali haijaweka mazingira Rafiki kwa vijana kupenda kilimo. *(Makofi)*

**MHE. ENG. AISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Na kwa bahati mbaya tunasema ajira, ajira!

**SPIKA:** Naona kuna taarifa nyingine tena endelea Mheshimiwa nimekuona.

**MHE. ENG. AISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji kwamba anachosema ni kitu sahihi kuna daktari mmoja nchini Afrika ambaye ameishauri Wizara husika ya kilimo katika nchi yake kwamba kilimo kinapaswa kufanywa kuwa *sexy* ili vijana wakivutie. Huwezi kuweka kitabu cha kilimo kina picha cha bibi mzee amechokaa kijijini *always* haiwezi kum-*attract* kijana kujiunga kwenye kilimo. *Let make the agricultural sector sexy to attract youth. (Makofi)*

**MHE. GODWNI E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa.

**SPIKA:** Unapokea taarifa hiyo Mheshimiwa Godwin?

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, naomba niseme jambo moja niliwahi kupata fursa ya kwenda *training* ya *quality* ya *infrastructure system* kule Japan Tokyo. Nilipofika kule walikuwa wakisema wa Japan wale,

wanaagiza chakula cha mwaka mzima kutoka nje ya nchi, ikiwemo nchi nyingi za Afrika, wanaitaja Zambia, wameitaja pia na Zimbabwe, *why not* Tanzania? *Why not* Tanzania hoja ndio kama hizi kwamba bado tuna changamoto kubwa hatujaweka mkazo mkubwa kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, itoshe tu kusema kwamba tukiweza kuongeza thamani kwenye mazao ya kilimo itatusaidia ku-*export* na faida kwenye uchumi uki-*export* sana halafu leo hii cha ajabu zaidi tuna ardhi ya kutosha, tuna yenye rutuba, lakini bado tunaagiza mazao yanayotokana na kilimo nje ya nchi kwa mfano suala la sukari, leo hii sukari unaagiza nchi ya nje kuliko Tanzania kweli?

Mheshimiwa Spika, mimi nataka kusema tu kwamba hasara tunayoipata Watanzania kwa kuagiza sukari na ngano, wachumi watanisaidia kwenye uchumi kuna *terminology* tunasema *capital flight* ambapo ni kitendo cha kukusanya fedha za ndani ya nchi kwenda kubadilisha na dola kununua bidhaa nje ya nchi. *Definitely,* tutapata *inflation* ambayo inasababishwa na *capital flight* lakini tukizalisha kwa wingi mazao ya kilimo tutakuwa na *balance of payment* na nchi yetu ita-*invest* na kuwekeza kwenye maendeleo mengine ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitisha bajeti ya Mheshimiwa Waziri naomba mambo mawili; jambo la kwanza anieleze ni lini skimu yangu ya umwangiliaji Udagaji inakwenda kuendelea, maana mpaka sasa imetelekezwa na shilingi milioni 30 imepelekwa pale.

Mheshimiwa Spika, jambo la la pili Mheshimiwa Waziri au kaka yangu Mheshimiwa Bashe Naibu Waziri, baada ya Bunge hili kwisha niwaombe twende wote Jimbo la Mlimba mkaone utajiri wa Jimbo lile kwenye kilimo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Godwin.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Ndiyo

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa naomba tu mwongozo na huu unjuka tulionao, baada ya mchangiaji kuongea kuna Mheshimiwa mmoja alikuwa amezungumzia kwamba tukifanye kilimo kiwe *sexy* kwa sababu tunaweka picha nzuri pale ya kuweza kum-*attract* hata vijana hawa waweze kulima.

Mheshimiwa Spika, lakini nachoelewa tu ni kwamba *old is gold,* sasa sijui tunaweka hapo katika nafasi gani? Nasema hivyo kwa sababu inaweza ikakaa picha pale siyo tu ya kijana lakini ikawa mama amependeza yuko *mashallah* halafu mambo ya kilimo yakawa yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo katika jambo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge alichosema alisema ukweli kwa sababu hiyo *argument* ya huyo mtaalam iko *YouTube*, yeye ana *argue* kilimo kiwe *sexy* siyo *sex. (Makofi)*

Anasema kwamba ma-*pamphlet* na *booklets* na kadhalika, zinazo-*promote* masuala la kilimo utakuta kwenye *cover* amewekwa bibi mzee, mtu aliyechokachoka, mtu aliyechakaachakaa na jembe la mkono, sasa vijana wakiona ile hawawezi kutamani kuwa kama yule.

Kwa hiyo, alikuwa ana-*argue* kwamba katika *promotion* za masuala ya kilimo wajitahidi sana wawe wanaweka vitu ambavyo vinavutia yaani kule kuvutia ndiyo kuwa *sexy*. Kwa hiyo, iko vizuri tu. *(Makofi/Kicheko)*

Ahsante, tunaendelea na Mheshimiwa Nollo atafuatiwa na Mheshimiwa Judith Kapinga.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, nami nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Wizara hii ya Kilimo ambayo ndiyo Wizara mama na ni tegemeo katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza mimi niseme kwa masikitiko makubwa matarajio niliyokuwa natarajia bajeti hii kutoka kwa Profesa Mkenda si kwa kiwango hiki ilivyokuja.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na matarajio makubwa sana, nilijua Wizara hii bajeti yake itakuwa na *transformation* lakini ukiiangalia na bajeti zilizopita *it is all most the same.* Sioni picha kubwa ambayo nilikuwa nayo ya Profesa Mkenda. Kwa kweli bajeti hii binafsi sijaridhika kutokana na nilivyokuwa na matarajio makubwa kutoka Profesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti hii kwenye miradi ya maendeleo imetengwa shilingi bilioni 150 ukiacha matumizi mengine. Hivi kweli kilimo cha nchi hii unakipangia bilioni 150 Tanzanian shillings, kwa kweli hatuendi mbele.

Mheshimiwa Spika, nikija Kanda ya Kati kupitia kwenye bajeti huoni *strategic vision* kwamba hapa Kanda ya Kati kilimo kinakuja kuwekwa sawasawa, huoni programme, huoni chochote. Ukiisoma bajeti imegusagusa tu kwa kudonyoadonyoa na ni *story* kwamba hapa tulifanya hivi na pale tulifanya vile, lakini picha hasa kubwa ya Wizara ya Kilimo tunaelekea wapi huioni kwenye bajeti.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka niseme na nashauri Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri tukimaliza bajeti hii hebu waende nje; Waziri aende Egypt lakini Naibu Waziri aende Zimbabwe. Zimbabwe wamenyang'anya mashamba kutoka kwa Wazungu na dunia nzima ikajua sasa Zimbabwe inaenda kufeli lakini wamefanya mapinduzi makubwa sasa kwenye kilimo, kwetu hapa hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu hailimi, tuko *strategically positioned* kwa ajili ya kuilisha *Middle East* na Uarabuni...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji unakatiza kati ya mzungumzaji na Kiti lakini pia nilishazuia watu kumfuata Waziri Mkuu, ulikuwa haupo ndiyo maana, endelea Mheshimiwa.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, sisi tumekaa katika *position* nzuri ya kuilisha *Middle East* na nchi za Kiarabu ambazo wenzetu kule ni jangwani, lakini ukienda kwenye masoko ya Doha na Abu Dhabi vitu vyote vinatoka South America hadi ndizi na mchicha sasa hii nchi tunaenda huko lini? Ukiwa kwenye ndege unatua hata tu barabarani unakwenda Arusha unakwenda wapi hakuna *plantation* zozote katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, matreka yanayoingia hapa huwezi kulinganisha na Zimbabwe ambao Waafrika wenzetu wameingiza. Kwa hiyo, mimi nachoona bado tunapiga *mark time*, ASDP I&II zilifadhiliwa sana na *donner partners* walivyojitoa kwenye *basket fund* ile ya kusaidia kilimo sasa hivi hakuna ni *story* tu, *ASDP II* haina kitu.

Mheshimiwa Spika, nadhani kwenye kilimo tuwe *serious,* aligusia Mheshimiwa Kandege hapa hakuna kitu ndugu zangu tuseme ukweli kama tunataka kweli twende kwenye kilimo hatujaamua ndugu zangu. Wenzangu wameongelea Minjingu na maeneo mengi hatufanyi vizuri. Sasa nchi hii tunataka kuendelea, lakini tunaendeleaje kilimo tunakipuuzia? Kwa kweli nataka niseme bajeti hii imekuja chini ya kiwango hai-*reflect* hasa tunataka twende wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu kama nilivyosema tumejaaliwa tunalima sana mahindi na nchi zinazotuzunguka wanatutegemea sisi lakini bado hatujakaa sawasawa. Hatuwezi kulisha South Sudan, kuna watu tu wametu-*block* hapo karibu basi hatuwezi kwenda South Sudan. Congo walikuja wanataka...

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa.

**SPIKA**: Ndiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI**: Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa mchangiaji rafiki yangu Nollo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema sana ya maelezo yake juu ya mchango wa sekta ya kilimo, naomba nimpe *comfort* kidogo, najua baadaye Mheshimiwa Waziri ataeleza, lakini katika bajeti hii ya mwaka 2021/2022 *ASDP* II kupitia mradi utakaofadhiliwa na *IFAD*, Wizara ya Kilimo (mazao na mifugo na uvuvi) tutapata zaidi ya shilingi bilioni 150. Pesa hizi zitakwenda moja kwa moja katika vikundi kusaidia mambo ya mbegu na mengineyo. Kwa upande wa mifugo huko tutakapofika katika Wizara yangu pia vilevile itaonekana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimpe *comfort* na ikimpendeza baadaye nafikiri kupitia Mheshimiwa Waziri atamuonyesha kwa undani zaidi.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Nolla unapokea taarifa hiyo.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, siipokei taarifa hiyo kwa sababu hatujapata hizo fedha kutoka *IFAD*, tunaanza kujadili kwamba tukiokota fedha tugawane, sasa ni *story* hiyo.

**MBUNGE FULANI:** Maoteo.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Hatuwezi kujadiliana maoteo.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nachotaka kusema Serikali iwe *serious* kwenye kilimo kwani bado hatujawa *serious*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye Jimbo langu la Bahi tuna skimu za mpunga za umwagiliaji, hazijafanyiwa ukarabati muda mrefu. Mara ya mwisho zimefanyiwa

ukarabati mwaka 1998. Skimu ya Ntitaa mwaka 2004 *IFAD* walitujengea ilifanya kazi mwaka mmoja lile tuta likavunjwa mabilioni ya shilingi hatujawahi tena kuendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nachotaka kusema hebu tuichukulie Wizara hii kama *MSD* inavyofanya kazi. Kilimo kikianza kufanya kazi kama *MSD* tutaendelea. Tuchukulie kwamba huu ni uhai wa nchi. *MSD* inaleta dawa na ndiyo maana tunaendelea kuwa na afya, lakini kwenye kilimo bado tunacheza.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Judith Kapinga atafuatiwa na Mheshimiwa Kunti Majala.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Mkoa wa Ruvuma ni mojawapo ya mikoa inayoongoza kwa uzalishaji wa chakula nchini. Kwa nini Mkoa wa Ruvuma unaongoza ni kwa sababu tuliwaambia Wanaruvuma nendeni mkalime muongeze chakula katika nchi hii na walitumia jembe la mkono na mbinu duni za kilimo na mpaka mwaka jana wakaongeza tani 50,628 za mahindi kwa ajili ya akiba ya chakula cha nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tuliwaambia Wanaruvuma nyie ni kati kati ya mikoa mnayozalisha mazao ya chakula kwa wingi katika nchi hii. Mwaka jana waliongeza ziada ya chakula tani 877,048 kwa kuwa mahitaji ya chakula ya kimkoa yalikuwa tani 469,172 na wao Wanaruvuma kwa mikono yao walizalisha tani 1,346,220.

Mheshimiwa Spika, leo hii baada ya kuwapetipeti sana wazalishe mazao ya chakula kwa ajili ya akiba ya nchi hii, tumewasahau. Tumesahau jasho walilolitoa kwa dhati ya mioyo yao kulima, tumesahau nguvu waliotumia kwa mikono yao kulima na leo hii wanalala na mahindi yao ndani, wanahangaika na mahindi yao ndani, wanalia na mahindi yao ndani. Kwa takribani miaka mitatu hakuna soko la

mahindi Wilayani Mbinga na Mkoani Ruvuma kwa ujumla huku tukijua Mkoa wa Ruvuma ndiyo unaozalisha kwa kiasi kikubwa mahindi na chakula cha nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naongea haya kwa uchungu sana kwa sababu wana Ruvuma wamekuwa *disparate*. Mwaka jana akatokea tajiri tapeli anayejulikana kwa jina la Njako akaenda pale Mbinga Kigonsera akachukua mahindi ya wakulima yenye thamani ya shilingi bilioni 5 na mpaka leo hii tunapozungumza tunaenda kwenye mzunguko mwingine wa kuuza mazao mpaka leo wakulima hawajapata fedha. Vilevile mpaka leo hawana soko ambalo wataenda kuuza mahindi yao.

Mheshimiwa Spika, wakati haya yote yanafanyika *NFRA* ambao wao wanasema wana jukumu la kununua mazao kwenye mikoa inayozalisha sana walikuwepo na hawajawahi kununua hata debe moja la mahindi Wilayani Mbinga. *NFRA* ambao wao wanasema wana jukumu la kununua mazao kwenye mikoa inayozalisha sana, wameweka vituo kwenye miji wamegeuka ma-*God father,* wanasubiri mkulima atembee kilomita 60, 100, 200 aende kuwapelekea gunia zake 10 za mahindi. Mkulima huyu ataweza vipi kwa sababu mpaka aende kilometa 100 gharama zote za uzalishaji zimeisha pale. *NFRA* watuambie kama wao wamegeuka ma-*God father* sisi tunataka usuluhisho wa masoko ya wakulima kwenye nchi hii ikiwemo Mkoa wa Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kinachosikitisha zaidi wananchi wa Mkoa wa Ruvuma wamelima kweli kweli mahindi mwaka huu, wananchi wa Mbinga wamelima mahindi kweli kweli, kuna kizungumkuti mwaka huu wanaenda kuuza wapi? Kwa hiyo, nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri leo hapa nitamkamatia shilingi yake. Mwaka jana tumetapeliwa, fedha zetu hazijarudishwa mwaka huu bila kutuambia tunaenda wapi kuuza mahindi yetu tunakamata shilingi yake hapa Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, nakupa taarifa kabisa uje na majibu yanayoeleweka kwa wananchi wa Ruvuma na Mbinga kwamba mahindi yetu tunayapeleka wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru Mheshimiwa Rais anazunguka nchi jirani kwenda kuongea na majirani zetu kuweza kujua mahindi yetu tunayauza wapi? Kinachotusikitisha wataalamu wetu wamekaa wanamshangaa Mheshimiwa Rais, yaani Mheshimiwa Rais kashatafuta masoko wanategemea mkulima atabeba gunia zake 10 aende akauze mahindi yake Malawi au Msumbiji, wataalamu wetu mnatuangusha. Haiwezekani mpaka tuje hapa tulalamike ndipo mtafute suluhu ya matatizo yetu, mlipaswa kuyaona mapema kabisa kwa sababu msimu wa mahindi sasa ndiyo umeanza. Sasa ndiyo tunataka Mheshimiwa Waziri atuambie tunaenda kuuza wapi sisi mahindi yetu wananchi wa Ruvuma kwa sababu tumechoka na kutapeliwa na kwa muda mrefu sasa tunahangaika huku na huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi inasemaje kuhusiana suala la kilimo. Inasema: "Chama cha Mapinduzi kinatambua kwamba mageuzi ya kujenga uchumi wa viwanda ni lazima yaendane na mageuzi ya kuongeza tija kwenye kilimo". Namkumbusha Mheshimiwa Waziri Ilani ya Chama chetu inasema nini kwenye masuala ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nimalizie kwa kumnukuu Mwalimu Nyerere alisema kama ifuatavyo: "*Tarmac roads, too, are mostly found in towns and are of especial value to the motor-car owners. Yet if we have built those roads with loans, it is again the farmer who produces the goods which will pay for them".* Tutawalinda wakulima wa nchi hii Mheshimiwa Waziri tunaomba majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Judith Kapinga. Mheshimiwa Kunti Majala, atafuatiwa na Mheshimiwa Daimu Mpakate.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia Wizara hii muhimu ambayo inatusababisha tuendelee kuishi.

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa Pili wa Bunge hili, niliuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusiana na suala nzima la kilimo cha kutegemea mvua ya Mwenyezi Mungu. Waziri Mkuu majibu aliyoyatoa alisema kama Serikali inatoka sasa kwenye kilimo cha kutegemea mvua ya Mungu na kwenda kujikita kwenye kilimo cha tija, kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siku za nyuma sekta ya umwagiliaji ilikuwa Wizara ya Maji lakini kwa kuona ufanisi wake ni mdogo tukashauri sekta ya umwagiliaji itoke kwenye Maji iende Kilimo ili watu wa Kilimo waweze kuisimamia sekta hii na iweze kuleta tija ndani ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini cha kushangaza na cha kustaajabisha baada ya sekta hii kutoka Wizara ya Maji kuletwa Wizara ya Kilimo mwaka 2020/2021bajeti iliyoisha mwaka jana, Wizara ya Kilimo, Sekta ya Umwagiliaji Fungu Na.5 ilipitishiwa au iliidhinishiwa shilingi bilioni 17, fedha za maendeleo za ndani zilikuwa shilingi bilioni 3 na fedha za nje zilikuwa ni shilingi bilioni 9. Sasa katika hizi fedha za ndani shilingi bilioni 3 Serikali haijatoa fedha hata shilingi moja kwa ajili ya kwenda kwenye umwagiliaji na badala yake fedha za nje wenzetu wakatoa shilingi bilioni 5. Tunasema Serikali tunakwenda kujikita kwenye kilimo chenye tija cha umwagiliaji mnatenga wenyewe bila ya kulazimishwa mnasema hii ndiyo tutakayoiweza hata kuitoa nako ni shughuli, imeshindikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najiuliza kama Bunge tuna sababu gani ya kukaa humu ndani na jadili na kupitisha fedha halafu haziendi kwenye kazi ambayo tumekwenda kuipitisha? Leo Fungu Na.5 linaomba fedha za maendeleo shilingi bilioni 5, shilingi bilioni 3 haikupewa shilingi bilioni 5 itapewa? Hivi vitu vinakwaza, vinakatisha tamaa, vinaturudisha nyuma na

wakati mwingine tunaona hatuna sababu ya kuendelea kuchangia Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inakiri kwamba sekta hii ndiyo ambayo imeajiri zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania. Hivi inasema imeajiri kwa wakulima mmoja mmoja kuhangaika huko kwa majembe ya mikono, kwa mikopo ya gharama kubwa, ilhali tuna Benki yetu ya Kilimo ambapo lengo na madhumuni ilikuwa ni kwenda kuwasaidia wakulima wetu kuweza kupata fedha na mitaji kwa ajili ya kuhakikisha wanakwenda kulima kilimo chenye tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe kwa Serikali kwa kuwa Benki ya Kilimo iko chini ya Benki Kuu ambayo masharti yake yanakwenda kubaki vilevile kama benki nyingine, tuone namna gani tunakwenda kuitoa Benki hii ya Kilimo ili tuweze kuipunguzia masharti wananchi wetu waweze kupata mikopo ya yenye tija na hatimaye waweze kilimo chenye tija.

**TAARIFA**

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, taarifa

**SPIKA:** Taarifa naipokea.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU**: Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa mchangiaji kwamba Wizara ya Kilimo wana Mfuko unaitwa *Agriculture Trust Input Fund* ambapo ni mfuko huu, pamoja kwamba ni mfuko chini ya Wizara uko *one hundred percent commercial.* Wanamkopesha mkulima anayetegemea mvua, wanamkopesha mkulima ambaye hapati masoko lakini katika kipindi cha miaka minne ambayo wamempangia kurejesha akisharejesha anakuta kuna *interest* ambayo inazidi asilimia 50 ya hela halizokopa. Kwa hiyo, matokeo yake watu wengi wanaona hakuna tofauti ya hela inayosimamiwa na Wizara ambayo ilipangwa kwa ajili ya kuwasadia wakulima na ile inayotoka kwenye benki za biashara.

Mheshimiwa Spika, nakushuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti unapokea taarifa hiyo.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nimshukuru kaka yangu Mheshimiwa Kanyasu, haya yote ndio tunayazungumza suala zima la kumsaidia mkulima, Serikali dhamira na nia yenu ni kuwasaidia wakulima kuweza kuhakikisha wanakwenda kupata fedha ama mikopo yenye riba nafuu na itakayokwenda kutolewa kwa muda mrefu hili waweze kuhakikisha kwamba wanalima mazao yao na wanapata fursa ya kuweza kuyauza kwa tija na hatimaye waweze kurejesha hiyo mikopo.

Mheshimiwa Spika, lakini stakabadhi ghalani Waheshimiwa Wabunge wenzangu hapa wamesema suala zima la stakabadhi ghalani na Mkoa wangu wa Dodoma tuliathirika sana na wakati wizara inatulekea stakabadhi ghalani Mkoa wa Dodoma, Mheshimiwa Bashe alituita pale ukumbi wa Msekwa tulimkatalia tukamwambia stakabadhi ghalani kwa kuwa Serikali hamjajipanga kuleta stakabadhi ghalani kwa kuwa wananchi wetu hawana taarifa hawaelewe ni chochote. Lakini pili hamjaweza kuwasaidia wakulima wa Mkoa wa Dodoma na mpaka mfikie hatua ya kwenda kutuletea stakabadhi ghalani.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wao wana mabavu, wana vyombo vya dola wana kila kitu wakaamua kutuletea stakabadhi ghalani watu wetu walipigwa walinyanganywa mazao yao lakini pili mbaya zaidi Wilaya ya Chemba, Kata ya Mpendo tunapakana na Bahi shughuli zote na kata ile ndiyo inayolima ufuta kwa wingi Kata ya Mpendo wanapata huduma Wilaya ya Bahi, wakulima wa Mpendo walikuwa mazao yao wakivuna wanapeleka Bahi wanauza.

Mheshimiwa Spika, baada ya stakabadhi ghalani kwa kuwa zoezi hili lilikabidhiwa kwa Wakuu wa Wilaya wananchi na wakulima wa Kata ya Mpendo walikuwa wanalazimishwa awe ana kilo mbili awe ana debe moja awe na gunia atoke Mpendo kilometa 97 mpaka Makao Makuu ya Wilaya ya

Chemba pale kwenye ghala aende akaweke bodaboda ukikodi ni shilingi 35,000, kilo ya ufuta ni shilingi 2,000 ana debe moja ni Shilingi 40,000huyu mkulima mnamuinua kwa namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana stakabadhi ghalani wabaki nayo wao Bashe aipeleke kule pamoja na Mheshimiwa Mkenda pelekeni kwenye majimbo lakini kwetu kwenye Mkoa wa Dodoma tunawashukuru kwa huduma hiyo lakini hatuhitaji hata kuisikia na nitakuwa wa kwanza kwa ajili ya stakabadhi ghalani sitaki kusikia stakabadhi ghalani sitaki kusikia stakabadhi ghalani ndani ya Mkoa wangu wa Dodoma. *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Nilimwambia waziri jana kwamba yani sisi Dodoma kuwa na ufuta halafu kwenda kwenye mambo ya stakabadhi ghalani ni sawa kabisa na ukiwa na bangi, yaani *harassment* yake ni sawasawa tu huna namna, vinginevyo utapambana. Kwa hiyo, kama walivyosema Wabunge kuna maeneo mengine inaelekea inaweza ikafanya kazi lakini yako maeneo ambayo kama hapa Dodoma yaani haiwezekani. (Makofi)

Mheshimiwa Daimu Mpakate nitaongeza muda kidogo angalau wa nusu saa Waheshimiwa kwa sababu ya idadi ya watu tulionao na umuhimu wa hii bajeti tuvumiliane kidogo nusu saa si nyingi Mheshimiwa Daimu Mkakate.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Anafuatiwa na Mheshimiwa Neema Mwandabila.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika mhana huu kuchangia bajeti ya kilimo kwanza naunga mkono hoja pamoja na kuunga mkono hoja naomba nichangie katika maeneo mawili jambo la kwanza ni suala la mfumo wa

stakabadhi ghalani na jambo la pili ni suala la *export levy* kwenye zao la korosho.

Mheshimiwa Spika, tujiulize ni kwa nini mfumo wa stakabadhi ghalani ulileltwa na Serikali naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tupitie sheria ya mwaka 2005 iliyeanzisha mfumo wa stakabadhi ghalani na sheria ile iliyeanzisha *export levy* kwenye zao la korosho kwa nini tulianzisha hivi vitu viwili.

Mheshimiwa Spika, stakabadhi ghalani ilianzishwa kwa ajili ya kutatua changamoto ya masoko kwenye zao la korosho na mazao ya biashara mwaka 2005, baada ya kuanzisha na kweli mwaka 2006/2007 korosho zilikuwa zinauzwa 150 mpaka shilingi 200 kwa kilo moja baada ya mfumo wa stakabadhi ghalani kuanzishwa korosho ikawa inauzwa shilingi 600 mpaka 800 kwa kilo moja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ndugu zangu naomba sana Wabunge wezangu tuende tukaangalie sheria hii na hapa ninaomba wanaye husika bodi ya leseni za maghala, Wizara ya Kilimo pamoja na viwanda na biashara kuna haja ya kutoa elimu ya mfumo wa stakabadhi ghalani kwa wakulima na hasa ukianzia kwa Wabunge wenyewe tuliokuwa humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Mkoa wa Mtwara Lindi Tunduru ukimwambia habari ya mfumo wa stakabadhi ghalani haufai kwenye korosho haufai kwenye ufuta utapigwa mawe. Lakini tunapoanza na jambo hili changamoto lazima ziwepo kwa sababu mfumo wa stakabadhi ghalani unakata mirija ya watu waliokuwa wanafaidika na mnyororo wa biashara hii ya ufuta, mnyororo wa biashara ya korosho mnyororo wa biashara ya kahawa na mazao mengine ambayo yako kwenye sheria ya mfumo wa stakabadhi ghalani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mtwara tulipoanza mfumo wa stakabadhi ghalani wakati huo nakumbuka Tyson ndiye aliyekuwa waziri alitukanwa hadharani kwenye mkutano wa

hadhara, viongozi wa shirika waliathirika mazao yao mikorosho ilikatwa nyumba zilichomwa moto kwa sababu ya watu wa kati ambao walikuwa wafaidika katika mfumo wa kawaida ili kujua kwamba...

**MHE. ESTER A. BULAYA**: Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Mpakate.

**TAARIFA**

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nampa taarifa mbali na mchango wake mzuri kwa sababu imeingia kwenye *hansard* aliyekuwa waziri wa kilimo aitwe Tyson anaitwa Stephen Wasira. *(Makofi)*

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika naipokea taarifa kwa mikono miwili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpakate anayekupa taarifa anamjua vizuri Mheshimiwa Stephen Wasira kwa hiyo yuko sahihi. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, yuko sahihi naipokea taarifa yake wakati huo vurugu zilikuwa ni kubwa kuliko hizi unazoziona leo hapa kwenye korosho kwa sababu wafaidika wa mfumo wa zamani ndio waliokuwa wanawaambia wakulima wagome kufuata mfumo wa stakabadhi ghalani na haya ndio yanayotokea maeneo mengine kwenye mazao mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Naomba turejee kwenye sheria ya mfumo wa stakabadhi ghalani na kwa nini Serikali iliamua kuanzisha huo mfumo stakabadhi ghalani. Na bahati nzuri zaidi ni sheria iliyopitishwa kwenye Bunge hili la Jamhuri la Muungano wa Tanzania, walianza na mazao makuu ya uzalishaji 2009 wakaongeza kwenye mazao mchanganyiko sikatai kuna changamoto ambazo Serikali inatakiwa izifanyie kazi, naomba changamoto zote zilizojitokeza kwenye mfumo

wa stakabadhi gharali pamoja na ucheleweshaji wa wakulima kupata siwezi kufanya. *(Makofi)*

**MHE: DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa unapewa Mheshimiwa Mpakate endelea Mheshimiwa.

## TAARIFA

**MHE: DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa rafiki yangu mtani wangu Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate kwamba kila mfumo ambao utawekwa kwa ajili ya kununua mazao ya biashara ama ya chakula utakuwa na *losers* na *winners.*

Mheshimiwa Spika, mfumo uliokuwepo awali una *losers* na winners' wake, na huu mfumo wa stakabadhi ghalani nao una *losers* na *winners* wake miongoni mwa watu ambao ni *winners* ama wafaidika mfumo huu mpya ni watu ambao wanakaa kwenye kikao kuzigungua zile zabuni wakishaona killichowekwa mle ndani utoka nje kwenda kwa wale wanunuzi ambao wame-*submit* zile zabuni na kuzungumza kuhusu asilimia 10 ambayo inawekwa *over and above* bei ambayo alikuwa ameiweka pale ambayo ulipwa pembeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hao wanafaidika na hiyo *ten percent* hao ni *winners,* kwa hiyo hata ule mfumo wa zamani nao ulikuwa na watu ambao walikuwa wanafaidika na watu ambao walikuwa wanaonewa na huu mpya pia una watu ambao wanafaidika na watu wanaoonewa kwa hivyo Serikali ifanyie kazi hayo mapungufu ya hiyo *ten percent* ambayo huwa ilikuwa inawekwa juu ya bei ambayo mtu ame-*bid* kwenye karatasi nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Daimu unapokea taarifa hiyo

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikubaliane kwamba kila mfumo una *winners* na *losers* na ndio maana nimesema hata mfumo huu unachangamoto ambazo zinatakiwa zifanyiwe kazi na Serikali kwa hiyonakubaliana na maelezo yake kwamba wanatakiwa wafanyie changamoto zote zilizojitokea katika utekelezaji wa mfumo wa stakabadhi ghalani hili wakulima waendelee kunufaika kuliko vile ambavyo vilikuwa mwanzo. Naamini mfumo huu unawasaidia sana wakulima kufaidika ingawa kuna changamoto hizo ambazo mwezangu amezieleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye *export levy* mwaka 2018 Serikali ilivyoamua kubadilisha sheria ya *export levy* iliahidi mambo yote ambayo yalitokana na maamuzi ya wadau wa zao la korosho kukubaliana *export levy* waanzishe yatayafanya. Miaka mitatu iliyopita Serikali imekusanya zaidi ya bilioni 210 kutoka kwenye sekta ya korosho kama *export levy* mwaka wa fedha 1920/2021/2018/ 2019 lakini Serikali haijapeleka hata shilingi moja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpakate bahati mbaya muda ndio huo.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika ahsante naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Neema Mwandabila akifuatiwa na Mheshimiwa Professor Patrick Alois Ndakidemi.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kidogo katika wizara hii nyeti, lakini pia niseme kwamba nina imani na wizara hii kwa sababu ina viongozi makini ambao wamekuwa wakiendelea kufanya kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mambo machache ambayo ningependa kuongelea kupitia wizara hiikwa maana ya kukjenga ili tuweze kuona tunaelekea wapi katika kuboresha kilimo nchi hii, nilikuwa napitia taarifa tuliyopewa hotuba ya

waziri kuna mambo baadhi niliweza kuyaona yakanipa shaka kwamba hivi tunakoenda tutafanikiwa kweli au tataendelea kupiga *mark time.*

Mheshimiwa Spika, niliona suala la takwimu wakakiri wazi kwamba hakuna takwimu zinazoonyesha mahitaji ya mbegu nchini, wakulima wapo tunawafahamu na tunajua kabisa maeneo gani wanalima nini na maeneo gani wanalima kilimo gani, watusaidie kupata hizi takwimu ili wanapokuja kama ni suala la mbolea tujea wanatuletea mbolea kiasi gani ambazo zinahitajika na watanzania. Lakini kama ni suala la mbegu wajue kwamba ni kiasi gani cha mbegu kinachohitajika Tanzania ili tuweze kuwa na uhakika wa hizo mbegu.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujikita kwenye suala la uzalishaji wa mbegu nchini hapa Tanzania tunamekuwa na baadhi ya makampuni *private* ambayo yamekuwa yakiendelea kuzalisha mbegu, lakini tuna shirika pia la kiserikali ambalo limekuwa likiendelea kuzalisha mbegu. Hatujapata takwimu kujua kwamba ni makampuni mangapi Tanzania mpaka sasa yanazalisha mbegu.

Mheshimiwa Spika, naamini kama wizara itajikita kwenye kuwawezesha wazalishaji wa mbegu, hizi tunazohitaji nchini nchi yetu itaweza kufanya vizuri, ndipo ambapo tunaweza kuona kwamba kilimo kinageuka kuwa ni fursa ya kiuchumi kwa maana kwamba tutaweza kuzalisha mbegu nyingi na tutaweza kuuza nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa niliyo nayo mpaka sasa Tanzania tuna kampuni moja tu ambayo inauza mbegu nje ya nchi na nimesikia kwamba uwa wanauza Rwanda. Lakini changamoto ambayo wanayo haya makampuni ya mbegu mojawapo imekuwa ni kwamba hawajapata *support* ya kutosha kutoka Serikalini na wao kama wao wangependa kuona kwamba Serikali inaitambua hii sekta na kuipa kipaumbele hili waweze kufanya vizuri katika uzalishaji wa mbegu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na kiufupi ni kwamba tume-*experience* kwa nyakati tofauti kumekuwa na uhaba wa mbegu mfano kwetu sisi Songwe tumekuwa tukiona kabisa wazi mbegu wakulima wanachukuwa Zambia wanakuja kupanda Tanzania kwa upande fulani inakuwa ni *Illegal business* lakini ndio inayowasaidia kama Tanzania tukijipanga vizuri kwenye mbegu naamini tutaweza kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, makampuni haya yanatamani kungekuwa na uwezeshaji kwa namna ya kwamba kuwe angalau na *grants* hizi ruzuku lakini pia kufanyike uwezekano kwa mabenki ambayo yanatoa mkopo kwa riba nafuu ili yaweze kuijenga vizuri. Kwa mwaka 2014/2015/2016 tunafahamu sote, haya makampuni ya mbegu yalipewa kazi ya kugawa mbegu kwa mawakala kwa njia ya ruzuku na tunachofahamu mpaka sasa makampuni haya mengi hayajalipwa pesa zao.

Mheshimiwa Spika, na kwa maana hii kwa kutokulipa pesa hizi kwa wakati Serikali kwa makampuni haya yanashusha uwezo wamakampuni haya kuweza kujiendesha na mengine yamefilisika yamekufa. Kwa hiyo, nilitamani sana kusikia kauli ya Serikali kuona kuwa watalipa lini fedha zao ili makampuni haya kama yanakosa ruzuku kama wanakosa mikopo basi pesa zao wapewe ili waweze kuzalisha kwa upana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya kusema hayo pia nimepitia eneo la uzalishaji wa mbolea nikaona kwamba mahitaji ya mbolea Serikalini tumeweza kufanikisha kuyafikia kwa asilimia 94.4, ni kiwango kizuri wizara imejitahidi lakini katika eneo hili kuna baadhi ya mambo niliweza kuona kama ni changamoto.

Kwanza niliambiwa kwamba mbolea ambayo inazalishwa nchini ni tani 32239 nikajaribu kutafuta *percent* kwa kujua mbolea iliyopo nchi iliyozalishwa ndani ni ngapi nikapata ni asilimia 4.75 kitu ambacho nikaona kama uzalishaji wa ndani ni mdogo hivi mbona ni shida.

Mheshimiwa Spika, na sisi tunakiwanda chetu cha Mijingu...

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Neema.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika ahsante naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa *Professor* Patrick Ndakidemi atafuatiwa na Mheshimiwa Tunza malapo.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, ahsante nianze kwa kumpongeza sana Waziri wa Kilimo na naibu wake pamoja na timu ya wataalam kwa kazi nzuri wanayoifanya Wizara yetu ya kilimo. Nitachangia kwenye sehemu mbili ya kwanza ni umuhimu wa kuongeza bajeti ya kilimo nataka niiombe Serikali kitu hapa na cha pili ni fursa zilizopo Mkoani Kilimanjaro kwenye sekta ya umwagiliaji hasahasa kwenye jimbo langu la Moshi Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wote tunakubaliana kabisa kimsingi kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wetu na muhimili mkuu kwenye kukuza uchumi wa Tanzania. Kilimo inachangia vitu vingi sana asilimia 65 ya watanzania wako kwenye kilimo inachangia asilimia 27.5 kwenye pato la Taifa asilimia 24.7 kwenye fedha za kigeni asilimia 60 kwenye malighafi za viwanda na asilimia 100 kwenye chakula cha nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na umuhimu huo wa kilimo hawa watu wanapewa hela ndogo sana, Serikali inatenga pesa ndogo sana kwenye hii Wizara na tunamlaumu waziri na timu yake lakini kusema ukweli shida haiku kwa hawa watu. Kwa sababu hata wewe Mheshimiwa Spika jana uliongea nikafurahi sana, ni mtoto wa mkulima unaguswa na kuna kitu kizuri hakiko sawa sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pesa ambayo Wizara ya Kilimo imetengewa kwenye bajeti ambayo waziri ameaomba ni asilimia 0.08 haijafika hata *one percent* Mheshimiwa Spika

mnataka waziri afanye nini na timu yake jamani, sisi kama Serikali, hela hii ni kidogo na haitoshi tukilinganisha bajeti za nchi zingine za nchi za Afrika Mashariki ambazo Kenya Uganda na Rwanda hawa wanawekeza vizuri sana kwenye kilimo ukilinganisha na sisi watanzania ambao tunalima kwa uhakika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika niishauri Serikali ni muhimu kabisa tuongeze bajeti ya kilimo tukisema tumewapa pesa tuwape hili wafanye kazi, bila hivyo tutakuwa tunalalamika na hatuwatendei haki wakulima wetu. Niseme kwamba kuna *declaration* ya Malabo ambayo Serikali yetu iliingia mwaka 2014 tarehe 26 mpaka tarehe 27 Juni. Viongozi wa nchi wakakubaliana kwamba tutatenga angalau asilimia 10 ya bajeti iende kwenye kilimo kwenye haya mataifa maraisi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naona hatujafika hata *one percent* jamani tunakwenda wapi niombe tu angalau tungekubaliana na hiyo *ten percent* kilimo leo tungukuwa tunawapa kitu kama tirioni 3.6 ambayo wangeweza wakafanya kiti kidogo, wakaboresha utafiti wakaboresha ugani, na vitu vinginevyo ambavyo wameweka kwenya mpango wao. Kwa hiyo, ombi langu kwa Serikali na Waziri Mkuu wetu yupo hapa baba yetu Waziri Mkuu tunaomba kabisa Wizara ya Kilimo iangaliwe kwa jicho la huruma kwa sababu tunavyokwenda sio sawa kabisa nakubaliana na Mheshimiwa Joseph Kandege bajeti ya kilimo ni ndogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo niende kwenye jimbo langu sasa Mkoa wa Kilimanjaro una fursa nyingi sana za kilimo cha umwagiliaji eti tumebarikiwa kuwa na ule mlima unatiririsha maji mengi sana kutoka mlimani na yanaishia bahari ya Hindi. Bahati mbaya sana maji haya hayajatumika vizuri, nina naishauri wizara itumie hii fursa ya yale maji badala ya kuishia baharini na kuuwa watu kwenye mafuriko tuwekeze tujenge skimu za kutosha tuboreshe ile mifereji ili kilimo kule Kilimanjaro tutoe mchango kama tulivyokuwa tunafanya zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo ya ukanda wa tambarare kule jimboni kwangu, eneo la Mabogini tunaweza tukajenga skimu mpya, kuna kama hekta 1,350. Kata ya Arusha Chini tunaweza tukajenga skimu mpya kwenye vijiji viwili, kuna hekta kama 2,000. Kuna eneo la Old Moshi Mashariki kwenye Kijiji cha Mandaka Mnono kuna hekta 1,250. Tukiwekeza katika maeneo haya, nina uhakika tutachangia kikamilifu katika zile hekta ambazo Serikali inategemea kuboresha kwenye kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba kuunga mkono hoja. Naomba sana tuifikirie Wizara ya Kilimo kwenye *funding.* Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tunza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi mchana wa leo nami nichangie kidogo kwenye Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la kilimo cha umwagiliaji hapa pana changamoto nyingi. Tunafahamu kilimo kinahitaji maji na siyo lazima yawe maji ya mvua ndiyo maana tunasisitiza kwamba kuwe na kilimo cha umwagiliaji. Ukiangalia eneo linalofaa kwa umwagiliaji ni asilimia ndogo sana inatumika. Hata ile inayotumika ufanisi wake bado ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa kwenye Kamati ya Kilimo, tumepita kwenye miradi ya umwagiliaji, utasema nao kule kwenye miradi wanalima kwa kutegemea mvua. Binafsi nilikuwa nategemea kwamba tunapokwenda sehemu ambayo ina skimu ya umwagiliaji tukute shughuli za kilimo zinaendelea mwaka mzima lakini mambo yanayoendelea pale hayaridhishi. Unaambiwa pesa nyingi za Serikali ziko pale lakini kinachoendelea hakieleweki. Huko kwenye umwagiliaji miradi mingi pesa imepigwa, vyanzo vya mapato havieleweki ile miradi ambayo ipo...

**T A A R I F A**

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Kunti.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba nimuongezee tu Mheshimiwa Tunza kwamba vyanzo vya mapato vinavyotarajiwa kukusanywa mwaka huu wa fedha kupitia sekta ya umwagiliaji ni uuzaji wa nyumba pamoja na magari chakavu ambapo wanatarajia kukusanya shilingi milioni 15.

Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo sekta ya umwagiliaji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tunza, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, naipokea kwa mikono miwili, inaonesha ni namna gani Serikali haiko *serious* kuwekeza kwenye umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano ukija Mkoani kwetu Mtwara, Mkoa mzima wa Mtwara wameainisha kwenye hotuba yao kwamba eneo linalofaa kwa umwagiliaji ni hekta 24,317 lakini zinazotumika ni 3,729, ni asilimia 15 tu. Matatizo haya ya kutokuwekeza kwenye kilimo kingine tofauti na korosho ndiyo maana watu wa Mtwara korosho ikifanya vibaya utasema tuko msibani. Kama sasa hivi nenda Mtwara uikute hali yake, mimi nimetoka huko juzi. Kilimo cha mazao ya korosho, mpunga, mahindi hayaeleweki, kilimo cha umwagiliaji kiko asilimia 15 tu; nenda huko kwenye skimu kwenyewe hakuna kinachoeleweka.

Mheshimiwa Spika, hii Wizara inatakiwa iwe *serious.* Ukipita kwenye skimu zote za umwagiliaji zina migogoro. Kwa nini wanawekeza pesa sehemu ambazo hawajatatua migogoro? Watu wanashindwa kulima kwa sababu ya migogoro iliyopo pale; Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri ni mashahidi. Tatueni migogoro, wawezesheni

watu walime ili tutoke hapa tulipo tusonge mbele. La sivyo, kila siku tutakuwa tunaimba lakini kile tulichokikusudia hakiwezi kuleta tija kwa sababu hatuweki misimamo iliyo sahihi na thabiti kukiendea kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee korosho kidogo, wenzangu wameongea sana, mwenye masikio asikie. Sisi watu wa Mtwara hatutaki kuchanga ile pesa ya pembejeo; yaani huo ndiyo msimamo wetu, hatutaki. Hatutaki kuchanga kwa sababu gani? Mtu hauwezi kukataa bila kuwa na sababu. Sisi hatutaki kuchanga kwa sababu kuna *export levy* imekusanywa, ninyi mnajua, siyo chini ya bilioni 400.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, hawa Wamakonde wakikwambia kitu fulani hatutaki yaani wanamaanisha. Ukisikia hatutaki chichi hicho kitu yaani ujue hawataki. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Tunza, endelea. *(Kicheko)*

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru unatuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa watu wana hela zetu na wanajua wanazo, kwa nini leo wanatulazimisha tuchange? Zile hela zetu ambazo mnazo kule tangu msimu wa 2017/2018 mpaka leo mmezitumia kufanyia nini?

Mheshimiwa Spika, mimi nikiwa Mbunge ninayetokea Mkoa wa Mtwara, tunawaambia kabisa tafuteni namna sisi tupate pembejeo, watu walime tuvune korosho tuuze. Hizo habari za kutuzungukazunguka kutuambia sijui tukatwe shilingi 110 kutoka kwenye kila kilo ya korosho hatutaki kwa sababu hela zetu mnazo. Yaani ninyi msituzugezuge kutuona kama sisi hatuelewi, sisi tunaelewa vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho nalotaka kumalizia; mimi najiuliza sisi kama nchi hivi ni zao gani kabisa

tunajivunia kwamba hili zao ndiyo tunalilima kwa kiasi kikubwa?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Tunza, dakika ndiyo hizo.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Wanachosema watu wa Mtwara Wizara ya Kilimo msiwazingue. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Innocent Kalogeris awe mchangiaji wetu wa mwisho asubuhi ya leo.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii nyeti ambayo imegusa maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya katika Wizara lakini vilevile kuwapa pole kwa haya ambayo yanaendelea kutokea. Yote haya naamini kabisa yanatokana na ufinyu wa bajeti ambapo kwa namna moja au nyingine kama wangeweza kupata fedha nyingi haya yasingetokea.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi kubwa ambayo Wizara inafanya, naomba niseme bado kuna kazi kubwa ambayo Wizara inaifanya katika kuinua kilimo kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mimi nijikite kwenye eneo moja tu; naamini kabisa kilimo chenye tija na cha uhakika kwa Mtanzania ni kilimo cha umwagiliaji. Hadi hivi sasa tunavyozungumza kupitia Tume ya Umwagiliaji, tunaambiwa kwamba kuna lengo la kulima hekta milioni moja na laki mbili

na hadi hivi sasa tumefikia asilimia 58 ambayo ni hekta 695. Ombi langu na ushauri wangu kwa Serikali, naomba tujikite kwenye maeneo ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, nianze na moja tu, tunapoteza maji mengi ambayo yanakwenda baharini na Serikali imekaa hatuingii huko. Mfano, nataka nizungumzie kwenye Bonde la Kongwa unapoingia Kibaigwa, maji yanatiririka mwaka mzima, yanakokwenda hapajulikani lakini pale tungeweza kuchimba mabwawa watu wakafanya kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Mto wa Dumila, mpaka tunaharibu barabara, zinakatika. Mimi niishauri Serikali katika maeneo kama yale ya Dumila, Ruvu, hebu tungechimba mabwawa watu waweze kufanya kilimo cha umwagiliaji ambacho kitaweza kuleta tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Watanzania wanalima maeneo makubwa, dhamira kubwa ni kukusanya kidogokidogo kwenye kila hekta ili kuweza kupata tija. Nilipata nafasi ya kwenda China mara mbili, mtu analipa hekta tano, tatu analima mpunga mbili analima kilimo cha *horticulture,* ndani ya mwaka anapata tija kubwa kuliko Mtanzania ambaye analima hekta mia katika Tanzania yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naamini kabisa kilimo cha umwagiliaji ndicho ambacho kitamkomboa Mtanzania. Mkoa wa Morogoro umeambiwa ni FAMOGATA – Fanya Mkoa wa Morogoro kuwa Ghala la Taifa la Chakula. Ndani ya Mkoa wa Morogoro tuna eneo ambalo linatosha kwa kulimwa kwa kilimo cha umwagiliaji hekta 230,000 lakini mpaka hivi sasa tumetumia hekta 28,000 tu. Kama kweli *we are serious* na kilimo hebu tu-*inject* hela katika kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu la Morogoro Kusini tuna mradi wa Kongwa Tulo ambao una uwezo wa kulima hekta 3,000. Hadi hivi sasa zimetumika hekta 200 tu. Kuna

mradi wa Mbangarawe, kuna hekta 230 tumetumia hekta 200 tu bado 30. Kuna mradi wa Lubasazi, una uwezo wa kulima hekta 120, hadi hivi sasa kuna shilingi milioni 800 imewekwa pale lakini bado mradi haujaendelea, maana yake tumeweka fedha ambazo hazitumiki. Kuna mradi wa Kirokwa ambao una hekta 105, mpaka dakika hii tunatumia hekta 40.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ukijaribu kuangalia, tuna-*ijnect* fedha kwenye miradi lakini haifanyi kazi. Tumeomba katika mradi wa Kongwa Tulo ili tuweze kuendelea mwaka karibu wa pili huu sasa, nilikuwa Mbunge miaka mitano iliyokwisha, miaka mitano nimekwenda likizo, hakuna kilichowekwa. Sasa hivi tumeomba tena shilingi bilioni 1.4; Mbarangwe shilingi bilioni 1.5; Lubasazi shilingi bilioni 1.5; Kiroka shilingi bilioni 3, ukijumlisha ni shilingi bilioni 7. Fedha hizi tukipeleka pale nina uhakika tutanyanyua kilimo cha Watanzania na wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nizungumzie suala la masoko. Kwa kweli watu wengi wamezungumzia suala la masoko; ni kero kwa wakulima wetu. Hivi ninavyozungumza kuna wakulima wangu kule mazao yako ndani na wanakaribia kuuza nyumba zao kama hatutaweza kuwasaidia kuwapatia masoko.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Innocent Kalogeris kwa mchango wako.

Niendelee kuwashukuru sana wale wote ambao mmechangia toka asubuhi na wale ambao hamjapata nafasi bado majina yenu ninayo. Tuwahi tu kurudi jioni, niwahakikishie kila ambaye aliomba kuchangia atapata nafasi kabla ya Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na Mawaziri wengine ambao watakuwa wamejiandaa kwa ajili hiyo kuanza kujibu hoja zetu.

Kwa hiyo, tufike mapema; Mheshimiwa Rehema Migilla, Mheshimiwa Ramadhani Ighondo, Mheshimiwa Zuena Bushiri, Mheshimiwa Daniel Awack, Mheshimiwa Elibariki Kingu, Mheshimiwa Jacqueline Msongozi, Mheshimiwa Jeremiah Amsabi, Mheshimiwa Francis Ndulane, Mheshimiwa Aysharose Mattembe, Mheshimiwa Martha Mariki, Mheshimiwa Benaya Kapinga, Mheshimiwa Hassan Kungu, Mheshimiwa Maimuna Pathan, Mheshimiwa Mrisho Gambo, Mheshimiwa Furaha Matondo na mwisho kabisa atachangia Mheshimiwa Dkt. Bashiru Ally Kakurwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tuendelee kujiandaa ili tuzidi kuwajenga ndugu zetu. Kama tulivyosema, bajeti yao kwa kweli ni ndogo sana, tuzidi kuwajenga na mwakani tuwajenge zaidi. Hata wale ambao wanatoa mifano ya Zimbabwe, ni kweli Zimbabwe kuna kilimo kizuri na mzee Mugabe alipofanya *Africanization* ile alilaumiwa sana lakini leo Waswahili wenzetu wale wa Zimbabwe sasa wameelewa masuala ya kilimo na wanakwenda mbele.

Ukiwa na bahati ukaruka na ndege *across* Zimbabwe lakini ikawa haiko juu sana kiasi ambacho unaweza kuchungulia ukaona chini, kitu kimoja ambacho utakiona kwanza ni ramani nzuri sana ya mashamba unavyoyaona tofauti na kwetu ambako unaona kama msitu tu. Kubwa zaidi utashangaa kuona mabwawa, yaani mabwawa ni mengi sana.

Mimi naamini hata sisi bajeti zinazokuja mwakani tukiwawezesha wakanunua magreda, ma-*D6* na madudu gani, tukachimbua mabwawa nchi hii mengi iwezekanavyo ili tuwe na kilimo cha mwaka mzima, tutapiga hatua kubwa sana, pamoja na michango mingine ambayo imetolewa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tuendelee kujiandaa, tuendelee kuchangia Waheshimiwa Wabunge.

Kwa hatua hii, basi naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja kamili leo jioni.

*(Saa 7.33 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge naomba tukae. Tunaanza na Mheshimiwa Rehema Migilla.

Katibu!

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA KILIMOKWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Majadiliano yanaendelea, Mheshimiwa Rehema Migilla na wengine watafuata baada ya muda si mrefu.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kunipatia nafasi hii awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai mpaka leo nipo hapa Bungeni.

Lakini sambamba na hilo nianze kwa kuwapongeza viongozi wa wizara hii Kaka yangu Mheshimiwa Profesa Mkenda na kaka yangu Mheshimiwa Bashe pale mnafanyakazi vizuri Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikianza na mchango wangu kwenye hii wizara nikiwa kama mkulima wa zao la tumbaku namwakilishi wananchi waliowengi wanaolima zao la tumbaku naiona kabisa Serikali haina nia ya dhati kabisa ya kuhakikisha hili zao linaendelea kuwa ni kitega uchumi cha wananchi wetu, lakini pia ni mbadala wa kuweza kuhakikisha hawa watu badala ya mazao mengine yanayowafanya waweze kudidimia liweze kupanda mbele.

Mheshimiwa Spika, zao hili limekuwa na changamoto sana pamoja na kuwa Serikali ilituahidi mambo mazuri sana kuanzia mwaka juzi na mwaka jana, lakini bado naona kama ahadi zake hazitekelezeki na zaidi ya yote tunawadanganya wakulima wetu. Ni miongoni mwa wakulima watumbaku, nimefaidika sana na tumbaku, lakini kwa miaka mitano iliyopita bado hili zao limekuwa lina misukosuko mingi na bado mbadala wake hatujapata.

Mheshimiwa Spika, mfano leo hii tuliahidiwa wakulima tumbaku kwamba tutakuwa na uhakika wa soko la tumbaku yetu. Ninachokuambia kwenye jimbo langu wanunuzi watumbaku badala ya kununua bei elekezi iliyopangwa na Serikali ambayo ilikuwa ni dola 1.61, leo hii wakulima wameuza tumbaku yao chini ya bei elekezi dola 1.2. Wakati gharama za uzalishaji wazao hili kwa kilo moja ni dola 1.4, leo hii, gharama za uzalishaji zinakuwa kubwa halafu unakwenda kununua tumbaku ya huyu mkulima kwa bei ndogo, tunania ya dhati kuhakikisha kweli huyu mkulima anasonga mbele au tunamrudisha nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali kama tunania ya dhati kabisa kuhakikisha ili zao na wakulima wetu wanasonga mbele hebu tuweze kuhakikisha haya masoko ya tumbaku yanakuwa yanafuata bei elekezi, lakini pia yawe na uhakika wa kununua hizi tumbaku. Tunaona kuna makampuni mengi yatumbaku halafu tunaita ya wazawa hayana uwezo wa kununua tumbaku matokeo yake wananchi wetu wanakuwa na madeni siku baada ya siku hawalipwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niiombe sana Wizara na Kaka yangu Bashe pale nakumbuka tumeongea sana hili suala la hawa wakulima wa tumbaku, kuna kampuni kama ya *GRAND*, kuna kampuni ya *MAGEFA* hizi kampuni zina waletea mzigo sana wananchi wetu. Tunaona kabisa, kwanza kuna riba ya asilimia nane ya mkopo, anayesababisha hii riba iongezeke ni hawa hawa wanunuzi wanashindwa kupeleka pesa kwenye vyama vya msingi matokeo yake anayekuwa *responsible* kwa ajili ya kulipia hiyo riba ya asilimia nane ni mwananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini sasa Serikali msione kuna haja ya huyu anayesababisha hii riba iongezeke ndiyo awajibishwe. Nataka Kaka yangu Mheshimiwa Bashe na Kaka yangu Mheshimiwa Prof. Mkenda pale mkija ku-*windup* mtuambie hawa wanaouza kwanza tumbaku yetu chini ya bei elekezi mnawachukulia hatua gani? Lakini pia hawa wanaosababisha riba ya asilimia nane iongezeke ili hali Serikali imekaa kimya tunataka mtupe majibu la sivyo nitashika shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini, nakumbuka mwaka jana tukiwa kwenye kampeni Mheshimiwa Bashe tulikuwa naye kule na Mama Samia Suluhu wananchi wa Urambo, Kaliua, Ulyankulu wa Tabora kwa ujumla walipewa matumaini kwamba mwaka huu tumbaku yao itauzwa kwa bei nzuri na hata yale makinikia yale ma-*reject* yatauzwa kwa shilingi 500, nataka niwaulize hivi mlishawahi kufanya *research* kwamba hivi haya makinikia haya ma-*reject* mnaenda kuyanunua kwa shilingi 500 mnakwenda kuyafanyia kazi gani? Hatujawahi kuambiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia tunaona mwaka jana kuna mnunuzi kutoka Kenya na Sudan walikuwa wayanunue haya ma-*reject* kwa bei ya shilingi 100 je, mliweza kujifunza kwamba huko wanakoyapeleka wanayafanyia shughuli gani? Kuliko kuwaacha wakulima wetu huku mnanunua kwa shilingi 500 kumbe yanaweza kuwa yanabei kubwa huko nje ya nchi kuliko kuwakandamiza wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini niombe tena suala jingine, suala jingine niombe sasa kulikuwa kuna mnunuzi mkubwa *TLTC* ambaye alikuwa anauhakika wa kununua tumbaku yetu...

*(Hapa kengele ililia na kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana, malizia sentensi moja tu, basi angalau umeshakaa nakushukuru sana Mheshimiwa Rehema

Migilla, Mheshimiwa Zuena Bushiri, atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Awack.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kukushukuru kunipa nafasi hii kuchangia katika Wizara ya Kilimo. Nianze kwa kuwapongeza Waziri wa Wizara ya Kilimo, Naibu Waziri na Watendaji wake wote kwa kazi nzuri sana wanazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitajielekeza katika kilimo cha umwagiliaji, umwagiliaji wa mpunga pamoja na tangawizi. Kilimo cha mpunga ni kilimo cha chakula na biashara, kilimo cha mpunga kinaingizia kipato sana wafanyabiashara, kilimo cha mpunga ni kilimo ambacho kinahitaji maji ya kutosha, lakini kwa tabia ya nchi mvua zimekuwa chache sana hivyo mazao ya kilimo cha mpunga yamekuwa machache sana.

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba Serikali imejipanga mipango mizuri sana ya kuweza kuwezesha kuweka miundombinu endelevu katika sekta ya umwagiliaji. Nitoe mfano katika kilimo cha umwagiliaji wa mpunga katika *Lower Irrigation* Moshi, *Lower Irrigation* Moshi ilianza na hekta 2300 lakini hadi sasa hivi zinalimwa hekta 1100 hii inatokana na miundombinu chakavu ambayo imejengwa tangu mwaka 1987. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kweli Serikali nia yetu ni kuboresha miundombinu hii katika skimu zetu ni vizuri tukaelekeza nguvu ili tuweze kufanyakazi ya kusaidia wakulima wale ambao wametengeneza mabwawa yao ili Serikali iongeze nguvu ya kutengeneza mabwawa ya kutosha ili kilimo cha umwagiliaji kiwe kilimo endelevu.

Mheshimiwa Spika, nije katika suala zima la kilimo cha tangawizi, wote tunatambua kwamba kwa kipindi hiki cha *Corona* tangawizi imekuwa ni kilimo ambacho kimeleta tija sana nje na ndani ya Tanzania, hakuna familia ambayo inaweza ikalala bila kukosa kipande cha tangawizi. Kule Same Mashariki katika Mkoa wa Kilimanjaro wilaya ambayo inalima sana zao hili la Tangawizi, wakulima wamekuwa

wakilima kilimo hiki kwa shida sana kwa sababu ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilimo cha tangawizi kinahitaji maji ya kutosha, wamejaribu kujisukuma wao wenyewe na kutengeneza miundombinu ya maji kwa maana ya kutengeneza mabwawa Wapare wanaita *ndiva*. *Ndiva* ni mabwawa madogo.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali ili kusaidia kilimo hiki kiweze kukua iweze kusaidia wakulima wale kuwatengenezea mabwawa ambayo yatavuna maji kipindi cha mvua ili kilimo hiki cha tangawizi kiwe kilimo endelevu na kiweze kuwaingizia mapato wakulima wetu pamoja na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nije katika zao la vitunguu, zao la vitunguu linalimwa mkoani Kilimanjaro ni biashara kubwa sana kwa akina mama kule Kilimanjaro ukienda utakuta akina mama wamebeba makarai wanauza vitunguu, vitunguu vinalimwa Himo, vitunguu vinalimwa Hai, vitunguu vinalimwa Ruvu, vitunguu vinalimwa katika Kijiji cha Gonja, Mahore, Mpirani, Kalung'oyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakulima wanatumia nguvu nyingi sana katika kilimo hiki, lakini nguvu zao zote zinaishia pale ambapo maji yanakuwa hayapatikani ya kutosha. Bado niendelee kuiomba Serikali ili kilimo hiki kiweze kushamiri na kuwapatia mapato wananchi. Naomba iendelee, hoja yangu iendelee ile ile ya kuomba Serikali itengeneze mabwawa, na kilimo hiki kimeleta manufaa sana kule Kilimanjaro kwa sababu vitunguu vingi vinauzwa Kenya, soko la Himo ndipo wafanyabiashara wanaotoka Kenya wanapovuka pale na kununua vitunguu hivi, kwa hiyo, ni zao ambalo linawaingizia mapato. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Zuena Bushiri.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana nakushukuru. Mheshimiwa Daniel Awack atafuatiwa na Mheshimiwa Jacqueline Msongozi. Mheshimiwa Daniel Awack.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa nafasi kuweza kuchangia wizara hii ya kilimo. Katika Jimbo la Karatu tunalima mazao kama aina takribani nne hivi, tunalima mbaazi, tunalima ngano, tunalima vitunguu na tunalima mahindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kilimo hiki cha kitunguu kipo Tarafa ya Eyasi na ni tarafa ambayo ina-*history* kubwa kwa sababu ni tarafa inayolima vitunguu Afrika Mashariki inasambaza kwa mwaka mzima. Na kama alivyoeleza mzungumzaji aliyeongea kwamba vitunguu vyetu vinaenda Kenya kwa asilimia kubwa sana, na soko letu kubwa lipo Kenya kwa asilimia kama 90 hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile katika eneo hili la kitunguu pale Bonde la Eyasi Serikali ina skimu ambayo imegharimu zaidi ya bilioni moja na andiko tumeandika wizarani mara nyingi kwamba sasa ile miundombinu ya zaidi ya bilioni moja naa katika Kata ya Baray imeweza kufukiwa na mafuriko kwa mbele sasa miundombinu ile kwa takribani sasa miaka mitano haiwezi kufanya kazi na tumetuma andiko wizarani kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, lakini ukienda katika eneo hili la mbaazi kwa mwaka 2014/2015 mbaazi iliweza kufika shilingi 300,000 gunia moja mpaka shilingi 400,000 lakini kwa muda huu mbaazi inauzwa kwa gunia moja shilingi 25,000 mpaka shilingi 30,000, shilingi 35,000. Sasa nilikuwa nafikiri wizara wajiulize wale waliokuwa wanakula mbaazi 2014/2015 wamekwenda wapi au sasa kwenye nchi hizo nini kilichotokea kwamba mbaazi yetu sasa imeshuka kutoka shilingi 300,000 mpaka shilingi 400,000 kuja shilingi 30,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini katika eneo la ngano, sisi ni wakulima wa ngano na kubwa sana wanalima katika Tarafa

ya Bulumburu katika eneo hili la wakulima wa ngano watu wa *TBL* wanatoa vifaa vyote, lakini wameweka *limit* ukiivisha kwa heka moja wanasema usiivishe zaidi ya gunia saba, sasa wakulima wangu wao wanaivisha gunia saba mpaka gunia 10 mpaka gunia 12, lakini ukiivisha zaidi ya gunia saba, zile zingine zinazozidi hawataki kabisa na itakuwa ni mgogoro mkubwa katika Tarafa ile ya Bulumburu katika eneo hili la wakulima wa ngano.

Mheshimiwa Spika, sasa wenzangu watu wa wizarani wanatakiwa hilo waliangalie kwamba wanaweka *limit* kwamba heka yako ikitoa zaidi ya gunia saba ina maana hiyo utajua mahala pa kwenda kuuza, kwa maana watu wa wizarani waangalie sana hilo katika Tarafa ya Bulumburu na imetokea mara nyingi sana na mwaka jana ilitokea na kukatokea mgogoro mkubwa mpaka wananchi wale wakashindwa kulima zao hili la ngano kutokana na kwamba mgogoro unaotokea kwenye kampuni ya *TBL*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini katika eneo lingine la mahindi wizara sasa hivi bei ikiwa 20,000, 25,000 watasema mipaka ipo wazi, lakini ikatokea bei ikaenda kwenye 60,000, 70,000 wanafunga mipaka wakidhani kwamba ndani ya nchi hii kuna njaa ya chakula. Lakini, nashauri wizara kwa muda mrefu kama ilivyokuwa mpaka sasa uko wazi uweze kuwa wazi kwa muda wote wa miaka ijayo, ili wananchi hawa waweze kupata masoko yao maeneo mengine. Kwa wale wanaotokea Kanda ya Kaskazini na imetokea mara nyingi Mkuu wa Mkoa anaweza akatokea akasema kwenye ndani ya mkoa wake kuna njaa, wakati kuna maeneo mengine mahindi yanalimwa mengi yanatakiwa yatolewe kwenye hiyo mikoa mingine ziende kwenye mkoa huo ambao Mkuu wa Mkoa anajidai kwamba Mkoa wake una njaa.

Mheshimiwa Spika, sasa imeshatokea mara nyingi kwamba Wakuu wa Mikoa kusema mikoa yao ina njaa na kwamba watu wa mikoa mingine wanashindwa kuuza mazao yao iwe fursa kwenda kuuza mazao haya kwenye mikoa mingine ambayo ina shida ya chakula. Wenzangu wa Kanda ya kule Ruvuma watu jana waliongelea kwamba kule kwao

mahindi yanakosa soko sasa kama kuna mkoa mwingine ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawezi kufunga na imetokea mara kwa mara katika Mkoa wa Kilimanjaro, katika Mkoa wa Arusha, Tanga wakisema kwamba kwenye ukanda ule kuna njaa na mimi nadhani hakuna siku itatokea sisi watanzania tukaagize mahindi Kenya sisi tutaendelea kuuza mahindi Kenya na maeneo mengine kwa nchi zilizotuzunguka ndani ya Tanzania hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana wenzangu wa wizara wasifunge mipaka hii kwa muda muda wafungue mipaka hii kwa muda wote wa miaka yote ambayo sasa wakulima wa Tanzania ili waendelee kupata fursa ya kuweza kuuza mazao yao maeneo mengine ndani ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina mengi sana ya kuongea lakini wenzangu wa wizarani nilikuwa nafikiri kwamba sasa ni muda, lakini leo wametuletea makaratasi haya wakidai kwamba tuweze kuandika maeneo yenye skimu. Sasa wasiwasi wangu ni kwamba, ina maana hii wizara haina watalaamu mpaka sisi wabunge watuletee ndiyo tuwaletee hapa kwenye Bunge hili tuwaandikie kwamba kuna skimu sehemu fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna vitu vingine vya kushangaza katika wizara hii ya Kilimo, leo Mbunge nilete skimu ina maana hakuna mtaalam kwenye Ukanda huu wa Jimbo la Karatu wa kuleta taarifa kwenye wizara hii kusema kwamba kuna skimu iliyolala, kunaskimu inayoendelea kufanya kazi, leo tunaletewa sisi Wabunge tujaze hizo nafasi kwa taaluma ipi tulizonazo sisi Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wizara hii inatakiwa ijitafakari sana katika maeneo haya na naamini kwamba inaonekana uwajibikaji kwa watumishi wa eneo hili la kilimo wapo nyuma mno hawaendi na nchi hii ya Tanzania jinsi inavyokwenda. Watu wa wizara waangalie sana hili suala lakini vile vile ni....

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Daniel Awack.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, huyo ni mbunge wa Karatu na ni mmoja wa wakulima wakubwa kule Karatu hata Mheshimiwa Cecilia Paresso anamfahamu vizuri. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Jacqueline Msongozi.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, nakushuru sana, na ninaomba Mwenyezi Mungu aniongoze katika mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, naanza na Chama cha Msingi cha UMANA katika Kata ya Lisimunji, Wilaya ya Namtumbo. Kwenye hiki chama kuna mgogoro mkubwa sana Mwenyekiti na viongozi wengine wa chama hiki wametumia fedha za chama hiki vibaya. Kwa hiyo, wananchi ambao ni wanachama wameamua kumkataa huyu Mwenyekiti, lakini kilichojitokeza sasa wakati wa zile vurugu za kumkataa yule Mwenyekiti Diwani alijitokeza akaenda kushirikiana na wale wananchi kwa ajili ya kutaka kujua hatma ya suala zima la chama hiki juu ya huyo mwenyekiti na viongozi wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini viongozi kutoka wilayani kwa maana ya Serikali wakaenda wakamchukua yule Diwani wakamweka ndani, jambo ambalo si sawa, Diwani alikuwa anatetea haki za wananchi wake, lakini amewekwa ndani hii si sawa na niombe Serikali yangu, niiombe Serikali ishughulikie suala hili kupitia waziri mwenye dhamana aende akachunguze kule kulikuwa na tatizo gani na ikiwezekana huyu Diwani alipwe fidia kwa kufedheheshwa na kuwekwa ndani wakati akitetea maslahi ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ni kuhusu na suala la ushirika, ushirika kupitia *AMCOS* na *UNION* mimi nadhani kwamba hawa watu hawajajipanga vizuri, hawako sawa, kupitia *AMCOS* na *UNION* hawa watu hawana

wanachokifanya cha kuwasaidia wanachama badala yake wameweka kama ni sehemu yao ya kujinufaisha wao wenyewe migogoro imekuwa mingi na wananchi hawasaidiwi kwa namna yoyote ile na ndiyo maana kumekuwa na kelele nyingi kuhusiana na suala la stakabadhi ghalani. Wananchi hawahitaji stakabadhi ghalani inayohusiana na mazao madogo madogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, stakabadhi ghalani imeletwa na Serikali kwa maana nzuri kabisa ili iweze kuleta tija na imefanya vizuri sana kwenye mazao makubwa kama korosho, pamba lakini kwenye ufuta, soya na mazao mengine madogo madogo ambayo yanakwenda kumsaidia mkulima haijafanya vizuri. Mkulima mdogo amelima ufuta maana ni zao ambalo linamsaidia auze aweze kujikimu kwa mambo madogo madogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali inavyoingilia kati na kusema kwamba mwananchi huyu apeleke zao hili kwenye stakabadhi ghalani maana yake ingekuwa ina tija kwa wananchi hawa wasingekuwa na kelele.

Mheshimiaw Spika, nitoe ushauri kwa Serikali hii, irudi ikajipange upya iondoe suala la stakabadhi ghalani kwenye mazao haya madogo madogo iache kwenye mazao makubwa kama korosho na mazao mengine lakini siyo ufuta. *(Makofi)*

## TAARIFA

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Msongozi unapewa taarifa.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, napenda tu kumpa taarifa mzungumzaji, anayoyazungumza ni ya msingi zaidi na hii ndiyo sababu unaona Mkoa wa Dodoma leo hii hawalimi zao la ufuta. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana, Mheshimiwa Msongozi endelea.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, sasa mtani wangu wewe umechangia asubuhi halafu unanipotezea muda.

Mheshimiwa Spika, namba choroko, soya, ufuta hivi havina haja ya stakabadhi ghalani. Kwa mfano, wanawake wa Mkoa wa Ruvuma unapolima mahindi, korosho, tangawizi unaweka shamba dogo la mama kama kuna UPATU, *VICOBA*, kumpeleka mtoto zahanati na mambo mengine kadha wa kadha ndio ule ufuta unasaidia. Ukimwambia mwanamke achukue ule ufuta debe mbili apeleke huko akasubiri, mnamtakia nini huyu mwanamke wa Mkoa wa Ruvuma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala hili haliwezekani asilani abadani. Mimi niwaombe Waziri na Naibu Waziri waje na majibu mazuri wakati wa *wind-up* waondoe suala hili la stakabadhi ghalani kwenye mazao madogo madogo. Mazao madogo madogo haya ni aibu jamani kwani ndiyo yanamsaidia mwananchi. Siku moja Mheshimiwa Flatei alisema ataruka sarakasi mimi kuhusiana na suala hili nauliza nipande juu ya meza? *(Makofi)*

**SPIKA:** Hapana.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Nipande juu ya meza kama Kanuni inaruhusu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Msongozi usipande juu ya meza.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, kwa kweli kwa Mkoa wa Ruvuma hatukubali. Naomba suala hili liondolewe na Wizara ikajipange upya hata mwakani waje wakati wametoa elimu kwa wananchi lakini pia...

**SPIKA:** Mheshimiwa Msongozi usipande juu ya meza leo hapa kitaeleweka kuhusu stakabadhi ghalani. Waziri yuko

hapa, leo hapa leo hapa, malizia Mheshimiwa Msongozi nilitaka tu usipande juu ya meza. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa sababu mimi nilisema leo labda ningepanda juu ya meza dunia ijue na Tanzania nzima waone kwamba hatuhitaji suala hili.

Mheshimiwa Spika, nikushawishi uniongezee dakika moja niendelee kuongelea suala hili. Wako vijana wetu wamemaliza vyuo, wametoka JKT wamefanya mafunzo lakini wamerudishwa nyumbani ajira hakuna. Hawa vijana wamejikita kulima mazao ambayo yanaweza kuwaletea pesa kwa haraka ikiwemo ufuta, soya na vitu vingine lakini wanakatishwa tamaa. Hili zao la ufuta sasa limekuwa kama vile mtu unalima bangi, ukishavuna debe mbili za ufuta basi unafuatwa unazingirwa. Hata mambo mengine ndani ya nyumba hayawezi kuendelea vizuri kwa sababu unafuatiliwa huko yaani muda wowote unagongewa kuulizwa zile debe mbili ziko wapi? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, vijana wetu hawa watakuwa majambazi sasa kwa sababu wanataka wawekeze kwenye ufuta lakini Serikali inawapiga danadana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Msongozi leo kitaeleweka hapa kuhusu suala hili siyo kesho.

Tunaendelea na Mheshimiwa Jeremiah Amsabi, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Ndulane.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii ya kuchangia Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naipongeza sana Wizara hii ya Kilimo kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya ambapo tunaona kwa mwaka jana imechangia zaidi ya asilimia 58 ya ajira katika nchi yetu. Ukiangalia Serikali yetu katika mapato inavyo vyanzo vingi, ikiwemo kutoka katika bandari, madini na utalii lakini tukienda kwa kipato cha mwananchi mmoja mmoja kule vijijini zaidi ya asilimia 95, 98 sehemu zingine wanategemea kilimo peke yake. Leo kilimo kinapoendelea ku-*perform poorly* maana yake wananchi watakuwa na hali mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, kule tunapotoka Wabunge wote wanafahamu hali za wananchi ni mbaya sana na hakuna *initiative* ya maana na ya pekee inayoweza kusaidia sana, yenye *high potential for poor growth* kama kuwekeza katika kilimo. Hata hivyo, *trend* zinaonesha sasa hivi hasa kwenye Jimbo langu na Majimbo mengine jirani naona kilimo kinaendelea kushuka na kila wakati watu wanaendelea kukata tamaa. Sababu kubwa ni masoko, kwa kweli masoko yanaendelea kuwa shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikitoa mfano, katika takwimu za Shirika la Chakula na Kilimo la Dunia *(FAO)* Agosti, 2020 wameonesha Tanzania ni nchi ya tatu katika Afrika kwa kulima tumbaku kwa wingi ambapo Kenya ni ya tisa na South Africa ni ya saba. Hata hivyo, katika uuzaji wa *cigarette,* Shirika la *FAO* limeonesha South Africa ni ya kwanza, Kenya ni ya pili na Tanzania ni ya sita. Kwa hiyo, unaona wenzetu wamewekeza sana katika viwanda vya kilimo. Kwa hiyo, lazima Wizara sasa iende kuangalia inavyoweza ku-*priotize* katika masoko. *Motivation* kubwa sana ya kilimo kwa wananchi ni masoko tu kuwepo, haya mambo mengine yatakuja. Tukiwa na masoko ya uhakika wananchi watalima sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaombe sana Wizara waangalie pia katika suala hili zima la kilimo biashara, bado kuna *high cost of production* katika nchi yetu kwa sababu ya *inputs* za *agriculture* zinauzwa kwa bei kubwa. Kwa mfano, mbolea au pembejeo kwa ujumla wake gharama ni kubwa, sasa

hatuwezi kushindana katika masoko na wenzetu wakati sisi uzalishaji wetu ni gharama kubwa ukilinganisha na wenzetu. Ukienda nchi zingine zao lilelile katika *unit* ileile *price* inakuwa chini ukilinganisha na kwetu kwa sababu *inputs cost* yake iko chini sana. Kwa hiyo, niombe sana Wizara iende kuhangaika sana na suala hili.

Mheshimiwa Spika, watu hawashindwi jambo kwa sababu hawana uwezo wakati mwingine watu wanashindwa kwa sababu ya *wrong priority*. Kwa hiyo, niombe *priority* kubwa sana katika Wizara hii sasa i-*shift* kwenda kuwekeza fedha nyingi katika kutafuta masoko, tutafute masoko ndani na nje ya nchi kwa wingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe sana pia Wizara iende kuangalia, wakati mwingine hatufanyi vizuri katika masoko kwa sababu ya *unfavorable terms of trade.* Ukiangalia wenzetu Kenya katika *exportation* maeneo mengi kuna *free tariffs* lakini kwetu bado *cost* zetu hata katika kusafirisha ni kubwa. Kwa hiyo, niombe sana Wizara iangalie suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna kazi ilifanyika pale Serengeti katika Skimu ya Nyamitita. Leo ukienda pale Nyamitita kumewekwa fedha nyingi na Serikali lakini bado skimu ile ya umwagiliaji haijakamilika niombe Wizara waende kuikamilisha.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo mengine mazuri sana ya umwagiliaji ambapo wananchi wanapambana sana lakini wanafeli kwa sababu hawajapata *support* ya Serikali.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Spika, maeneo kama ya Isenye, Nata, Nyambuleti yanahitaji skimu za umwagiliaji.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jeremiah Amsabi. Tunaendelea na Mheshimiwa Francis Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuzungumza. Kwanza, napenda kuishukuru na kuipongeza Wizara ya Kilimo kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya kwa wakulima wetu na kuongeza kasi ya maendeleo katika sekta hii ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, mimi napenda kujikita katika zao la ufuta. Wilaya ya Kilwa ninayotoka ni wilaya ambayo inaongoza kwa kilimo cha zao la ufuta katika Mkoa wa Lindi. Katika zao hili kumekuwa na changamoto kubwa hasa wakati wa minada. Katika mwaka uliopita Wilaya nzima ya Kilwa yenye vijiji 90, kata 23, tulishuhudia tukiwa na kituo kimoja tu cha mnada wa zao hili la ufuta hali ambayo ilipelekea kuwepo kwa biashara ya holela ya zao hili la ufuta almaarufu kule tunaita chomachoma, wenzetu wale wa Kagera nilisikia pale asubuhi kuna kitu wanaita butura. Kule kwetu tunaita chomachoma yaani biashara ya magendo ambayo ina dhulumati nyingi kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, vilevile wapo wakulima walikata tamaa kuuza zao hili wakabaki na ufuta wao mpaka mwaka huu. Hivi napozungumza sasa hivi hawajauza ufuta wa mwaka jana kutokana na hii hali ya kuwa mnada ni mmoja tu na uko eneo la mbali, ambalo ni zaidi ya kilometa 200 toka kule ambako mashamba yaliko. Pia mzunguko wa fedha ukawa umepungua lakini hata bei kwa wale ambao walimudu kupeleka sokoni au mnadani mazao yao walijikuta wanauza kwa bei ya chini sana. Hii ni kutokana na kwamba wale wanunuzi walikuwa wanafidia gharama zao za usafirishaji wa yale mazao toka kwenye vyama vya msingi. Kwa hiyo, kwa ujumla kumekuwa na shida katika huu mfumo wa minada.

Mheshimiwa Spika, jana kulikuwa na taharuki kubwa katika Wilaya ya Kilwa kwa sababu ratiba ambayo ilitumika mwaka jana ndio ambayo jana imetangazwa tena, tuna kituo kimoja tu cha mnada kupitia Chama cha Ushirika cha Msingi cha Muungano kule Kilanjelanje. Naomba Wizara itusaidie kuhakikisha kwamba inaongeza vituo vya minada ili wakulima wetu waweze kuuza mazao yao maeneo ya karibu.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuwa na vituo vingi itasaidia wakulima kushiriki kikamilifu na kuwa na *ownership* wakati mnada unafanyika tofauti na hali ilivyo sasa. Mnada ukiwa mbali wakulima wanashindwa kuhudhuria mnada badala yake wanakuwa na wawakilishi tu ambao pengine ni viongozi wa vyama vya msingi na hatimaye unakuta hata bei wanayoipata inakuwa ni shida. Kwa hiyo, naomba Wizara ilisimamie suala hili, ile ratiba iliyotolewa na Chama Kikuu cha Ushirika cha Mwambao iweze kurekebishwa tupate hata maeneo matatu au manne katika Wilaya ya Kilwa ya kufanya minada na kuuza mazao yetu bila shida ili wakulima wetu waweze kunufaika na bei ambazo zinaridhisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo napenda kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Kilimo ni suala la Kampuni ya Mbolea Tanzania. Katika taarifa ya *CAG* kampuni hii imekuwa ni miongoni mwa taasisi za umma 11 ambazo zilishindwa kuwasilisha hesabu zake za mwaka kwa *CAG* katika mwaka wa fedha uliopita. Siyo mwaka huo tu, hata miaka mitano, sita iliyopita kulikuwa na hali kama hiyo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Ndulane Francis, dakika zako zimekwisha.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Kwenye *gallery* asubuhi nilikuwa na wageni sijui kama bado wapo Dkt. Jacqueline Mkindi, Mtendaji Mkuu wa *TAHA*. Karibu sana, tunafarijika kwa uwepo wako. Pia yupo Ndugu Deo Tarimo, ametoka, ahsante sana ni mfanyabiashara wa mazao ya kilimo ya biashara.

Tunaendelea na Mheshimiwa Aysharose Mattembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Ramadhani Ighondo. *(Makofi)*

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mezani. Kipekee nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema. Nitajielekeza moja kwa moja kuchangia zao la alizeti pamoja na kitunguuu endapo muda utatosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Singida ni Mkoa unaoongoza kwa kuzalisha zao la alizeti. Serikali imekuwa ikisema kwamba zao hili ni la kimkakati lakini mkakati huu upo katika maandishi na wala si kwa vitendo. Niiombe sana Serikali mkakati huu wa kuzalisha zao la alizeti uwepo kwa vitendo ili wananchi wa Mkoa wa Singida waweze kunufaika na ukulima wenye tija wa zao hili la alizeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mkoa wa Singida wamekuwa wakikabiliwa na changamoto nyingi katika kulima zao hili la alizeti. Hivi majuzi kulikuwa na uhaba mkubwa wa mafuta ambayo yanatokana na zao la alizeti. Kama Serikali ingetoa kipaumbele basi nina uhakika kabisa zao hili la alizeti lingeweza kumaliza changamoto kubwa ya uzalishaji wa mafuta lakini pia lingeweza kukuza uchumi wa nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Singida ndiyo inayoongoza kwa kulima alizeti bora kabisa Afrika ya Mashariki na Afrika ya Kati lakini kilimo hiki cha alizeti kimekuwa hakipewi umuhimu. Niiombe sana Serikali iweze kufungua milango kwa wakulima wetu kwani wakulima wengi wamekata tamaa na hata kwa msimu uliopita, alizeti hii imezalishwa kwa kiwango cha chini sana. Kwa kuwa, Serikali inayo dhamira nzuri ya kuanzisha

mashamba ya kimkakati, basi itenge maeneo ambayo sasa yatakwenda kufungua fursa za uzalishaji wa kilimo hiki cha alizeti katika halmashauri zetu kwani halmashauri za Mkoa wa Singida zote zinalima zao hili la alizeti, zikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Mkalama, Ikungi, Manyoni pamoja na Iramba.

Naishauri sana Serikali iweze kufungua milango kwa wawekezaji waje kuwekeza katika zao hili la alizeti ili sasa tija iweze kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa katika zao letu hili la alizeti ni uzalishaji wa mbegu. Niiombe sana Serikali iweze kutoa kipaumbele kwa taasisi zetu hizi za *ASA* pamoja na *TARI,* ambazo zimekuwa zikizalisha mbegu aina ya *records* ziweze kupewa bajeti ya kutosha ili ziweze kuzalisha mbegu hizi na kuweza kumaliza changamoto hii. Wakulima wetu wamekuwa wakinunua mbegu hii kwa Sh.3,500 kwa kilo lakini imekuwa ikizalishwa tu kwa tani 500 kwa mwaka wakati viwanda vyetu vinaweza kuzalisha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA**: Ahsante Mheshimiwa Aysharose Mattembe.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ramadhani Ighondo.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii angalau niwasemee wananchi wenzangu ambao kwa asilimia 95 ni wakulima katika Jimbo langu la Singida Kaskazini. Uhai wa wana Singida Kaskazini unategemea sana zao la alizeti, lakini kilimo hiki wamekuwa wakilima kwa jembe la mkono jambo ambalo limeshindwa kabisa kutuletea tija ya uzalishaji wa zao hili kama ambavyo ingeweza kuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kiwango kikubwa zao la alizeti kuanzia kupanda mpaka kuvuna ni miezi mitatu tu lakini mkulima anakosa kulima kiwango cha kutosha kwa sababu ya changamoto hasa hasa za vitendeakazi. Zana za kilimo, mbegu pamoja na mitaji. Nikuombe sana na niiombe Serikali, Wizara hii watuletee mbegu na mbegu hizi ziwe kwa bei ya chini ili wakulima waweze kumudu gharama. Haiwezekani kilo mbili ziuzwe shilingi 60,000 na zaidi halafu gunia moja lije liuzwe 50,000. Hii inamuumiza sana mkulima na inampotezea muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kama haitoshi niombe sasa Serikali tuhakikishe kwamba tunaleta kilimo cha *irrigation,* cha umwagiliaji. Katika Jimbo la Singida Kaskazini mabwawa matatu yameungana imekuwa ziwa. Niombe sasa maji haya yatumike ipasavyo kwa kuleta miundombinu ya umwagiliaji ili vijana waliojitokeza waliohamasika kutumia maji haya walime hata wakati wa kiangazi. Bwawa la Masoqeda, Kisisi, yameungana yamekuwa ni ziwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana maji haya Serikali iyatumie ipasavyo kwa kuhakikisha vijana wanapelekewa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji ili tuweze kuongeza tija katika uzalishaji wa alizeti na hata viwanda vilivyopo pale viweze kupata *raw materials* ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu sasahivi viwanda vinakosa malighafi kwa sababu tunazalisha kwa kiwango kidogo sana na kwa mwaka huu alizeti haijalimwa kwa sababu ya kukosekana mbegu na bei kuwa ndogo. Kwa hiyo, watu wanaamua waende kwenye mazao mengine na kuachana na alizeti. Ndiyo maana mnaona mwaka huu mafuta yamepanda bei na yameadimika kabisa. Kwa hiyo, niombe sana eneo hili litazamwe kwa jicho tofauti sana. Nashukuru kwamba zao la alizeti limeingizwa kwenye yale mazao ya kimkakati, basi isiwe ni kwenye makarasha tu. Yaende kwenye utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongee kidogo kuhusu zao la kitunguu ambalo ndilo hasa sisi watu wa Singida tunalima

kitunguu bila kutumia madawa. Ni kilimo cha asili kabisa, unapanda kitunguu, unavuna bila kutumia dawa. Kitunguu hiki hakijawekewa mkakati, ni mkulima mwenyewe anahangaika kwa nguvu zake binafsi, hakuna mkono wa Serikali hata kidogo. Sisi tunaishia tu kujivunia kwamba watu wanalima lakini hatuwasaidii. Tuhakikishe tunawapelekea hawa watu mbegu. *Subsidies* zipelekwe kwenye mbegu lakini pia tuwape vijana mitaji waweze kuongeza tija, waweze kuzalisha vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa spika, lakini hapo hapo eneo la masoko, soko la kitunguu lipo lakini shida ni utaratibu mbovu unaopatikana pale sokoni. Mkulima anapopeleka zao lake sokoni utaratibu ni mbovu anaishia kuteseka madalali wajanja wajanja.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, sasa ni vyema utaratibu mzuri uwekwe ili watu hawa nao wanufaike na kilimo chao hiki wanachoteseka nacho muda mrefu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa haya machache. Naunga mkono hoja lakini niiombe Serikali itusikie haya tunayoyazungumza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ramadhani Ighondo, Mbunge wa Singida Kaskazini. Sasa naomba nimuite Mheshimiwa Martha Mariki na baada ya Martha Mariki atafuata mchangiaji wetu wa mwisho Mheshimiwa Dkt. Basiru Ally Kakurwa. Mheshimiwa Dkt. Bashiru utapata dakika 10 Mheshimiwa Martha Mariki. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu ya kilimo. Kwanza naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jinsi

ambavyo wanaendelea kushughulikia matatizo yanayojitokeza katika Wizara hii ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitajikita moja kwa moja kwenye suala la masoko. Mkoa wangu wa Katavi, wananchi wa Mkoa wa Katavi kwa asilimia kubwa sana wamekuwa wakitegemea kilimo. Lakini wanazalisha mazao mengi, masoko yamekuwa ni tatizo na ukizingatia kwamba pembejeo zimekuwa na bei sana. Katika Mkoa wetu wa Katavi huwezi kuamini, gunia la kilo 100 linauzwa hadi shilingi... *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tusikilizane, tupunguze sauti. Tumsikilize Mbunge mwenzetu. Huyu anaitwa Mheshimiwa Martha Mariki na anafunga ndoa hivi karibuni sana, kwa hiyo... *(Makofi/Vigelegele)*

Zile kadi za michango Mheshimiwa hakikisha zinafika kote. Endelea kuchangia.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Spika, nilichokuwa nasema wananchi wa Mkoa wa Katavi hususan akina mama maana jambo lolote katika Taifa hili linapokuwa suala ni gumu sana sana lazima limguse mwanamke yeyote wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa maana kuwa, katika Mkoa wangu wa Katavi akina mama na akina baba wa Mkoa wa Katavi wamekuwa wakizalisha mahindi kwa wingi lakini masoko yamekuwa ni mtihani. Gunia la kilo 100 limekuwa likiuzwa mpaka shilingi 18,000. Hapo tunamuumiza sana mkulima huyo ukizingatia pembejeo zimekuwa zikiuzwa bei sana. Hivyo, niiombe sana Serikali kupitia Wizara yetu ya Kilimo waweze kumtamfutia mwananchi huyu masoko ya uhakika ili tuhakikishe mkulima huyu tunamkomboa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala langu la pili nitakalozungumzia ni suala la *irrigation schemes.* Katika Mkoa wetu wa Katavi tuna maeneo ambayo ni *potential* yakiwepo maeneo kama ya Mwamapuli, Mwamapuli tuna takriban

hekta 13,600 ambazo zinaweza kukubali kilimo cha umwagiliaji. Hivyo, niiombe sana Serikali katika Mkoa wetu wa Katavi hususan eneo la Mwamapuli ambalo ni *potential* sana kwa kilimo cha mpunga, Mkoa wa Katavi umekuwa maarufu sana kwa kulima mpunga ambao ni *first class* ambao hata nchi za jirani zimekuwa zikija katika Mkoa wetu wa Katavi kuja kukusanya mpunga huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo, niiombe sana Wizara ya Kilimo katika eneo la Mwamapuli tuweze kuwekeza kwenye *irrigation schemes* ili mwananchi wa mkoa huo aweze kulima, yani tufanye bandika bandua ili tuweze kumkomboa mwananchi na Taifa letu liweze kupata uzalishaji ulio bora. Wananchi wa Mkoa wa Katavi tunalima mpunga ambao ni *first class* na nikuambie tu Mkoa wetu wa Katavi mchele unaotoka pale ni mchele ambao ni *first class,* mchele wa kienyeji. Mchele ambao ukiupika lazima jirani asikie harufu kwamba ni mchele wa kienyeji uliopikwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo, niiombe sana Serikali tuwekeze eneo hili ili mwananchi yule aweze kulima na Taifa letu liweze kuingiza mapato kupitia kilimo. Niiombe sana Serikali yangu Sikivu na tukufu. Tukiwekeza katika kilimo tutakuwa tumemkomboa mwananchi kwani kilimo ni uti wa mgongo na wananchi wengi wa maeneo yale wanategemea sana kilimo hivyo tuwekeze hasa katika uchimbaji wa mabwawa makubwa ambayo tukiwekeza katika mabwawa makubwa yatasaidia katika kilimo hicho kikubwa na pia akina mama wa Mkoa wa Katavi watafanya kilimo cha mbogamboga na hivyo tutakuwa tumemgusa mwanamke wa Mkoa wa Katavi kwa kulima pia mbogamboga kwa kutumia umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo, niiombe sana Serikali, kwa kuwa muda ni mchache pia tuna maeneo mengine kama eneo la Kalema. Kalema ni eneo ambalo ni *potential,* hivyo niiombe Serikali tukiwekeza katika eneo hilo tutaweza kufanya kilimo chenye tija. Ukizingatia kwamba katika eneo la Kalema kumekuwa kuna miradi ya kimkakati ikiwepo ujenzi wa bandari ambao unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tukitumia kilimo tukazalisha kwa wingi na tukatumia bandari yetu ambayo tunajengewa na Serikali yetu Sikivu katika maeneo haya ya Kalema, tutaweza kwenda kufanya biashara na majirani zetu wa Kongo Kalemi kwa kupeleka mazao yetu kwa kutumia bandari hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na Serikali imetuhakikishia kwamba tunaenda kujengewa meli za kusafirisha mizigo. Hivyo, niiombe sana Serikali tukiwekeza katika kilimo tutakwenda kumkomboa mwananchi na Serikali yetu itaingiza mapato na Taifa letu litaenda kusonga mbele. Pia, tutakuwa tumemsaidia kijana wa Kitanzania kwa kuweza kupata ajira nyingi sana zitakazotokana na kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo kwa unyenyekevu mkubwa ninaiomba sana Serikali kupitia Waziri wa Kilimo aweze kutusaidia wananchi wa Mkoa wa Katavi kwa kufanya uwekezaji katika maeneo ambayo ni *potential* ili Serikali yetu iweze kumsaidia mwananchi kujikomboa. Wananchi wa Mkoa wa Katavi wanaipongeza sana Serikali kwa juhudi zao wanazoendelea kupambana ili kuhakikisha kwamba tunatatua matatizo ya wananchi. Hivyo, wananchi wa Mkoa wa Katavi tunaamini Serikali yetu Sikivu itatusaidia kwa kuweza kuwekeza katika maeneo hayo ambayo ni *potential.*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Martha Mariki kutoka kule Rukwa.

**MBUNGE FULANI:** Ni Katavi…

**SPIKA:** Ni Katavi, eh? Ah, huko huko kwa wachawi huko. *(Kicheko)*

Ahsante sana. Sasa nimkaribishe Mheshimiwa Dkt. Bashiru kwa dakika 10 halafu atafuatia Mheshimiwa Naibu Waziri moja kwa moja.

**MHE. BALOZI DKT. BASHIRU A. KAKURWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kw akunipa nafasi ya kuongea katika Bunge hili tukufu kwa mara ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru pia kwa kunipa upendeleo wa muda wa dakika 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara ya kwanza kuongea, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuneemesha na kuivusha nchi yetu katika kipindi cha misukosuko baada ya kupata msiba mkubwa ambao haujawahi kutokea katika historia ya nchi yetu. Na, nina uhakika Mwenyezi Mungu hatatutupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yamekuwepo majaribio ya kupitisha maneno na kutuchonganisha na wakati mwingine kudhalilisha watu na kutunga maneno ya uwongo ili nchi itikisike lakini nasema wameshindwa na wamelegea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze viongozi wetu wapya. Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu na Dkt. Isdory Mpango Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa kushika barabara usukani na hatamu za uongozi wa Taifa letu na kutuwekea mazingira ya matumaini huko tunakoelekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni Mbunge wa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais, na ni upendeleo mkubwa kwa sababu ziko nafasi 10 tu za Kikatiba na hadi sasa tuko nane. Nimshukuru sana kwa kuniamini na nimuahidi kwamba sitamuangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe kwa kuongoza Bunge letu kwa weledi na kwa umakini na hasa kwa siku hizi mbili tangu jana na leo wakati Bunge hili linajadili bajeti ya Sekta Muhimu kwa uhai wa Taifa letu, Sekta ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze pia Wanasimba, Timu ya Taifa kwa kutufuta machozi angalau ya kurejesha

mabao matatu kati ya manne. Niwape moyo haikuwa riziki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nianze kuchangia, tangu jana kusema ukweli nimeandika mengi katika *notebook* yangu na mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kilimo inayoongozwa na mama shupavu Mheshimiwa Dkt. Christina Ishengoma. Naweza nikasema kwamba sina jipya la kuongea, mengi yamezungumzwa. Baadhi yapo kwenye hotuba ya Waziri, mengine yapo kwenye hotuba ya Kamati. Kwa hiyo, nitakachokifanya ni kufanya muhtasari wa yale ambayo nimeyaona yanajitokeza moja kwa moja yanayohitaji kufanyiwa kazi na kamati yetu lakini pia na Bunge lako. Wabunge wamezungumza kwa uhakika, kwa uchungu lakini wametoa mawazo mazuri sana ambayo yanaweza yakatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri au mbaya ninaweza nikasema kilimo chetu kimepata sifa tatu katika mjadala wa tangu jana. Sifa zote tatu ni mbaya, ya nne ndiyo nzuri tu. Sifa ya kwanza ni kwamba kilimo chetu kwa kweli tija yake ni duni. Uduni wa tija hiyo unaathiri uzalishaji wa mazao yote ya kilimo. Hiyo sio sifa nzuri na maoni ya Waheshimiwa Wabunge ni kwamba tubadilishe sifa hii mbaya kwa kuongeza tija na wote tunakubaliana kuhusu sifa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sifa ya pili ambayo imesemwa nzuri sana na ni mbaya pia ni kwamba mazao mengi ya kilimo yanayozalishwa yanauzwa bila kuongezewa thamani. Sifa ya tatu mbaya, ni kwamba kilimo chetu hakijapata masoko ya uhakika na yenye manufaa kwa wakulima. Sifa moja nzuri iliyojitokeza ni kwamba Tanzania imejaaliwa kuwa na wakulima wenye huruma, wenye hisani na uungwana, wanazalisha kwa shida na kunyonywa lakini wameweza kuzalisha chakula cha kutosheleza nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kilimo chetu kinatuweka katika hali ya kuwa na usalama wa chakula. Hii sio sifa ndogo, tunapo mahali pa kuanzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kama sifa hizi tatu ndizo tunazotaka kuzibadilisha yamesemwa mengi mapendekezo ya kufanya. Wengine wameelekeza mawazo yao katika uongezaji wa bajeti ya kilimo, nakubaliana nao. Wengine wanataka tubadilishe mbinu zetu katika maeneo ya umwagiliaji, masoko n.k

Mheshimiwa Spika, bila shaka ni ya kwanza hiyo maana mimi ni *form one* humu. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Bado dakika mbili.

**MHE. BALOZI DKT. BASHIRU A. KAKURWA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachotaka kupendekeza ni kwamba Bunge lako la Kumi na Moja, limechangia sana kuleta mabadiliko makubwa katika Sekta ya Madini. Changamoto tuliyonayo kwa Bunge hili la Kumi na Mbili, ambalo nimepata bahati ya kuwa Mbunge, tujipe ajenda Bunge liweze kuwa na mchango wa uhakika wa kubadilisha Sekta ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge la Kumi na Moja, katika historia litatambulika kwa kuleta mabadiliko makubwa sana ya kisera na kisheria kwenye Sekta ya Madini na tumeona matokeo yake. Hili la Kumi na Mbili, chini ya uongozi wako na ndani ya Serikali chini ya mama Samia tujipe jukumu la kubadili Sekta ya Kilimo ili sifa hizi mbaya za tija duni, za ukosefu wa masoko na kutoyaongezea thamani mazao yetu ya kilomo zibadilike ili tufanane na Sekta zingine zinazobadilika haraka kama vile miundombinu, mawasiliano n.k. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nakuomba ama unaweza ukaelekeza Kamati yetu au kwa busara yako kufikiria namna ya kufanya kujibu maswali matatu yafuatayo. La kwanza, tunajifunza nini kutokana na mafanikio tuliyoyapata katika Sekta ya Kilimo lakini na makosa tuliyofanya katika Sekta ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yako mabadiliko huku nyuma yamefanywa. Tume ya Ardhi ilifanya kazi kubwa ikatusaidia

kuweka msingi wa kusimamia ardhi yetu. Tume ya Umwagiliaji Awamu ya Tatu, hata Tume ya Ushirika Awamu ya Nne na Sera zingine. Tusikimbie kufanya mabadiliko bila kujiridhisha kwa kufanya tathmini, wapi tumefanikiwa na wapi tumefanya makosa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili la kuzingatia, Bunge hili la Kumi na Mbili linaweza kutoa mchango gani mpya katika kuchochea mapinduzi ya kilimo. Suala la tatu, tuweze kujibu hoja kwa nini mabadiliko makubwa yaliyotokea nchini katika sekta za miundombinu, fedha, sayansi na teknolojia, ongezeko la watu, elimu, mawasiliano, havichochei ukuaji wa kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nilidhani kwa makofi hayo mngeweza kusimama angalau. Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Nakushukuru sana Mheshimiwa Bashiru Ally Kakurwa kwa mchango wako mzuri sana na kwa kweli, tunafarijika na kufaidika. Tunampongeza Mheshimiwa Rais, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kukuleta kuwa miongoni mwetu. Tunaamini kwa pamoja tutapiga hatua nyingi zaidi za maendeleo kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa Bunge hili ambalo kama alivyosema Mheshimiwa Bashiru la kufanya mabadiliko makubwa katika sekta ya kilimo, si rahisi kila Mbunge akapata nafasi ya kusema. Nimejitahidi sana, lakini bado nina watu kadhaa ambao walikuwa wanataka kuchangia jioni ya leo lakini haitawezekana.

*Actually,* nichukue nafasi hii tu kufafanua kwamba wakati bajeti hii ya Wizara ya Kilimo ina wachangiaji wengi kupindukia na ni kwa sababu hizi ambazo nimezieleza kwamba ukereketwa wa Waheshimiwa Wabunge kwenye sekta hii ni mkubwa sana, kesho tuna Wizara ya Ardhi lakini

ina wachangiaji wachache sana ambao tayari wameshaji-*register.* Kwa hiyo, tunafanya mabadiliko Wizara ya Ardhi yenyewe itachangiwa kwa siku moja, kesho peke yake, halafu Wizara ya Mifugo badala ya kuwa Ijumaa na Jumamosi sasa itakuwa Alhamisi na Ijumaa ya wiki hii, tarehe 27 na 28, siku mbili. *(Makofi)*

Jumatatu na Jumanne ambayo ilikuwa Wizara ya Maliasili na Utalii siku moja Wabunge wengi wameonesha *interest* ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Maliasili na Utalii kwa hiyo, yenyewe itakuwa siku mbili. Halafu Nishati itafuata Jumatano na Alhamisi kama ilivyopangwa kwenye ratiba. Kwa hiyo, tunabadilisha kwa kesho kuwa Ardhi siku moja, Mifugo na Uvuvi ni siku mbili, lakini inakuwa Alhamisi na Ijumaa na Jumatatu na Jumanne ni Maliasili na Utalii ambayo ilikuwa siku moja sasa itakuwa siku mbili. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hayo ndiyo mabadiliko ambayo tunafanya ili tuweze kuendana na hali halisi ya mambo. Nafanya hivyo kwa kutumia Kanuni ya 5 ambayo inanipa mamlaka ya kuweza kufanya mabadiliko ya hapa na pale katika mambo ya uendeshaji.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Waziri wa Kilimo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Uvuvi na Maji kwa kuwasilisha vizuri hotuba ya bajeti na Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Bunge. Pia niwapongeze sana wataalamu wa Wizara pamoja na wadau wa maendeleo kwa mchango mkubwa sana kwenye sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa umeainisha nafasi ya sekta ya kilimo katika uchumi wa Tanzania kwani sekta hiyo inaajiri asilimia 65 ya nguvu kazi ya Watanzania, huchangia asilimia 27.5 kwenye pato la Taifa, asilimia 24.7 fedha za kigeni na asilimia 60 ya malighafi ya viwanda hapa nchini. Kilimo huchangia asilimia 100 ya chakula kinachotumika hapa nchini. Kwa bahati mbaya

sana, umuhimu huu wa sekta ya kilimo haujaonekana kabisa kwenye bajeti ya Wizara. Kwa mfano, bajeti ya Wizara ya Kilimo ya mwaka 2021/2022 ni shilingi 294,162,071,000, hii ikiwa ni asilimia 0.08 ya bajeti ya Taifa ambayo ni trilioni 36.260.

Mheshimiwa Spika, Rais wa Awamu ya Sita alipohutubia Bunge alieleza kuwa Serikali yake itatoa kipaumbele kwenye sekta ya kilimo ili kuwakwamua wakulima wetu. Kwenye hili, Serikali haijazingatia ahadi ya Rais wetu. Asilimia 0.08 ya bajeti ya kilimo katika bajeti yote ya Taifa ni kidogo sana na haiendani kabisa na ahadi ya Rais ambaye ni kiongozi wetu mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kilimo ndio roho ya uchumi wa nchi yetu, ni vyema Serikali ikaiwezesha kikamilifu Wizara ya Kilimo ili waweze kutatua changamoto za wakulima.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali itekeleze lile Azimio la Malabo lililoazimiwa Equatorial Guinea na wakuu wa nchi za Afrika tarehe 26-27 Juni, 2014 ambapo waliazimia kuwekeza asilimia 10 ya bajeti zao za Taifa kwenye kilimo. Kwa mantiki hiyo, bajeti ya kilimo ingekuwa takribani shilingi trilioni 3.626.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali itawekeza kikamilifu kwenye kilimo, naishauri Wizara ya Kilimo iwekeze kwenye mambo makuu muhimu yafuatayo:-

(a) Utafiti wa mazao ya chakula na biashara (uzalishaji wa mbegu bora na mbinu za kuongeza tija); taasisi za utafiti wa kilimo ziwezeshwe.

(b) Utafiti wa udongo kwenye kila eneo linalolimwa ili kujua changamoto za rutuba ya udongo.

(c) Utafiti wa mabadiliko ya tabianchi.

(d) Utafiti wa masoko ya kilimo na kuzingatia intelejensia ya masoko.

(e) Kuboresha ushirika kwa kubadilisha sheria kandamizi za ushirika na kusaidia kwenye eneo la uongozi wa ushirika.

(f) Uboreshaji wa shughuli za ugani.

(g) Uzalishaji wa mbegu bora za mazao ya kimkakati kupitia Wakala wa Mbegu *(ASA).*

(h) Uwekezaji wa kutosha kwenye kilimo cha umwagiliaji, kwa kuelekeza fedha kwenye maeneo yenye maji ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa pili ni kuhusu fursa za kilimo cha umwagiliaji katika Jimbo la Moshi Vijijini, Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kilimanjaro una fursa kubwa sana za kilimo cha umwagiliaji. Hii ni kutokana na ukweli kwamba Kilimanjaro kuna mito mingi inayoanzia mlimani na kuishia Bahari ya Hindi bila kutumika kikamilifu kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali ijenge skimu mpya na kukarabati ile mifereji ya asili ili haya maji yatumike kuzalisha mazao badala ya kuishia baharini.

Katika jimbo langu la Moshi Vijijini, ninaishauri Serikali ifanye yafuatayo:-

Mosi, Serikali iwekeze kikamilifu kwenye kuboresha na kujenga upya mifereji ya asili. Miundombinu hii imechoka, na ni muhimu sana kwenye kilimo cha kahawa, ndizi, mbogamboga na matunda. Mifereji hii ikiboreshwa kikamilifu itasaidia katika *block farms* za asili za mazao hayo katika jimbo langu la Moshi Vijijini.

Pili, Serikali ijenge skimu mpya za umwagiliaji katika maeneo ya tambarare ambayo hukumbwa na mafuriko makubwa kila mwaka. Maji ya mafuriko yaelekezwe

shambani kuzalisha chakula (mpunga na mazao mengine). Mafuriko ya mwaka huu yamesababisha maafa makubwa, na Wizara ya Kilimo ilipeleka misaada ya chakula na ya kibinadamu katika Kijiji cha Mandaka Mnono kilichopo Kata ya Oldmoshi Magharibi.

Mheshimiwa Spika, pia Wizara ijenge skimu mpya Kata ya Oldmoshi Magharibi katika kijiji cha Mandaka mnono ambapo kuna 1250 ha. Pia Wizara ijenge skimu mpya Kata ya Arusha Chini katika Vijiji vya Mikocheni na Chemchem ambako kuna 2000 ha. Wizara pia ijenge skimu mpya Kata ya Mabogini ambapo kuna 1350 ha.

Mheshimiwa Spika, skimu hizi mpya zikijengwa, zitaongeza 4600 ha kwenye kilimo cha umwagiliaji na kuongeza uzalishaji wa chakula na kuchangia kikamilifu katika uchumi wa wananchi na Taifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA ALI MZEE:** Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iwatumie wanafunzi wa Kitivo cha Kilimo *SUA* kufanya tafiti mbalimbali za kilimo.

Kwa nini tunakuwa watumwa wa sayansi? Ikiwa wataalamu waliosomea sayansi hawawezi kuitumia sayansi kubadilisha mwelekeo wa idara wanazozifanyia kazi basi wanasayansi hao hawasaidii Serikali na inabidi Serikali ichue hatua.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iwaandae vijana kuweza kuwaendeleza kwenye kilimo kwa kupatiwa elimu, mikopo na masoko kuweza kujikwamua kiuchumi na kuzalisha ajira nyingi nchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMANNE A. SAGINI:** Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa maandishi ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, Serikali iongeze miradi ya umwagiliaji hasa kwenye Wilaya na Mikoa inayopakana na maziwa na mito ikiwemo Ziwa Victoria, Tanganyika, Nyasa, Manyara, Eyasi na Rukwa. Hii itasaidia kupunguza utegemezi wa mvua hasa kipindi hiki chenye changamoto ya mabadiliko ya tabianchi.

Pili, Serikali ifanye uamuzi wa makusudi wa kuajiri Maafisa Ugani wa kutosha kwenye Mikoa na Halmashauri ambazo kilimo cha mazao ndiyo shughuli yao kuu ya kiuchumi. Kwa kufanya hivyo, tutasaidia kuongeza kwa kasi tija katika kilimo cha mazao.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu wake Makatibu Wakuu na timu yote ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, hali ya ushirika katika Wilaya ya Nyasa si nzuri. Kuna malalamiko makubwa ya wakulima wa kahawa hasa *AMCOS* za Nambawala na Luhangalasi.

Mheshimiwa Spika, Bonde la Lituhi lina *potential* kubwa ya kilimo cha umwagiliaji na ndio eneo linalotegemewa zaidi kwa kilimo. Changamoto ni ukosefu wa miundombinu.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali isaidie kutatua changamoto hiyo.

Mheshimiwa Spika, eneo nililolitaja la Lituhi kwenye orodha ya skimu mliyotoa kwenye kiambatisno cha bajeti limetajwa kama Ruhuhu.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwa njia ya maandishi kwenye hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza kabisa naiomba Serikali ifikirie namna ya kurejesha *export levy* na ifanye kazi kwa malengo yaliyokusudiwa, asilimia 65 ni ya masuala ya korosho na asilimia 35 iende Serikalini.

Suala la pili ni kuhusu Bodi ya Korosho. Bodi hii haipo kwa muda mrefu kabisa, anaachwa *Director General* afanye mambo mengi wakati hata uwezo wa kufanya hayo mambo hawezi na badala yake ni kukuza migogoro kati ya watumishi na kujinufaisha zaidi, *Director General* wa korosho aondolewe, ameshindwa kusimamia tasnia, kazi ni maugomvi na wafanyakazi wenzake na wadau wa tasnia kwa sababu tu za kimaslahi.

Mheshimiwa Spika, pia programu za miche na pembejeo bure kwa wakulima zirudishwe ili kuweza kusadia maeneo mengine ambayo yanalima korosho.

Mheshimiwa Spika, bei ya gunia zipo juu sana hali inayomgharimu mkulima. Hata akichangiwa mnunuzi anapunguza bei ya mkulima, kwenye mjengeko wa bei, pale mnunuzi anapoongezewa gharama maana yake anakata pesa kwa mkulima.

Mheshimiwa Spika, ile sheria iliyofanyiwa marekebisho ni Sheria Na. 18 ya mwaka 2009 na kanuni zake za mwaka 2010. Kwa kubadili kifungu Na 17A ambacho kilikuwa kinaelekeza jinsi ya kukusanya *export levy* na kuigawa ambapo asilimia 65 ilikuwa inatakiwa ipelekwe kwa ajili ya maendeleo ya tasnia ya korosho na asilimia 35 ipelekwe kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Baada ya sheria hiyo Na. 18 ya mwaka 2009 kufanyiwa marekebisho mwaka 2017 kwenye kifungu na 17A; ikaelekezwa kwamba fedha zote zipelekwe katika Mfuko Mkuu wa Serikali na tasnia ikiwa na mahitaji itaomba.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba tangu fedha hizo zichukuliwe na Serikali tasnia imedorora, uzalishaji umeshuka kutoka tani 320,000 hadi tani 205,000 mnaweza kuona hasara ambayo Serikali imeisababishia *industry* ya

korosho na imepelekea kukosa mapato kwa wakulima, wadau na Serikali yenyewe.

Pia tangu hizo fedha kuzuiliwa Serikali imepeleka kiasi kisichozidi shilingi bilioni 15 kwa ajili ya maendeleo ya tasnia wakati madeni na mahitaji ya kuendeleza tasnia ni zaidi ya bilioni 100. Hivyo turejee kwenye sheria ile ya awali ambayo ilikuwa inapeleka *export levy* asilimia 65.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba wakati sheria inabadilishwa tayari tasnia ya korosho iikuwa inadai zaidi ya shilingi bilioni 150. Hivyo ni vyema fedha hizo zipelekwe kwenye tasnia ya korosho kwa kuwa sheria ikitungwa hairudi nyuma, bali huenda mbele.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na maneno mengi kuhusu suala la unyaufu, na Serikali bado haijaweka wazi suala hili, kuna haja ya kujibu hoja kwamba je, kuna unyaufu ama laa, Serikali ifanye utafiti wa kutosha kwa sababu katika kila jambo linalotokea huwa linaharibu sana mjengeko wa bei.

Suala lingine ni kuhusu madeni ya wazalishaji wa mbegu ambazo zilisambazwa maeneo mbalimbali nchini, watu hawa hawajalipwa, wengine walikopa kwenye mabenki sasa wanafilisiwa, akina mama waliunda vikundi lakini bado hawajaweza kupata pesa na madeni yako wazi, bado kuna watoa huduma ambao wadai Serikali, kuna walio-*supply* magunia msimu wa mwaka juzi, nao walikopa.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni yamefanyika mabadiliko katika ngazi mbalimbali za uongozi kwenye vyama vikuu, kumekuwa na utaratibu wa kurithishana madeni, *COASCO* wakafanye ukaguzi hasa Chama Kikuu cha Ushirika cha Mtwara na Newala, vinginevyo madeni haya yanabaki kwa wakulima na hasara inakuwa kwao.

Mheshimiwa Spika, irekebishwe sheria pia inayowatambua wakulima wote kama wanachama, kwa sababu pesa zinazokusanywa kwenye faida inayopatikana

kwenye mauzo wanakula viongozi, sawa na pesa za maendeleo zinazotokana na makusanyo, hazirudi kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, matumizi mabaya ya fedha ya Bodi kutoka kwa *DG* wa Bodi ya Korosho, zaidi ya shilingi bilioni mbili Wizara ichukue hatua za kinidhamu, rejea ukaguzi wa *COASCO.*

Mheshimiwa Spika, nawasilisha kwako Taarifa ya matumizi ya *Director General* wa korosho Kutoka Ofisi ya Mkaguzi wa Ndani. Wizara ya Kilimo inatakiwa kufanya ukaguzi mara moja ili kuepuka hasara ambayo Serikali inaweza kuipata.

TAARIFA ZA MATUMIZI MABAYA YA OFISI KWA MKURUGENZI MKUU WA BODI YA KOROSHO TANZANIA NDUGU FRANCIS ALFRED KWA KIPINDI CHA MWAKA MMOJA

A: TAARIFA YA MALIPO YA POSHO YA MAKARIBISHO (ENTERTAINMENT ALLOWANCE) AMBAYO AMELIPWA MKURUGENZI MKUU WA BODI YA KOROSHO BILA MUONGOZO WOWOTE NA BILA KUFANYA MAREJESHO KWA KIPINDI CHA MWAKA SASA

Naleta kwako ushahidi wa malipo, na kwa taarifa zaidi ziko uko Bodi ya Korosho.

1. 4/9/2019 000461 Francis Alfred Mwakabumbe Entertainment Kikao Wizara ya Kilimo 500,000 840,000 200,000;

2. 26/8/2019 000444 Francis Alfred Mwakabumbe Entertainment Kikao Wizara ya Kilimo 500,000 840,000

3. 28/10/2019 000065 Francis Alfred Mwakabumbe Entertainment Mkutano wa Wadau wa Korosho Mkoa wa Pwani 500,000 240,000

4. 13/09/2019 000035 Francis Alfred Mwakabumbe Entertainment Kikao Wizara ya Kilimo 500,000 1,080,000

5. 3/12/2019 000216 Francis Alfred Mwakabumbe Entertainment Ziara Maeneo Mapya ya Uzalishaji-Dodoma,Tabora,Katavi,Songwe,Mbeya &Njombe 500,000 1,200,000

6. 31/12/2019 000249 Francis Alfred Mwakabumbe Entertainment Kushughulikia Masuala ya Msimu Rufiji 500,000 360,000

7. 7/1/2020 000262 Francis Alfred Mwakabumbe Entertainment Kikao na Wakuu wa Wilaya-Tunduru 500,000 120,000

8. 4/1/2020 000130 Dodoma City Square Restaurant Huduma ya Maji na Chakula Kikao na Mh. Waziri wa Kilimo 1,650,000

9. 6/2/2020 000140 Francis Alfred Mwakabumbe Entertainment Kikao na ANSAF -Dodoma 500,000 1,080,000

10. 24/02/2020 000162 Francis Alfred Mwakabumbe Entertainment Kikao Wizara ya Kilimo 500,000 1,200,000

11. 27/03/2020 000434 Francis Alfred Mwakabumbe Entertainment Kikao na Mkuu wa Mkoa Lindi 500,000 840,000

12. 1/11/2019 000072 Francis Alfred Mwakabumbe Entertainment Safari Dsm Kituo cha ITV 500,000 180,000

13. 5/11/2019 000075 Francis Alfred Mwakabumbe Entertainment Kikao Dsm - issue ya ACA 500,000 600,000

14. 14/112019 000090 Francis Alfred Mwakabumbe Entertainment Kikazi Kipindi TBC 500,000 360,000

15. 20/11/2019 000099 Francis Alfred Mwakabumbe Entertainment Kikao na Clouds 500,000 720,000 150,000

16. 9/1/2020 000272 Francis Alfred Mwakabumbe Entertainment Kushiriki Ziara ya Waziri Mkuu-Pwani 500,000 480,000

17. 20/01/2020 000295 Francis Alfred Mwakabumbe Entertainment Kikao cha Wizara ya Kilimo 500,000 1,200,000 300,000

Mheshimiwa Spika, taarifa hii nimeitoa kwenye mfumo wa *Excel* unaweza usieleweke sana, lakini kuna umuhimu wa kupeleka wakaguzi ili taarifa hii iwe vizuri. Jumla 8,000,000 11,340,000 650,000 1,650,000

Mheshimiwa Spika, hakuna muongozo wowote unaompa haki *DG* ya kulipwa posho ya *entertainment,* ni maagizo yake tu ya mdomo.

Mheshimiwa Spika, hajafanya marejesho mwaka umepita. Matumizi mabaya ya ofisi na madaraka na ufujaji wa fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, *issue* ni matumizi mabaya ya ofisi kwa kuwa fungu hilo halikuwa kwenye bajeti.

Mheshimiwa Spika, *DG* ametumia bilioni 1.5 kutoka Mei, 2019 hadi Septemba, 2019 kinyume na bajeti iliyoombea fedha hizo Wizara ya Fedha kupitia Wizara ya Kilimo bila idhini ya mamlaka. (Bajeti iliyoombea fedha hizo imeambatishwa).

Mheshimiwa Spika, *DG* amefanya *addendum* ya pembejeo kwa msimu 2019/2020 na kampuni za *BAJUTA International Ltd*. *sulphur* tani 11,000 na kampuni ya *TFC sulphur* tani 8,000 bila idhini ya Kamati ya Zabuni *(Tender Board).* Ukiukaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 na kanuni zake za mwaka 2013 *(addendum* hizo zimeambatishwa kama vielelezo).

Mheshimiwa Spika, usimamizi mbovu wa mikopo ya pembejeo kwa wakulima hivyo kupelekea zaidi ya shilingi bilioni moja kutolipwa msimu 2019/2020. Fedha hizo zisipopatikana italazimu Serikali itafute fedha za kuwalipa wazabuni ambao waliikopesha *CBT* pembejeo ili iuze kwa wakulima kisha walipwe fedha.

Mheshimiwa Spika, matumizi mabaya ya ofisi, kwa mfano kutotumia muundo wa bodi uliopo katika kufanya kazi za ofisi mfano aweza kwenye idara akamtuma *junior staff* bila Mkuu wa Idara kuwa na taarifa hivyo kuleta migongano katika Idara na kazi kwa ujumla. Hiyo imetokea katika Kurugenzi ya Fedha, Idara ya Fedha, Kurugenzi ya Masoko, Kitengo cha Manunuzi na Idara ya Utumishi na Utawala.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, leo tena naomba kuanza mchango wangu kwenye Wizara hii kwa kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa ya kusimamia Wizara hii nyeti. Hata hivyo naomba kuishauri Serikali katika mambo yafuatayo:-

Kwanza, kwa kuwa tunayo mazao ambayo kitaifa yanaonekana kuwa ni mazao ya kimkakati, ni ushauri wangu kuwa mkakati wa mazao hayo ni lazima uunganishwe na mikakati mingine. Kama vile mikakati ya utafiti ili kuboresha tija ya mazao hayo, uwepo wa miundombinu rafiki ya usafiri ili kuwezesha wakulima wa mazao hayo kuyafikia masoko kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, aidha, kuwepo na mkakati maalum wa kudumu wa kutafuta masoko kwa mazao hayo ya kimkakati utakaowahakikishia wakulima uwepo wa masoko kwa mazao yao. Kwa hali ilivyo sasa masoko ya mazao hayo ya kimkakati sio ya kuridhisha hasa kwa upande wa bei ya mazao hayo.

Pili, kwa zao la korosho ambalo ndio mgongo wa maendeleo kwa Mikoa ya Kusini na Taifa kwa ujumla. Ili kuendeleza zao hilo naiomba sana Serikali kuimarisha kituo chetu cha utafiti pale Naliendele kwa kukipatia chuo hiki fedha za kutosha ili kukiwezesha kuendelea na tafiti mbalimbali.

Jambo la pili naishauri Serikali kuona umuhimu wa kurejesha zile fedha za *export levy*, fedha ambazo zilikuwa mahususi kwa kuendeleza zao hili la korosho, kwani uzoefu unaonesha kuwa tangu Serikali Kuu kuchukua fedha hizo, uzalishaji wa zao hilo umeshuka sana, hii ni kutokana na wakulima wengi kushindwa kumudu gharama kubwa ya pembejeo.

Nikiendelea kuishauri Serikali katika kuimarisha kilimo chenye tija, liko suala la uhaba wa watumishi wa ugani kwenye Halmashauri zetu, na wale wachache waliopo hawafanyi shughuli za ugani na badala yake wamekuwa wanakaimu kama watendaji wa kata na vijiji na hivyo kusahau kazi zao walioajiriwa nayo. Kutokana na uhaba wa watendaji wa kata na vijiji sehemu nyingi huwatumia wataalamu hawa kama watendaji wa kata na vijiji.

Mwisho niombe Serikali kuifanyia mapitio Sheria ya Ushirika, sheria hii kwa sasa ina mapungufu sana, mfano iko taasisi ya *COASCO;* taasisi hii badala kuwa mkombozi wa vyama vya ushirika imekuwa adui wa ushirika. Hivyo niombe sana Serikali kuifanyia marekebisho sheria hii ambayo imepitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naiomba sana Serikali kuhakikisha bei za mbegu, pembejeo hasa zinazozalishwa nchini zikawa na bei rafiki kwa wakulima. Kwani hadi sasa wakulima wengi bado wanatumia mbegu zao za asili ambazo tija yake kwa mkulima ni ndogo sana na Serikali bado haijawekeza vya kutosha ili kuhakikisha mbegu zinapatikana kwa bei nafuu.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maoni yangu kwa maandishi kama ifuatavyo; kwanza naipongeza sana Serikali hasa Wizara ya Kilimo kwa ushirikiano mkubwa ambao Wilaya ya Kilolo tulipata wakati wa kukarabati *scheme* ya Ruaha Mbuyuni baada ya mkondo wa maji kuhama kutoka katika *scheme* hiyo. Kwa namna ya pekee napongeza moyo wa kujituma wa watumishii wa

Wizara waliotumwa kufanya kazi ile kwa umahiri na weledi wao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi, napenda kutoa maoni yafuatayo kwa Wizara; nakupongeza wewe Waziri na Naibu Waziri kwa ushirikiano pamoja na Katibu Mkuu na Mkurugenzi wa Umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mpango wa Serikali kugawa miche bure kwa mazao ya kimkakati kama ilivyo kwa kahawa na michikichi nashauri Wizara ianze mara moja kuotesha na kugawa miche ya parachichi bure katika Wilaya ya Kilolo ambayo kilimo hicho kinakuwa kwa kasi kubwa na ni mkombozi katika mazao ya biashara. Tayari nimefanya maongezi na Naibu Waziri wa Kilimo na Mkurugenzi wa *TARI* kuhusu suala hili, hivyo naomba msukumo wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, nafahamu Wizara inazo taarifa kuhusu shamba la chai la Kidabaga ambalo lilikuwa linamilikiwa na *TTB* na ambalo ni miaka 30 sasa tangu limetelekezwa. Lakini pia katika eneo la Kidabaga na kata za jirani wapo wakulima waliolima chai yao na wanaendelea kusubiri kiwanda cha chai kwa miaka hiyo yote. Hivi sasa kuna tishio la wananchi kung'oa chai hiyo na kupanda mazao mengine baada ya uvumilivu wa miaka mingi bila mafanikio.

Naiomba Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Uwekezaji na Wizara ya Viwanda na Biashara mlete majibu ya ufumbuzi wa kiwanda cha chai cha Kidabaga. Nitashukuru kama kwenye hitimisho lako utakuja na majibu ya suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tume ya Umwagiliaji wapo wafanyakazi wa tume wamewekwa kwenye ngazi ya mkoa. Kwa bahati mbaya watumishi wale hawana bajeti na sina uhakika kama wana maelekezo ya kutosha kuhusu kazi zao na uhusiano na Halmashauri zetu. Naomba jambo hili liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, zao la pareto ni kati ya mazao ambayo sasa yanapanda katika soko la dunia, wapo wakulima katika Wilaya ya Kilolo naomba kusiwe na urasimu katika upatikanaji wa vibali vya wanunuzi kwenye zao hili.

Mheshimiwa Spika, kuna magonjwa ya mazao hasa nyanya yamejitokeza ambayo hayakubali dawa zilizopo, naomba timu ya wataalamu itumwe kwa ajili ya uchunguzi.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Waziri wa Kilimo pamoja na timu yake kwa kazi nzuri na yenye tija wanayoifanya, na kwa hakika vipaombele vyote hivi vikifanyiwa kazi nchi yetu itakuwa imetimiza malengo yake ya asilimia 75.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina asilimia 75 ambayo ni wakulima, lakini kinachoonekana wakulima hawa hawapati huduma kama inavyotakikana. Ushauri wangu kwa Serikali ijipange kuhakikisha inapeleka pembejeo za kutosha na kwa wakati, mfano nchi yetu ina mazao ya kibiashara zaidi ya sita ikiwemo kahawa; na kahawa hii inalimwa pia katika Milima ya Usambara ila cha kushangaza na kusikitisha zao hili la kahawa linakufa, hivi ninavyoandika Lushoto kahawa imekufa.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hii naomba niishauri Serikali yangu tukufu iende ikafufue zao la kahawa katika Wilaya ya Lushoto kwani zao hili lilikuwa linainua sana uchumi wa Lushoto. Kwa hiyo, niendelee kuiomba Serikali iende kufufua zao hili la kahawa pamoja na kupeleka wataalam wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Lushoto ni ya wakulima wa mbogamboga na matunda, na mazao haya ndio mazao tegemezi kwa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, lakini sijawahi kusikia wakulima hawa wanapelekewa pembejeo, lakini pamoja na hayo mazao ya wakulima hawa mengi yanaozea mashambani. Kwa hiyo, niiombe Serikali yangu iwapelekee wakulima hawa wa mbogamboga na matunda pembejeo pamoja na kuwatafutia masoko wakulima hawa.

Mheshimiwa Spika, pia Wilaya ya Lushoto ina milima na mabonde mengi, hivyo wakati wa msimu wa mvua kunakuwa na maporomoko makubwa ambayo yanaleta asali kwenye mashamba pamoja na kuharibu miundombinu ya barabara na kupelekea hasara kubwa kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya kujenga mabwawa kwa ajili ya kukinga maji hayo ili wakulima wetu hasa wa Wilaya ya Lushoto waweze kulima kilimo cha umwagiliaji kuliko ilivyo kuwa sasa ardhi yote yenye mbolea inasombwa na maporomoko yanayosababishwa na mvua?

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali itenge pesa za kutosha ili iwajengee mabwawa wakulima wa Jimbo la Lushoto.

Mheshimiwa Spika, naunga hoja mkono kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK:** Mheshimiwa Spika, mimi nawaomba Waziri na Naibu Waziri wajitambue na watambue kwamba nafasi walizoaminiwa na Rais si nafasi za kazi bali ni nafasi za kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kimaendeleo katika jamii ya Watanzania, na ili mabadiliko hayo yaonekane na kila Mtanzania ni wajibu kufanya kazi zitakazobadilisha fikra za Watanzania hasa hasa wakulima; na ili fikra za Watanzania zibadilike, ni lazima Watanzania hao washirikishwe katika mambo yanayowahusu na wakati huo huo Mawaziri wanatakiwa washiriki katika shughuli za wakulima moja kwa moja katika maeneo wanayofanya kazi, waache kabisa maofisi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, wangeamua kuanzisha kilimo cha umwagiliaji kwa kwenda kwenye maeneo wakawaomba wananchi kuchimba mitaro wenyewe akiwepo Waziri au Naibu Waziri na wataalam wa ndani ya Wizara. Jambo hili lingejenga ujasiri na ufanisi wa uongozi, lingewajengea heshima Serikali, lingewasaidia

wananchi ambao ni wakulima na lingepunguza matumizi makubwa ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iwe na takwimu mahsusi ya wakulima wa kila zao linalolimwa Tanzania, kisha wafanye tathmini ya malengo ya Serikali waliojiwekea. Je, malengo na idadi ya wakulima italingana? Baadaye wafanye marekebisho yanayohitajika.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iweke mitandao ya masoko kwa kuweka wafanyabiashara wakubwa watano hadi kumi watakaoishi nchi mbalimbali ambao watauza bidhaa za Tanzania za kilimo na hata za viwanda nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, soko lingine lipo ndani, Watanzania ni milioni 65, Serikali iwatumie Watanzania hawa kama soko, hivi inakuaje Zanzibar wawe wanatumia mchele wa mapembe kutoka India na nchi nyingine ambao ni rahisi na isitumie mchele kutoka Tanga. Serikali iondoe mifumo itakayosababisha mchele wa Mbeya na bidhaa nyingine na bei kubwa huko Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali izuie vijana kucheza *betting* na badala yake Serikali iwaandae kuwa wakulima, fedha ambazo vijana wanazitoa kuwapa Wachina ni nyingi mno na iwapo vijana hao wangezitumia fedha hizo kwenye kilimo Tanzania ingepaa angani kwa utajiri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja nikiamini kuwa kilimo ni uti wa mgongo, kwa maana ndio *axis* ya maendeleo ya nchi yoyote. Ahsante.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, zao la kahawa mkoa wa Kagera limegubikwa na tatizo la mfumo wa soko. Soko linaua zao la kahawa Kagera. Mfumo wa *AMCOS* ni hatari kwa ustawi wa zao la kahawa Kagera. Nashauri tufungue milango kwa wafanyabiashara, turuhusu wafanyabiashara binafsi kwa ajili ya kukuza ushindani wa zao hili. *Stop protectionism* ya *AMCOS*. Serikali kupitia Tume ya

Ushindani iweke mazingira shindani kwa ustawi wa soko na uchumi wa nchi yetu.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimpongeze wewe binafsi Mheshimiwa Waziri, Naibu wako pamoja na wasaidizi wenu wote kwa namna mnavyoisimamia vizuri Wizara hii nyeti iliyotoa ajira kwa Watanzania walio wengi (75%) na kuchangia 24% ya pato la Taifa. Kutokana na umuhimu huo, na mimi naomba kuchangia yafuatayo:-

Kwanza, Serikali iingie ubia na wawekezaji wa ndani na nje ili kuweza kujenga viwanda vikubwa vya mbolea hapa nchini ili isaidie kupunguza gharama kwa wakulima wetu. Mfano toka Ludewa *DAP* inauzwa shilingi 80,000 kwa mfuko 24/05/2021, *CAN* mfuko mmoja unauzwa shilingi 58,000 na *UREA* ni shilingi 55,000.

Pili, kodi za matumizi ya maji kwa watumiaji wa maji ziangaliwe vizuri ili kodi hizo zisiwe mzigo kwa wakulima na hivyo kudidimiza sekta ya kilimo. Wizara ya Kilimo ikutane na Wizara ya Maji na Mamlaka za Mabonde ili kujadili hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo; mazao yote ni mazao ya biashara hivyo mtizamo wa kuwa kuna mazao ya chakula na mazao ya biashara unatuchelewesha kuboresha kilimo cha mahindi, alizeti, karanga na ufuta kufanyika kibiashara na kumnufaisha mkulima. Mazao yote haya ni malighafi kwenye viwanda.

Mheshimiwa Spika, Wizara za Serikali zijenge utamaduni wa kukutana na kujadili masuala mtambuka, mfano barabara za vijijini zikiwa bora na zipitike msimu wote hakika zitachangia sana kuinua sekta ya kilimo na viwanda vya uongezaji thamani ya mazao. Wakulima walioko maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa mazao wanakabiliwa na changamoto kubwa za ubovu wa barabara Ludewa. Mfano barabara ya Lusitu-Madilu-Ilininda-Mundindi kuna viazi, chai, kahawa, mahindi, maharage, njegere, mbao na parachichi. Pia barabara ya Kigasi-Milo-Ludende-Amani au Muhoro-

Ludende-Mkongobaki-Lugarawa; barabara ya Ludewa-Ibumi-Masimavalafu au Nkomang'ombe-Iwela-Bandari ya Manda na Luilo-Lifua-Liugai na maeneo mengineo.

Mheshimiwa Spika, vyuo vikuu vya kilimo vishiriki kwa vitendo katika kufanya utafiti, ubunifu na kuelimisha wakulima ili kuongeza tija vyuo viendeshe mashamba ya mfano hasa mazao yatakayouzwa nje na kuingiza mapato ya kigeni.

Mheshimiwa Spika, vijana wanaomaliza mafunzo ya JKT wapewe mikopo chini ya uangalizi na waanzishe mashamba ya miwa, alizeti ili kuzalisha sukari na mafuta ya alizeti na karanga.

Mheshimiwa Spika, wahitimu mbalimbali wa vyuo vikuu nao wawezeshwe mitaji ili kujiajiri kwenye kilimo cha kibiashara na kukuza uchumi wa nchi na kujiongezea kipato chao.

Mheshimiwa Spika, Serikali iajiri wataalam wengi wa kilimo na kuwasambaza kwenye kata na vijiji vyetu nao wapewe malengo, wafuatiliwe ili watende kazi kama sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka zake mbalimbali sisi pamoja na Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano na Sita kwa jitihada kubwa iliyofanya katika sekta hii muhimu sana ambayo ndiyo uti wa mgongo kwa Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbulu naungana na Watanzania wote kumwombea kwa Mwenyezi Mungu Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano, Ee Mungu umpokee mtumishi wako mwaminifu, mtiifu, mzalendo, mwana

mapinduzi mahiri wa Afrika katika ufalme wako wa milele mbinguni, Amina.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hasan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuapishwa kupokea uongozi wa Taifa letu tuendelee kumwombea kwa Mwenyezi Mungu aweze kumlinda na kumjalia baraka zake katika kutuongoza.

Aidha, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wetu wote wa Wizara hii kwa ngazi mbalimbali katika jitihada zao kutekeleza, kusimamia na kushauri kwa weledi mkubwa katika nyakati mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa mchango wangu kupitia hotuba ya mapendekezo ya bajeti ya Wizara hii kupitia kwa Mheshimiwa Waziri na Mwenyekiti wa Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, Serikali isimamie suala la ubora wa pembejeo, uwepo wa Maafisa Ugani na mashamba darasa kwa kila kijiji hususan mashamba ya taasisi na shule za sekondari za kata katika maeneo yanayofikika kwa urahisi ili kuwasaidia wakulima wengi ambao kwa sasa wanapata mavuno ya gunia tano mpaka kumi kwa ekari moja wakati wangeweza kupata hadi gunia 40 kwa pembejeo bora.

Mheshimiwa Spika, kimsingi hadi sasa wakulima wetu wengi bado hawajafikia kile kiwango cha kilimo cha kisasa chenye tija. Hivyo basi ni muhimu sana Serikali ione utaratibu wa uhamasishaji wa kilimo chenye tija, pamoja na kuangalia uwezekano wa Maonesho ya Nane Nane kwa ngazi ya Wilaya kwa kufanya mapitio ya gharama za kuwezesha ili kuondoa gharama zisizo na tija.

Mheshimiwa Spika, Serikali iajiri Maafisa Ugani walau kwa ngazi ya kata na kuwapatia walau pikipiki na mafuta kupitia Halmashauri ili waweze kupanga ratiba ambayo

itakuwa wazi kwa wananchi kwenye vijiji vya kata husika kama ilivyo kwa kada zingine za watumishi.

Mheshimiwa Spika, Serikali iache utaratibu wa kuzuia mauzo ya mazao ya wakulima kwenye masoko ya nje kwa kuwa wakulima nao hulima kwa gharama kubwa. Hivyo basi kama sababu kubwa ya kufanya hivyo ni upungufu wa mazao hayo Serikali inunue kupitia wakala wake na baadaye iuze kwa bei mbili tofauti ya soko la ndani na nje kwa kuwa tunawakatisha tamaa wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itazame upya majukumu ya msingi ya kada za kilimo na ushirika kwa ngazi za Halmashauri za Wilaya, Kata na Vijiji kwani kwa sasa kata hizi katika maeneo mengi nchini zinakosa tija katika kutoa huduma kwa wananchi utakuta Afisa Ugani yuko kwenye ngazi fulani lakini hana mpango kazi.

Mheshimiwa Spika, naunga hoja asilimia 100 na naomba kuwasilisha.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, nianze na suala la utafutaji wa masoko ya bidhaa za kilimo.

Mheshiiwa Spika, ushauri Serikali iangalie mahitaji ya ndani ya bidhaa au mazao ya kilimo, kisha ifanye *zoning* ya kuhakikisha hitaji hilo litashughulikiwa na wakulima wa kanda fulani. Mfano tunahitaji mafuta ya kupikia nchini, hivyo ianishwe mikoa ambayo itatakiwa kuchangia *market share* hiyo. Hii itasaidia Serikali, kuelekeza nguvu kubwa za uwekezaji hasa katika utafiti, mbegu bora, upatikanaji wa masoko, kuweka miundombinu bora, pia itavutia wawekezaji.

Pili, miji yetu pia ni masoko ya bidhaa za kilimo kama mbogamboga, iangaliwe miji ambayo mito inapita katikati yake, halafu ifanyiwe mkakati wa kilimo bora cha mbogamboga na ufugaji wa samaki wa kizimba, bila kuathiri mazingira. Mfano Mji wa Iringa unapitiwa na Mto Ruaha, Njombe, Mto Ruhuji na kadhalika.

Tatu, fedha za wafadhili katika kilimo ziwafikie walengwa ikiwa ni pamoja na za Serikali zilizowekezwa kwenye mabenki ya Kilimo.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Spika, natoa shukurani zangu za dhati kwako kwa kinipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Wizara ya Kilimo. Wizara hii ni miongoni mwa Wizara muhimu sana katika nchi yetu.

Pili nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha na hatimaye kuiwakilisha katika Bunge lako Tukufu kwa ufasaha na umakini mkubwa. Hotuba hii ni imesheheni mambo ambayo kwa sasa yanahitajika katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia maeneo yafuatayo, nikianza na umwagiliaji na ushirika.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza kwa dhati Serikali yetu kwa namna inavyochukua jitihada kubwa katika kuboresha kilimo katika nchi yetu. Kama inavyojulikana kuwa kilimo ni uti wa mgongo katika nchi.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri imetaja namna inavyoendelea kuchukua juhudi za kutengeneza maeneo ya unwagiliaji katika nchi yetu. Hivyo imeonesha kuwa kuna engezeko la hekta 330 kutoka mwaka 2020 mpaka 2021.

Mheshimiwa Spika, hotuba imeonesha kuwa mwaka 2020 ilikuwa na hekta 694,715 na mwaka 2021 ni hekta 695,045 za umwagiliaji; sawa na ongezekko la hekta 330.

Mheshimiwa Spika, hili ni ongezeko dogo sana ukilinganisha na umuhimu wa kilimo katika nchi yetu. Aidha, ni ongezeko dogo sana ukilinganisha na ukubwa wa eneo la ukubwa wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali ni kuongeza juhudi kwa kasi ya zaida kuongeza maeneo ya umwagiliaji.

Pili ni upatikanaji wa pembejeo; wananchi wa Tanzania wanajitahidi sana pamoja na watendaji wa Wizara hii ya Kilimo kutaka kufikia malengo yao ya kimaisha kupitia kilimo. Lakini juhudi hizi zinakwama kutokana na matatizo makubwa ya pembejeo na zana za kilimo. Bado kuna ukakasi mkubwa wa upaikanaji wa pembejeo. Wakulima wanapata shida kupata pembejeo katika maeneo yao.

Aidha, wakulima wetu wanapata shida na wanashindwa kumudu kununua zana za kisasa za kilimo. Bado upatikanaji wa zana hizo ni jambo ambalo ni gumu kwa wakulima wa kawaida. Mfano Serikali ina lengo la kuwatoa wakulima kutumia jembe la mkono, lakini mpaka leo bei ya trekta moja ni kubwa sana kiasi ambacho sio rahisi kwa wakulima wa hali ya chini ambao ni kundi kubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali kuhusu jambo hili ni kuangalia namna ya kuboresha upatikanaji wa pembejeo na urahisi wa bei za zana za kilimo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, niwapongeze Mawaziri wa Kilimo wote wawili.

Mheshimiwa Spika, ni kweli inawezekana Mkoa wa Dar es Salaam hatufanyi kilimo lakini naomba kuongelea Halmashauri ya Temeke.

Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo ndio msingi mkubwa wa kukuza kipato na chakula kwa familia na jamii. Jumla ya Kaya 6,118 zenye wakulima 11,270 wanajihusisha na kilimo cha mbogamboga kwenye hekta 6000. Karibu hekta 250 za mihogo na hekta 5,750 za matunda na mbogamboga na uchangiaji wa zaidi ya asilimia 75.

Mheshimiwa Spika, huduma za ugani zinafanyika kwa kutoa ushauri kwa wakulima kuhusu maghala na masoko na maeneo ya uwezeshaji Idara ya Kilimo ya Halmashauri ya Temeke.

Mheshimiwa Spika, tunawakaribisha kuja tuwekeze katika maeneo ili kuleta tija katika sekta ya kilimo. Pia kuwekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji ambazo hazijaanza kwa Temeke, upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo cha mihogo /matunda/mbogamboga yapo na viwanda vya kutengenezea bidhaa za mazao ya kilimo kama zao la muhogo/mbogamboga/na matunda.

Mheshimiwa Spika, nauga mkono hoja na kazi iendelee.

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA:** Mheshimiwa Spika, wote ni mashaidi kwa muda mrefu ushirika umekuwa ukikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kukosekana kwa viongozi wa ushirika wenye uwezo wa kusimamia kikamilifu utekelezaji wa majukumu ya vyama kwa unafanisi. Hali hiyo imesababisha kukithiri ubadhirifu wa fedha na mali za wanaushirika hivyo kuwakatisha tamaa wakulima kujiunga na vyama hivi.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali kuweka mazingira rafiki wezeshaji kwa ajili ya upatikanaji wa masoko ya mazao ya uhakika ndani na nje ya nchi. Najua Serikali ilianzisha Kitengo cha Masoko *(Agricultural Marketing Unit)* katika Idara ya Maendeleo ya Mazao inayosimamia utafutaji wa masoko na tafiti za masoko na bei za mazao pamoja na kufuatilia mifumo ya uuzaji, pia Serikali inapaswa kuweka bajeti ya kutosha kufanya haya majukumu ili kusaidia hawa wakulima wetu wanapata shida.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ya Awamu ya Sita kuendelea na utekelezaji wa programu ya kuendeleza kilimo awamu ya pili *(ASDP II)* hii itasaidia sana sekta ya kilimo. Serikali inapaswa kuboresha mifumo ya taasisi, bodi na sheria

za kilimo kwa ajili ya usimamizi wa maendeleo ya mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapaswa kuunganisha wakulima wadogo na mashamba makubwa ili kuendeleza kilimo biashara, kupata ujuzi na maarifa ya kilimo. Wizara inapaswa kuharakisha upatikanaji pembejeo na masoko.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara pia kuwekeza nguvu katika ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji, maghala, masoko na miundombinu bora ya kuhifadhi mazao ya kilimo. Pia naiomba Serikali kuimarisha uzalishaji wa mbegu bora na upatikanaji wa pembejeo nyingine za kilimo na kuzisambaza kwa wakulima.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sekta ya kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa letu basi Serikali ilipe kipaumbele suala hili la bajeti ili kukidhi mahitaji ya Maafisa Ugani, mbegu, mbolea bora na pembejeo kwa ajili ya kuchochea hali ya wakulima na hivyo kuchochea uzalishaji bora wa mazao ya chakula na biashara.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali izamilie kuwasaidia wakulima wetu kuuza mazao kwa bei yenye tija na kupata masoko ya uhakika hasa kwa mazao ya kahawa, pamba na kadhalika ili kuwezesha mkulima kunufaika ipasavyo na kilimo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukosefu wa mbolea umewafanya wakulima wetu hasa waliopo karibu na mipaka mfano Wilaya ya Tarime wakulima wamekuwa wakinunua mbolea Kenya ili kukidhi mahitaji ya kilimo hii pia ni kwa kuwa mbolea yetu haiwafikii kwa wakati lakini pia ikiwepo huuzwa kwa bei ya juu zaidi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ifanye haraka upatikanaji wa mbolea katika mipaka hiyo ili pia kuzuia magendo ya mbolea, kwa sababu wakulima wanafuatwa mpaka mashambani na *TRA* kuwakamatia mbolea hizo.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Spika, kuhusu *Agricultural Trust Input Fund (AGTIF),* hiki chombo lazima kifanyiwe maboresho, badala ya kusaidia wakulla kinachangia kuua *morale* wa kilimo Tanzania. Mfano mkulima amekopa shilingi milioni 40 na amewekewa *cummulative interest* ya shilingi milioni mbili na *total* ni shilingi milioni 42 kwa miaka mitano, hapa taasisi inafahamu kilimo cha Tanzania ni cha mvua na masoko hayapo. Lakini mkulima baada ya kulima akipata mazao soko hakuna, yanauzwa au anauza *underprice* wakati huo *AGTIF* madai yao yapo pale pale.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kwa kuwa analima kwa kutegemea mvua, kilimo kinategemea msimu na hali ya hewa. Sasa inatokea hakuna mvua ya kutosha, ratiba ya malipo ya *AGTIF* ipo pale pale, mkulima baada kuona kilimo hakimlipi atakopa pesa popote kulipia mkopo wote wa *AGTIF* kwa muda uliopangwa wa miaka mitano mitano, lakini atakutana na riba kubwa ya zaidi ya asilimia 50 ya *principal.*

Mheshimiwa Spika, hili jambo halikubaliki Serikali kuuza mali za wananchi waliokwisha kulipa *principal* yote pamoja na *interest* ya Serikali bado *AGTIF* wanataka kuuza sababu ya *penalt interest* ya kuchelewa kurejesha.

Mheshimiwa Spika, naomba kuishauri Serikali inapokopesha mkulima iwe na *backstop follow up* kujua *situation* anayo *face* mkulima na iondoe kabisa riba kwa mkulima aliyelipa mkopo wote ndani ya muda wa mkataba.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya uchangiaji sasa kwa taratibu zetu Mawaziri wanahitimisha hoja kwa nusu saa tu. Kwa hiyo, huwa nawagawia Naibu Waziri dakika 10 na Waziri dakika 20 lakini kwa hoja hii ina uzito wake, nimewatengea saa moja. Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri dakika 25, Mheshimiwa Waziri mwenyewe dakika 35; mjibu hoja za Wabunge wawasikilize vizuri na naomba Waheshimiwa Wabunge tuwasikilize.

Kwa hiyo, moja kwa moja ili nisipoteze muda nimkaribishe Mheshimiwa Naibu Waziri na ili tukusikie vizuri njoo hapa mbele, karibu sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa hii na kutujalia sote afya na kushiriki kujadili mjadala huu unaohusu maslahi ya wananchi wa nchi yetu. Vilevile nitumie nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa dhati kabisa kwa michango yao ya hizi siku mbili na maoni waliyoyatoa.

Mheshimiwa Spika, ili nisipoteze muda, niende moja kwa moja katika hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wametoa. Hoja ya kwanza ambayo imejadiliwa kwa uchungu na maoni mengi ya Waheshimiwa Wabunge ni hoja ya stakabadhi ghalani. Kama unavyofahamu stakabadhi ghalani inatekelezwa kwa mujibu wa sheria. Mfumo wa stakabadhi ghalani ni moja kati ya mifumo ambayo inatumika katika mauzo ya mazao. Wizara ya Kilimo sio mara moja wala mara mbili tumesema hadharani msimamo na mwelekeo wa Wizara ya Kilimo katika suala la stakabadhi ghalani. Naomba nitumie nafasi hii kuliambia Bunge lako Tukufu na kuwaambia wakulima wa nchi hii kwamba msimamo wetu tutalinda haki za wakulima na tutafanya maamuzi kwa maslahi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala hili, hatuwezi kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani katika kila zao. Kila zao lina tabia na mfumo wake. Yapo maeneo ambayo hatuwezi kuuondoa mfumo wa stakabadhi ghalani kwa sababu umefanya vizuri. Mfumo wa stakabadhi ghalani umefanya vizuri katika zao la korosho, hatuwezi kuuondoa mfumo wa stakabadhi ghalani wala mfumo wa ushirika. Mfumo wa stakabadhi ghalani umefanya vizuri katika zao la tumbaku, hatuwezi kuuondoa mfumo wa stakabadhi ghalani na mfumo wa ushirika katika zao la tumbaku. Tutarekebisha changamoto zilizoko katika eneo hilo lakini sio kuuondoa mfumo wa stakabadhi ghalani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hatuwezi kutekeleza mfumo wa stakabadhi ghalani kwenye maeneo ambayo hakuna miundombinu ambayo imeainishwa kisheria na kikanuni. Tumesema hatuwezi kutekeleza mfumo wa stakabadhi ghalani katika Mikoa ya Dodoma, Singida, Manyara, Songwe na Katavi. Katika mikoa yote hii hatutekelezi siyo kwa nia mbaya bali ni kwa sababu mikoa hii haina mifumo ambayo inaweza kumfanya mkulima akafaidika na mfumo wa stakabadhi ghalani. Ni jukumu letu kuendelea kuijenga mifumo hiyo na wakati ukifika tutatoa elimu na tutaenda kwenye stakabadhi ghalani, lakini siyo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini yako mazao hatuwezi kupeleka katika mfumo wa stakabadhi ghalani sasa hivi mfano ni ufuta, choroko, dengu na mbaazi. Hata katika mikoa ambayo tuna-*practice* mfumo wa stakabadhi katika Mikoa ya Shinyanga, Simiyu, Mara na mikoa ambayo inazalisha pamba, hatutatekeleza mfumo wa stakabadhi ghalani katika dengu wala choroko, tutaweka nguvu katika mfumo wa ushirika na mfumo wa stakabadhi ghalani katika maeneo hayo. Kwa hiyo, nilitaka nimtoe hofu Mheshimiwa Mulugo, hatutatekeleza mfumo wa stakabadhi ghalani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, mwenye mamlaka na *instrument* na kanuni ya kutoa maelekezo zao gani liingie katika mfumo wa stakabadhi ghalani ni Waziri wa Kilimo. Huyu ndiye mwenye mamlaka. Sisi kama Wizara na nitumie nafasi hii kuwaambia Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote, atakayetoa mwongozo zao gani linaingia katika mfumo wa stakabadhi ghalani ni Waziri wa Kilimo na wala siyo mtu yeyote. Kwa hiyo, nataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge ambao walikuwa wamedhamiria kushika shilingi kwa sababu ya hoja ya mfumo wa stakabadhi ghalani kama kulitokea makosa tutarekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfumo wa stakabadhi ghalani kote unatumika kwa ajili ya *financing.* Sisi kama Wizara tunashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa ajili ya kufanya mapitio na kuungalia mfumo huu. Tunafanya *pilot* na benki za biashara, tumefanya Igunga na

Katavi, sasa hivi wakulima wa mpunga wanahifadhi mipunga yao katika ghala, wanapewa risiti, ile risiti inaenda katika benki na kuwa *discounted,* anakuwa na fedha, akiwa na fedha wakati anasubiri zao lake liongezeke bei ataliuza wakati atakapoamua yeye.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nirudie tena kwamba stakabadhi ghalani itatekelezwa katika maeneo ambayo imeonesha mafanikio. Hatuwezi kuwa na mfumo mmoja ukahudumia mazao yote, tutatengeneza mifumo ya kuuza mazao kutokana na hitaji la eneo na zao lile. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge walielewe hili na sisi tutaendelea kuwasiliana na wenzetu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa wasiweze kubughudhi wanunuzi wanaonunua ufuta katika Mkoa wa Dodoma, wanaonunua mbaazi, choroko na dengu, mazao haya madogomadogo tunayaacha ili *competition* ichukue nafasi yake yaweze kukua na *volume* iongezeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tuna zao la soya, kama nchi tumepata mkataba wa miaka mitatu wa kuuza zao la soya katika nchi ya China na wakulima ndio wameanza kwenda kulima. Itakuwa ni jambo la ajabu tunaenda kuchukua zao la soya ambalo linalimwa kule Songea Vijijini, mkulima anapewa na mnunuzi Sh.1,000/= bei ya shambani halafu tunalazimisha liingie kwenye stakabadhi ya ghala ili liingie katika mfumo wa ushirika aanze kukatwa tozo mbalimbali siku ya mwisho anaondoka na Sh.800/=. Hii hatutaruhusu Waheshimiwa Wabunge na ninataka niwape *commitment* ya Wizara ya Kilimo kwamba tutajenga mifumo ya masoko kutokana na zao na mahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, korosho iteandelea kubaki katika mfumo wa stakabadhi ghalani katika Mikoa ya Kusini. Tarehe 29 tunazindua mfumo wa kuuza ufuta katika Mkoa wa Lindi na tutauza kwa stakabadhi ya ghala kwa sababu umeonesha mafanikio katika maeneo hayo, hivyo hatuwezi kuua mfumo huu.  Niwaombe Waheshimiwa Wabunge tusiuwe mifumo tunayoijenga, turekebishe matatizo yaliyopo katika mifumo bila kuathiri mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limeongelewa na Waheshimiwa Wabunge kwa uchungu mkubwa ni suala la *export levy* kwenye zao la korosho. Sisi kama Wizara ya Kilimo tunaamini mazao haya ya kilimo yana uwezo wa kujiendesha yenyewe. Takwimu, tathmini na *experience* imeonesha kwamba wakulima wanaweza kujiendesha wenyewe tukiwajengea mazingira mazuri na sisi ndiyo kazi yetu. Kwa hiyo, nataka niwahakikishie kwanza suala la *intervention* ku-*disturb* mifumo iliyojengwa vizuri hatuwezi kulirudia jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini suala la *export levy,* nataka nitoe *commitment* katika Bunge lako kwamba tunalichukua tunaenda kulifanyia kazi, lakini sasa hivi tunaenda shambani. Tunazo takwimu zao la korosho lilifikia *metric tons* 320,000 wakulima walipewa pembejeo, uzalishaji wa korosho mkulima akienda shambani ili aweze kuzalisha korosho kwa gharama za *input* peke yake anatumia Sh.327/= kwa kilo, gharama zake za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, mimi namshukuru sana Mbunge wa Liwale na Mheshimiwa Nape, msimu uliopita baada ya maua ya korosho kuanza kuanguka walipiga kelele tukatuma watu wa *TARI* Naliendele waende wakafanye *study* kwa nini maua ya korosho yanaanguka. Spika nawe ni mkulima wa korosho unafahamu changamoto ya kuhudumia zao la korosho, hatuwezi kumuachia mkulima wa korosho mfumo wa huria katika ku-*finance input,* ni lazima tutafute njia ya kumpunguzia gharama.

Mheshimiwa Spika, dude lile la kupulizia peke yake, mimi nimefika shambani kwako nimekukuta wewe ukihangaika na Afisa Magereza wa Gereza la Mpwapwa, lile bomba peke yake linauzwa shilingi 1,000,000, mkulima gani anaweza kulinunua bomba lile, ni *difficult*.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge tukiwa wakweli ni lazima tutafute njia ya ku-*finance* namna hii. Hatua ya kwanza tuliyochukua ni kuanzisha *bulk procurement system.* Kule Kusini na Bunge lako lifahamu, mkulima wa

korosho inapofika wakati wa kwenda kununua *sulphur* anaenda kukopa. Akienda kujiandikisha kwamba anataka kukopa kuna *microfinance* ziko kule, *sulphur* ambayo mkulima anaenda kukopa kwenye *market price* ni shilingi 32,000 lakini wakulima wananunua mpaka shilingi 40,000 mpaka shilingi 50,000.

Mheshimiwa Spika, akienda kukopa kwenye *microfinance* anajaza idadi ya mifuko anayotaka halafu yule mwenye *microfinance* anaenda kwa *supplier* anamwambia nipe *sulphur,* yeye anaichukua kwa shilingi 32,000 halafu anampa mkulima kwa shilingi 40,000 halafu ile shilingi 40,000 inatozwa *interest* ya *2%* kila mwezi. Wanao-*benefit* ni *service provider* na wala sio *farmer.* Tumechukua hatua, tumeamua safari hii vyama vyote vya ushirika vimeleta mahitaji, tumekitumia chama kimoja, bei ya *sulphur* imeshuka mpaka shilingi 29,750. Kwa kukokotoa kwetu huku katika *market rate* mkulima alikuwa anatumia shilingi 300 kwa kilo kwenye *input.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge la kwanza, suala la *export levy* tunaenda kulifanyia kazi, tumewasikia, tutatafuta *solution,* lakini wakulima watagawiwa pembejeo zote kutokana na mahitaji yao. Kwa mara ya kwanza mpaka sasa sekta hii inadaiwa zaidi ya shilingi bilioni 30. Sisi sote tunafahamu, Mheshimiwa Katani na Mheshimiwa Nape wanafahamu, kila mmoja anafahamu kule kwenye korosho mkulima akivuna anaeenda kukopa kwenye chama cha msingi ni Hussein, anayeenda kuuza ni Nape. Matokeo yake sekta yote inadaiwa, mkulima anadaiwa, chama cha ushirika kinadaiwa, Bodi ya Korosho inadaiwa, sekta haikopesheki, taasisi za fedha zinajitoa kuhudumia sekta hii. Kwa hiyo, njia pekee na sisi tuwaahidi kwamba tunaamini katika kuanzisha mifuko ya kuendeleza mazao, hiyo ndio njia itakayomsaidia mkulima. Kwa hiyo, hii hoja ya *export levy* tunaichukua tunaenda kuifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hapa tumejadili suala la korosho ya Pwani. Kwa muda mrefu humu ndani tunazungumzia korosho ya Pwani haina ubora, kwa nini haina

ubora? Majibu yanakuja kwamba inapata unyevu. Korosho ya Pwani inapata unyevu, iki-*mature* inakuwa nyeusi.

Mheshimiwa Spika, Pwani kuna mvua nyingi. Kwa hiyo, kama Wizara tumechukua hatua gani ambayo tunaanza kuitekeleza sasa hivi? Vyama vyote vya msingi na nimshukuru sana Mheshimiwa Ulega, Mheshimiwa Mchengerwa na Mheshimiwa Twaha, safari hii tumeamua wakulima wote wa Pwani kuanzia mwezi ujao vyama vya msingi vyote tutavigawia maturubai kwa ajili ya kuanikia korosho zao, hili ni jambo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, katika sekta ya korosho kuanzia Pwani, Lindi, Mtwara mpaka Ruvuma wana *AMCOS* 623, tumeamua kila *AMCOS* tutaigawia bomba kwa ajili ya kupulizia korosho za wakulima wao kwa sababu watu wana-*make profit in the middle.* Tutatumia mifuko ya mazao ku-*finance* na ku-*subsidize input* kwenye sekta ya kilimo na hili linawezekana. Kwa hiyo, tunaomba Waheshimiwa Wabunge mtupe fursa tuweze kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la *export levy* tumelichukua, sasa hivi tunaenda kwenye msimu na tutalifanyia kazi. Tutajadiliana ndani ya Serikali ili tuweze kupata *solution* ambayo haitamuumiza mkulima.

Mheshimiwa Spika, niongelee suala la tumbaku. Takwimu zinaonesha tumbaku ilifika *metric tons* 120,000. Mimi nishukuru humu ndani kwa siku hizi mbili nimejifunza, jedwali lile linaonesha *trend* ya tumbaku kwa kipindi cha miaka kumi, kuanguka kule kwa tumbaku hakujasababishwa na mkulima hata mmoja. Humu ndani tumekuwa tukisikia kauli kwamba korosho, tumbaku, pamba na kahawa ni mazao ya siasa, sio kweli, haya ni mazao ya kibiashara. Kwa hiyo, *let us put aside politics* kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumbaku hii imeporomoka kwa sababu ya policy zetu mwaka 2014-2015 tulienda kushtaki makampuni yote na *pressure* ilitoka ndani tukayapiga faini ya trilioni saba *TLTC* aliondoka kwenye nchi hii tunachukua

hatua gani. Mwaka jana kupitia Bunge lako Tukufu hili, tulibadilisha sheria ya *LCC*, tukawaondolea faini zote makampuni haya. Wakalipa tozo ya shilingi dola 300,000 kutoka trilioni saba *it was unfair* na haikuwa haki, hawa wanafanya biashara matokeo yake makampuni yaka-*pull out* sekta ya tumbaku ikaanguka mpaka tani 36,000 mwaka jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa hatua tulizochukua mwaka huu wakulima wa tumbaku wamepeleka sokoni tani 67,000 ambazo tumeanza kuziuza. *Just* kwa maamuzi madogo tu ya kufuta tozo tulizowapiga, faini kuwapiga na kukaa nao mezani wanunuzi wamekuja zao letu tunalouza safari hii ni tani 67,000 kutoka tani 39,000 na sisi tuwaahidi kwamba tutalinda wakulima na tutawalinda wanunuzi wanaonunua mazao ya kilimo hakuna njia nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili ambalo tunafanya kwenye tumbaku, mkulima wa tumbaku zao za tumbaku linakuwa *determined* na biashara ya dunia unapozalisha tani moja ya tumbaku mnatakiwa mpande miti 600 lazima wanunuzi wajiridhishe. Kinachotokea mkulima anakatwa 0.092 dola kwa kilo kwa ajili ya ku-*finance* mfumo wa kupanda miti. Nataka nikwambie kwa mwaka wakulima wa nchi hii wanachangia bilioni 25 lakini miche hile haipandwi popote tumechukua hatua tumebadilisha mfumo sasa hivi fedha zile zitakusanywa kwenye *one account* tutatangaza *tender* tutaingia makubaliano na *TFC* miche itapandwa na itaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwasababu hivi zilikuwa ni shughuli za watu wanagawana viongozi Mikoani Mheshimiwa Kakoso anafahamu watu wanaotoka Katavi wanafahamu kilichotokea baada ya maamuzi haya tunabadilisha mfumo wa uharamiaji kwenye tumbaku. Mkulima wa tumbaku anakwenda kukopa yeye na *AMCOS* yake *at the interest of 7 percent USD* hawezi kupata faida, atapata hasara tu tumeamua tumebadilisha mfumo kwanza *procurement* ya *input* yote tunaagiza kutoka kwa *producers* hatutotumia watu wa kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili tumesema kwamba tunatumia *LC model* kwamba *supplier* anapeleka pembejeo tunamlipa baada ya siku 360 baada ya mnada mkulima anapata bila riba na tumevizuia vyama vyote vya ushirika kwenda kukopa katika benki zinazozalisha tumbaku kwa dola na kwa riba kwa sababu mbolea tutapeleka, dawa tutapeleka, *supplier* atapewa *LC* baada ya siku 360 mtoa huduma atapata fedha yake na tumekubaliana na taasisi za fedha hili tunalifanya.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ambalo nilitaka niliongelee ni zao la pamba, zao letu la pamba lilidondoka mpaka tani 120,000 na sisi wote tunafahamu na *graph* ile inaonekana tulifika tani 348,000 mwaka 2019 mkulima alivyopewa mbegu alipewa dawa tukabadili *policy* zao likadondoka, hatua gani tumechukua safari hii, cha kwanza tumewagawia wakulima wa pamba wote mbegu bila kulipia, la pili tumewagawia dawa zote bila usumbufu wowote tumekaa na wanunuzi na vyama vya ushirika lakini tumewapatia *input* hizi bila wao kwenda kukopa benki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, benki zimetupa *LC* watoa huduma wamepeleka pembejeo baada ya kupeleka pembejeo zitalipwa pembejeo baada ya mkulima kuuza zao lake. Mwaka huu tunavuna *metric tonnes* kati ya 350,000 hadi 400,000 na mkulima ataenda kuuza kwa bei ya kuanzia 1050 bila ukatwa hata shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niliombe Bunge lako Tukufu tupo tayari kufanya mabadiliko, tupo tayari kuchukua hatua tutakubaliana na maoni na ushauri wenu tusaidiane kwa sababu jambo hili hatuwezi kulifanya peke yetu. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ambalo nilitaka niliongelee ni suala la umwagiliaji ni kweli bila mfumo mzuri wa umwagiliaji hatuwezi kupiga hatua. Wizara kwanini tunafanya tathmini? Tunafanya tathmini kwa sababu *experience* yetu ya muda mfupi imetuonesha kwamba tunahitaji kufanya mabadiliko makubwa kwenye tume yetu

ya umwajiliaji, tutawaleteeni sheria hapa. Tunataka kuibadilisha tume kuwa wakala wa umwagiliaji kuwa *agency* kama ilivyo *TARURA* kama zilivyo nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili tunabadili mifumo kwasababu hii mifumo ya umwagiliaji tunatumia gharama nyingi kujenga mradi mmoja tumeamua katika bajeti hii ambayo mtatupitishia Waheshimiwa Wabunge la kwanza tumeanzia kitu kinaitwa *irrigation development fund* ambayo kwa kutumia fedha zetu za ndani tumetenga zaidi ya bilioni 30.

Mheshimiwa Spika, lakini hatua ya pili tutakayoichukua ni kwamba tume ya umwagiliaji tumewaagiza kwamba watangaze *tender* kwa ajili ya kununua vifaa, ili kuanzia mwaka huu wa fedha kwenda mbele kazi yetu ya kwanza pamoja na ku-*repair* miradi iliyopo lakini nikuchimba mabwawa maeneo yote ambayo tunaona kwamba kuna uwezekano wa kuhifadhi maji, hii ndio itakuwa *priority* yetu tutaangiza vifaa tutakuwa navyo wenyewe tumefanya *pilot project* kwenye mradi wa Ruaha chini na Mheshimiwa Mbunge yule pale shahidi tumetumia *excavator* zetu wenyewe bila kutumia fedha nyingi kwa ajili ya kuu-*repair* ule mradi.

Mheshimiwa Spika, nilitaka niliongelee jambo jingine kuhusu suala la mahindi, ni kweli mwaka jana mahindi yalifika mpaka kilo 1,000 -1,100 lakini sasa hivi mahindi yameonekana bei imeshuka. Nashukuru nimalizie tu kuwaambia waheshimiwa Wabunge kwamba tunaamini kwamba bila kui-*engage* sekta binafsi katika sekta ya kilimo hatuwezi kwenda mbele na sisi tutajenga mazingira kuhakikisha kwamba sekta binafsi inakuwa sehemu ya safari ya kilimo ili tuweze kupiga hatua. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ufafanuzi mzuri, tunakushukuru sana, sasa tumwite mtoa hoja

Mheshimiwa Profesa Mkenda karibu sana hapa mbele, karibu sana. (*Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru sana kwa fursa hii naomba kwanza niweke kumbukumbu sahihi, kwamba ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 294,162,071,000 kupitia fungu namba 43, Fungu namba 5 na Fungu namba 24 kama ilivyoainishwa katika hotuba ya bajeti ambayo tuliwasilisha mbele yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe shukrani nyingi sana kwa Wabunge wote kwa michango yao mingi sana tumepata wabunge 87 waiochangia katika hotuba hii kati yao tumepata vile vile michango kwa maandishi kwa Wabunge tisa. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba kila lililozungumzwa na tulililoletewa tutalitafakari kwa kina, tutalizingatia na pale inapowezekana tutalitekeleza kwa hiyo ninawashukuru sana kwa michango yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe shukrani za pekee kwa Kamati yako ya kudumu ya Kilimo Mifugo na Maji chini ya uongozi mahiri wa Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Dkt. Ishengoma na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Almas Maige na wajumbe wote kwa kweli tumefanya nao kazi kwa pamoja na nitatoa mfano mmoja tu. Hivi mnavyoona dodoso la umwagiliaji wakati tunapeleka taarifa yetu ya umwagiliaji kwenye Kamati ndio baadhi ya Wabunge wakatuambia hapa mbona kinachoelezwa hapa sicho hasa tunachokiona kule. Kwa hiyo, tulishapanga na Mheshimiwa Bashe tutawanyike nchi nzima lakini basi hapa katikati mara nzige, mara misiba nakadhalika. Lakini tutaanza safari baada ya Bunge na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge naombeni mjaze haya madodoso tutayafanyia kazi kwa sababu tunahitaji kuwasikiliza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tulianza kuyasikia yale kwenye kama Kamati na tutayafanyia kazi. Kwa namna ya pekee napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Hussein Bashe Naibu Waziri wa Wizara yetu ndio Mheshimiwa anasema

mzigo mzito mpe Mnyamwezi aubebe ninamshukuru Mheshimiwa Rais kunipa Mnyamwezi kama Naibu, tunafanya kazi vizuri kwa ushirikiano ni mbunifu na kadri tunavyojua Mheshimiwa Bashe haja-*change* tulikuwa tunamsikia hapa Bungeni akiongea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi nafasi aliyopo mengine alikuwa anaongea anayafanyia kazi huku sio kila kitu anaweza akakisema kabla hakijakamilika ninawahakikisha kwamba Mheshimiwa Bashe ni yule yule ana moto ule ule na ubunifu ule ule ninashukuru sana na kumpongeza kwa kufanya nae kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda sana kutoa shukrani kwa Katibu Mkuu Andrew Massawe, Naibu Katibu Mkuu Profesa Tumbo, watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwakweli wanafanya kazi kubwa na mimi ninasema tu kama kuna matatizo, matatizo ni kwa Waziri kwa sababu tunachowaambia wanafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiona hakijakwenda vizuri labda hatujawaambia kwa hiyo lawama anabeba Waziri wa Kilimo, wana roho nzuri sana mambo yakiharibika labda Waziri ndio atakuwa mwenye roho mbaya.

Mheshimiwa Spika, kilimo na hili ni muhimu sana lipo *ASPD* Ilani ya Chama, lipo kila *document* na hili lazima tulikumbuke tatizo la kilimo ni tija ndogo na Mheshimiwa Bashiru amelieleza vizuri sana na Waheshimiwa Wabunge wengi sana hapa, na nitalifafanua kidogo kwa sababu mikakati tuliyoichukua kwa bajeti ile ile haijaongezeka na nitawaeleza tumefanya nini kuhakikisha kwamba tunashughulika na suala la tija ndogo ni muhimu sana na sisi tunajitahidi tusishindwe kwa sababu tunachojaribu kukifanya tukishindwa pengine nguvu ya kujaribu kukifanya itapotea.

Mheshimiwa Spika, ngoja ianze ku-*aggregate data* ukiangalia pato la Taifa tunaona kwamba Kilimo kinachangia, kilimo kwa ujumla wake maana mifugo na kila kitu kinachangia asilimia 26-point *somethings*. Kwa sababu

kilimo cha mazao tu ni takribani asilimia 18 lakini watu walioajiriwa kwenye Kilimo ni takribani asilimia 58 maana yake ni nini?

(i) Maana yake ni kwamba pato la Taifa ambalo uzalishaji wetu takribani theluthi mbili inazalisha theluthi moja tu maana yake uzalishaji ni mdogo sana kwa mtu mmoja mmoja, tija ni ndogo sana;

(ii) Umaskini ni mkubwa kwenye kilimo;

(iii) mgawanyo wa mapato ni mbaya, maana yake ni kwamba pato la taifa ndio keki tunayokula inapokuwa wakulima ambao ni theluthi mbili ya watu wote wanakula theluthi moja tu ya pato la Taifa anayekula theluthi mbili ni nani? Kwa hiyo huo ni mgawanyo mbaya wa mapato, na yote hayo ni kielelezo kwamba tija ni ndogo na Mheshimiwa Rais alivyohutubia Bunge lako Tukufu hapa alizungumzia cha kwanza tatizo kubwa ni tija na kama hatuchukui hatua za kunyanyua tija hatua nyingine sio *sexy* lakini lazima zichukuliwe ili tuweze kusonga mbele hiyo ni *aggregate data.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hebu twende kwa zao moja moja kabla ya hatujaangalia pale niwasomee hapa pamba, nadhani kuna Waheshimiwa walizungumza hapa sisi tunapolima kwenye hekari moja pamba tunapata kilo 200, 300, 350 kwa hekari moja *West Africa* kuna nchi zinapata kilo 1000 kwenye hekari moja. Kwa hiyo, hata tukizungumza masoko hapa tutazungumza masoko sana lakini tija ikiwa ndogo unaenda kushindana kwenye soko la Dunia na mtu ambaye kwenye hekari moja anapata kilo 1,000 halafu sisi tunapata hekari moja kilo 200,250 na ndio maana nitaeleza hatua ambazo tunazozichukua tena kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kusogea ebu tuchukue michikichi na Mheshimiwa Waziri Mkuu atatusaidia sana kwenye hilo sasa hivi tuna matatizo ya mafuta ya kula wanasema michikichi ilitoka Kigoma. Sisi kwenye hekta moja ya michikichi tunapata mafuta ya mawese tani 1.6 lakini huko

tunaponunua mafuta ya mawese sasa hivi kwenye hekta moja wanapata mpaka tani 10 za mafuta. Kwa hiyo, tunaweza tukazungumza masoko sana na tutayazungumza kwa hiyo, kipaumbele cha kwanza kitakuwa nini. Kwa hiyo, soko la mafuta lipo hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siku zote tunatumia mafuta hapa hatujaacha kutumia mafuta shida iko wapi sio kwamba tu kila mara likiwepo soko basi uzalishaji unakwenda soko mafuta halijawahi kuondoka lakini uzalishaji ndio huo. Hatuwezi kushindana tumeongeza *import duty* kwenye mafuta wanasema bora kuletwe *refine oil* sasa *import duty* unaiongeza pale wananunua mafuta *refine* wanaleta hapo wanauza kwasababu kwenye hekta moja wanapata *almost* tani kumi ya mafuta hilo tatizo tusipolitatua hatuendi popote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua kitu kingine hapa juzi nilienda Kongwa, nilienda mchana kidogo nimeangalia mtama, sijui kama picha ipo hapa niliona mtama huwezi kuamini kwa utafiti wetu tu tumegundua mtama aina ya *Masiha* ambao kwa mkulima sasa hivi kwa hekta moja mtama anapata tani 0.9 akilima vizuri 0.9 kwa mbegu mpya tuliyoipata kwa utafiti wetu sisi hekta moja unapata tani 3 hadi tani 3.8. Kwa hiyo, ukiingia kwenye soko uzalishaji wako tija ni dogo utahangaika kweli kweli kama wenzako tija nzuri na sisi Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano tumesema ni kujenga uchumi shindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana yake kuzalisha kwa gharama ndogo ili uweze kuuza, sasa naweza nikatoa mfano mmoja hadi mwigine hadi mwingine hadi mwingine. Lakini hili suala la tija ndio kubwa katika kilimo tusipolitatua tutaendelea kuzungumza kilimo ni uti wa mgongo kilimo ni *oxygen* tutalizungumza hilo lakini ufumbuzi upo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spia, sasa tunafanya nini? Kwanza kwenye tija na hiki ni vizuri tukisema tunapokuwa tunataka kujenga uchumi wa Viwanda hapa nchini kwa kweli tunataka

malighafi iwe ni bei ndogo maana yake ni kwamba tunataka tuweze kupata mazao kwa bei ndogo. Lakini tunataka mkulima apate fedha nyingi na njia pekee unayoweza kutimiza hilo ni kuwa na tija kubwa huyu mkulima wa Pamba tunataka kuanzisha *Textile Industry* tungependa aweze kuzalisha kilo 1,000 kwa ekari moja ili hata kama bei imeshuka yule mwenye *Textile* anunue pamba kwa bei nzuri bado kipato cha mkulima kiongezeke.

Mheshimiwa Spika, na hata mishahara sisi kilimo tunaweza tunaongeza mshahara tunaita mshahara halisi *real wage* tunaongezaje bei ya chakula ikishuka kwa kipato chako hicho hicho unaweza ukala na kununua vitu vingi zaidi kuliko kabla bei ya chakula haijashuka walio-*industrialize* wote walihakikisha bei ya chakula ndani ya nchi inashuka, tunafanyaje? Tija kwa njia zote hizo mbili; *to pathways to industrialization; the cost of raw material that used in the country should go down, the price of food should go down* lakini *challenge* yetu vile vile tunataka kipato cha Mkulima kiongezeke jibu lake tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tunafanya nini? Kipaumbele cha kwanza utafiti na Mheshimiwa Rais alivyotoa hotuba hapa alizungumzia hicho hicho na niwaeleze ni kwa nini nimewaeleza hapa kilimo cha Mtama hapo Kongwa ninawaalika mkaangalie kuna mashamba yapo *side by side* kilimo ambacho ni *tradition* na kilimo kinachotumia utafiti *agronomy* nzuri na mbegu nzuri unaona kwa macho huna haja ya kuambiwa.

Mheshimiwa Spika, mihogo tunapata soko sasa hivi la Mohogo China lakini tuna mbegu pale Kibaha tumeigundua inaweza sasa hivi kwa hekta moja kupata kuanzia tani 22 hadi tani 50 na hauwezi kudanganya ule muhogo ukiushika unauona. Sasa hivi tunapata tani tatu tukienda sana tani nane. Kwa hiyo ninashangaa soko linafunguka soko lipo tunashindwa kulishika kwa sababu ya tija ndogo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utafiti ni kipaumbele cha kwanza na kitasaidia hata kwenye soko kwa sababu ni suala la ushindani tu. Hapa kuna nchi moja tulipata matatizo mpakani unasikia minong'ono labda wamenunua mahindi kutoka Latin America bei ndogo kuliko mahindi yaliyoko hapa na gharama yote ya usafiri, inakuwaje, tija ndogo, sasa tumefanyaje hapo? Bajeti ya Wizara ya Kilimo iko pale pale, haijaongezeka lakini sisi ndani ya Wizara kwa panga pangua tumeongeza bajeti ya utafiti kutoka shilingi bilioni 7.35 mpaka shilingi bilioni 11.63 ongezeko la asilimia 63. Ndiyo maana nasema watumishi wetu wana roho nzuri, tumekaa hapo mimi na Naibu Waziri nawaambia tutafuteni hela tumeongeza hela hizo za utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tumegundua kwenye sheria tunaruhusiwa kuanzisha Mfuko wa Utafiti, haujaanzishwa kulikuwa hamna kanuni. Kanuni tunazikamilisha inawezekana fedha hizi tulizozipata tukaziongeza kutokana na Mfuko wa Utafiti. Tutaongea na wadau wa maendeleo tuongeze hela ili vituo vyetu vyote vya utafiti vifanye vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano sasa hivi kwenye korosho, kila mahali tunataka kuzalisha korosho safi lakini ukiangalia tija yetu ya korosho bado iko chini. Tunaweza tukazalisha *twice as much* pale Mtwara peke yake, kwa hiyo, tunaenda *extensive* lakini *intensive we are not doing anything*. Nasikia *Ivory Coast they are doing the best* kuliko sisi hapa kwa sababu ya utafiti. Ukiviangalia vituo vyetu vya utafiti vimechoka, kwa kweli ni sawa na yule yule dada daktari alivyosema *it is not sexy* kwa sababu utafiti ni pata potea, unaweka hela unajaribu unakosa, unaweka hela unajaribu unapata. Nadhani Prof. Ndakidemi yeye alishagundua mbegu moja, kwa hiyo inachukua muda lakini lazima tufanye. Hicho ni kipaumbele cha kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika utafiti la kwanza utafiti kuhusu mbegu, tumeona wataalam wetu wamegundua mbegu nyingi na nzuri; za mtama, mihogo na michikichi inayooteshwa chini ya uongozi wa Waziri Mkuu.

Wananiambia ile mbegu ikiota sasa hivi kwa hekta moja tunaweza tukapata mafuta takriban tani tano, kwa hii michikichi mipya ambayo tunaotesha hapa. Kwa hiyo, tutakomaa na utafiti tu inawezekana tukaondoka Wizarani hatujamaliza lakini tunaanza nalo, tunakomaa nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili kwenye utafiti ni kilimo bora. Kwenye pamba tunaambiwa hata *spacing* tu inaweza ikaongeza tija zaidi ya asilimia 50 na hiyo ni matokeo ya utafiti. Kwa hiyo, kipaumbele cha kwanza kinabaki utafiti haina maana kwamba masoko siyo kipaumbele kwa sababu haina maana kwamba tutafanya utafiti tukimaliza ndiyo twende kwenye masoko, vyote hivyo tunavibeba. Pia kuna vipaumbele vingine hivi tumeviita vipaumbele vikuu vya mkakati, yako mambo ya kujenga vihenge, sumu kuvu na kila kitu. Hivi ni vipaumbele vikuu vya kimkakati ukiona kimekuwa cha kwanza na kile cha masoko tutakwenda navyo hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele kikuu cha mkakati cha pili uzalishaji wa mbegu. Bajeti ya Wizara imebaki vilevile, panga pangua tumeongeza fedha kwa *ASA* kutoka shilingi bilioni 5.42 kwenda shilingi bilioni 10.58. Kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri hela za umwagiliaji tutakazozipata kwenye Mfuko wa Umwagiliaji, cha kwanza mashamba yote 13 ya *ASA* mengi yapo tu ni mapori yanatuletea ugomvi na wananchi tunaenda kuyafufua na tutayafanyia umwagiliaji ili tuweze kuzalisha mbegu *throughout the year*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeanza kwenye ngano, tumehamasisha kilimo cha ngano, tumeingia makubaliano na *importers;* ngano kilo moja sasa hivi itakuwa Sh.850, *the best price,* wanasema wenyewe wanatudai mbegu ziko wapi? Nimetoa kibali tumeagiza mbegu kutoka Zambia, *just across the border,* hatuna!

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia alizeti hapa, *record* ime-*improve* sana sasa hivi haitoshi. Kwa hiyo, hata kwenye mkakati wa mafuta ya kula ambao nitauzungumzia hapa tuta-*import* mbegu na

tutatumia *revolving fund* kuwapa wakulima kuhakikisha tunazidi kuzalisha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunahitaji mbegu ya kila kitu. Nimesikia Waheshimiwa Wabunge hapa wanazungumza mbegu za mahindi zinakuja kinyemela kutoka Zambia, za viazi zinakuja kinyemela kutoka Kenya na matokeo yake tukiwa tegemezi kwenye mbegu uhakika wa chakula *(food security)* utakuwa mashakani sana. Kwa hiyo, tumeongeza hilo, mashamba yote ya *ASA* tutayafufua tutayafanyia umwagiliaji. Tutatumia na sekta binafsi na tutapambana na mazingira mazuri ya kibiashara waongeze uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya utafiti umepata mbegu nzuri, unapata kilimo bora kinamfikiaje mkulima, huduma ya ugani. Bajeti ya Wizara haijabadilika. Bajeti tunayomaliza nayo shughuli za ugani tulitenga shilingi milioni 603 tu. Kwa hiyo, wakati unazungumza idadi ya Maafisa Ugani wachache lakini hata fedha zenyewe ndiyo hizo.

Mheshimiwa Spika, sasa panga pangua, bajeti *ceiling* ni ileile tumetoka kutoka kwenye shilingi milioni 603 za ugani kwenda mpaka shilingi bilioni 11.5. Wakati tunafanya haya unaambiwa sasa Waziri, Naibu Waziri Maafisa Ugani wako TAMISEMI, kwa nini tukate huku tupeleke TAMISEMI, tunapeleka hela hiyo Maafisa Ugani wawe TAMISEMI wawe popote wanatumikia Serikali moja kwani hatutasogea bila kuboresha ugani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wako wakulima wakubwa, viko vyama vya ushirika kama Kahama wameajiri Maafisa Ugani na unaanza kuona matokeo lakini sehemu nyingi mtu hajui afanye nini. Hapa Dodoma tukisema tulime alizeti watu wengine wanavuna mbegu ile ile wanaenda kuotesha, *productivity* inakuwa ndogo sana, unaotesha lini na kwa utaratibu gani?

Mheshimiwa Spika, tutakachofanya kwenye ugani hicho hasa ndiyo tunasema tunataka tusishindwe na tutajitahidi tusishindwe, tutafanya nchi nzima mambo mengi

na tunashirikiana na vyama vya ushirika na makampuni binafsi kama ile *NOSC – Njombe Out Growers Services Organization* na Kahama *Cooperative Society* na nchi nzima tutapeleka huduma nyingi. Hata hivyo, pamoja na yote tutakayofanya katika nchi nzima tumechagua mikoa mitatu ambayo tunataka kufanya huduma za ugani kwa namna ambayo pengine hatujaifanya kwa muda mrefu au tangu tupate uhuru. Tumechagua Dodoma, Singida na Simiyu, tumeongozwa na umuhimu wa kuzalisha mazao ya mafuta, alizeti *at the heart of it.* Tunajua tukifanikiwa tutarudi kwa Waziri wa Fedha ule mwaka unaokuja, unaona matokeo haya, unaona shughuli za ugani zinavyolipa hebu twende tukafanye kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika hii mikoa mitatu pamoja na baadhi ya Maafisa Ugani wengine tunawapa *mobility* (pikipiki). Nilishasema hapa tunawasaidia kwa fedha za Serikali wawe na mashamba yao, walime, tuweze kukagua unalimaje wewe, mashamba darasa yote yanafufuliwa na ya mwanakijiji ambaye anaonekana anaweza akawasaidia. Pia tutawapatia mafunzo rejea, wengine wameshafunzwa miaka 20, 25 wanafanya kazi hawajafundishwa upya *new technics* na *new discoveries* ambazo tunazo.

Mheshimiwa Spika, tutahakikisha tunawapa *spark smartphone* ambazo zitasaidia vitu vingi. Moja watakuwa wana-*monitor* masoko lakini pili sisi tutawa-*monitor* wanafanya nini. Kila siku kuanzia Jumatatu mpaka Ijumaa lazima ajaze kwamba amefanya nini kwenye *mobile* kilimo. Umeenda kumtembelea Mheshimiwa Gambo lazima ujaze ulienda saa ngapi, tatizo lake lilikuwa nini, umemshauri nini na simu yake. Kwa hiyo, tunaweza tukakaa ofisini tukapiga tukamuuliza Mheshimiwa Gambo eti alikuja bwana shamba hapa? Kwa hiyo, tunafanya hayo katika mikoa hii mitatu.

Mheshimiwa Spika, vilevile tutawapa *soil tool analysis kits* kwenye kila halmashauri na kadhalika. Katika suala la alizeti ambalo nitalizungumzia mbegu hazitoshi kwa hiyo tutatoa huduma ya ugani na hii huduma ya ugani kwenye alizeti na pamba kwa Simiyu na alizeti itaongeza masuala

kama mtama na mazao mengine yote pamoja na Mheshimiwa Mavunde alivyosema suala la kilimo cha zabibu. Kwa hiyo, mazao yote mabwana shamba watafundishwa upya namna ya kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, baada ya mwaka mmoja tutapima matokeo ya hiki tunachojaribu kwenye mikoa mitatu. Tutafanya kazi na Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya na tutafuatilia kwa karibu na Waheshimiwa Wabunge tunawa-*invite* muangalie.

Mheshimiwa Spika, sasa labda nilisemee hapa hapa kwamba katika hiyo mikoa mitatu nguvu kubwa sana itaenda kwenye alizeti na mazao mengine, mbegu tutapata wapi? Sasa hivi tumeshazungumza na taasisi moja ya kimataifa nadhani tumeshapata hela ya kuanzia. Juzi nimefanya mkutano kwa *Zoom* inaweza ikaongezeka, hela hiyo ikija tunaita mkutano wa wakamua mafuta, tutazungumza nao na ma-*bankers* kuhakikisha kwamba wakulima kwenye vyama vyao vya ushirika wanapata *contract farming* tunawapa mbegu ya chotara (*hybrid*) ambapo kwa sababu hatuna *record* ya kutosha tutawaletea wakati wa mawazo tuta-*recovery* halafu tutakuwa *revolving fund*. Kwa wakulima wakubwa bila kujali Mikoa ya Dodoma, Singida na Simiyu iwe ni Kiteto, Simanjiro, Manyara au Morogoro tutawa-*encourage* na sisi wapate mbegu waingie kwenye *contract farming* ili sasa viwanda vya kukamua mafuta ambavyo sasa hivi vinafanya kazi miezi miwili, mitatu, minne vinafungwa kwa uhaba wa mbegu za mafuta viweze kuingia kwenye mikataba na wakulima katika mikoa hii.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele kingine sitavitaja vyote tulizungumza ni umwagiliaji. Kwenye umwagiliaji bajeti tumeongeza kutoka shilingi bilioni 17.7 kwenda shilingi bilioni 51.5. Pili tumeanzisha Mfuko wa Umwagiliaji ambao tunaamini tutautumia kwa ajili ya kuimarisha shughuli za umwagiliaji na tutajaribu kuongea na wadau mbalimbali tuhakikishe kwamba tunapata fedha nyingi na kuchukua hatua ambazo Naibu Waziri amezieleza.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kidogo kuhusu masoko. Kwanza nianze na tumbaku na Mheshimiwa Naibu Waziri nakushukuru sana kwa maelezo, tunazungumza na ile kampuni ambayo iliondoka hapa, *prospect* ni kubwa watakuja kurudi kwenye biashara. Wamewasiliana na Mheshimiwa Bashe na tumekubaliana. Walitaka kutuma *consultant* tumesema hapana tunamtaka yeye mwenyewe aje tuzungumze kwa sababu tunakosa ushindani. Tumbaku ni zao pekee ambalo nilikuta watu wamekamatwa huko Katavi wanaambiwa eti umelima tumbaku bila kibali wakanyang'anywa hela zao, nimetoa amri warudishiwe hela zao. Halafu unapewa pembejeo na makampuni hayo unalima tumbaku ukitaka kuuza unambiwa wewe hukupewa *contract* ya kulima tumbaku yako ni makinikia wananunua kwa bei ya kutupa, hilo tutalishughulikia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu chai, tunaanzisha mnada wa chai kama ambavyo tumeshaeleza.

Mheshimiwa Spika, sasa twende kwenye mahindi. Tumebarikiwa sasa hivi tuna ziada kubwa ya mahindi. Kwanza niwahakikishie hata kabla ya changamoto ya mpaka na Kenya tuliita mkutano mkubwa wa wafanyabiashara wa nafaka hapa Dodoma kuhimizana twendeni tukatafute masoko kwa sababu haya masoko kazi ya *private sector* kazi yetu ni ku-*facilitate.* Tulizungumza tukaunganisha na Mabalozi wote wa nchi jirani za DRC, Zambia, Malawi, Burundi, Rwanda, Kenya, tukazungumza na kuweka mikakati ambayo mingine tumeanza kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kenya niseme mahindi yetu yanayoenda Kenya tunapima sisi ni salama. Nadhani hata wakati yamezuiwa bado kwa namna fulani yalikuwa yanaenda. Sasa Mheshimiwa Rais ameenda Kenya tumesikia wote tangazo mahindi yanakwenda. Natoa wito kwa wafanyabiashara sombeni mahindi pelekeni Kenya maana yanapendwa sana kule. Natoa wito tena kwa vyombo vyetu vya usalama barabarani mmetusaidia sana, tukiona mtu anasafirisha mahindi na ufuta siyo bangi watu wetu wamekuwa *harassed* sana kule mpakani acha yaende

yauzwe kwa vyovyote na yauzwe popote, nendeni Serikali itasimama na nyie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ninavyozungumza *rate* ya kupeleka mahindi Kenya ni wastani wa tani 2,000 kwa wiki. Kwa hiyo, mahindi yanakwenda na tunafuatilia mpakani. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa safari yake ya kwenda Nairobi na mimi nilikuwa kwenye msafara wake na nilipata fursa ya kuongea na Waziri wa Kilimo wa Kenya alikuja mwenyewe mpakani Namanga na alinipigia simu. Kwa hiyo, biashara ipo na ni soko kubwa tulichangamkie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya Kenya ni tani 600,000 ya mahindi bado tunacho-*supply* kule ni tone tu. Twendeni tukauze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko imetoka Sudan ya Kusini, wamefanya mazungumzo mazuri sana na wafanyabiashara wa Sudan ya Kusini watakuja hapa kwa ajili ya kukamilisha maelewano ya namna ya kuuza mahindi na mchele na mazao mengine Sudan ya Kusini.  Mimi binafsi nimepanga tunaenda na msafara wa wafanyabiashara baadaye Sudan ya Kusini na tutaenda DRC, mchele Zimbabwe na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Zimbabwe wana mahindi ya kutosha wanahitaji mchele. Humu ndani kuna Mbunge mwenzetu ni mfanyabiashara, namsifu sana ametusaidia kufungua soko la Eswatini Swaziland, c*onsignment* ya kwanza imeenda. Kwa hiyo, tunataka kufungua masoko South Afrika na maeneo kama hayo. Tumekubaliana Wizarani mtu anapoomba kibali cha kusafirisha mazao akishasema nia yake hata asiporudi tunamtafuta na tumekubaliana utamfuata popote umsaidie kujaza *online* apate kibali bidhaa zetu ziende. Kwa hiyo, tunaendelea kuchakarika kupeleka mazao sehemu nyingine mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niwahakikishie mahindi sasa hivi Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko imepata shilingi bilioni 10 tumewaambia waingie sokoni bei ya mahindi

ni ndogo wale wanafanya biashara nunueni mchangamshe soko nendeni mkauze. Kwa hiyo, tumekubaliana wataanza kufanya biashara hiyo. Tuna mazungumzo vilevile na *World Food Program*, tuna mkataba pamoja na hivyo kuna mahitaji mengine ya mahindi ambayo yanaendelea. Pamoja na changamoto hii tunaamini kwamba sasa soko litatulia na hasa wafanyabiashara wakiona fursa ipo na mambo yanakwenda.

Mheshimiwa Spika, kwenye mchele sasa hivi tunauza sana Uganda. Tunataka kwenda Saudi Arabia na nchi nyingine kwa ajili ya kufanya kitu kama hicho. Niishie hapo ili nisiache mambo mengine muhimu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tuna changamoto ya ushirika, ni kweli kumetokea wizi mkubwa na ubadhirifu Mheshimiwa Waziri Mkuu amelisimamia sana. Mali za ushirika ziliibiwa mchana kweupe lakini chini ya uongozi wa Waziri Mkuu na Ikulu wakati huo na sasa hivi mali nyingi imerudi. Kweli tumekuwa na majizi humo lakini siyo wote ni majizi kwenye ushirika.

Mheshimiwa Spika, tulimualika Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika cha Kahama, nitamualika hapa siku moja ananunua pamba kwa bei nzuri kuliko mtu mwingine yeyote. Kahama sasa hivi pamba inatoka sehemu nyingine inakimbilia kule, analipa hela na baadaye analipa na nyongeza na wameajiri na Maafisa Ugani. Tusimame na ushirika na Waheshimiwa Wabunge naomba tusaidiane tujenge ushirika ndiyo nguvu ya mnyonge Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matatizo hayo ni pamoja na aliyosema Mheshimiwa Saashisha. Mheshimiwa timu ilishaenda kufanya uchunguzi, ripoti ilikuwa haijafika kwangu ilikuwa kwenye Tume nimeipata na nimepitia tusipuuze anachosema Mheshimiwa Saashisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Bashe nimemuomba ajipange aende Kilimanjaro kwenye ziara mojawapo atakwenda kulishughulikia hili. Mambo ambayo nimeyaona

siyasemi sasa hivi lakini hatutapuuza alichosema Mheshimiwa Saashisha watu wasije wakadhani kwamba unaropoka, umetusaidia sana kutueleza hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu stakabadhi ghalani, narudia tena Mheshimiwa Bashe amelieleza vizuri sana na nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote walioeleza changamoto na faida. Kwa hiyo, tutamuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye hili mamlaka ibaki Wizara ya Kilimo. Pamoja na kwamba kuna maduhuli kwenye mazao tusianzishe stakabadhi ghalani kwa lengo la kukusanya maduhuli ya Serikali hata kama tunahitaji maduhuli hayo. Hii ni kwa sababu tunamuadhibu yule anayepeleka kwenye ghala halafu tunaacha hao wengine. Vilevile kuna *geographical factors* na wingi wa mazao yanayozalishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi ndiyo tutakaotoa kibali kwamba zao hili liingie stakabadhi ghalani. Napenda kuwahakikishia tutafanya hivyo *consultatively,* tutakaa chini wote na Waheshimiwa Wabunge na wawakilishi wananchi mtashirikishwa pale ambapo tunaona inaweza ikafanya kazi tutapenda tuje tusishirikiane tufanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie mambo mawili harakaharaka; moja nashukuru Waheshimiwa Wabunge na napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wetu wote wa Siha, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Longido, Monduli, Simanjiro na Mwanga wakati tunapambana na nzige tulijifunza mambo mengi tukagundua kwamba kilimo anga ni kama vile hatukukiendeleza. Mheshimiwa Waziri Mkuu ulitoa maelekezo na sasa tumetoa, tulikuwa na shilingi milioni 150 za kilimo anga sasa hivi kwa bajeti ileile narudia bila kuongeza *ceiling* panga pangua tumeweka bilioni tatu na humo ndani mojawapo tutanunua ndege, hizi ndege za mashirika mengine ni zetu pamoja.

Mheshimiwa Spika, Shiriki la Ndege la Jangwani sisi ni wanachama na naamini ni nchi mbili tu Tanzania na nchi nyingine ndiyo zimelipia ada. Kwa hiyo, mlivyosikia tunapiga kelele ndege irudi ni ndege yetu kama ilivyo ya Kenya,

Ethiopia, Sudan na kadhalika lakini tunahitaji moja ya akiba hapa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunapambana na kwereakwerea na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao tulishirikiana, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, mwisho suala la mitaji limezungumzwa sana humu, Benki ya Maendeleo ya Kilimo imesemwa na kadhalika. Tutaomba tuwe na siku ifanyike semina, tutakuomba kwa sababu *modules* ya ile benki sizo ambazo kila mtu anavyoiamini. Halafu kama kuna mawazo tutaongea lakini ukweli ndiyo hivyo kuna namna inavyofanya kazi na kuna maeneo mengi sana imefanya kazi kubwa sana; nimeenda Minjingu nimekuta wamewekeza vizuri sana kwenye upanuzi wa viwanda. Tumeenda maeneo mengine wamekopesha wakulima wadogowadogo, kwa hiyo tutawale hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeunda kamati, *high level panel* na nimemchagua Mheshimiwa Bashe awe *chairman* nawashukuru sana wakuu wa mabenki wote pamoja na Mkuu wa *PAS* yupo pale kwenye *Speakers Gallery* pale, wamekubali watakaa kwenye hiyo kamati watafanya kazi kwa takribani miezi minne. Watapata fursa ya kuongea na kila mtu ili tuweze kupana namna ya ku-*fund* kilimo kwa namna ambayo sio ya gharama kama hii.

Mheshimiwa Spika, labda la mwisho ambalo nimelisahau nimalize kwenye ushirika tunapitia sheria upya na kabla hatujaja na sheria hapa tutahitaji kuwa-*consult* Wabunge wote. Tunataka twende kwa makini sana kwa sababu tunataka ushirika ukue, *AMCOS* zifanye vizuri, hatutaki zife lakini tunataka tujue ni nini vikwazo ambavyo tunavipata sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa muda huu, Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana...

**SPIKA:** Kabla hujamalizia kuna Wabunge walikulaumu kidogo kwamba kwenye hotuba yako hukugusa masuala ya *horticulture* kabisa na kwenye majibu hapa pia umesahau *horticulture* ama una neno moja mawili ya kusema. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nimeongea *strategic intervention* bila kutaja zao lolote. Tuliposema utafiti hatukusema kwenye zao gani ni mazao yote. Kwenye hotuba ya bajeti nadhani tunaweza tukaonesha hapa alivyosema Mheshimiwa Dkt. Kimei tulimpelekea kitabu na kumuonesha *reference* na sio kwa bahati mbaya tulimualika Dkt. Mkindi hapa kama mgeni wetu kwa sababu *horticulture* ni kati ya mazao ya mkakati na Mheshimiwa Waziri Mkuu ametu-*guide.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda nitoe na mfano, Arusha tutakuwa na kikao cha *investment forum into agriculture European* watakuja Arusha. Suala kubwa ambalo tunataka kuongea nao ni kurudisha ile *logistical arrangement* ambayo inasaidia sana kwenye ku-*export horticulture.* Kulikuwa na *call chain system* walikuja hapa kwa namna fulani wakashindwa wameenda Ethiopia wanafanya vizuri sana. Niliongea na Balozi nadhani wa Uholanzi alivyonieleza nikasema nataka tuwaite tena tukae nao tuone kama wanaweza wakarudi ili mkulima wa parachichi Njombe pale aweze kuli-*export* haraka sana na bila uharibifu. Kwa hiyo, kwa kweli hatuwezi kupuuza *horticulture.*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunakushukuru sana. Nafikiri makofi hayo hayatoshi Waheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wamejitahidi sana kusomesha somo hili gumu la kilimo lakini wamejitahidi sana, tunawapongezeni sana. *(Makofi)*

Sasa Katibu!

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 43 – WIZARA YA KILIMO**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Waheshimiwa Wabunge sasa tunaingia kwenye ma-*book* sasa, haya Katibu.

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management*...........Sh. 6,534,709,119

**MHE. FATMA H. TAUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa. Mimi nilikuwa nataka *commitment* ya Serikali kwamba zabibu ya Dodoma ni zabibu pekee duniani ambayo inavunwa mara mbili kwa mwaka.

Sasa nilitaka kupata *commitment* ya Serikali kuhusu kutenga maeneo maalum katika Wilaya zote saba za Mkoa wa Dodoma katika kuendeleza zao la zabibu. Sina nia ya kukamata shilingi lakini nilikuwa nataka *commitment* ya Serikali. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufafanua hoja ya Mheshimiwa Mbunge kwamba zabibu ni kati ya mazao muhimu sana ambayo tunayafanyia kazi na tuna taarifa namna ya kuyaendeleza. Mojawapo ni kuendeleza ushirika na jingine ni kutenga ardhi. Tutafanya kazi na wenzetu wa TAMISEMI na uongozi wa Mkoa kuhakikisha kwamba kweli tunatenga maeneo na tunayasaidia ili kuongeza kilimo cha zabibu.

**MHE. FATMA H. TAOFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Taufiq na tulishamuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba katika mazao yale ambayo amewapa kipaumbele cha kipeke yake ikimpendeza basi aongeze zabibu liwe ni mojawapo ya mazao ambayo atayachukua ayajumuishe na katani na michikichi basi na zabibu nayo iweze kuingia kwa sababu ina changamoto za aina yake kwa kweli, Mheshimiwa Judith Kapinga*. (Makofi)*

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Mimi ningependa kupata maelezo kwa Mheshimiwa Waziri kwamba mikoa ambayo imekuwa ikilima mahindi kwa kiasi kikubwa Ruvuma, Katavi, songwe, Rukwa na Njombe imekuwa ikikosa masoko ya mazao haya. Tunashukuru *commitment* ya Serikali kwamba iafungua masoko na imeipa Bodi ya Nafaka pesa lakini tatizo kubwa ni mkulima wa chini kufikia masoko hivyo kufanya walanguzi kuchukua mazao kwa wakilima na kwenda kuuzia bodi kwa bei elekezi na hivyo mkulima mpaka mwaka jana ameuziwa kilo moja ya mahindi kwa shilingi 320 na sio 1,000 kama aliyosema Naibu Waziri kwa sababu bei elekezi inauzwa na mlanguzi lakini sio ya mkulima kule chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata *commitment* ya Serikali na maelezo ni kwa njia gani mkulima wa chini atafikiwa ili ile bei elekezi ambayo inatakiwa basi iweze kumfikia mkulima wa kule chini lakini sio walanguzi ambao wanaweza kufikia masoko na hizi bodi ambazo Mheshimiwa Waziri amesema. Nikipata majibu yanayoeleweka basi sina nia ya kushika shilingi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Judith bado haujaeleweka, kwani wewe pendekezo lako lilikuwa nini? Namna gani ambayo mkulima wa chini atafikiwa ili Serikali iangalie kama inakubakiana na pendekezo lako au haikubaliani.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ilikuwa ni uanzishaji wa hivi vituo vya Bodi ya Nafaka viweze kuanzishwa kwenye maeneo ambayo wakulima

wapo kwa kiasi kikubwa, kwa sasa hivi vituo vipo mjini. Mfano, pale Songea Mjini mkulima ili aweze kufikia kituo inabidi aende Zaidi ya kilometa 100 au 60 ili aweze kufikia kituo cha kuuza mazao yake lakini kwa mfano Mbinga ambapo wanazalisha mazao kwa kiasi kikubwa hakuna hivi vituo kabisa. Kwa hiyo, nilikuwa napenda kupata *commitment* kwa Serikali hivi vituo ambavyo anavizungumzia Mheshimiwa Waziri vitaenda kuanzishwa kwenye maeneo ambayo wakulima wapo...

**MWENYEKITI:** Yaani una maana angalau kila Tarafa kituo kimoja au unapendekeza, kitu cha namna hiyo si ndio.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio...

**MWENYEKITI:** Maana huwezi kuanzisha kwenye kila Kijiji.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Sio kila Kijiji...

**MWENYEKITI:** *NFRA* haiwezi kwenda yaani *extensive* kiasi hicho, sasa nimekuelewa. Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, natolea maelezo hoja ya Mheshimiwa Kapinga kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hasa Bodi yetu ya Nafaka na Mazao mchnganyiko haina mtandao wa kutosha kwenda ndani sana. Walau *NFRA* wapo vizuri pamoja na kuwa bado kuna changamoto ya kufika mbali. Tumekubaliana kwamba Bodi ya Mazao Mchanganyiko itakapokuwa inanunua tujaribu kutumia vilevile mtandao wa *NFRA* ili kuhakikisha kwamba walau tunafika mbali zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba wakati Serikali kama hivyo inaenda kununua inachangamsha soko na watu wataanza kujua kwamba mahindi yananunuliwa na bei itaanza

kupanda. Na tunakusudia sasa hivi kuanza kutoa matangazo ya bei ambayo tunaona ipo ili hata mkulima popote alipo aweze kujua bei inaendaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitoweza sasa hivi ku-*commit* mpaka tufanye walau tujue itatugharimu kiasi gani na tuna uwezo wa kufanya kiasi gani kwamba tunaweza tukafungua kituo Tarafa hadi Tarafa. Lakini tutawaelekeza wajitahidi kadiri inavyowezekana kama wanaweza wawe na *mobile center* za kununua ili waweze kuzikusanya kwa pamoja, nashukuru sana.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, kwa kuwa kwa muda mrefu hoja ya bei ya mkulima ndiyo imekuwa kama kaburi la wakulima na kwa kuwa mkombozi wa hoja hii ni pato la mkulima. Sasa ningependa kupata *commitment* ya Serikali inatuhakikishiaje itaanzisha mchakato wa kutuondoa kwenye kumtathmini mkulima kwa bei badala ya mapato jambo ambalo ndilo litawezesha kuimarisha tija ya kilimo chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu kwa miaka mitano iliyopita, Wizara ya Kilimo imeondoa Zaidi ya tozo 100 lakini bado bei kule ya mkulima imebaki ileile na pato la mkulima limekuwa haliongezeki na hii inachangiwa kwa kiasi kikubwa na tija yetu ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa kupata *commitment* ya Serikali inapanga vipi kutuondoa kutoka kwenye dhana ya kuangalia na kupigania bei ya mkulima na kuanza kupigania pato la mkulima ambalo litapelekea kuongeza tija yetu ya kilimo lakini pia litatuwezesha kuwa na ubora na viwango ambavyo tutaweza kushindana kwenye masoko ya kikanda na ya kimataifa, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Hii *concept* yako huwa ngumu kui-*capture* vizuri lakini unamuuliza maswali Profesa kwa hiyo ufafanuzi wa hilo.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa fursa hii, naomba nitolee maelezo kidogo hoja aliyoitoa Mheshimiwa Neema Lugangira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anachosema, ninachoamini ni kama tulichokuwa tunajaribu kukifafanua hapa kwamba lengo letu ni kumuongezea mkulima kipato kwa sababu si kwamba wakati wote bei ikipanda kipato kinaongezeka. Kwa mfano, kukiwa na ukame mkubwa sana bei ya mazao inaweza ikaongezeka lakini kwa sababu ni machache sana kipato cha mkulima kikaanguka. Na kukiwa na *bumper harvest* unaweza ukakuta bei inashuka sana na kipato cha mkulima bado kinashuka japokuwa amevuna kwa sehemu kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia tija lengo letu kwa kweli ni ku-*focus* kwenye kipato cha mkulima. Tunachotaka ni kwamba mkulima aweze kuzalisha kwa wingi kwa gharama ndogo au kwa eneo lile lile analozalisha ili atakapouza hata kama bei imeshuka ule wingi wa mazao *itself* u-*offset* lile anguko la bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kama nilivyosema hapa kwa hakika sipendi kulirudia hili lakini lengo letu kwa mazao tunayotumia ndani ni kwamba bei iweze kushuka lakini pato la mkulima liongezeke. Maana yake ni kwamba *productivity yield* iongezeke sana hata bei inaposhuka lakini mkulima anazidi kufurahi kwa sababu anazidi kupata zaidi. Na mikakati tuliyosema ni kama hiyo lakini cha kwanza kabisa ni utafiti; kuwa ne mbegu bora na *better agronomy,* ulimaji ambao ni mzuri zaidi.

**MWENYEKITI:** Ahsante naendelea, Mheshimiwa Nusrat Hanje.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kweli nitakuwa sijafaanya jambo jema kama sitawapongeza wamejitahidi sana ku-*incorporate* angalau maoni ya Wabunge wengi walivyochangia, wamejitahidi sana mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida ni kwamba hakuna *umbilical cord* kwenye nchi, unaweza kupata viongozi, Mawaziri *smart open minded* kama hawa halafu wanakuja wengine *with different ideas* na mind tofauti kabisa kama nchi mbili tofauti. Kwa hiyo, naona ni busara sana ku-*acknowledge* kwamba wamejitahidi pakubwa *almost* vitu vingi ambavyo ndiyo *thinking* ya watu wa leo wameyaweka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nafikiri mnapaswa kupiga makofi jamani; unapopata *opinion* kama hiyo kutoka kwa walio wachache nafikiri ni kitu cha kupongeza, ahsante Nusrat malizia. *(Makofi)*

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najaribu kuwa *honest* na Mungu wangu pia...

**MWENYEKITI:** Kweli kabisa

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** kwa sababu vitu vinaonekana kabisa vingine *sometimes.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu sana ipo kwenye ugani *(extension officers)* wakati nachangia asubuhi nilizungumza kwa kushauri namna ambavyo Wizara inaweza ku-*militarize.* Niliona nitumie *terminology* ya ku-*militarize* lakini lengo langu lilikuwa ni kuwafanya maafisa ugani wawe askari wa miguu yaani wawe wanajeshi, polisi wenu ndiyo jicho lenu kwenye *ground.* Sasa tuna maafisa ugani 6,704 *of course demand* ni 20,000 na sitaenda huko kwa sababu ndiyo hawa tunao kwenye *finger tips* zetu na wanakula mshahara wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ripoti ya *CAG* ilikuwa inaonesha asilimia moja tu ya wakulima ndiyo wamepewa mafunzo ya mbinu bora kutoka kwa hawa 6,700. Sasa nataka kusikia Serikali pamoja na kwamba nishukuru pia Mkoa wangu wa Singida upo miongoni mwa mikoa mbayo ni *pilot* kwa ajili ya utafiti kuangalia ni namna gani wanaweza pamoja na kwamba wamejikita kwenye mazao ya mafuta peke yake kwa ajili yaku-*solve.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitaji kufahamu Serikali pia wakati mnaendelea na mazao ya mafuta kwa mikoa mingine ambapo pia kuna maafisa ugani ni namna gani ambavyo mnaweza mkawafanya waishi fikra zenu kwa kuwafuatilia, kuwachunga na kufanya kila kitu kuhakikisha kwamba mwaka mzima ni mmoja tutarudi hapa wale wengine wanafanya nini kule walikobakia*, commitment* ya Wizara nahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Nusrat. *Point* hii ni muhimu sana Mheshimiwa Waziri, bahati nzuri ulikuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili ume-*militarize TANAPA,* Ngorongoro wale nyoronyoro wote sasa hivi hakuna watu wamekaa kisawasawa ndio maana umeona ujangiri hakuna, kazi hii umeifanya.

Huwezi ukawa na wale watu wazima kidogo mnajua mabwana shamba wale walikuwaje? Walikuwa kwanza wana *uniform (combat* na buti) wakipita mashambani kila mtu anajua bwana shamba amepita hapa. Sasa hawa wamekaa kiraia raia nyoronyoro tu, wapo wapo kwanza huwezi kumjua bwana shamba ni yupi na... *(Makofi)*

Sasa kuna mpango gani angalau hata wangekuwa wanapita sijui *JKT* au wapi wakapiga kwata sawasawa kidogo bwana shamba akawa bwana shamba, anaweza kutemebelea wakulima kadhaa kwa muda mfupi; ndicho anachokisema Mheshimiwa Nusrat yaani kuwa-*militarize* hawa watu kuwachangamsha wafanane na *extension officer. (Kicheko)*

Ufafanuzi Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, k wa kweli nakushukuru sana Mheshimiwa Nusrat Hanje kwa maneno yako ya kutia moyo. Na ni kweli kwa hali ya huduma ya ugani kwa namna fulani wengine wamechoka, huo ni

ukweli wenyewe lakini wamechoka kwa vile na sisi tulikuwa hatuna mfumo wa kutathmini na kufuatilia na hatukuwapa vitendea kazi vya kufanya kazi. Kwa hatua ya kwanza kabisa ni kuwapa vitendea kazi na kujenga mfumo wa kuwafuatilia halafu *next* pengine tutaenda hatua ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakachofanya kama nilivyoeleza tunanunua pikipiki 1,500; hizi pikipiki hazitakuwa kwenye hii mikoa mitatu tu lakini hakuna bwana shamba wa mkoa huu ambaye hatapewa pikipiki na kuwa-*trained* kuhakikisha kwamba anaweza kuiendesha anapata mafuta na kadhalika. Pikipiki nyingine zitaenda kwenye mikoa mingine. Kuna baadhi ya fedha ambazo tumeongea na ofisi ya Mheshimiwa Mhagama tutaenda kwenye mikoa mingine ya kuongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza vilevile na bodi zetu za mazao kwa mfano Bodi ya Pamba na yenyewe ijaribu kufanya kitu hikihiki ambacho tunakifanya ili kutawanya huduma hii maeneo mengi zaidi, Bodi ya Chai na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie kwamba hata hawa katika mikoa hii mitatu hawatabaki kwenye mafuta tu kwa sababu haitasaidia. Kuna mkulima ambaye ataamua yeye anataka kulima mtama tu au mwingine anataka kwa mfano Simiyu wanalima pamba kwa hiyo mafunzo rejea yataenda kwenye mazao yote yanayolimwa katika mikoa hiyo; msisitizo utakuwa kwenye mazao ambayo yanazalisha mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hatua ya sasa hivi tunajua wanafanya nini. Kama nilivyosema tunawanunulia simu lakini hizi simu ni mtego kwa sababu kila siku *DED, DAICO*, watu wote wanaweza wakamfuatilia anafanya nini? Tumejadili sana ndani ya Wizara tukasema tuwawezeshe kama anashamba na yeye alime na hii haita-*replace* mashamba ya darasa. Wanasema bwana shamba akilima vizuri watu watasema kwa sababu kasomea, mashamba darasa mengine yatakuwepo, lakini yeye tutamuwezesha

alime wakati wa kumtembelea bwana shamba cha kwanza tutamwambia tuonyeshe wewe unalimaje, *of course* tutaangalia na mashamba darasa. Kwa hiyo, kwa kuanzia ni hivyo lakini nadhani hatua zaidi zitaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoamini sasa hivi ni kwamba endapo tutafanikiwa katika jaribio hili la mikoa mitatu na tunamuomba Mungu tufanikiwe, itakuwa rahisi sana kuomba Hazina fedha zaidi. Tumeongea na Wizara ya Fedha niwahakikishie, Waheshimiwa Wabunge wametusemea sana lakini na Wizara ya Fedha imetusemea kwamba watajitahidi kutoa fedha na tutajitahidi tuzipate *upfront.* Kwa hiyo, *procurement ya* hizi pikipiki ianze mapema ili tukianza tarehe 1 Julai, tusije tukachelewa sana na kuanza kazi mara moja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Majala.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Nishukuru na niwapongeze Waziri pamoja na Naibu wake kwanza kwa kuweza kutuondolea stakabadhi ghalani Mkoa wa Dodoma, hakika sana ninyi ni watu wasikivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili nishukuru kwa Wizara kuona Mkoa wa Dodoma unastahili kuwa kituo cha mfano cha mazao ya kwenda kuzalisha mafuta ili kuondokana na upungufu wa mafuta nchini. Tumhakikishie tutawapa ushirikiano wa kutosha ili ndoto yao iweze kutimia kwa maslahi mapana ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu hapa nahitaji *commitment* ya Serikali, pamoja na mipango mizuri mlioyoipanga Wizara na Mheshimiwa Waziri ametuambia kwamba pamoja na bajeti hii kutokupanda atajitahidi kuhakikisha kwamba hiihii kidogo itakwenda kutimiza wajibu na majukumu ambayo wameyapanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kama Serikali isipokuja na majibu ya kuniridhisha nitakwenda kushika shilingi, hofu

yangu ni mtiririko wa utoaji wa fedha kwenda kwenye Wizara ya Kilimo. Ukiangalia mtiririko wa fedha kwa miaka mitano mfululizo 2016/2017 Wizara ya Kilimo ilipewa asilimia 2.2 ya fedha za maendeleo; 2017/2018 asilimia 11, 2018/2019 asilimia 42, 2019/2020 asilimia 15, 2020/2021 asilimia 26, hata nusu tu haijafikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii mipango yote mizuri tunakwenda kuitekeleza kwa namna gani kama Serikali bado haiko tayari kutoa fedha ya kutosha ili kwenda kukidhi mahitaji ya Wizara na sekta hii muhimu ambayo inaajiri zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Tayari muda wako.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nisipopata majibu ya kuridhisha nitashika shilingi ya mshahara wa Waziri.

**MWENYEKITI:** Hili silo la Waziri kwa kweli, hili ni la Waziri wa Fedha. Mheshimiwa Waziri wa Fedha hoja imejitokeza sana ndani ya mjadala huu, karibu sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo pamoja na Naibu wake, ni kweli wamekuja na mapendekezo ya hotuba ya Wizara yao ambayo yanatia matumaini kwa sekta hii. Tumepanga tuwe na kikao kingine pamoja na kwamba wanamaliza bajeti yao leo ili tuweze kuboresha mpaka kwenye Sheria yetu ya Fedha ambayo tutaileta kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa umuhimu huo wa mambo tuliyoyawekea kipaumbele tunaamini kwamba tutazingatia na kwenye utoaji wa fedha ili haya yaliyopangwa yaweze kutekelezwa. Kwetu sisi Wizara ya

Fedha, Wizara ya Kilimo ni kipimo kizuri sana cha kuendelea kwa nchi yetu kuwa katika nchi ya kipato cha kati na kwenda kiwango cha juu. Kwa hiyo, tutatekeleza hii mipango waliyoiweka kwa kuitolea fedha na tumepanga namna ambavyo tutalitekeleza hili waweze kutimiza haya malengo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimuombe Mheshimiwa Mbunge aridhie tu kurudisha shilingi hiyo na tunaweka *commitment* hiyo kwamba tutatoa fedha kwa wakati ili waweze kutekeleza malengo hayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Kunti kubali wanajikaanga sana kwa bajeti yao ileile ya mwaka jana. Kwa hiyo, hata kama siyo mwaka huu lakini matarajio ya Bunge hili ni kwamba mwakani kutakuwa na mapinduzi makubwa sana katika kiwango cha fedha kinachopewa Wizara hii. Kwa sababu mmesikia mapendekezo ambayo hata Mheshimiwa Bashiru aliyatoa kama ambavyo *achievement* yetu kwenye madini Bunge lililopita lilikuwa ni kubwa, tunafikiria kuhamia kwenye kilimo. Sasa *as* tunahamia kwenye kilimo kama Bunge maana yake tunakuandaa na wewe Wizara ya Fedha ujiandae kutoa fedha za kutosha kwenye kilimo. Hata kama safari hii tunapita hivi tulivyo lakini mwakani tukikutana hapa hilo muondoke nalo Wizara ya Fedha, tunataka fedha kwenye kilimo, hiyo ndiyo *point* tunataka ku-*register*. *(Makofi)*

Upande wa Wabunge akina mama nimekwishamaliza wote, sasa twende kwa wakinababa. Nianze na Mheshimiwa Tabasam ulikuwa na neno fupi sana kwa dakika moja.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nilikuwa nauliza kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, wakati sisi tunakua tulikuwa tunaona wale mabwana shamba wanavaa *stocking*, nguo za kaki wako *smart* wanaingia katika mashamba wanakuonyesha kamba kwa hekari na kwa rula. Sasa hivi hawa mabwana shamba wa *certificate* kwa nini mliwafuta, maana hawa wenye

*degree* wanaogopa umande hawawezi kuja kwa wakulima, huu mpango ukoje tutakamata shilingi yako. Mimi nipo hapa nakusubiri, tunaomba *commitment* ya Serikali kuhusiana na suala hili, hawa watu wa *certificate* mmewaweka wapi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hoja yake ni kwamba kwa kweli bwana shamba ambaye mkulima anamuhitaji ni wa *certificate,* ndiyo mazoea yetu sisi. Unajua sasa hivi tumekariri *degree* kila mahali na hili siyo tu bwana shamba hata mwalimu tunayemhitaji kufundisha kule darasa la kwanza na la pili ni wa *certificate*. Sasa hii kupeleka *degree* mpaka chekechea na wapi nayo inatuchanganya kidogo, maana huyu mwenye *degree* ni Afisa Kilimo siyo bwana shamba au bibi shamba. *(Makofi)*

Hicho ndicho Mheshimiwa anajaribu kusema nah ii ina-*apply* kwenye mifugo na sekta zote kutokana na sera ya Serikali kiutumishi. Haya ma-*degree* ambayo tunayashusha kwa mwananchi wa kawaida inakuwaje? Ni suala la mazoea sijui *comment* yako Profesa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Mheshimiwa Tabasam anachosema ni sahihi lakini kwa sasa hivi tunaomba tu asishike shilingi atabasamu tuendelee mbele kwa sababu ni hatua ya kwanza kuna masuala mengine mpaka tumalize mchakato tuweze kuyasema. Kuna masuala ya kiutumishi, tumezungumza idadi ya maafisa ugani hatuwezi kuweka *commitment* sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa hali ilivyo sasa hivi tunahitaji hatua za haraka na hatua za haraka kama nilivyosema ni *mobility* kwa sababu unakuta bwana shamba anahudumia sehemu kubwa lakini hawezi kutoka sehemu moja hadi nyingine. Sasa hayo mengine yote pamoja na mavazi na kila kitu ni mambo lazima tutayazingatia mbele ya safari. Nafikiri kwa sasa hivi namuomba tu Mheshimiwa Tabasam atukubalie tuanzie hapo halafu tuone tunavyokwenda mbele. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Tabasam pia nakuomba ukubali kwa sababu ni jambo la Serikali kulitazama kwa upana wake.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vyuo, mfano kama Ukiriguru na kadhalika, hivi vyuo vilikuwa vinatoa watu wa *certificate*.

**MWENYEKITI:** Umeshaeleweka Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maana unamleta mtu anaogopa umande kwa sababu ya *degree* yake tuleteeni hawa tufanye mapinduzi.

**MWENYEKITI:** Umeshaeleweka na ndiyo maana nakuwekea vizuri wewe kaa tu.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Haya basi hiyo naiacha lakini nafikiri *messege* imefika.

**MWENYEKITI:** Kaa tu Mheshimiwa tumeshaelewana.

Waheshimiwa Wabunge, hili jambo nafikiri ni *across* katika mtazamo wetu Kiserikali ambapo Serikali inapaswa kuangalia sera za kiutumishi. Kila baada ya dakika tunaajiri watu ambao ni wasomi zaidi, nitoe sijui mfano gani, askari kwa mfano umetoka kule kwenye hifadhi, askari ninayemjua mimi wa darasa la saba ni wenye nidhamu, wanafanya doria, hawana wasiwasi na wanatii maelekezo. *(Makofi)*

Hawa wasomi wenu sijui *form* six, sijui *form* ngapi anaingia kama askari baada ya muda anataka kwenda kusoma diploma, baada ya muda *degree,* sasa mtakuwa na maofisa watupu watamtuma nani. Ile kazi kwenye *ground* atafanya nani? Matatizo hata yale yaliyotokea ambayo bado tunaendelea kuyafuatilia wanaodai nani ameuwawa wapi na wapi, askari yule wa darasa la saba alikuwa akifanya doria akiona vichaka havielewi ana-*crawl* kwa magoti na tumbo anachunguza ni kitu gani kile. Hawa wasomi wanapita na *Land Cruiser Defender* wakiona kichaka kimetikisika kule

wanapiga *SMG.* Hana muda akanyage umande ule aangalie ni binadamu au lah. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ziko kazi za darasa la saba yaani ziko kabisa na ziko nyingi lakini kila mahali tunabandika watu ambao wana ndoto za kuwa maofisa. Sasa hawa darasa la saba jamani nao wana kazi zao au hawa wa *certificate* ndiyo wanatakiwa wakutane na mkulima wanaelewana hata lugha. Sasa huyu msomi akienda na ma-*theories* yake kwanza anamchangaya tu mkulima. Anaanza kusema *you know*, *because,* sasa hii siyo kwenye kilimo peke yake pia kwenye mifugo ni kada zote. Katika hizi kada hata wakati wa ajira tuwachukuwe watu kwa nafasi zao bado zinahitajika, *technician* nao wana nafasi yao mahali pao siyo *degree* zinachukua nafasi ya *technician* halafu tukafikiri nchi itaenda mbele. Ni *argument* ya Serikali kuitazama kwa ujumla wake.

Tunakushukuru Mheshimiwa Tabasam. Sasa ni Mheshimiwa Nape.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nimuunge mkono dada yangu Mheshimiwa Hanje kusema kwamba wamejitahidi sana. Niwapongeze kwa kazi nzuri walioifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo dogo lakini ni kubwa kwetu wakulima wa korosho na niseme toka mwanzo kwamba nakusudia kukamata shilingi. Suala la pembejeo Serikali imeweka mpango mzuri wa kupeleka pembejeo na baadhi ya pembejeo ziko *site* tayari. Shida tuliyokutana nayo ni kwamba mfumo wa kuwakata wakulima fedha hizi kwenye mauzo yao umewafanya wakulima wagome kuchukua pembejeo na nina hakika Serikali mnazo taarifa hizi. Jimboni kwangu peke yake maeneo mengi kabisa wananchi wameacha kuchukua, wanasema hatuwezi kuchukua kwa sababu huu mfumo uliowekwa unawaumiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natamani kupata *commitment* ya Serikali, kweli mmesema mtaliangalia upya suala la *export levy*, lakini kwa mazingira ya leo sasa ambapo

tayari muda wa kupuliza umeanza kutupita, watu wanatakiwa kupuliza mashamba yao lakini kwa sababu pembejeo imefika na hawawezi kuichukua, natamani kupata sasa kauli ya Serikali ili iwafanye wakulima waichukue pembejeo wapulize kwa sababu kwa kweli muda umekwisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tunza Malapo ndiyo hilihili ndiyo ulikuwa unasema asubuhi kwamba hamtaki, nakupa nafasi useme hapo hapo uunganishe. *(Makofi)*

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo, ni kwamba sisi wakulima wa korosho tunatamani Serikali igharamie pembejeo kwa sababu kuna ile pesa ya *export levy* ambayo tunaamini kabisa sisi tuna haki yetu pale. Tunaona tukiendelea kumkata mkulima tena pesa ni kama tunamuongezea gharama za uzalishaji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ufafanuzi wa jambo hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwashukuru Waheshimiwa Wabunge na niwashukuru kwa dhati kabisa Waheshimiwa Wabunge wanaotoka Ukanda wa Korosho.

Napenda kuwaambia wakulima wa korosho kwamba Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa ya Pwani, Lindi, Mtwara, Ruvuma, wanapigana na kulinda maslahi yao na sisi Wizara ya Kilimo tunashirikiana nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba wakulima wachukue pembejeo, mawazo yote ya Wabunge na mwelekeo wa kutokuwapa mzigo tumeyapokea. Wakulima waende shambani wachukue pembejeo, tumewasikia, tumewaelewa, tutatafuta njia sahihi ambayo itakuwa ni *win-win* wakati huo kuwalinda waliotusaidia ku-*finance* na wakati huohuo kutokuwapa mzigo wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe ndugu yangu Mheshimiwa Nape tumekuwa na *engagement* ya muda mrefu na yeye na wenzie chini ya Mwenyekiti wao, Mheshimiwa Chikota niseme kwamba tumewaelewa, tumewasikia na tutafanyia kazi yale ambayo tumejadiliana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nape na Kiti nacho kinakuomba ukubali maelezo haya.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikiri kwamba kwa hizi siku mbili, tatu umeliendesha Bunge vizuri sana na naomba uendelee hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kauli yako napata tabu kuendelea na hii hoja lakini najua Wabunge wa Mikoa hii sijui kama tutakuwa tunawatendea haki. Ukiweza na nikuombe sana mimi mdogo wako, hebu tulijadili hili jambo kidogo na hapa nakusihi sana kuna kitu kilifanyika, tulikutana Wabunge tukajadiliana bahati mbaya sana nadhani watu wa Bodi wakapeleka barua kwenye *AMCOS* wakieleza kwamba Wabunge tumekubaliana hii fedha ikatwe kwa wakulima, hili jambo limekuwa mwiba kwetu sisi Wabunge. Hili jambo lililetwa kama majadiliano, tukaanza kujadiliana kabla hatujafika mwisho mwenzetu wa Bodi kakimbia wamepeleka maelekezo kule kwamba Wabunge tumekubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili jambo litawaumiza sana Wabunge wa Kusini, nilikuwa natamani sana Serikali zaidi ya hapo kwanza barua ile ifutwe kwa sababu hayakuwa makubaliano. Kwa hiyo, wasitumie mgongo wa Wabunge kwenda kuwakata wakulima, haikuwa makubaliano. La pili ni hiyo kwamba *timeframe* ya kuimaliza jambo hili itolewe ili wakulima waendele na *process* ya kuchukua pembejeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama ikikupendeza, vinginevyo utoe maelekezo, lakini ikikupendeza naomba sana Wabunge wa Mikoa hii angalau wawili au

watatu tuweke maelezo kwenye hili jambo ili na sisi utuweke mahali salama. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Natamani kufanya hivyo lakini kwa sababu ya muda pia ukiuangalia na nina orodha ya watu kidogo hapa inanipa shida. Kwa sababu barua kama hiyo inayosema Wabunge wamekubaliana wanamaanisha na Mheshimiwa Waziri Mkuu ni katika Wabunge waliokubaliana. *(Makofi/Kicheko)*

Ndiyo maana nikasema hili jambo walivyosema mimi nimewasoma, nimewaelewa hebu tuwaamini tuwaachie, kwa sababu lina mpaka na bosi wetu Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, mimi naamini litakaa vizuri tu. Waheshimiwa naomba mlichukulie kwa uzito wake ule bila haja ya kuongeza Wabunge wengine kusema.

Tunaendelea na Mheshimiwa Philipo Mulugo.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kusema kwamba nisipopata majibu vizuri natazamia kushika shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru kwa namna ambavyo Serikali imetoa majibu ya suala la stakabadhi ghalani jioni ya leo, lakini nina jambo moja dogo tu Serilikali iweze kusaidia. Kwa uzoefu wa kukaa Bungeni humu Awamu Tatu, ninao uzoefu kwamba Serikali ikishaahidi hapa katika mfumo huu wa kushika shilingi na nakadhalika, huwa huko mbele jambo hilo halitekelezeki wasipotoa barua au waraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la stakabadhi ghalani kwa baadhi ya mazao tuliyoyasema ya ufuta na mengine madogo madogo kwa sababu wanasema kwamba wamefuta Mikoa ya Dodoma, Songwe na hiyo mikoa walioitaja mpaka hapo miundombinu mizuri itakapofanyika, naomba kesho ikiwezekana kwa sababu kule Songwe ufuta ndiyo kipindi hiki kuanzia tarehe 1 Aprili tupate barua ya *commitment* kwa watendaji wa Serikali ngazi za mikoa na

halmashauri kwa sababu wanasema kule ni siasa tu, yaani wanadharau sana Bunge lako kama hujui. Tunaoishi na wale wataalam ni dharau tupu wanasema yanayoongelewa Bungeni ni siasa tu, hatuna waraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka hata wakati ule wa masuala ya *fire* kwenye mashule ilikuwa hivyo hivyo mwaka mzima tumehangaika kwa sababu Mheshimiwa Jafo hakutoa waraka. Naomba kesho tupate barua na Wabunge tupate nakala kwenye maeneo ambayo stakabadhi ghalani inasubiri miundombinu rafiki. Naomba sana suala hili litekelezwe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wanaoafiki kuhusu hoja hiyo? *(Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Nafikiri hili ni la utekekelezaji halina haja ya kuchuwa muda la utekelezaji kwa sababu usumbufu huu ambao huu umeongelewa kwa siku mbili mfulululizo ni mkubwa sana kila mahali, hata hii Dodoma sasa hivi ndio wanavuna ufuta. *(Makofi)*

Kwa hiyo ni jambo la kuchukuwa hatua mara moja hiki ndicho ulichoaidi Bunge ndio umeahidi nchi kwa hiyo tunaomba iwe mara moja maana bado tuko hapa, vinginevyo Mheshimiwa Waziri wa Fedha sijui utapitia dirisha gani kwenye bajeti yako. Kwa hiyo, na wewe sio Waziri wa Kilimo tu na wewe nilakufuatilia vilevile ili mambo yako yakae sawasawa vinginevyo siku hiyo itakuwa shughuli badala ya bajeti itakuwa ni shughuli ya stakabadhi ghalani ambayo usalama hautakuwepo. Mheheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangala.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA**: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa fursa hii napenda kupata maelezo kwenye eneo lifuatalo na kama nisiporidhika nitatoa hoja kuondoa shilingi kwenye mshahara wa Waziri. Kwa kuwa kwenye miaka ya 90 Taifa letu liliingia kwenye Azimio la

Zanzibar ambalo kimsingi liliondoa mfumo wa *planned economy* na kuleta mfumo wa soko huria, lakini baada ya mfumo ule kuingia kumekuwa kuna utaratibu ambapo Serikali imekuwa hai.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa huku mzee hapa.

**MWENYEKITI:** Hiko upande gani hiyo taarifa.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Hapa!

**MWENYEKITI:** Hivi umehamia huko siku hizi!

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Hapana nimekuja tu kuweka elimu vizuri.

**SPIKA:** Ahsante sana haya taarifa hiyo.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Kigwangala anayezungumza saa hizi kwamba ndani ya nchi hii hakuna kitu kinachoitwa Azimio la Zanzibar kuna mkutano na makubaliano yaliyofanyika Zanzibar lakini hakuna Azimio la Zanzibar ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kigwangala unaipokea hiyo taarifa.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti siipokei ni mjadala mrefu kidogo wakisomi akipenda baadaye tunaweza tukajadili naomba niendelee na hoja yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo makubaliano ya Zanzibar ambayo yalileta mfumo wa soko huria na kuondoa mfumo wa kupanga kwa maana *planned economy* ambao ndio ulikuwa msingi uliowekwa kwenye azimio la Arusha yalipelekea kubadilisha mifumo ya namna ambavyo shughuli za kiuchumi zilikuwa zikiendeshwa katika Taifa letu. Mojawapo

ya shughuli muhimu ambayo inafanywa na watanzania ni kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye kilimo sasa kwenye kilimo kumekuwa kuna utaratibu ambapo Serikali mwisho huku ambapo haikumsaidia mkulima pembejeo, haikumsaidia kumpa huduma za ugani, hata kuja kumsaidia kupata soko la uhakika kwa maana ya kuwa na mfumo wa viwanda haijafanya chochote cha kutisha kwenye eneo hilo, mwisho huku Serikali inaingia inaleta utaratibu wa soko kwa maana ya ku-*control* ambapo mkulima anaweza akauza mambo kama leo usiuze mazao nje ya nchi kesho uuze kwa hivyo kumekuwa sintofahamu ambayo inatengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa mfumo wetu sasa wa kiuchumi hususani kwenye mazao ya kilimo, ya chakula na biashara umekuwa na mkanganyiko mkubwa ambapo kuna wakati tunatumia *planned economy* kuna wakati tunatumia *free market economy,* umekuwa unaleta utaratibu ambao mwisho wa siku unamwangusha mkulima unawaangusha wafanyabiashara na pengine mazao mengine yamekuwa yakianguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwanini Serikali ambapo imeamua kuingia katika mfumo huu wa *free market economy* lakini ambao huna *elements* za *planned economy* isianzishe mifumo ya kulinda bei ambazo mkulima mwisho wa siku atapata kama ambavyo nchi zenye mfumo wa *free market economy* kama Marekani, kama India zimeanzisha mfumo wa *price stabilization* ni kwa nini na sisi tusiwe na mfuko ambao utatoa uhakika kwamba bei ya mkulima chochote kitakachotokea mwisho wa siku itabaki kuwa nzuri na mkulima atapata ujira wake.

**MWENYEKITI:** Umeeleweka Mheshimiwa na kwanza naongeza nusu saa hili tuweze kwenda vizuri hapa lakini bahati nzuri swali hilo linaulizwa kwa wote wawili wana kitu kimoja *in common* wachumi hao kwa hiyo, swali la kichumi hili *professor*.

**WAZIRI WA KILIMO**: Mheshimiwa Mwenyekiti naomba nitolee hoja ya Mhehimiwa Dkt. Kigwangalla kuhusu kwanza kuna suala la kihitikadi katiba yetu ukisoma ilani ya chama sijua kama itikadi hasa imebadilika, nani suala la namna ya kuendesha uchumi na tafsiri yake sio rahisi sana. Mfano ni kweli tunataka wakulima na biashara ziwe huru lakini ni uhuru upi tunaozungumzia ni kweli vilevile tunataka Serikali itafute masoko, kwa hiyo, tunataka Serikali iwe na jukumu kwa hiyo ni suala la ku-*define* mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani tukasema Serikali ipange bei na kusema tuendeshe uchumi huria, na hivi ni vitu viwili tofauti kwa kweli tunachofanya kwa nchi yetu ni aina fulani ya *missed economy* Serikali ina nafasi yake na hasa kwenye kilimo, ikijitoa wakulima wataumia na baadhi ya hatua ambayo Serikali wanazichukuwa zinaweza kuoneka zinaingili lakini zina linda na mimi nime-*study* wakati Mheshimiwa Bashe anajaribu kuelezea na ile ya pamba inavyopanda na kushuka inapanda na kushuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kinachotokea ni nini kuna wakati Serikali imejitoa jumla imeshuka wakati mwingine imefanya vizuri imepanda wakati mwingine Serikali imeingilia imefanya vibaya inashuka. Kwa hiyo suala kubwa hapa ni Serikali ina *play role* gani, sasa hivi Serikali inajenga mazingira wezeshi, hilo la kwanza. Ili watu wafanye shughuli zao, pale ambapo tunahisi huyu mkulima tusipomwekea utaratibu wakumlinda na lazima iwe kwa maslahi yake Serikali inaingia kumsaidia mkulima lakini tutajitahidi kuingilia huku kusiwe ni kero na mojawapo ni suala la ushirika nadhani kama Mheshimiwa Saashisha alivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirika ni aina fulani ya umoja watu wengine wanasema ujamaa kwa sababu nchi za *western* Denmark na nini ushirika ni kitu kikubwa sana. Lakini ushirika lazima uwe ni hiari ila kwa kiasi fulani Serikali lazima iweke misingi kwa sababu mali ya ushirika ni mali ya umma sio ya Serikali, Serikali lazima iende ikaangalie ile mali kwamba inatunzwa. Vilevile hapa tumezungumza kwenye bei bodi ya

nafaka na mazao mchanganyiko tumeiambia itumie hizi hela kwenda kununua mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchumi huria kabisa hiyo ni *anathema* watu ambao wanaangalia *free market* watakuambia Serikali inaenda kufanya nini kule ijitoe kwa hapa tunakwenda kama-*mixed* kujaribu kufanya vitu ambavyo vitalea uchumi na vitamlinda yule ambaye kweli asipolindwa na *system* anaweza asisimame vizuri ni *balance* ambayo ni ngumu sana sio lazima kuilezea hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini narudia tena nikisikia Waheshimiwa Wabunge wanazungumza na shilingi yangu mshahara wangu karibu uondoke kwamba mazao, kwenye *free economy* unamwambia Serikali mazao, masoko yake yako wapi hapana ni jukumu la Serikali kusaidia masoko, ni jukumu letu kwenda *DRC, South Sudani* hata kama kwa sehemu kubwa tunatumia *free market economy* kwa hiyo *line* ni *verifies.*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kigwangala nina orodha kubwa ya watu hapa na muda sio wangu basi nikupe dakika moja hivi *at least u-summarized*

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kama tumeingia kwenye mfumo wa *mixed economy* na kwamba Serikali nyakati fulani upanga bei maana yake *safeguard* pekee ambayo ataipata mkulima ni uwepo wa *price stabilization fund* kwamba kama Serikali imepanga bei bahati mbaya imeanguka kule kwenye soko la kimataifa basi Serikali itainunua pamba yote kwa bei ambayo haitoathiri maisha ya mkulima itakaa nayo halafu bei zikipanda tena kule Serikali itauza kule ita-*recoup* fedha zake kwa sababu hili limejitokeza kwenye sekta ya pamba miaka miwili iliyopita tulipiga siasa hapa Bungeni sisi watu tunaotoka kwenye pamba tukataka mkulima apewe zaidi ya shilingi 1200 matokeo yake bei zilivyoanguka kwenye soko la dunia na huku chini sasa wafanyabiashara wetu hawezi kumpa mkulima bei ambayo angestahiki kupata*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na matokea yake Serikali ikarudi tena kwa wafanyabiashara ikawa-*convice* wanunue kwa bei ileile ambayo haiwalipi kule kwenye soko kwa maana ya kwamba mwisho wa siku Serikali ingewa-*compensate* wale wafanyabiashara mpaka leo Serikali haijafanya hivyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo nishauri Serikali tu ianzishe huo mfuko ili mambo kama hayo yakijitokeza waweze kuyatatua kwa wakati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Umeeleweka vizuri Mheshimiwa Dkt. Kigwangala na Mwenyekiti wa Kamati ya kilimo naye anakusikia ni moja ya mambo ambayo mtaya-*peak* na hata mkumuhitaji Waziri wa Fedha kwenye kamati yenu ya kilimo nyinyi niambieni lakini baada ya mambo haya yani huko mbele tunakoenda huko.

Tunaye mchumi mwingine ni eneo linahitaji kuangaliwa namna tunavyokwenda ile jana nilikuwa natania nasema ukigeuka huku Serikali, ukigeka huku ndio haya lazima mtu apate kidogo lakini Serikali haiwezi kutoka kabisa nao wakulima wetu na unyonge wao ulivyo watapigwa na baridi ya hawa wafanyabiashara wakubwa itakuwa tena shida nyingine tutakuja hapa tukilia. Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama!

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niwapongeze sana Mheshimiwa waziri na Naibu Waziri kwa namna ambavyo wamejibu hoja za Wabunge kwa kina na kwa ubobezi. Hata hivyo, Mheshimiwa Mwenyekiti hivi ninavyozungumza wananchi wengi wakulima wadogo wanalalamika na wanatukumbusha kwamba, Serikali iliweka utaratibu kuhusu ushuru wa mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba mwananchi yeyote mkulima anapofika kwenye mageti ya kukusanyia

mapato ya halmshauri ushuru wa halmashauri kama ana mzingo au ama mazao ambayo ni chini ya tani moja hatakiwa kutozwa ushuru. Lakini hali iliyopo sasa mtu mwenye kilo 100 mwenye kilo 50 mwenye kilo 200 wote wanatozwa ushuru, nini kauli ya Serikali kuhusu jambo hili mahususi ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Halmashauri huko zinatweta! Ushuru wa halmshauri Mheshimiwa Ummy alishika kichwa aliniangalia halmashauri zitaendaje Mheshimiwa Naibu Waziri ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina *position* ya Serikali mpaka sasa haijabadilika na chini ya tani moja mkulima hatakiwi kulipa ushuru wa aina yeyote haya ndio maelekezao na ndicho tulichoahidi wapiga kura na ndio *commitment* ya Chama Cha Mapinduzi ambayo tuliwapa wananchi. Kwa hiyo, tutumie tu nafasi hii kumuomba Mheshimiwa Mbunge kwamba pale ambapo inatokea kesi za namna hiyo na sisi tumekuwa tukipokea meseji na simu nyingi tutakuwa tunawasiliana na wenzetu wa TAMISEMI ninaelewa kinachotokea katika *level* ya halmashauri na sisi wote ni Wabunge tunajua kinachoendelea kwamba unaweza ukakuta *trader* amenunua gunia nyingi za kutosha pale amezihifadhi *somewhere* halafu anazisafirisha kwa bajaji hiyo nayo ni kesi ambayo ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naamini kwamba *position* ya Serikali na maelekezo na ahadi tuliyoitoa kwenye uchaguzi mkulima anayelima chini ya tani moja hawezi kutozwa ushuru, na sisi kama Wizara tutaisimamia hili. Lakini vilevile halmashauri nadhani pale ambapo kunatokea kutumia hiyo *loop hole* kwa *traders* kwa ajili ya kukwepa ushuru hilo nalo tunaweza tukalitafutia utaratibu namna ya kui-*deal* nalo lakini *position* ya Serikali haijabadilika mpaka sasa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana nashukuru sana kwa sababu ya muda tuendelee Mheshimiwa Keneth Nollo.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba busara ya Serikali kuhusu bajeti yetu ya kilimo kuwa ndogo ione namna ya kuiapandisha na nimefanya hivi kwa kuangalia katika *East Africa* nimechukua nchi kubwa ya Uganda, na Kenya bajeti ya Kenya ni tirioni 1.2 kwa hela ya Tanzania, bajeti ya Uganda ni bilioni 863 kwa hela ya Tanzania.

**MWENYEKITI:** Hujaeleweka bado!

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema nilikuwa natoa hoja.

**MWENYEKITI:** Bajeti ya Wizara ya Kilimo ya Kenya?

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Ya Kenya.

**MWENYEKITI:** Aaah! Hebu irudie sasa.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekit, ni tirioni 1.2 bajeti ya kilimo Wizara ya Kilimo Uganda ni bilioni 863.9 bajeti yetu inakuja bilioni 294, nilikuwa naomba busara ya Serikali ebu wajivutevute tufanane na majirani zetu hawa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Nollo nilikuruhusu uendelee tu lakini tayari lilishakuwa *covered* na ndio tumesema kwamba Waziri wa kilimo kwa mwaka huu twende hivyo lakini aendelee kuangalia kwa sababu bado Waziri wa Fedha bajeti yake hatujaipitisha. *(Makofi)*

Tukawa tume-*question* kuanzia mwakani na kwenda mbele moja ya bajeti ambazo sisi Kama Bunge tutazitazama kipeke yake ni bajeti za Wizara ya Kilimo, na tunakushuru sana Mheshimiwa Nollo kwa kutupatia hizo *comparison* za majirani zetu tu hapa karibu jinsi ambavyo wanatenga fedha katika sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, *seriously* sisi mwakani wenzetu Serikali mtuelewe mapema natukisema kilimo maana yake ni katika

upana wake kilimo mifugo uvuvi katika eneo hili, msituambia habari ya mabarabara nayo ni kilimo sijui umeme ni kilimo, aaah! Hii kilimo mifugo hapo. Kwa hiyo, tumekwisha mfikikishia Waziri wa Fedha pale na mawaziri wapo hapa wamesikia mwakani tunataka *at least* inaweza hata ikadouble kwa kuanzia hiyo bajeti ili tuweze kwenda. *(Makofi)*

Hizi bilioni 200 si lolote si chochote bilioni 200 mbona tumeambiwa kwa *figure* hapa sijui aliye-*calculate* amepata ngapi tuliambiwa ni *less than one percent* sijui *exactly* ni ngapi kwa toto bajeti. Sasa ni aibu kama kweli tunatoa *less than one percent* endapo hesabu hiyo ni kweli ni kitu ambacho lazima tuone aibu.

Huwezi kuwapa asilimia zaidi ya ngapi wananchi wa Tanzania ambayo ndio *large population activity* yao hiyo tukatoa fedha hizi ambazo tunazitoa kwa mwaka huu tuvumilie lakini mwakani tusiendelee kuwalaumu mawaziri wetu na wataalam wetu hawa wakati hatuwapi fedha ya kufanya mabadiliko makubwa kwenye kilimo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Nollo tuko pamoja na wewe. Mheshimiwa Seif Gulamali. *(Makofi)*

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru kwa kunipa nafasi katika *windup* ya Mheshimiwa Waziri au wizara tulikuwa tumezungumzia juu ya kulinda viwanda vya ndani na tukatolea mfano kiwanda cha Minjingu ambacho kinazalisha mbolea kwa ajili ya mazao yetu. Hivyo nilikuwa naomba *commitment* ya wizara juu ya kulinda viwanda vya ndani atueleze Bunge *then* tutajua kama tutaendelea au tutamwachia ahsante.

**MWENYEKITI:** Wakati unachangia jana ulikuwa unazungumzia kama vile Minjingu wanazalisha *NPK* sijui! Lakini sio kama Minjingu wanazalisha *forcepate* peke yake no sure lakini waziri atatufafanuliwa kuhusu Minjingu mlisikia mchango wao Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutolea maelezo hoja ya Mheshimiwa Gulamali kama

ifuatavyo;- kwanza ni kweli wanazalisha *double* Minjingu lakini bahati nzuri na sisi tumeliona hilo, la viwanda vya ndani kwa sababu sana tunatumia fedha nyingi sana kwa ajili ya kuagizia pembejeo kwa ujumla wake ikiwa ni pamoja na viwatilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefanya ziara kwenda Minjungu nimezungumza nao nimekuta wanapanua uzalishaji na tuliwawekea *commitment* kwamba kila mbolea ambayo inaonekana ina ubora sawa na ndani tutahakikisha kwamba tunainunua kabla ya kununua ya nje. Kwa hiyo, tunahitaji ubora na wasiwe wamepiga bei tofauti sana na nj lakini wakiweza kuweka bei wakifikia bei ya ile mbolea inatoka nje na ubora unalingana tutachukuwa ya ndani. Naomba nitangaze ili kupitia Bunge lako Tukufu kwamba na wawekezaji wengine tunawakaribisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanye hivyo hivyo na tunafanya hivyo kwa pembejeo zote kuna viwanda viwili sasa Arusha vimefunguliwa kwa ajili ya viwatilifu na tumewahakikishia hivyohivyo kwamba watakapozalisha ndani wasiongeze bei ubora ubaki uleule tutanunua vya ndani kabla ya kununua nje.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Mheshimiwa Bashe nilimuomba akae na kufanya mazungumzo na watu wa Minjingu, ameendelea na mazungumzo nao. Lakini vilevile kuna mbolea ya tumbaku, ambayo hawa wanatuambia kwamba inafanya kazi vizuri lakini ainunuliwe tumewaambia wafanye majaribio haraka ili tuchukue mbolea ambayo inatoka ndani ya nchi hiyo ni *commitment* ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mrisho Gambo.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakusudia kushika shilingi kama sitapata majibu ya kueleweka. Mkoani Arusha kulikuwa kuna mashamba ya maua 17 maana kwa nchi nzima lakini mashamba 11 tayari yameshafungwa. Na Serikali inakosa ajira zaidi ya elfu 4 kiasi

cha kuongeza wamachinga kule mjini, lakini pia na fedha ya kigeni US dola milioni 24,450,000. Lakini cha kushangaza sasa hivi Serikali moja ya mashamba hayo shamba la Arusha *groum* wamewapatia watu wa SUMA JKT ambao wanalima mahindi badala ya kulima maua na mbogamboga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba kupata mkakati wa Serikali wana mpango gani kama ikionekana kwamba wawekezaji hawa wameshindwa kutafuta wawekezaji ambao watawekeza kwenye jambo lile hili tuweze kupata ajira lakini pia tuweze kupata fedha za kigeni ili tupate pesa nyingi zaidi na mwisho wa siku tuweze kuongeza bajeti ya Wizara ya Kilimo.

**MWENYEKITI:** Hilo shamba walilopewa SUMA kabla lilikuwa linazalisha nini?

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lilikuwa linazalisha mbogamboga *(vegetables).*

**MWENYEKITI:** Shamba la *horticulture* linalimwa mahindi ambayo hata Kongwa yanaweza yakalimwa. *(Kicheko)*

Ufafanuzi wa jambo hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikiri alichokisema Mheshimiwa Mbunge na nitumie nafasi hii ku-*recognize effort* iliyofanywa na *Tanzania Horticulture Association* kwenye issue hii ya mashamba haya ambayo yalifungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe Mheshimiwa Waziri alinituma nikaenda, nimetembelea mwenyewe mashamba hayo. Baada ya kuyatembelea hayo mashamba Wizara ya Kilimo tumeandika *paper* kupeleka Wizara ya Fedha kwa sababu haya mashamba waliyokuwa wamekabidhiwa walipewa mikopo na *Tanzania Investment Bank* ili wa-*invest* katika mashamba haya waka-*divert* zile fedha na hawakuyaendeleza, *then* wakashindwa kurudisha ile mikopo. Serikali ikayatwaa mashamba haya na baada

ya kuyatwaa sisi kama Wizara tulivyokwenda kuyatembelea yote tumejiridhisha kwamba tunahitaji ku-*revive* sekta ya *horticulture* na tutawekeza katika maeneo hayo. Tumepeleka andiko Wizara ya Fedha ili lile deni ambalo lilikuwa la *TIB* lichukuliwe kama *part* ya *equity* katika hayo mashamba na turuhusu *private sector* ya Kitanzania iwekeze katika mashamba hayo ili tuweze ku-*revive. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mjumbe kwamba tumepeleka tayari maandiko ya hayo mashamba yote pamoja na hilo alilolitaja ambalo lina miundombinu ya *cold chain facilities* na vitu vingine ili liweze kurudi katika shughuli zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, katika mashamba hayo kulikuwa na wazalishaji ambao bado wako makampuni matano, walikuwa wana *issues* ambazo zinahusiana na masuala ya *TRA.* Kama Wizara kwa sababu sisi ni *interested party,* tumezi-*compile issue* zote tunafanya majadiliano na wenzetu wa Wizara ya Fedha ili tuweze ku-*unlock.* Tumemuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu hivi karibuni ataongoza kikao ambacho kitahusisha hao wawekezaji walioko kwenye hiyo *subsector* na kuyamaliza matatizo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe, naamini *with time* haya matatizo yaliyoko katika hayo mashamba na sekta nzima ya *horticulture* tutakuwa tumeya-*resolve.*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mrisho Gambo kwa sekunde chache.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Serikali imeweza kuwapa hawa SUMA-JKT, haioni sasa umefika wakati wa kuwapatia wawekezaji wengine ambao wataelekeza kwenye sekta hii hii wakati wanashughulikia na changamoto nyingine? Maana mwisho wa siku changamoto bado ziko palepale; ajira hakuna pamoja pia na masuala ya fedha za kigeni.Naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kwa sababu katika yale majibu yao wamesema kutakuwa na kikao ambacho hata Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa Mwenyekiti, hebu tuwape nafasi waende wakafanyie kazi kwanza, *including* haya mapendekezo ambayo umeyatoa. Ahsante sana.

Mheshimiwa Rehema Migilla kwa kifupi sana.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda nami nipate ufafanuzi kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika zao letu la tumbaku tumeona Serikali ilikuwa imepanga bei elekezi kwa ajili ya kununua tumbaku ambapo ilikuwa ni dola 1.61. Hata hivyo, hawa wanunuzi wamekwenda kununua tumbaku yetu kwa wakulima wetu kwa dola 1.2 ambayo ni kinyume kabisa hata na gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nijue, hawa wanunuzi kwa nini wamekwenda kinyume na bei elekezi ya Serikali? Hatuoni hapo kama tunakwenda kumdidimiza mkulima ambaye anatumia gharama kubwa, je, Serikali iko nyuma ya hawa watu au vipi?

**MWENYEKITI:** Umeeleweka Mheshimiwa Mjumbe. Mheshimiwa Naibu Waziri, ufafanuzi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tuseme kwamba siyo kwamba tumetoa bei elekezi, katika *Tobacco Council* zile *grading,* kuanzia *grade one* mpaka ya mwisho baada ya kubadilisha madaraja na mwaka huu tumeanza kubadilisha madaraja; dola 1.6 ni *average price,* kwamba ni bei ya wastani ambayo tunaitarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa Mkoa wa Tabora Wilaya za Kaliua na Urambo, wanachokifanya katika hatua za awali kwamba hupeleka sokoni yale madaraja ya chini. Mpaka sasa nimhakikishie Mheshimiwa Mjumbe, tunafanya *follow up* kwa karibu sana jambo linalofanywa na

Kampuni ya *Alliance.* Kampuni ya *JTI* inatoa mpaka dola 1.8, dola 2 mpaka dola 2.2. Kwa hiyo tumewatuma watu wetu wa Bodi kwenda kuangalia mnada mmoja uliofanyika ambao *Alliance* wamenunua kwa dola 1.5, kama wamefanya *any cheating* au kama kuna mchezo wowote wanaofanya katika kubadilisha zile *grades,* niwahakikishie tutachukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Mjumbe kwamba atupe nafasi na sisi kama Wizara, kwa sababu mpaka sasa imefanyika minada sita tu ya tumbaku katika haya maeneo yote kuanzia Kahama mpaka maeneo hayo. Kwa hiyo, tunaamini kwamba wanunuzi watanunua kwa makubaliano tuliyokubaliana katika *Tobacco Council* na kama kuna *any foul play* inafanywa tutachukua hatua zinazostahili.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, sasa Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN – KATIBU MEZANI:** *Guillotine.*

**FUNGU 43 – WIZARA YA KILIMO**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management*...........Sh. 6,534,709,119
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*...Sh. 1,422,654,661
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit* ... ... Sh. 1,736,401,177
Kifungu 1004 – *Agriculture Training Institute*....Sh. 21,153,550,387
Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit* ... ... ... ... ... ... Sh. 438,816,315
Kifungu 1006 – *Procurement Mgt Unit* ... ... ... ... Sh. 480,061,906
Kifungu 1007 – *Government Communication Unit*................................................Sh. 379,288,885
Kifungu 1008 – *Legal Services Unit* ... ... ... ... ... Sh. 488,406,489
Kifungu 1009 – *Mgt Information Systems Unit* ... Sh. 455,491,465
Kifungu 1010 – *Environmental Management Unit*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 340,236,533
Kifungu 2001 – *Crop Development* ... ... ... Sh. 22,747,950,642
Kifungu 2002 – *Agricultural Mechanization* ... ... Sh. 772,078,539
Kifungu 2003 – *Agriculture Land Use Planning & Management*..............................Sh. 848,465,885

Kifungu 2004 – *Plant Breeders' Unit* … … … … Sh. 220,267,381
Kifungu 5001 – *National Food Security* … … … Sh. 6,104,863,616

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 24 – TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management Division…* … … Sh. 1,795,551,160
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit* … … Sh.279,467,840
Kifungu 1003 – *Planning Monitoring and Evaluation Unit* … … … ... ... ... ... .... ... ... ... ...Sh.211,469,000
Kifungu 1004 – *Government Communication Unit* … … … ... ... ... ... ... ... ... ... ...Sh. 258,164,000
Kifungu 1005 – *Legal Services Unit* … … … … ... Sh. 194,220,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit* .... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh.126,560,000
Kifungu 1007 – *Information Communication Technology* … ... ... ... ... ... ... ... Sh. 705,073,000
Kifungu 1008 – *Internal Audit Unit* … … … … ... Sh. 206,244,000
Kifungu 1009 – *Research and Training Unit* … Sh. 4,061,869,000
Kifungu 4001 – *Cooperative Prom. & Coordination Section* … … ... ... ... ... ... ... ... ... ...Sh.301,488,000
Kifungu 4002 – *Cooperative Microfinance Section*..........................................Sh.229,260,000
Kifungu 4003 – *Regional Cooperative Offices*… ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...Sh. 5,120,496,000
Kifungu 4004 – *Cooperative Marketing & Investment Section* … ... ... ... ... ... ... ... ... ... ..Sh.129,058,620
Kifungu 4005 – *Registration Service Section* … Sh. 178,800,000
Kifungu 4006 – *Inspection and Supervision Service Section* … … ... ... ... ... Sh.2,782,406,380

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## FUNGU 05 – TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management*... ... Sh. 1,167,344,600
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit* ... ... Sh. 337,521,800
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation* ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 305,417,700
Kifungu 1004 – *Government Communication Unit*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...Sh. 98,339,200
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 173,824,600
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit* ... ... ... ..... .... Sh. 101,185,700
Kifungu 1007 – *Information Communication Technology Unit* ... ... ... ... ... ... Sh. 100,379,000
Kifungu 1008 – *Legal Services Unit* ... ... ... ... ... Sh. 129,582,300
Kifungu 1009 – *Environmental & Social Management Unit* ... ... ... ... ... ... .... .... ... ... ... Sh. 159,789,300
Kifungu 2001 – *Design and Research Division* ... Sh. 858,965,600
Kifungu 2002 – *Irrigation Infrastructure Development* ... ... ... ... ... ... Sh. 736,755,600
Kifungu 2004 – *Operations Division* ... ... ... ... ... Sh. 591,492,600
Kifungu 2005 – *Compliance & Quality Assurance Section* ... ... ... ... ... ... ... ... .. . Sh. 226,852,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## KITABU CHA NNE

## MIPANGO YA MAENDELEO

## FUNGU 43 – WIZARA YA KILIMO

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management* ... ... ... ... ... ... Sh. 2,019,500,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit* ... ... Sh. 10,998,000,000
Kifungu 1004 – *Agriculture Training Institute* ...Sh. 34,995,500,000
Kifungu 1009 – *Management Information Systems Unit* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...Sh. 150,000,000
Kifungu 2001 – *Crop Development* ... ... ... ...Sh. 22,900,000,000

Kif.2002 – *Agricultural Mechanization* ... ... ... ... Sh. 800,000,000
Kifungu 2003 – *Agriculture Land Use Planning & Management* ... ... ... ... ... ... ... Sh. 800,000,000
Kifungu 5001 – *National Food Security* ... ... Sh. 92,085,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 05 – TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI**

Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation*... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 68,500,000
Kifungu 1007 – *Information Communication Technology Unit* ... ... ... ... ... ... Sh. 750,000,000
Kifungu 1009 – *Environmental & Social Management Unit* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...Sh. 100,000,000
Kifungu 2001 – *Design and Research Division* ... Sh. 351,500,000
Kifungu 2002 – *Irrigation Infrastructure Development* ... ... ... ... ... Sh. 15,000,000,000
Kifungu 2004 – *Operations Division* ... ... ... ... Sh. 30,200,000,000
Kifungu 2005 – *Compliance & Quality Assurance Section* ... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 30,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarudia.

*(Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mheshimiwa Waziri, taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imepitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Fungu 43 – Wizara ya Kilimo, Fungu 24 – Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Fungu 05 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, naomba Bunge lako Tukufu liyakubali na kuyapitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyo ada, ni wakati wa kuifanyia maamuzi hoja hii ya kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na ndiyo wakati muhimu kwa kweli kuliko wakati mwingine wowote.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2021/2022 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Wote wameafiki kabisa. *(Makofi)*

Ni maajabu makubwa sana kwamba hakuna ambaye amepinga bajeti hii ya Kilimo. Ni heshima kubwa sana kwamba Bunge limewapigia saluti Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote

ambao mmefuatana na Katibu Mkuu mlioko huko kwenye *gallery*. *(Makofi)*

Kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge niwapongeze sana kwa kazi nzuri ambayo mmeendelea kuwa mnaifanya katika mazingira ambayo bajeti yenu kwa kweli ni ndogo sana. Mmejitahidi sana na Wabunge wamefanya kazi yao ya kuwashauri, tena sana na bado watu wamekosa nafasi ya kuendelea kusema, ni ile kuwiwa. Mmewasikiliza vizuri, mlikuwepo; tunamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwepo, amesikiliza na tunamshukuru kwa jinsi ambavyo huwa anatenga muda wake maalum, kwa kweli yako mazao ambayo amejaribu kuyapa kipaumbele kikubwa na kipekee. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mara kwa mara mnamuona Mheshimiwa Waziri Mkuu jinsi anavyokazania kupambania mazao hayo. Ingawa sikumsikia katika siku mbili hizi Mbunge hata mmoja wa Kigoma akizungumzia michikichi. Sasa nilikuwa najiuliza kulikoni lakini mambo haya tuyabebe sote, siyo tu Waziri Mkuu anapokuja huko; Wabunge tuwe ndiyo mstari wa mbele kabisa katika kubeba hoja hizi. *(Makofi)*

Wale wa kutoka Tanga, Morogoro na kwingine, pamoja na siasa tunazoongea tuongelee katani pia katika kuiendeleza. Maeneo mengine, hata Dodoma tunaweza tukalima katani. Wanasema katani inaweza ikalimwa maeneo mengi sana.

Kwa hiyo, tunapongeza sana yote ambayo mmeyasema kuhusu *horticulture,* ushirika, masoko, umwagiliaji, mbegu, mambo ya butura, kangomba na kadhalika jinsi mtakavyopambana nayo, kwa kweli kilimo kina mambo mengi sana. Kama tulivyosema, ukishakuwa Waziri au Naibu Waziri wa Kilimo, una mzigo mzito sana. Kwa sababu ni matatizo kushoto kuna hiki la kufanya, kulia kuna mashamba, kwanza sijui hata kama mnalala, mambo ni mengi sana kwenye kilimo. Tunawaombea, ndicho tunachoweza kufanya na kuwaunga mkono muweze kufika mbali katika kuwasaidia Watanzania hawa.

Nawaagiza Kamati ya Kilimo kwa kweli kupitia mjadala huu na ninyi kwa upande wenu na mtushauri huku tunakokwenda tujipange namna gani ili Bunge hili la Kumi na Mbili liweze kuisukuma Serikali ili tuweze kufanya mapinduzi makubwa sana katika kilimo. Jambo hili la kilimo liwe ni moja ya malengo yetu, kama alivyosema Mheshimiwa Balozi Dkt. Bashiru ambapo tutakapomaliza Bunge hili la Kumi na Mbili, angalau tuwe na jambo moja kwamba tumesogeza agenda hii ya kilimo mahali, maana yake imekwama miaka mingi sana. Sasa sisi safari hii tujaribu kujitwisha jambo hili la kilimo, tusimuachie Waziri Mkuu au mtu mwingine peke yake, tujitwishe sote kwa pamoja tuone tunakwenda nalo wapi. Nami naamini kwa pamoja tunaweza. Kwa hiyo, mtatushauri namna ya kwenda. *(Makofi)*

Binafsi nawashukuru na kuwapongeza sana Kituo cha Utafiti cha Naliendele, sijui kama Mkurugenzi wake yupo au hayupo, lakini salamu zao ziwafikie. Vituo vingine vya Utafiti wa Kilimo ambavyo vinafanya *applied kind of research* basi navyo viwaige wale. Wasijifungie tu huko wanafanya *research* zao huku wamejifungia, haitusaidii sana, lazima wahakikishe wanafanya kazi kama ya Naliendele. Naliendele wanashuka mpaka kwa mkulima, yaani wanajitahidi kwelikweli wale watu. *(Makofi)*

Naamini na wenyewe walitetereka kidogo baada ya zile fedha za korosho kuleta taabu kwa sababu nadhani *percent* fulani walikuwa wanapata pia katika uendelezaji wa zao hili. Mjitahidi Naliendele wasirudi nyuma, ni *key* katika kukuza zao la korosho, *very key. (Makofi)*

Jambo moja halikusemasemwa sana lakini na lenyewe ni muhimu sana na ni tatizo kubwa huku tunakokwenda kwenye kilimo ni palizi. Palizi kwa maoni yangu ndiyo *stumbling block* kubwa kuliko kitu kingine chochote. Sikuona mtu akiliongelea, lakini palizi ni pasua kichwa. Wewe lima eka 300, 500 za mahindi, nani anakuja kupalilia hilo shamba lako? Vijana wote waliomaliza *form four* sasa hivi na kuendelea wasomi, alichokuwa anasema Mheshimiwa Tabasam wasomi wale, shida, vibarua hakuna, palizi hamna.

Hatusemi watu wawe vibarua, wala sipigii debe vibarua maana kwa teknolojia za wenzetu wanalimaje mashamba makubwa, huko Zimbabwe, Zambia; wanalimaje, kwa kutegemea palizi ya nani?

Kwa hiyo, lazima masuala ya magugu haya ili watu waweze kulima tuje na teknolojia na *techniques* za kupambana na jambo la palizi. Palizi ni mtihani, siyo utani, kwa mtu ambaye anashughulika na kilimo mtakupaliana na mimi. Utapiga palizi ya kwanza, ya pili majani yako hapa, unaanza kutweta. Vijana wa siku hizi hata wa Dodoma hapa mahali pa labda eka moja ungeweza kupalilia Sh.10,000, wanashika kiuno wanakwambia bwana hapa bila Sh.50,000 eka moja utalima mwenyewe. Eneo la palizi nalo mlitazame Mheshimiwa Profesa na miaka inayokuja hao watu wa kufanya hizo kazi hawapo, itazidi kuwa ngumu sana *as we go.*

*Otherwise,* tuko nanyi, tunawapongeza. Pale ambapo tulikuwa wakali zaidi basi chukulieni *light* kwa sababu ni kazi na watu wana mihemko tofauti kwa sababu ya mazingira halisi na watu wanataka kuona matokeo.

Nina matangazo mawili, matatu; la kwanza, Mheshimiwa Waziri Mkuu anaomba niwatangazie Wabunge mnaotoka maeneo ya korosho mkutane Msekwa kesho, tarehe 26 Mei, saa nane na nusu mchana, wakiwepo Waheshimiwa Mawaziri na *CEO* wa Bodi pia atakuwepo, Katibu Mkuu na wengine. Kwa hiyo, Wabunge kutoka maeneo haya mkutane pale Msekwa saa nane na nusu mchana kesho.

Mheshimiwa Chaya na wewe uende pale, siyo wakisema maeneo ya korosho unawaachia Lindi na Mtwara. Mimi korosho ya wakulima wangu bado kidogo hatujafika kwenye *category,* lakini na sisi miaka miwili, mitatu ijayo tutahudhuria, tutaanza kuwa ni wakulima sasa.

Tangazo lingine linatoka kwa Katibu wa Bunge; anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Ofisi

ya Bunge imeingia makubaliano *(MoU)* na Mfuko wa Pembejeo za Kilimo *(Agricultural Inputs Trust Fund)* kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa mikopo ya matrekta kwa Waheshimiwa Wabunge unaotolewa na Mfuko huo wa Pembejeo. Masuala ya msingi katika *MoU* hiyo ni kama ifuaatvyo: -

(i) Riba ya mkopo ni asilimia saba kwa mwaka na kiwango cha juu cha mkopo ni shilingi milioni 300. Mkopo unatakiwa kurejeshwa kabla ya tarehe 30 Juni, 2025;

(ii) Mkopaji hatapewa pesa taslimu, atapewa trekta kwa utaratibu uliokubaliwa kwenye mkataba; na

(iii) Wabunge wenye sifa za kupata mkopo huo ni wale ambao bakaa ya mishahara yao, *balance* yao, inaruhusu kukopeshwa kiwango husika kwa uthibitisho wa Ofisi ya Bunge ambayo itakuwa na wajibu wa kukata marejesho kwenye mshahara wa mkopaji na kupeleka kwenye Mfuko kwa mwezi hadi mkopo utakapokamilika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, watakaohitaji huduma hiyo wanaweza kupata maelezo zaidi kutoka Ofisi ya Katibu wa Bunge.

Matrekta yapo ya shilingi milioni 45, kuna ya shilingi milioni 50 inategemeana na aina ya treka. Kwa hiyo, hatuzungumzii mkopo wa shilingi milioni 300, hapana, tunasema *it can go up to* kutegemeana na lakini suala zima ni kukopa trekta na utakuwa *delivered* trekta na siyo fedha.

Kuna Wabunge huwa wanachukua trekta peke yake halina hata jembe, hiyo biashara hatukubali. Kama unachukua trekta na jembe lake ikiwezekana basi na *harrow* na kadhalika. Ni wale ambao mishahara inaruhusu.

Tangazo lingine ni kwamba Wizara ya Elimu inawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba kuna Maonyesho ya Pili ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Maonyesho ya kwanza yalifanyika mwezi uliopita tu, maonyesho ya pili

ambayo yameandaliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE)* kwa kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi *(TPSF)* yatafanyika pale kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma kuanzia tarehe 27 Mei hadi tarehe 02, Juni. Kutakuwa na maonyesho ya masuala ya kukuza ujuzi na maendeleo ya uchumi wa viwanda. Mnakaribishwa mkipata nafasi muweze kutembelea hapo.

Baada ya matangazo hayo na muda wetu hauruhusu tuweze kuendelea hata kidogo, basi niwashukuru tena kwa ushirikiano. Kesho ni Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa siku moja, siyo siku mbili. Siku itakayofuata itakuwa ni Mifugo ambayo ilikuwa nyuma kidogo, itasogea sasa mbele. Mifugo itakuwa siku mbili halafu watafuata wiki ijayo wanaoendelea na ratiba, tutawasambazia lakini ndiyo kama nilivyotangaza mwanzoni pale; watakuja Nishati na wengine watakaofuata. Maliasili ambao walikuwa ni siku moja sasa watakuwa siku mbili, hii siku ambayo tumewapunguzia Ardhi watachukua Wizara ya Maliasili kwa sababu dalili zinaonesha kuna mengi ya kusema kwenye Maliasili. Tutaliweka sawa kesho vizuri zaidi, kwa sababu ya muda, nashukuru sana.

Kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 2.23 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 26 Mei, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*